15 FEBRUARI, 2024

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA NNE

Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 15 Februari, 2024

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tuketi.

Katibu.

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

NAIBU WAZIRI WA FEDHA:

Muhtasari wa Tamko la Sera ya Fedha – Mapitio ya Nusu Mwaka 2023/2024 *(Monetary Policy Statement - Mid - Year Review 2023/2024)*.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC)* kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023.

MHE. ABDUL YUSSUF MAALIM K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023.

SPIKA: Ahsante sana.

Katibu.

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali.

Tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile, Mbunge wa Nachingwea, sasa aulize swali lake, kwa niaba yake Mheshimiwa Agnes Hokororo.

Na. 211

Kuligawa Jimbo la Nachingwea

MHE. AGNES E. HOKORORO K.n.y. MHE. AMANDUS J. CHINGUILE aliuliza: -

Je, lini Serikali italigawa Jimbo la Nachingwea?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Ummy Nderiananga, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile, Mbunge wa Nachingwea, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 75 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, imeipa mamlaka Tume ya Taifa ya Uchaguzi, kuchunguza na kugawa mipaka ya Majimbo ya Uchaguzi katika Jamhuri ya Muungano mara kwa mara na angalau kila baada ya miaka kumi baada ya kupata kibali cha Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, katika maandalizi ya kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025, Tume ya Taifa ya Uchaguzi itatangaza utaratibu na sifa za kugawa maeneo mbalimbali kwa ajili ya uchaguzi. Hivyo, napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge, kuwa mara Tume itakapotangaza kugawa au kubadili majina ya Majimbo ya Uchaguzi, awasilishe ombi lake la kuligawa Jimbo la Nachingwea kwa kuzingatia utaratibu utakaotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza.

MHE. AGNES E. HOKORORO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi na naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Jimbo la Nachingwea ni kubwa sana na lina kata ambazo zinapakana na Mkoa wa Morogoro lakini na Mkoa wa Ruvuma, Serikali pamoja na huo utaratibu haioni sasa ipo haja ya kugawanya maeneo ya kiutawala ili angalau kurahisisha upatikanaji wa huduma za kijamii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Jimbo la Ndanda, limetawanyika pia kuelekea Mkoa wa Ruvuma, ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Ndanda, ina sababishia wananchi watembee zaidi ya kilometa 80 kufuata huduma za Serikali. Je, Serikali haioni haja pia ya kugawa Jimbo hilo na kupatia halmashauri nyingine? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA): Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Agnes Hokororo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la kuongeza Maeneo ya Utawala nilikuwa namshauri Mheshimiwa Mbunge, aendelee kuwasiliana na wenzetu wa TAMISEMI, kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa, Mamlaka, Wilaya sura ya 287 na kifungu cha 87(a)(1)(2) cha Sheria za Mamlaka za Serikali za Mitaa, kama zilivyorekebishwa katika marekebisho ya Sheria mbalimbali ili waweze kufuata huo utaratibu wa kuanzia u-*DC*, *DCC*, *RCC* na baadaye kuja Taifa ili waweze kuona namna ya kuzingatiwa kipindi hiko ambacho TAMISEMI, watafanya jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili. Kuhusu Jimbo la Ndanda, kama nilivyojibu kwenye majibu yangu ya msingi kwa mujibu wa Ibara ya 75 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tume imepewa mamlaka. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge, muda utakapofika Tume itakapotangaza basi na yeye afuatae utaratibu huo ambao utawekwa na Tume ili kusudi kuona jambo hilo utekelezaji wake, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwenye jibu la msingi, Waziri anasema Mbunge, aombe, mimi naamini kunakuwa kuna timu ya kufanya utafiti kutokana na vigezo. Hiyo habari ya Wabunge kuomba unakuta maeneo mengine yanagawanywa kisiasa, linaitwa Jimbo la Mjini, lina kata saba vijijini mwisho wa siku linaleta athari kwenye Mipango Miji ya maendeleo kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, ni vigezo gani vya msingi ambavyo mnavitumia ili kuhakikisha jimbo linagawanywa kwa ajili ya kuleta maendeleo ya wananchi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA) Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nilipokuwa natoa maelezo yangu ya awali nilisema Mbunge aombe, maana yake ni baada ya Tume kuweka ule utaratibu sasa utafanya uweze kuomba, lakini vigezo naomba nivitaje kama ifuatavyo: -

(i) Ukubwa wa Jimbo husika, unaangaliwa;
(ii) Mipaka ya kiutawala;
(iii) Hali ya kiuchumi kama inaturuhusu;
(iv) Hali ya Kijiografia;
(v) Upatikanaji wa mawasiliano;
(vi) Jimbo lisiwe ndani ya Halmashauri au Wilaya mbili; na
(vii) Kata moja isiwe ndani ya Majimbo mawili.

Mheshimiwa Spika, lakini lipo sharti lingine la Ofisi yako ya Bunge, kutuambia kama tunayo nafasi humu ndani yakuendelea ku-*accommodate* idadi kubwa zaidi ya Wabunge. Kwa hiyo, nimetaja kwa uchache naomba niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge, muda utakapofika Tume ikitangaza basi vigezo na masharti vitakavyowekwa vitatuongoza kuona kwamba Jimbo hili linafaa kugawa au halifai, ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu yako yameeleweka kabisa lakini hoja inarudi, sasa hivi tunaye Waziri, tunayo Ofisi inayoshughulika na Tume ya Mipango, hii ni sehemu ya mipango, Serikali ijipange badala ya kusubiri maombi. Kwa nini? Kwa sababu hata humu ndani wapo Wabunge, wana kata arobaini na kitu, wako Wabunge wana kata nane, ni kwa sababu ya kukosa mipango. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Serikali iweke mipango, igawe kwa mipango yake kuliko kusubiria watu maeneo mbalimbali waombe. Kwa nini? kwa sababu ninyi ndiyo mnajua mipango ya Serikali, si ndiyo jamani, haya ahsante sana kwa majibu yako Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA): Mheshimiwa Spika, ahsante, tumeupokea ushauri wako.

SPIKA: Ahsante sana. Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 212

Fedha za madaraka kwa Waganga

MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza kulipa fedha za madaraka kwa Waganga Wafawidhi wa vituo vya afya na zahanati nchini?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kazi kubwa zinazofanywa na Waganga Wafawidhi wa Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali za Halmashauri ambao ndio wasimamizi wa vituo vya kutolea huduma za afya katika ngazi ya msingi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, iliaandaa andiko linaloonesha hitaji la kuwawezesha wasimamizi wa vituo vya kutolea huduma za afya kulipwa posho ya madaraka kama motisha kutokana na majukumu wanayotekeleza. Aidha, andiko hilo limewasilishwa

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa hatua zaidi, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage, swali la nyongeza.

MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kupata nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Naishukuru Serikali kwamba sasa inaenda kuwalipa posho ya madaraka Waganga Wafawidhi wa Zahanati na Vituo vya Afya kama inavyofanya kwa Walimu wa Sekondari pamoja na Walimu Wakuu wa Shule za Msingi.

Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza; swali la kwanza, kwanza naipongeza Serikali kwa kuendelea kuwalipa posho ya madaraka Watendaji wa Vijiji, japo kuna kusuasua kutokana na udhaifu wa baadhi ya Watendaji lakini kutokana na mapato madogo ya Halmashauri husika. Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya Halmashauri ambazo hazina uwezo kuanza kupata hizo posho kutoka kwa Serikali Kuu, kama ambavyo inafanya kwa Waheshimiwa Madiwani?

Mheshimiwa Spika, swali namba mbili, tunajua vizuri sana kazi kubwa na nzito wanayoifanya Watendaji wa Vijiji na Watendaji wa Mitaa. Je, Serikali haioni kama kuna haja ya hawa Watendaji wa Vijiji na Mitaa kulipwa posho ya madaraka? Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nipokee pongezi za Mheshimiwa Mbunge, kwa Serikali kwa kazi kubwa ambayo inafanywa, lakini nimhakikishie tu kwamba, kama ambavyo nimejibu kwenye swali la msingi kwamba linafanyiwa kazi na baada ya kufanyiwa tathmini na Wizara ya Utumishi, Menejimenti na Utawala Bora, basi tutaona namna gani tunakwenda kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusiana na posho za Watendaji wa Kata. Serikali ilishaanza kulipa Watendaji wa Kata posho kila mwezi na nitumie fursa hii kusisitiza Wakurugenzi wa halmashauri, kote nchini ambao hawajawalipa Watendaji wa Kata posho zao, wawalipe mara moja kwa sababu zimeshaingizwa kwenye bajeti na ni haki yao kulipwa na ni wajibu wa Wakurugenzi kuhakikisha wanawalipa. Sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tutafuatilia na kuchukua hatua pale ambapo tutathibitisha kwamba kuna Mkurugenzi hajalipa posho hizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na posho za Maafisa Watendaji wa Vijiji na Mitaa. Naomba niseme kwamba bado tuna mzigo mkubwa sana wa kulipa posho kwa wataalam wetu, tunatambua kazi kubwa inayofanywa na Watendaji wa Vijiji na Mitaa. Niombe kwanza tulichukue hili tukalifanyie tathmini kuona uwezekano na uwezo wa kibajeti kulitizama huko kwa siku za usoni, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Mohamed Monni, swali la nyongeza. Haya naona alisimama amepata dharura. Mheshimiwa Joseph Annia Tadayo, Mbunge wa Mwanga, sasa aulize swali lake.

Na. 213

Ukarabati wa Kituo cha Afya Lang'ata - Mwanga

MHE. JOSEPH A. TADAYO aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ukarabati wa Kituo cha Afya Lang'ata – Mwanga?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la

Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, Mbunge wa Jimbo la Mwanga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya tathmini ya Vituo vya Afya Vikongwe vinavyohitaji ukarabati. Hadi kufikia Disemba, 2023 jumla ya vituo vya afya 202 chakavu vimeainishwa kote Nchini kikiwemo Kituo cha Afya Lang'ata ambapo vitatengewa bajeti kwa ajili ya ukarabati kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Vituo vya Afya Chakavu, pia ziko Hospitali Kongwe 50 za halmashauri zilizofanyiwa tathmini, na hospitali 38 zimeshapelekewa jumla ya shilingi bilioni 34.2 kwa ajili ya ukarabati katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 na 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, Serikali itatoa kipaumbele cha ukarabati wa Kituo cha Afya Lang'ata katika bajeti zijazo, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Anania Tadayo, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH A. TADAYO: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa kituo hiki kilijengwa takribani miaka 40 iliyopita na hakuna ukarabati wowote ambao umewahi kufanyika kiasi kwamba mpaka sasa hivi vyoo vimefungwa. Na kwa kuwa, eneo hili ni eneo la uvuvi na lina watu wengi sana na halina majisafi na salama kwa hiyo lina magonjwa mengi. Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kuidhinisha angalau milioni 100 za dharura ili kuondokana na changamoto hii inayotishia afya za watu?

Mheshimiwa Spika, swali la pil, je, Mheshimiwa Naibu Waziri, yuko tayari baada ya Bunge hili tuongozane akajionee mwenyewe hali ya kile Kituo cha Afya ili aone umuhimu wa kutoa hizo fedha za dharura, ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika,

ahsante sana. Kwanza nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, kwa namna ambavyo amefuatilia suala la Kituo cha Afya cha Lang'ata, lakini tulishamuelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mwanga, kwamba Kituo cha Afya ni sehemu nyeti sana na sio rahisi kuruhusu Kituo cha Afya kisiwe na vyoo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nitumie fursa hii kumkumbusha na kumuelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mwanga, mapema iwezekanavyo atenge pesa za dharura kwenye mapato ya ndani wajenge vyoo, Kituo cha Afya kiwe na vyoo wananchi wapate huduma bora. Na sisi tutafuatilia kwa sababu hili ni jambo muhimu sana na ni changamoto kuwa na Kituo cha Afya ambacho hakina vyoo.

Mheshimiwa Spika, lakini pili, nipo tayari kufuatana na Mheshimiwa Mbunge, kwenda Mwanga kwa ajili ya ziara lakini ninaamini wakati tunakwenda tutakuta tayari vyoo vimejengwa na wananchi wanapata huduma bora za afya katika eneo hilo, ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Sisi Namtumbo, tuna Vituo vya Afya vitatu, Kituo cha Afya cha Mkongo, Kituo cha Afya cha Lusewa na Kituo cha Afya cha Mputa vilivyojengwa miaka ya 70 na vimechoka kabisa na havina vyumba vya upasuaji wala Wodi za kina Mama na Watoto. Je, Serikali imeweka katika *list* ya hivyo vituo chakavu na ambavyo vitafanyiwa ukarabati?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba nimhakikishie Mbunge wa Jimbo la Namtumbo, Kaka yangu Mheshimiwa Vita Kawawa, kwamba ameshawasilisha yeye mwenyewe vituo hivi vitatu na ameshaeleza kwamba ni vituo vikongwe na sisi tumeshatuma timu zetu zimefanya tathmini ni kweli havina baadhi ya majengo

muhimu kama Majengo ya Upasuaji, Majengo ya Afya ya Mama, Baba na Mtoto na majengo mengine.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie ni miongoni mwa vituo ambavyo vimeingia kwenye orodha ya ukarabati na mara tukipata fedha tutahakikisha tunatoa vipaumbele kwa ajili ya ukarabati wa vituo hivyo, ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

MHE. GRACE V. TENDEGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona, Kituo cha Afya kilichopo Ikungwe, Jimbo la Kalenga kimekamilika lakini kuna changamoto ya waganga pamoja na vifaatiba. Ni lini Serikali itapeleka vitu hivyo? *(Makofi)*

SPIKA: Sijaelewa kama hili lilikuwa ni sehemu ya swali la msingi, maana swali la msingi linahusu ukarabati, sasa hapa naambiwa watumishi.

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Kituo cha Afya cha Ikungwe, ambacho Mheshimiwa Mbunge, amekisemea hapa ni kweli kimekamilika, lakini nimhakikishie tu na nina uhakika yeye ni shuhuda kwamba Serikali hii ya Awamu ya Sita, inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imefanya mapinduzi makubwa sana katika, kwanza kuajiri Watumishi wa Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka hii mitatu Serikali imeajiri Watumishi wa Afya 18,878 lakini imeshapeleka vifaatiba vyenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 300. Nikuhakikishie kwamba kituo hiki kipo kwenye orodha na tutapeleka watumishi lakini pia tutapeleka Vifaatiba, kwa ajili ya kuboresha Huduma za Afya, ahsante.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge nimewaona. Niwakumbushe, anaposimama mwenye swali la msingi ndipo na ninyi

mnasimamama, husimami baada ya maswali ya yule aliyeuliza halafu nikuone. Kwa hiyo natakiwa nikuone umesimama pamoja na yule mwenye swali lake, usisimame baadaye kwa sababu utaleta lawama.

Mheshimiwa Ighondo Ramadhani.

MHE. ABEID R. IGHONDO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Wananchi wa Kata ya Kinyagigi Jimbo la Singida Kaskazini wamejitolea nguvu zao na kuweza kujenga kituo cha afya, kwa maana ya jengo la *OPD* na baadhi ya majengo, lakini bado kunahitaji gharama za ukamilishaji ambazo ni shilingi milioni 100.

Je, Serikali sasa haioni haja ya kuwasaidia wananchi hawa ili kumaliza jengo hilo ili kituo hicho kianze kufanya kazi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza niwapongeze Wananchi wa Kata ya Kinyagigi ambao wamejitolea nguvu zao na kujenga majengo haya. Nikuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itatafuta fedha aidha kupitia mapato ya ndani ya halmashauri au Serikali kuu kwa ajili ya kupata hii milioni 100 kwa ajili ya kukamilisha majengo hayo.

SPIKA: Mheshimiwa Zuena Bushiri, swali la nyongeza.

MHE. ZUENA A. BUSHIRI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kituo cha Afya cha Umbwe hakina maabara, *OPD* na *mortuary*.

Je, ni lini Serikali itajenga vitu hivyo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, vituo vingi vya afya hapa nchini hasa vile vilivyojengwa miaka ya nyuma vina upungufu wa baadhi ya majengo. Ndiyo maana Ofisi ya Rais TAMISEMI imefanya *mapping* ya vituo vyote kote nchini na kuvitambua vituo ambavyo vina majengo pungufu ya yale ambayo yanahitajika kwa ajili ya vituo vya afya kikiwemo kituo hichi cha Umbwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba vituo hivi pamoja na hiki kituo kipo kwenye mpango na Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuongeza majengo hayo ili viwe na majengo ili viwe na majengo yale yanayohitajika kwa ngazi ya kituo cha afya.

SPIKA: Mheshimiwa Minza Simon Mjika, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 214

Hitaji la Vituo vya Afya Kata za pembezoni – Simiyu

MHE. MINZA S. MJIKA aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kujenga vituo vya afya kwenye kata za pembezoni mwa Mkoa wa Simiyu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Minza Simon Mjika, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha miaka mitatu ya fedha 2021/2022, 2022/2023 na 2023/2024 Serikali imejenga jumla ya

vituo vya afya 466 vilivyogharimu shilingi bilioni 718.1 katika maeneo ya kimkakati kote nchini. Katika Mkoa wa Simiyu jumla ya vituo vya afya nane vimejengwa katika kata za kimkakati kwa gharama ya shilingi bilioni nne.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa awamu kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya katika kata za kimkakati kote nchini zikiwemo kata katika Halmashauri za Mkoa wa Simiyu.

SPIKA: Mheshimiwa Minza Simon Mjika, swali la nyongeza.

MHE. MINZA S. MJIKA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kuishukuru sana Serikali kwa majibu mazuri, kwa majibu hayo kwa kweli nimeridhika. Ninaomba tu Serikali iendelee basi kujenga kwa kata ambazo hazijapata vituo hivyo, ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako, lakini ngoja, subiri kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, hapa wameuliza kuhusu vyoo na wewe kwenye majibu yako ukatoa majibu kuhusu vyoo. Nafikiri kwa nchi yetu tulipofikia ni mahali ambapo hatutakiwi kuwa tunazungumza vyoo kwenye zahanati, vyoo vituo vya afya, vyoo shule za msingi, vyoo shule za sekondari. Yaani utokee angalau mwaka mmoja limalizike hili jambo tuwe tunazungumza mambo mengine. Mambo makubwa sana Serikali inafanya sasa nafikiri kwenye mipango embu jipangeni kujenga hivyo vitu tuwe tumemaliza halafu tuanze kujadili mambo mengine. Haipendezi kuwa tunajadili mambo ya vyoo humu Bungeni, choo kimoja pale, vyoo viwili pale, aah, Serikali inafanya kazi sana na hakuna sababu ya kujadili vyoo humu ndani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Waziri ameshaulizwa maswali ya kumtosha. Ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 215

Ujenzi wa Barabara ya Same – Mkomazi

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA aliuliza: -

Je, nini kinakwamisha ujenzi wa barabara ya Same - Kisiwani - Ndungu hadi Mkomazi licha ya kutengewa fedha miaka minne mfululizo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Barabara ya Same – Kisiwani – Ndungu hadi Mkomazi yenye urefu wa kilometa 98 ulikamilika mwezi Novemba, 2020 na uthamini wa mali za wananchi watakaoathirika na mradi ulikamilika mwezi Septemba, 2022. Baada ya kukamilika kwa kazi ya usanifu, Serikali ilianza ujenzi kwa kiwango cha lami kwa kipande cha kilometa 5.2 kutoka Maore hadi Ndungu mwezi Septemba, 2021 ambapo kazi za ujenzi zinaendelea na zimefikia asilimia 55 na zinatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024.

Mheshimiwa Spika, Serikali ipo katika hatua za mwisho kukamilisha taratibu za kusaini mkataba na makandarasi wawili ili kuanza kujenga sehemu iliyobaki yenye urefu wa kilometa 92.8 kwa kiwango cha lami ambayo imegawanywa katika sehemu mbili ambazo ni Same - Maore yenye urefu wa kilometa 56.8 na Ndungu - Mkomazi yenye urefu wa kilometa 36, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka, swali la nyongeza.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Spika, ahsante na nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ujenzi wa kilometa 5.2 umechukua zaidi ya miaka miwili na nusu na kazi imefanyika kwa asilimia 55 tu, kwa maana kila kilometa moja imejengwa kwa mwaka mmoja.

Je, sababu gani imechelewesha ujenzi huu kwa kiasi hicho?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Mheshimiwa Waziri anaweza kutuambia kwamba kama imechukua mwaka moja kujenga kilometa moja katika barabara hiyo je, kujenga kilometa 92.8 itachukua miaka mingapi? Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza nataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hizi kilometa 5.2 ambazo tulianza kuzijenga wakati huo tuna mpango wa kujenga kwa awamu zitakamilishwa. Sababu kubwa iliyofanya eneo hili liweze kuchukua muda, kwanza tulikuwa tunajenga kwa awamu lakini sasa hivi tukaamua kujenga kwa kiwango kikubwa kwa maana sasa tunajenga barabara yote.

Mheshimiwa Spika, barabara hizi zina madaraja. Kwa kila daraja lina ukubwa wake na ubora wake wa kulijenga. Nimkumbushe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba pia eneo hili ambalo lilichaguliwa kujengwa ni eneo ambalo lina changamoto kubwa, ni udongo ambao wanasema tindiga. Kwa hiyo, lazima lijengwe kwa kiwango cha juu na bahati nzuri anayejenga ni mkandarasi. Kwa hiyo, tuko asilimia 55 na tuna uhakika mwaka huu tutakamilisha hicho kipande.

Mheshimiwa Spika, kwenye swali lake la pili, kuhusu hizo kilometa 92 kama nilivyosema sasa tumeamua kuijenga barabara hii yote kwa kiwango cha lami kwa kilometa ambazo zimebaki, kilometa 92. Kama nilivyosema tutakuwa na wakandarasi wawili ambao tumegawa kwenye *lot* mbili na tayari tunachosubiri sasa hivi tu ni kusaini mkataba ili barabara hiyo yote iweze kujengwa yote kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge tumejenga barabara nyingi sana ambazo tumezikamilisha kwa muda na nakuhakikishia kwamba hii pia tutaikamilisha kwa muda, ahsante

SPIKA: Mheshimiwa Jackson Kiswaga, swali la nyongeza.

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwanza tunaishukuru Serikali kwa kutangaza *tender* ya kujenga Barabara ya *Ruaha National Park*. Sasa Wananchi wa Iringa wanauliza lini tuta-*sign* mkataba? Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, barabara hii tukishatangaza tutaisaini, kwanza inafadhiliwa na wenzetu wa *World Bank* kwa hiyo taratibu zitafuatwa na muda ukifika barabara hii tutaisaini ili ianze kujengwa, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Justin Nyamoga, swali la nyongeza.

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru, licha ya kutengewa fedha za ukarabati hivi sasa tunavyozungumza kata sita za Wilaya ya Kilolo hazina mawasiliano kutokana na Daraja la Kidabaga kutopitika kabisa kwa ajili ya uharibifu wa mvua zinazoendelea.

Je, Serikali ipo tayari kuagiza hatua za dharura zichukuliwe ili magari yale yaweze kupita na shughuli ziendelee?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza nitoe pole kwa wananchi ambao sasa hivi wamekosa mawasiliano; lakini tu nimjibu Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge mvua zinazoendelea nchi nzima zimeleta athari kubwa sana kwenye miundombinu yetu ikiwa ni barabara pamoja na madaraja.

Mheshimiwa Spika, tayari tulishawaelekeza Mameneja, pale ambapo kumekatika mawasiliano tumeshatengeneza timu katika kila barabara. Mvua inapokuwa imekatika basi waweze kufanya jitihada za haraka ili kurejesha mawasiliano wakati tukisubiri kuja kuijenga hiyo barabara wakati mvua itakapokuwa imekatika; lakini kwa sasa tunarejesha mawasiliano kwa sababu hatuwezi kuzijenga kwa kiwango kizuri kwa sababu mvua zinaendelea. Baada ya mvua kukatika tutahakikisha kwamba tunarudisha mawasiliano ya kudumu.

SPIKA: Mheshimiwa Samweli Hhayuma, swali la nyongeza.

MHE. SAMWELI X. HHAYUMA: Mheshimiwa Spika, naomba kufahamu Daraja la Munguri ambalo linaunganisha Kata za Nangwa, Wareta, Dirma, Gisambalang, Simbay, Sirop na kuunganisha na Kondoa ujenzi wake utaanza lini na karibuni tu Mheshimiwa Waziri na timu yake nzima walilitembelea hilo daraja?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nimetembelea na Mheshimiwa Waziri pia ametembelea. Wakishakamilisha usanifu, ujenzi wa barabara hiyo utaanza kuunganisha hii mikoa miwili Mkoa wa Dodoma na Mkoa wa Manyara, ahsante.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge maswali mafupi, maswali mafupi. Mheshimiwa Twaha Mpembenwe, swali la nyongeza.

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Hatua za awali za maandalizi ya ujenzi wa Bungo – Nyamisate zimeanza na wataalamu wamekuwa wakienda *site* mara kwa mara lakini kuna taharuki kubwa sana kuhusiana na swala la fidia.

Je, Serikali ina kauli gani kuhusiana na kadhia hii?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nilichukue hilo ili niweze kujua hiyo taharuki imetokana na nini. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge baada ya hapa tuweze kukutana ili tujue changamoto hasa ni nini ya hiyo taharuki ambayo imejitokeza, ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Lucy Mayenga, swali la nyongeza.

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa spika, Barabara ya Kolandoto kwenda Muze ni barabara ambayo ni kilio kikubwa sana kwa Wanakishapu. Wananchi hawa wamekuwa wakiteseka kwa muda mrefu barabara hii haijawahi kuwekwa lami.

Je, Serikali inasema nini kuhusu barabara hii na ni kwanini Serikali isiamue kujenga barabara hii walau kidogo kidogo kuanzia Muze ili walau ndoto za wananchi hawa wa Kishapu ziwe kweli? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ni kweli hii ni moja ya barabara zetu kuu ambayo inaunganisha Mkoa wa Shinyanga

na Mkoa wa Simiyu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tuliupangia bajeti na tunaamini katika barabara ambazo pengine zitapata kibali cha kuanza kujengwa na hii itakuwa ni mojawapo.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge nimewaona wale waliokuwa wamesimama awali, kwa hiyo nyinyi mnaoibuka baadaye tusameheane kidogo.

Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Barabara ya Dareda kule Dongobesh mlitangaza na mlituambia mnakwenda kusaini mkataba. Je, kwanini mkataba ule hausainiwi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Ni kweli barabara hii ilitakiwa isainiwe lakini kulitokea changamoto ambazo Mheshimiwa Mbunge na Mheshimiwa Mbunge wa Babati wanajua. Mara baada ya Bunge hili barabara hii inakwenda kusainiwa kwa sababu kila kitu kipo tayari. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Flatei, Bunge linaisha kesho kwa hiyo umeambiwa mara baada ya Bunge hili.

Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, swali la nyongeza.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Wananchi wa Tarime na Serengeti wamekongwa mioyo na Mheshimiwa Rais Mama Samia kuwaunganisha kwa barabara ya lami. Kipande cha Tarime – Nyamwanga kimeanza. Mheshimiwa Naibu Waziri lini mkandarasi atakuwa *site* kujenga barabara kwa kiwango cha lami kutoka Kunyagu – Nyamongo kwenda Serengeti – Mugumu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwamba anatambua kwamba Mheshimiwa Rais ameamua kuiunganisha Tarime na Serengeti kwa kiwango cha lami. Taratibu zote zimeshakamilika za kuanza ujenzi kipande hicho. Kwa hiyo nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge mara baada ya Bunge hili na nina uhakika mvua itakapokuwa imekatika mkandarasi ataanza kukijenga hicho kipande ambacho kimebaki.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula.

MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa na mimi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya *Airport* – Nyanguge yenye urefu wa kilometa 46 imekuwa ikiingia katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa vipindi viwili mfululizo na mwaka huu Serikali ilitangaza kujenga kilometa 10.

Je. Ni lini ujenzi huo sasa utaana ili kurahisisha *by pass* ya kwenda Serengeti kutoka Mwanza? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, habari njema kwa Mheshimiwa Mbunge *tender* ilishatangazwa ya kilometa hizo 10 zilizokuwa zimehaidiwa. Nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge mara tutakapokuwa tumekamilisha kazi za *tender* ujenzi utaanza kwa sababu tunatambua pia ndiyo barabara ambayo itapunguza foleni. Ni kama *by pass* ya Mji wa Mwanza kuelekea Simiyu na Mara kupitia Barabara ya *Airport*.

SPIKA: Mheshimiwa Daniel Sillo Baran, swali la nyongeza.

MHE. DANIEL B. SILLO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Swali langu ambalo nilitaka kuliuliza limeulizwa na Mheshimiwa Flatei na

nashukuru sana majibu ya Serikali kwamba baada ya Bunge hili mkataba unaenda kusainiwa Barabara ya Dareda kwenda Dongobesh. *(Makofi)*

SPIKA: Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Anna Lupembe, swali la nyongeza.

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Spika, je, ni lini Barabara ya Kawejense – Ugalla mpaka Kaliuwa itajengwa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ahsante, barabara hii tayari tumeshaanza kuijenga na kwa kipande tumeshaanza kwanza kujenga madaraja kabla hatujalifikia Daraja la Mto Ugalla ambao tuna uhakika hatuwezi tukalifikia mpaka kwanza tujenge madaraja unganishi. Tukishakamilisha tutakamilisha usanifu pia upande wa Tabora ili kuijenga barabara yote.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara swali la nyongeza.

MHE. DKT. THEA M. NTARA: Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na kazi nzuri iliyoanza pale katika Mlima Nyang'oro niombe kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri;

Je, Serikali ina mpango wa kuweka miundombinu ya taa pamoja na mawasiliano kwenye eneo hilo? *(Makofi)*

SPIKA: Haya. Taa, mawasiliano nadhani ni Wizara nyingine. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwa upande wa taa kuna kitu tunakifanya katika Mlima wa Kitoga; na limekuwa ni ombi *actually* la Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sababu ya kona nyingi tuweze kuweka taa ili watu waweze kuonana na hasa kunapotokea changamoto upande wa usiku. Tumelipokea na tunalifanyia kazi, ahsante.

SPIKA: Wizara ya Mawasiliano, Waziri, Naibu Waziri. Waziri wa Nchi kuna swali hapa linalohusu Mawasiliano. *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, BUNGE NA URATIBU: Mheshimiwa Spika, sahamani maana Mawaziri wa Nchi tupo kadhaa lakini ngoja nilibebe tunalichukua na…

SPIKA: Ngoja, ngoja, ngoja kwa sababu swali linahusu mawasiliano na hapa ndani hakuna Waziri wala Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, sasa wewe ndiye Waziri wa Nchi unayeshughulika humu ndani. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni suala linalohusu sekta maalum kwa hiyo tunalichukua na tutalifikisha kwenye sekta ili sekta iweze kutayarisha majibu na kumjibu Mheshimiwa Bunge ipasavyo. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa kuwa barabara ya kutoka Mkuyuni - Kanyerere mpaka Nyangurungu – Mahina ilishafanyiwa upembuzi yakinifu na *TANROADS* na ulishakamilika takribani miaka miwili. Je, Serikali sasa haioni ni muhimu kuanza kuijenga barabara hii kwa kiwano cha lami yenye jumla ya kilometa 9.8?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba *TANROADS* ilifanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii kutokana na maelekezo ya viongozi wa kitaifa, lakini barabara hii kwa sasa bado inaendelea kusimamiwa na wenzetu wa TAMISEMI, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hili tutawasiliana na wenzetu wa TAMISEMI, kwamba baada ya kufanyia usanifu kinachofuata sasa ni kuijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Dennis Londo, swali la nyongeza.

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Spika, Barabara ya kutoka Kilosa kwenda Mikumi, pamoja na uwekezaji mkubwa wa kimkakati Kilosa - Mbuga ya Mikumi pamoja na Kiwanda cha Illovo, nini kinakwamisha Serikali kuweza kuona kwamba barabara hii ni muhimu sana kwa uhai wa nchi na uchumi wa Taifa letu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kimsingi barabara hii tumeshaanza kuijenga kuanzia Turiani hadi Kilosa na bado Wakandarasi wako *site*, kipande kilichobaki ni Kilosa kwenda Mikumi. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba hii ni barabara ya kimkakati na sisi katika bajeti zetu tumeendelea kuitengea bajeti na tunaamini kwamba katika kipindi tunachoendelea pia tutaendelea kuitengea bajeti ili tuweze kuijenga yote kwa kiwango cha lami kuunganisha Mji wa Mikumi na Mji wa Kilosa, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Vunjo, sasa aulize swali lake.

Na. 216

Kuboresha uwanja wa michezo eneo la Polisi Himo

MHE. DKT.CHARLES S. KIMEI aliuliza: -

Je, lini Serikali itaboresha uwanja wa michezo katika eneo la Polisi Himo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Hamis Mwinjuma, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inayo nia ya dhati kuhakikisha kwamba uboreshaji wa miundombinu ya michezo nchini unafanikiwa ili kukuza ushiriki wa michezo na kuibua vipaji. Katika kufanikisha suala hili, Serikali imekuwa ikiwahimiza wamiliki wa viwanja na wadau mbalimbali wa michezo kushiriki katika kujenga na kuboresha miundombinu ya michezo katika maeneo mbalimbali nchini kama Sera ya michezo inavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, Serikali inahimiza wamiliki wa uwanja wa michezo wa Polisi Himo kushirikiana na wadau mbalimbali wa sekta binafsi katika kuboresha uwanja huo. Aidha, Wizara ipo tayari kutoa ushauri wa kitaalam kwa wamiliki na wadau wanaokusudia kujenga ama kuboresha miundombinu ya michezo nchini.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, swali la nyongeza.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Spika, inaonekana kwamba Serikali haina mkakati madhubuti wa kujenga viwanja kwenye maeneo ya vijiji na maeneo mengine nchini. Naomba niulize maswali mawili mengine ya zaida.

Swali la kwanza, je, endapo tutaweza kuhamasisha wananchi wetu pale Himo ambapo kusema kweli kwenye Jimbo letu hatuna kiwanja chochote tukasawazisha, Serikali itakuwa tayari kutupa *support* ya nyasi bandia?

Swali la Pili, ni kwamba tunajua Serikali sasa inaingia kwenye mitaala mipya ya elimu ambapo tunahamasisha mkondo wa amali na michezo ni mmojawapo, hili halitafanikiwa kama kwenye maeneo tunayoishi hakuna sehemu za kufanyia michezo ya aina mbalimbali na kukuza stadi zetu.

Je, Serikali inaweza kutoa kauli gani kuhusiana na suala hili zima la kusaidia kukuza stadi za michezo mbalimbali kwenye maeneo yetu? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mbunge Dkt. Charles Kimei kwa swali ambalo halina maslahi na manufaa kwa vijana na wanamichezo kwa ujumla wa Jimbo la Vunjo na Mkoa wa Kilimanjaro pekee yake bali kwa nchi nzima. Namshukuru kwa moyo huo wa kiuanamichezo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inayo nia thabiti ya kujenga, kukarabati na kuboresha miundombinu mbalimbali ya michezo. Mheshimiwa Mbunge atakuwa anafahamu mipaka mizito ya kibajeti ambayo Wizara yetu inayo lakini tunaendelea kuwasiliana na wenzetu wa Wizara ya Fedha kuona namna ambavyo tunaweza kuongezewa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali ina mpango wa kukarabati viwanja saba vikubwa vya michezo nchini vikiwemo viwanja vya Jamhuri wa Morogoro, Jamhuri wa Dodoma, Sokoine wa Mbeya, Majimaji wa Songea, Mkwakwani Tanga na vinginevyo ili kuhakikisha tunakuwa na maeneo thabiti kabisa ya kufanya shughuli za michezo katika Mikoa husika.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika, kwa sasa Serikali imechagua shule 56, shule mbili katika kila Mkoa wa Tanzania Bara kwa ajili ya kuzitengeneza kuwa shule maalum za michezo na kwa kuanzia tunaanza na shule tisa kwa sasa. Hii itasaidia kuongeza miundombinu ya michezo mashuleni na tunashirikiana kwa ukaribu na Wizara ambayo ina dhamana ya Elimu na wenzetu wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI katika kuhakikisha hili linatendeka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili kwamba wakisawazisha uwanja kama tunaweza kuwapatia nyasi bandia. Kama nilivyojibu tatizo letu kubwa ni mipaka ya kibajeti ambayo

tunayo lakini nitahakikisha nashirikiana na Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Vunjo kupata wadau kwa ajili ya kuwatafutia nyasi bandia wananchi hao kama watasawazisha uwanja wao, ahsante. *Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Festo Sanga, swali kwa kifupi.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alielekeza Serikali na Chama cha Mapinduzi mkae kwa ajili ya kurekebisa viwanja saba vya michezo; je, mmefikia hatua gani?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimejibu kwenye swali la nyongeza la Dkt. Kimei, viwanja hivi viko katika mipango yetu na sasa hivi tuko katika hatua ya kutafuta wakandarasi kwa ajili ya kukarabati viwanja hivi saba.

SPIKA: Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, swali la nyongeza.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, ni kwa nini Wizara hii isishirikiane na TAMISEMI kuhakikisha inaboresha na kujenga miundombinu ya michezo kwenye shule zote za sekondari na msingi nchini kwa sababu kuna shule zingine hazina miundombinu hii?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimejibu pia, mpango wetu ni kutengeneza viwanja vya michezo yote ya kipaumbele kwenye shule 56, shule mbili kwenye kila Mkoa wa Tanzania Bara kwa Mikoa 28 kwa sasa, kwa hiyo tunaendelea kushirikiana na wenzetu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kufanya jambo ambalo Mheshimiwa Mbunge analisema.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, swali la nyongeza.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kuanza kufikiria kuuboresha Uwanja wa Jamhuri wa Morogoro kwa sababu ni uwanja wa Kimataifa na wanachezea michezo ya Kitaifa. Je, ni lini mtaanza kuuboresha uwanja huu? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba pindi rasilimali fedha itakapokuwa imekaa sawasawa kwenye Wizara yetu tutaanza kuukarabati Uwanja wa Jamhuri Morogoro.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaenda Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 217

Watumishi wanaokaimu kwa muda mrefu Vyuo vya *FETA*

MHE. AGNES E. HOKORORO aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani kwa watumishi wanaokaimu nafasi kwa muda mrefu katika Vyuo vya *FETA* ikiwemo Mtwara?

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto za kimuundo *(organization structure)* ya Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi

(Fisheries Education and Training Agency - FETA) watumishi wengi waliokuwa wanakaimu kwa muda mrefu walishindwa kuthibitishwa katika nafasi zao. Changamoto hiyo ya kimuundo imeisha baada ya Muundo mpya wa *FETA* kuidhinishwa mwezi Oktoba, 2022.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Serikali inaendelea na taratibu za kujaza nafasi za uongozi katika Muundo huo mpya ikiwemo kuwafanyia upekuzi wote wanaokaimu ili wakikidhi vigezo wathibitishwe katika nafasi hizo au kama hawakidhi vigezo wateuliwe watumishi wengine kujaza nafasi hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza.

MHE. AGNESS E. HOKORORO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninayo maswali mawili ya nyongeza.

(a) Je, kwa nini Serikali haiwalipi Mameneja wanao kaimu katika Vyuo vya Uvuvi pamoja na Wakurugenzi ambao wamekaimu kwa miaka zaidi ya 12?

(b) Wizara haioni imedumaza maendeleo ya Vyuo vya Uvuvi nchini ikiwemo Mikindani Mtwara kwa kuwakaimisha mameneja wake na kutokuwa na taratibu za uendelezaji? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, nianze na hili la kwanza kwamba haiwalipi makaimu; utaratibu wa Serikali uko wazi kwamba mtumishi yeyote anaweza akakaimishwa nafasi yoyote kama ana vigezo na upekuzi ukikamilika anataeuliwa kushika nafasi hiyo rasmi kulingana na maelekezo ya Serikali yalivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kesi hii ya Mikindani, tumekuwa tukifanya upekezi kwa muda mrefu wenye sifa wanakosekana lakini tumeendelea kutafuta watu wenye uwezo wa kushika nafasi hizo katika maeneo hayo na sasa Serikali inaelekea mwishoni kukamilisha taratibu za uteuzi ili apatikane Mkurugenzi atakayekuwa ameshika nafasi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na kwamba anafuatilia sana kwa karibu jambo hili kwa muda mrefu, nimhakikishie kwamba ndani ya muda mfupi tutakwenda kukamilisha jambo hili. Lengo la Serikali ni kuweka watu wenye weledi, wenye uwezo wa kushika nafasi hizo na si lengo kudumaza vituo hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba kuwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, nadhani kulikuwa na swali la pili linalohusu kudumaa kwa wale wanaokaimu, kwamba wanashindwa kuendelezwa.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi tumeendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa wataalam wetu, kwa hivyo wataalam wale wanapopata mafunzo wanaojiendeleza wanakuwa na sifa za kushika nafasi hizo, kwa hiyo tumekuwa tukiangalia katika hao tuliowapa mafunzo, Je, wapi wana uwezo wa kushika nafasi hizi za kukaimu nafasi za juu katika uongozi?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tumeendelea kutoa mafunzo, mafunzo hayo yamezidi kuwasaidia wataalam wetu kujipatia uwezo wa kushika nafasi hizi na lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba wale wote wenye uwezo wa kushika nafasi hizi wanapewa nafasi hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Zacharia Issaay, swali la nyongeza.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Spika, samahani niliomba swali namba 218.

SPIKA: Mheshimiwa Felix Kevejuru, swali la nyongeza.

MHE. KAVEJURU E. FELIX: Mheshimiwa Spika, swali nililotaka kuuliza tayari amelitolea ufafanuzi.

SPIKA: Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Venant Daud Protas, Mbunge wa Igalula, sasa aulize swali lake.

Na. 218

Kuendeleza Sekta ya Mifugo- Igalula

MHE. VENANT D. PROTAS aliuliza: -

Je, lini Serikali itaajiri Maafisa Mifugo katika kila Kata ili kuwasaidia wafugaji?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Venant Daud Protas, Mbunge wa Igalula, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mwongozo wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa utoaji huduma za ugani wa mwaka 2011 unaelekeza katika kila Kata na kila Kijiji kuwa na Afisa Ugani. Hata hivyo, idadi ya Maafisa Ugani wa Mifugo waliopo kwa sasa ni 4,406 ikilinganishwa na mahitaji ya Wagani 20,537 nchini, sawa na upungufu wa Maafisa Ugani 16,131.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na upungufu uliopo na kuongeza wigo wa utoaji huduma za ugani, Serikali imeendelea kuajiri Maafisa Ugani kila mwaka, ambapo kati ya mwaka 2021 hadi 2023 jumla ya Maafisa Ugani 1,205 waliajiriwa na kupangiwa

vituo katika Kata na Vijiji mbalimbali hapa nchini. Aidha, Wizara inaendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuomba vibali zaidi vya ajira za Maafisa Ugani na kuendelea kuajiri Maafisa Ugani kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa Venant Daud Protas, swali la nyongeza.

MHE. VENANT D. PROTAS: Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, amekiri kila kata, kila Kijiji ni lazima kuwepo na Maafisa Ugani, pamoja na kutoa ajira na kuajiri, kwa nini Maafisa Ugani wanakwenda kuwekwa sehemu ambayo hawana uhitaji? Kwa mfano, unampeleka Afisa Ugani Kata za Dar es Salaam, Kata za Arusha, kwa nini wale wa kule msifanye *reshuffle* mkawapeleka vijijini ili wakawasaidie wafugaji wetu ambao ng'ombe wao wanapata adha kubwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, kumekuwa na tozo nyingi kwa wafugaji wetu kwa sababu ya kukosa elimu na Maafisa Ugani. Je, kama Serikali hamuoni kwamba mtengeneze mkakati mziondoe zile tozo, msaidie wale wafugaji ili sasa wafurahie matunda ya Serikali yao?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, nianze na hili la kuwaweka Maafisa Ugani maeneo ya Mijini. Kwanza tukiri kwamba Maafisa Mifugo wetu walioko katika Taifa letu wanahitajika mahali pote kwa sababu hata huko Mjini ambapo Mheshimiwa Mbunge anapasema pia kuna wafugaji. Kama si wafugaji wa kufuga ng'ombe wa kuchunga kama vijijini wako wafugaji wanafuga ndani kwa ajili ya kuzalisha maziwa. Kwa hiyo Maafisa Ugani tukubali kwamba wanahitajika maeneo yote.

Mheshimiwa Spika, *issue* hapa ni upungufu wa Maafisa Ugani tulionao katika nchi yetu, hii inatokana na uwezo wa

kifedha wa kibajeti ambao kama tungepata fedha za kutosha maana yake tungekuwa tunaajiri Maafisa Ugani wa kutosha katika Taifa letu, mijini na vijijini kwa sababu kote panahitaji Maafisa Ugani.

Mheshimiwa Spika, hili la pili kuhusu tozo. Sisi Wizara ya Mifugo hatuna tozo nyingi kiasi hicho. Tozo nyingi ziko katika Halmashauri ambako Mheshimiwa Mbunge ni Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Mipango, nafikiri kule wakikaa kwenye vikao vyao sasa waende kupunguza tozo kwa wafugaji wetu ili wafugaji wetu waweze kufuga ufugaji watija.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 219

Kuongeza uzalishaji wa zao la pareto

MHE. ROSE C. TWEVE aliuliza: -

Je, nini mkakati wa Serikali kuongeza uzalishaji wa zao la pareto?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali ya kuongeza uzalishaji wa zao la pareto. Mikakati hiyo ni pamoja

na kuimarisha utafiti wa zao hilo ili kubadili kilimo kuwa cha kibiashara, chenye tija, himilivu na kushirikisha sekta binafsi ili kuwa na kilimo endelevu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia misingi hiyo ya kuleta mageuzi katika kilimo cha zao la pareto, katika mwaka 2021/2022 Serikali ilitoa fedha kiasi cha shilingi milioni 200 kwenda Taasisi ya Utafiti wa Kilimo *(TARI)* kwa ajili ya kuzalisha mbegu bora za pareto ambapo kiasi cha kilo 1,400 zimezalishwa na kusambazwa kwa wakulima katika msimu wa mwaka 2023/2024. Mbegu hizo zinatarajiwa kupandwa katika eneo la ekari 5,600 na kuzalisha wastani wa tani 2,240 za maua ya pareto.

SPIKA: Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve, swali la nyongeza.

MHE. ROSE C. TWEVE: Mheshimiwa Spika, zao la pareto ni zao ambalo tuna uhakika na soko duniani. Wilaya ya Mufindi tuna kiwanda kikubwa cha pareto ambacho kina uwezo wa kuchakata tani 10,000 kwa mwaka lakini mpaka sasa hivi wanachakata tani 2,400 tu.

Swali langu kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, ni nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha hizi *program* kama za *BBT* ziweze kufika Mufindi, kwa sababu kitu kinachotakiwa pale ni eneo na vijana wa kufanya kazi hizo tayari wapo ili kuhakikisha tuna-*feed* kile kiwanda ili kiweze kuzalisha kwa uwezo ambao kiliwekwa pale? *(Makofi)*

Swali la Pili; sasa hivi zao la pareto limewekwa kwenye Bodi ya Mazao Mchanganyiko, kwa unyeti wa zao hili, Je, huoni zao hili sasa liwekwe kwenye bodi pekee ambayo italimamia ili zao hili liwe na tija? Nakushukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge na sisi kama Wizara tunatambua kwamba tunazalisha pareto kwa kiwango

cha chini na tunahitaji mikakati ya ziada ikiwemo kutumia kwenye programu zetu za *BBT* kuongeza uzalishaji wa zao la pareto.

Mheshimiwa Spika, Wizara jambo hili tumelipokea na tutalifanyia kazi hususan katika Eneo la Mafinga ili tuweze kuongeza tija katika zao hili na ambalo litasaidia katika vile viwanda ambavyo vinachakata pareto. Kwa hiyo hilo tumelipokea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu zao la pareto kupelekwa kwenye Bodi ya Mazao Mchanganyiko, ni kwamba sasa hivi liko kwenye mamlaka ambayo inaitwa *COPRA* ndiko ambako inaelekezwa, sababu kubwa ni kwamba awali kulikuwa na Bodi inayojitegemea na ilionekana haifanyi vizuri ikiwemo masuala ya *resources* na mambo ya kiutawala, kwa hiyo imepelekwa kule kwa lengo la kuongeza tija ili tuweze kuisaidia. Pamoja na yote bado Serikali inaweza kupitia mchakato na kuangalia namna bora ya kutoka hapa ambapo tulipo, ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, swali la nyongeza.

MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Serikali ina mpango gani wa kuendeleza zao la miwa katika Wilaya ya Kalambo, Mkoa wa Rukwa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, swali hili linaweza kuja kama swali la Msingi.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Kweli.

SPIKA: Lije kama swali la msingi?

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, ndiyo, tunaweza kulijibu kama swali la msingi, lakini…

SPIKA: Haya. Mheshimiwa Bupe, swali lako litajibiwa kama swali la msingi.

Mheshimiwa David Cosato Chumi, swali la nyongeza.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kama ambavyo imeelezwa katika swali la msingi, zao hili ni muhimu sana. Sasa ili kiwanda kipate malighafi kwa maana ya maua, kiwanda kile kiko kwenye mazungumzo na Wizara ya Mambo ya Ndani kupitia Jeshi la Magereza ili kukodi eneo katika Gereza la Isupilo ili waweze kuzalisha maua kama sehemu ya malighafi.

Je, Wizara ya Kilimo iko tayari kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani kuhakikisha kwamba mpango huo unakuwa *fast trucked* ili eneo hilo lipatikane kwa wakati? *(Makofi)*

SPIKA: Hayo maneno umesema hapo Kiswahili chake ni nini?

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Spika, je, Wizara ya Kilimo iko tayari kushirikiana na Wizara ya Mambo Ndani ili kuharakisha mchakato huo na hilo eneo lipatikane kwa haraka?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Wizara ya Kilimo kwenye jambo lolote jema na lenye tija ya kuongeza uzalishaji kwenye zao la pareto, tuko tayari kushirikiana na Wizara yoyote ikiwemo Wizara ya Mambo ya Ndani kupitia Jeshi la Magereza ili kuhakikisha tunapata eneo na kuongeza uzalishaji katika zao la pareto, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Buyungu, sasa aulize swali lake.

Na. 220

Kukarabati Skimu za Umwagiliaji – Kakonko

MHE. ALOYCE J. KAMAMBA aliuliza:-

Je, lini Skimu za Umwagiliaji za Katengera, Muhwazi, Gwanumbu na Ruhwiti katika Wilaya ya Kakonko zitakarabatiwa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO K.n.y. WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Jimbo la Buyungu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea na kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika Bonde la Buyungu linalojumuisha Skimu za Katengera, Muhwazi, Ruhwiti, Ruhuru, Mgunzu, Kayonza, Lukoyoyo, Chulanzo, Asante Nyerere na Kilimo Kwanza. Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu zinatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2024. Kukamilika kwa kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika skimu hizi kutawezesha kupatikana kwa gharama halisi za ujenzi na ukarabati, hivyo kuwekwa kwenye mpango wa ujenzi na bajeti.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Umwagiliaji Gwanumbu umeendelezwa kwa kujengewa mfereji mkuu. Mradi huu unahitaji kufanyiwa usanifu wa miundombinu ambayo haijakamilika. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 mradi wa umwagiliaji Gwanumbu utaingizwa kwenye mpango wa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili kujua gharama halisi za ukarabati kabla ya kuingizwa kwenye mpango wa ujenzi na bajeti.

SPIKA: Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, swali la nyongeza.

MHE. ALOYCE J. KAMAMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, moja, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Katika majibu ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ametoa, ameunganisha skimu mpya zinazotarajiwa kuanzishwa na skimu ambazo zipo sasa.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu kubwa ni kwamba, Skimu ya Murwazi, Ruhwiti na Katengera zipo. Tatizo ni miundombinu yake imeharibika na hivyo hazifanyi kazi inavyostahili. Swali langu, ni lini Serikali itapeleka fedha hizo kwa haraka ili kuhakikisha skimu hizo zinakarabatiwa na ujenzi unafanyika ili wananchi waweze kufaidi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari sasa baada kikao hiki twende pamoja ili kuhakikisha kwamba anaiona skimu hizi ili kutoa suluhisho haraka sana? Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza nimthibitishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, moja ya maelekezo ambayo tumeyapata kutoka kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni kuhakikisha kwanza tunakarabati skimu zote ambazo zilikuwepo na zimeharibika. Pili, tujenge maeneo mapya na kutambua maeneo yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Hayo ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, sasa katika maelekezo yake, sasa hivi tunapotaka kufanya maboresho ya hizi skimu zilizoharibika, ni lazima tufanye upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili tupate gharama halisi, tofauti na ule utaratibu uliokuwa unatumika zamani, mtu akiona tu dharura anapeleka shilingi milioni 500, lakini hajui kuna gharama kiasi gani zinahitajika. Ndiyo maana kulikuwa na mwendelezo wa matatizo mengi katika skimu zetu nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo kwa sasa hivi lipo katika utekelezaji na tukimaliza tu tutatenga fedha kwa ajili ya kuzikarabati na kuzijenga. Kuhusu kwenda, niko tayari mara tu baada ya Bunge lako Tukufu kumalizika.

SPIKA: Mheshimiwa Aysharose Mattembe, swali la nyongeza.

MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi; je, ni lini Serikali itampata mkandarasi katika Jimbo la Singida Kaskazini kwenye Skimu ya Umwagiliaji Msange.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, Mradi wa Isange, nafikiri Tume ya Umwagiliaji ipo katika mchakato. Pia, mnafahamu kwamba mchakato ni hatua, ukishakamilika tu maana yake tutatangaza mkandarasi ambaye anahusika katika ujenzi wa Skimu ya Msange, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 221

Ujenzi wa miundombinu Skimu ya Dongobeshi - Mbulu

MHE. YUSTINA A. RAHHI aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa miundombinu ya Umwagiliaji katika Skimu ya Dongobeshi kufuatia kukamilika ujenzi wa Bwawa la Dongobeshi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na kwa niaba ya Waziri wa kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika Skimu ya Dongobeshi kupitia mshauri elekezi ambaye anatarajiwa kukamilisha kazi hiyo mwezi Mei, 2024.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa kazi za upembuzi yakinifu na usanifu inayotekelezwa na mshauri elekezi, itawezesha kupatikana kwa gharama halisi zinazohitajika kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji. Kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu hiyo kutanufaisha zaidi ya wakulima 1,300 katika Kata ya Dongobeshi.

SPIKA: Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, swali la nyongeza.

MHE. YUSTINA A. RAHHI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Nami nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa Serikali imeshawekeza gharama kubwa kwenye Skimu ya Dongobeshi shilingi bilioni 2.5 kwa maana ya kukalimisha tuta na torosho la maji. Je, Serikali haioni sasa ni wakati wa kuweka kipaumble kukamilisha miundombinu iliyobaki kwa maana ya banio, vitorosha maji pamoja na kusakafia mifereji mikubwa?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; Serikali inawekeza gharama kubwa sana kujenga miundombinu ya umwagiliaji, lakini haitoi mafunzo kwa wakulima pamoja na viongozi wa Tume ya Maji. Je, kwa ajili ya kudumisha uendelevu wa miradi ya umwagiliaji, Serikali sasa haioni umuhimu wa kuwapa mafunzo viongozi wa Tume ya Maji kabla na baada tu ya kuimarisha miradi ya umwagiliaji? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, jambo moja ni kwamba, ndiyo maana atakapomaliza kazi Mshauri Mwelekezi Mwezi Mei ni kwamba kitakachofuata baada ya hapo ni kuweka huu mradi kwa ajili ya mwaka wa fedha unaokuja ili uanze kujengwa. Kwa hiyo, ni sehemu ya vipaumbele vyetu sisi kama Wizara kuhakikisha Mradi wa Dongobeshi katika mwaka wa fedha ujao unaanza kutekelezwa. Kwa hiyo, lipo katika kipaumbele chetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafunzo, tunafanya hivyo kwa sababu katika kila mradi tunaweka bajeti kwamba, baada ya mradi kukamilika, wale watumiaji wa maji kwa maana mradi mzima lazima wapatiwe mafunzo ya namna bora ya kutumia, na vilevile, kuutunza ule mradi husika. Kwa hiyo, jambo hilo lipo na kikubwa tu tutaongeza kasi ili tuweze kuwafikia watu wengi, ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi, swali la nyongeza.

MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itakarabati Skimu za Umwagiliaji za Nyendara, Muhambwe, Kumbanga na Kugorogondo katika Jimbo la Muhambwe?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nimthibitishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba moja ya wajibu mkubwa wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ambayo inafanya kazi sasa hivi, ni kufanya upembuzi yakinifu na ufafanuzi wa kina kwa miradi yote ya umwagiliaji, maana yake, malengo tuliyonayo sasa hivi ni kujenga mabwawa pamoja na *schemes* zikiwemo hizi ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja za Garara, Muhambwe na miradi mingine ambayo ameitaja hapa. Kwa hiyo, tuko katika kazi na tukishamaliza hapo, maana yake tutatenga fedha katika bajeti yetu ili tuanze kuzijenga na nyingine kuzikarabati, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Shabani Shekilindi, swali la nyongeza.

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Spika, kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha na kupelekea udongo wenye rutuba kwenda mabondeni, je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kujenga mabwawa katika Kata ya Makanya, Gare, Kwayi pamoja na maeneo mengine katika Jimbo la Lushoto?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mpango wa Serikali ni kujenga Mabwawa katika maeneo yote ambayo tunaweza tukakusanya maji yakatumika katika kipindi chote cha mwaka ili Watanzania waweze kuingia katika kilimo kinachotumia maji badala ya kutegemea msimu mmoja wa mvua.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mpango wetu ni pamoja na kutumia ikiwemo Bonde la Makanya, lipo katika mpango. Ndiyo maana mwaka huu wa 2022/2023 tuliomba Serikali itupitishie bajeti kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa 100. Kwa hiyo, hilo ndilo lengo la Serikali na tutafanya hivyo. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Uchukuzi Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, sasa aulize swali lake.

Na. 222

Ujenzi wa kipande cha Reli ya *TAZARA* - Tunduma hadi Bandari ya Kasanga

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE aliuliza:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuanza ujenzi wa kipande cha Reli ya *TAZARA* kutoka Tunduma hadi Bandari ya Kasanga?

SPIKA: Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa David Kihenzile, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuunganisha reli ya *TAZARA* na Bandari ya Kasanga ili kurahisisha usafirishaji wa mizigo katika ukanda huo hususani Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo *(DRC)*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *TAZARA* inamilikiwa na Serikali mbili; Tanzania na Zambia, tumeanza mazungumzo na wenzetu Zambia ili kutenga fedha katika bajeti ya *TAZARA* kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa reli hiyo kwa lengo la kubaini gharama za ujenzi wake na manufaa yake kiuchumi.

SPIKA: Mheshimiwa Josephat Kandege, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPHAT. S. KANDEGE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya kutia matumaini kutoka Serikalini, naomba niulize maswali mawili kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, juu ya *efficiency* ya *TAZARA* ni suala ambalo hatuna ubishani kama Taifa na hasa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, juu ya ufanyaji kazi bora wa *TAZARA*. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba ukarabati unafanyika na mtaji unawekwa ili *TAZARA* iweze kufanya kazi kwa jinsi ambavyo tunatarajia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa Serikali imefanya uwekezaji mkubwa na hivi tunavyoongea tayari imeshafanya upanuzi katika Bandari ya Kasanga, na lami imeshajengwa mpaka kufika Kasanga, je, Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka wa kuishirikisha sekta binafsi ili kuhakikisha kwamba kutoka Kasanga kwenda *DRC* na kui- *decongest* Bandari ya Dar es Salaam; na bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri anajua tuna makubaliano mazuri na *DRC,* ni wakati muafaka wa kufanya *extension* ili tuweze ku-*decongest* bandari yetu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, *TAZARA* ni reli muhimu kwa uchumi wa Taifa letu. Sisi sote tunafahamu tangu

ilipoanza kujengwa na kuanza kutumika mwaka 1976 kwa Sheria ya Bunge Na. 23 ya mwaka 1975 yenye urefu wa kilometa 1,860. Pia, sisi Watanzania tuna faida kubwa zaidi kwa sababu asilimia 52 ya reli hiyo ambayo ni 975 iko Tanzania na wenzetu ni 885.

Mheshimiwa Spika, ilipokuwa inatengenezwa wakati huo, ilikuwa imelenga kubeba mzigo wa tani milioni tano, lakini karibu miaka yote hiyo, hatukuwahi kufikia ufanisi huu, ni miaka michache tulifikia asilimia 24. Mamlaka za nchi kwa maana ya Tanzania, Zambia pamoja na wenzetu Wachina, baada ya kuitazama reli hii ndefu kabisa barani Afrika ambayo ina madaraja karibu 318, ina mahandaki karibia 22 na makaravati karibu 2,229, wakasema ipo haja ya kuanza kuitafakari upya.

Mheshimiwa Spika, hii inakwenda sambamba na uboreshaji mkubwa tunaoufanya pale bandarini. Tayari Rais wetu na Marais hawa wawili wako kwenye mazungumzo. Tunategemea ukarabati mkubwa sana kwenye miundombinu pamoja na vitendea kazi unaweza ukaanza kufanywa mwaka huu 2024 ili kuiboresha bandari hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwenye hoja ya pili aliyoisema ya *PPP*, tunatambua ni hoja yake ya muda mrefu Mheshimiwa Mbunge, anajenga hoja kwamba kutoka Kaprimposhi mpaka kule Lubumbashi ni Kilometa 1,000 wakati kutoka kutoka pale Kasanga - Mlilo ukivuka ng'ambo ni kilometa 400.

Mheshimiwa Spika, tumepokea ushauri wake, tutaufikisha Serikalini ili tuuchakate kama tunavyochakata mambo mengine ili tuone namna gani tunakwenda kuutekeleza, ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, maswali mafupi, narejea tena, maswali mafupi. Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, swali la nyongeza.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Ni lini Serikali itajenga reli kutoka Bandari ya Mtwara kuja Tunduru – Namtumbo - Songea, pale Matomondo - Mbinga mpaka *Mbamba Bay*? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, tayari tuko kwenye hatua ya kuhuisha *design* hiyo ya *southern corridor* kwa maana ya kutoka Mtwara kwenda *Mbamba Bay* mpaka Liganga na Mchuchuma. Itakapokuwa tayari, nafikiri Serikali itaanza kutekeleza mara moja.

SPIKA: Mheshimiwa Oran Manase Njeza, swali la nyongeza.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupewa nafasi. Kwa kuwa kuna ushindani mkubwa wa *Lobito Corridor,* je, Serikali ina mkakati gani wa haraka kuhakikisha miundombinu ya *TAZARA* inakuwa katika kiwango cha *SGR*?

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, katika majibu ya nyongeza nimezungumza mpango wa Serikali wa kuiboresha vizuri sana *TAZARA,* ambapo tayari viongozi wetu wameshaanza mazungumzo na yatakapokuwa tayari tutaanza kuyatekeleza mwaka huu wa 2024.

SPIKA: Mheshimiwa Maimuna Mtanda, swali la nyongeza.

MHE. MAIMUNA S. MTANDA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, lakini swali ambalo nilitaka kuuliza, ameshauliza Mheshimiwa Msongozi. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

MHE. DOROTHY G. KILAVE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nami swali langu limeshajibiwa, lakini naomba hizi kingo za *TAZARA* zinazopita Kilakala ziweze kutengenezwa mapema kwa ajili ya mvua zinazonyesha. *(Kicheko)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, swali la nyongeza.

MHE. VEDASTUS M. MATHAYO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Ni kwa muda mrefu sasa Serikali imekuwa ikiahidi ujenzi wa Reli kutoka Tanga – Arusha – Loliondo – Mugumu hadi Musoma, lakini ni miaka sasa imepita. Napenda kujua nini kauli ya Serikali kuhusiana na ujenzi wa hiyo reli?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge hoja hii aliyoizungumza ya Tanga – Arusha na Musoma baada ya hapa tupate muda wa kuijadili halafu tuweze kupata majibu kamili.

SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge mliopo sehemu ya Mawaziri, nilishasema hapa ndani, kwa sababu maswali yanapoulizwa Mawaziri wanakuwa hawajasikia halafu mimi nawaita ili wajibu. Wabunge mliokaa na Mawaziri mrejee kwenye viti vyenu, mtarejea kwa Mawaziri baada ya kipindi cha Maswali na Majibu ili kuwapa nafasi kusikiliza ili atakapoulizwa swali awe amesikia Mbunge ameuliza nini?

Mheshimiwa Halima James Mdee, swali la nyongeza.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, inasemekana kwamba Kampuni inayomilikiwa na Serikali ya Uchina imeshatoa pendekezo la ukarabati wa reli husika kwa thamani ya shilingi trilioni 2.5 na majadiliano yalianza na Serikali ya Zambia kupitia Waziri mwenye dhamana kama wewe. Hiyo imekuwa *reported* na gazeti la *Citizen* la tarehe 10 Februari, 2024. Serikali mnatuambiaje kuhusiana na hili? Hayo unayoyasema ndiyo kampuni inayomilikiwa na Serikali ya China?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, mazungumzo yanaendelea na kwa kuwa hatujafika hatua ya mwisho, itakuwa ni mapema sana kuanza kuzungumzia gharama na hatua tuliyofikia. Namuomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira, yakishakamilika taarifa hizi ni za wazi, basi ataweza kufahamu pengine ni mkandarasi gani anayefanya kazi hiyo.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu swali hili limekuwa likijirejea mara kwa mara na hili swali alilouliza Mheshimiwa Msongozi na umejibu hapa kwamba 2024 nafikiri ulikusudia kusema 2024/2025. Sasa ni muhimu ili 2024/2025 linahusu hii ya *TAZARA* au inahusu ile ya Mheshimiwa Jacqueline aliyouliza ile ya kuanzia Mtwara mpaka *Mbamba Bay*. Hii 2024/2025 inahusu ipi kati ya hizi mbili?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, mwaka huu 2024 nilichokizungumzia ni uboreshaji wa Bandari ya *TAZARA* kutoka Dar es salaam mpaka Kapirimposhi kilomita 1860 hii Reli ya *TAZARA* kutoka Dar es salaam mpaka Kapirimposhi huu ndio uboreshaji tunaozungumza kwamba mazungumzo yanaendelea kati ya nchi hizi tatu na tunategemea mwaka huu pengine tuanze utekelezaji wake.

SPIKA: Sawa umerejea tena 2024, ukisema 2024 maana yake ni mwaka huu wa fedha ule unaokuja unaitwa 2024/2025 wewe unakusudia kusema upi 2023/2024 au 2024/2025?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, nilikusudia kusema kwa maana kuanzia Januari hii mpaka Desemba hapa katikati tutakuwa tumefikia hatua nzuri ya utekelezaji.

SPIKA: Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Fedha Mheshimiwa Ameir Abdallah Ameir, Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi, sasa aulize swali lake.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya.

SPIKA: Wizara ya Afya, Mheshimiwa Ameir Abdallah Ameir Mbunge kutoka BaRaza la Wawakilishi, sasa aulize swali lake.

Na. 223

Mchango wa tafiti za tiba asili kwenye matibabu

MHE. AMEIR ABDALLAH AMEIR aliuliza:-

Je, tafiti zipi ambazo Taasisi za Tiba Asili zimekamilisha na kuweza kuwa suluhisho la maradhi mbalimbali kama Tiba Mbadala?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya Mheshimiwa Godwin Mollel, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ameir Abdallah Ameir, Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2021 – 2024 zaidi ya tafiti 50 zimefanyika ndani ya nchi juu ya ubora na usalama wa dawa zinazotumika kwa tiba asilia kwa kupitia Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu *(NIMR)*.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya tafiti hizo ni pamoja na utafiti wa dawa ya Saratani ya *NIMREGENIN,* Dawa ya *TANGHESHA* inayotibu Selimundu, Dawa ya *PERVIVIN* inayotibu tezi dume, Dawa ya *WARBUGISTAT* inayotibu magonjwa nyemelezi na Dawa ya *NIMRICAF* inayosaidia mfumo wa upumuaji.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa Ameir Abdallah Ameir, swali la nyongeza

MHE. AMEIR ABDALLAH AMEIR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa kuwa asilimia 60 ya Watanzania wanatumia matumizi

ya tiba asili lakini kuna miti dawa isiyopungua 12,000. Swali langu liko hapa, je, ni miti gani maarufu ambayo inatumika ambayo tunayo hapa nchini katika kutengeneza tiba asili au kutengeneza dawa za kisasa katika hizo tafiti 50 ambazo Mheshimiwa Waziri umezieleza?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kwa kuwa mitidawa mingi ya asili inatoweka, ikiwemo miti dawa maarufu ikiwemo ule mti unaitwa *BLUNAS AFRICANA* ambao unatumika kutibia tezi dume, je, Mheshimiwa Waziri Serikali ina mkakati gani sasa wa kuinusuru hii miti ya asili inayopotea na iliyopotea na hii mingine ambayo iko hatarini kupotea? Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia eneo hili nyeti na nimwambie tu kuna dawa, kuna miti ambayo iko Tanzania na inaoteshwa Tanzania na inatumika kutengeneza dawa ya Malaria kama hii yaluu ambayo tunayo tunaitumia kawaida hapa lakini kuna *Mkunyinyi* ambao uko kule kwa Mheshimiwa Shangazi ambayo nayo inatumika kutengeneza hii *drip* ya *quinine,* ipo mingi kwa sababu umesema 1000 na zaidi kwa hiyo ni shida kutaja yote hapa na kuna namna mbalimbali za kutengeneza dawa za binadamu.

Mheshimiwa Spika, suala lake la pili ni kuhusu kutunza hii miti maana yake mingi ipo Tabora, iko maeneo mbalimbali kwa kweli ni suala nyeti tunalichukua na tunashirikiana mpaka sasa na Wizara ya Maliasili kuhakikisha haya mambo muhimu kwenye nchi yetu yanatunzwa, na nikuombe na wewe na niombe Wabunge na Watanzania tutunze hii miti na tutunze mazingira kwa sababu tutafanya *reservation* ya hivi vitu muhimu kwenye nchi yetu na kwenye Wizara ya Elimu tutashirikiana nao ili kuweza kutengeneza watu wengi zaidi wenye akili vumbuzi kwa sababu sasa hivi tunatengeneza watu wengi wenye akili za kufanya kazi badala ya kutafakari. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 224

Madai ya wazee walioshiriki Vita vya Pili vya Dunia

MHE. CECIL D. MWAMBE aliuliza:-

Je, kweli kuna wazee wanaodai haki zao kutokana na ushiriki wao kwenye Vita vya Dunia au Jeshi la *KAR?*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge Ndanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wapo wazee waliopigana Vita ya Pili ya Dunia (1939 - 1945) wakiwa askari wa Jeshi la *KING'S AFRICAN RIFLES (KAR)* lililokuwa chini ya Serikali ya Kikoloni ya Uingereza. Haki wanazodai zinahusiana na mali walizoachiwa na Serikali ya Uingereza mara baada ya utawala wao Tanganyika kukoma.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Cecil David Mwambe, swali la nyongeza.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Spika, Vita ya Pili ya Dunia ilikwisha mwaka 1945 na wapiganaji Tanzania walikuwa 680 na sasa wamebakia 58 maana yake wanazidi kuisha na Serikali haijafanya uhakiki ili waweze kulipwa fidia ama kurejeshewa mali zao nataka nifahamu ni lini Serikali itamaliza zoezi la uhakiki ili hawa watu waweze kupata stahiki zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kulikuwa na Vita ya Kagera pia hapa Tanzania waathirika wa Vita ya Kagera pamoja na Wanajeshi Wastaafu wako mtaani, kila mara wamekuwa wanakwenda kwenye Ofisi za Wilaya kujiandikisha wakiamini kwamba wanastahili kupata stahiki zao lakini pia pamoja na pensheni na matibabu. Ni lini Serikali itakamilisha taratibu hizi ili hawa watu wetu ambao ni wazalendo waweze kupata haki zao za msingi? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, kuhusu lini tutamaliza zoezi hili naamini muda si mrefu kwa sababu awali tulikuwa tunawasiliana na Serikali ya Uingereza, baadaye tukabaini kwamba *KAR* hawa taarifa zao zilikuwa makao makuu ya wakati huo Nairobi, sasa hivi Wizara yetu ya Mambo ya Nje inawasiliana na wenzetu wa Kenya ili kupata taarifa hizo na kwa sababu kwa sasa waliopo ni wachache tunaamini baada ya miezi miwili tutakuwa tumepata taarifa hizi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hawa wa Vita ya Kagera tumeshajibu swali kama hili huko nyuma ni kwamba baada ya Vita ya Kagera askari waliokuwa na sifa ya kuendelea kubaki jeshini waliajiriwa na wale ambao walikosa sifa walilipwa malipo yao ya mkupuo na kutakiwa kurudi nyumbanI, lakini tumebaini kwamba majemedari wetu hawa baadhi yao wameendelea kuwa na changamoto za kiafya na hivyo Serikali ikakubali kuanza kuwahudumia kwenye Hospitali za Jeshi zilizo karibu na wao.

Mheshimiwa Spika, suala la pensheni lilishindikana kwa sababu kwa vigezo vya ajira hawakukidhi na hivyo ilikuwa ni

vigumu kuwaingiza kwenye utaratibu wa pensheni, nashukuru *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Deo Mwanyika, swali la nyongeza.

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na tunashukuru sana swali hili lilivyoulizwa mara ya mwisho ulitoa maelekezo kwamba wazee hawa washughulikiwe kwa haraka sana. Sasa Njombe wazee hawa wamefuata utaratibu wamekwenda kuripoti lakini bado wanasumbuliwa sana, tunaomba tuelewe hasa ni lini jambo hili litakamilika?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, kama anakusudia wazee wa *KAR* hawa 58 taarifa zao tunazo, uhakiki uliokuwa unafanyika ni kuthibitisha pasipo na shaka mali zao wanazostahiki ni zipi. Hadi sasa taarifa zinaonyesha karibu mali zilizopatikana zilizokuwa na utata ni za shilingi bilioni 15, kwa hivyo mara utakapo kamilisha kama nilivyosema wazee hawa watalipwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kama nawalenga wazee wa Kagera nimeshaeleza utaratibu uliopo kama kuna watu ambao kwa bahati mbaya wanaona hawakufikiwa wawasiliane na Kambi za Jeshi zilizo karibu na maeneo yao au Ofisi za Wakuu wa Wilaya ili taarifa zao ziweze kuchukuliwa na huduma stahiki ziweze kutolewa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge mliosimama nimewaona lakini sasa Naibu Waziri anajibu kwa niaba kwa hiyo kidogo maswali inabidi yawe machache.

Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, jambo la dharura.

SPIKA: Leo inaonekana ziko dharura nyingi humu ndani, sawa Waheshimiwa Wabunge nimewasikia, Waheshimiwa Wabunge mtaleta matangazo tuliyo nayo hapa mbele kisha tutaendelea.

Tangazo la kwanza linahusu wageni waliopo hapa Bungeni tutaanza na wageni ambao hapa tunaambiwa wamekaa Jukwaa la Spika lakini sioni wageni Jukwaa la Spika lakini inaonekana wapo humu ndani.

Tunao Wageni 80 ambao ni wageni wangu ambao wanatoka Chuo Kikuu cha Dodoma na huu ni Umoja wa Wanafunzi wa Mbeya na Songwe, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni mbalimbali ambao ni wageni wetu, kwanza ni mgeni wa Mheshimiwa Benaya Kapinga ambaye ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Yupo pia mgeni wa Mheshimiwa Jesca Kishoa, rafiki yake kutoka Jijini Mbeya. *(Makofi)*

Wapo pia wageni wawili wa Mheshimiwa Joseph Mkundi, wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Abeid Ighondo ambaye ni Mwenyekiti wa Kijiji cha Mangida. *(Makofi)*

Wapo wageni sita wa Mheshimiwa Shabani Shekilindi ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Wapo wageni 27 wa Mheshimiwa Kavejuru Felix ambao ni Wafawidhi wa Vituo vya Afya na Hospitali za Halmashauri kutoka Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Tunao wageni 17 wa Mheshimiwa Zaytun Swai ambao ni Viongozi wa Taasisi ya Mtetezi wa Mama kutoka Mkoa wa Arusha wakiongozwa na Mwenyekiti wa Taasisi hiyo. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunao wanafunzi 50 wa Ndaki ya Insia na Sayansi ya Jamii kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Pasikal Kayanda kutoka Wilaya ya Kigamboni Jijini Dar es Salaam. Tunao wageni wanne wa Kikundi cha *Girl's Performance Excellency* kutoka Jijini Dodoma; hiki Kikundi hicho kinajihusisha na Ufugaji wa Kuku na kuwasaidia wadada wanaoishi kwenye mazingira magumu, karibuni sana Bungeni wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo linalotoka kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake; Mheshimiwa Shally Raymond anawatangazia Wabunge wote kwamba leo kutakuwa na kikao changu Msekwa, kwa hiyo Wabunge wanawake wote mnaombwa kuhudhuria kwenye kikao hicho. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia kuna tangazo la uteuzi wa kuzawadiwa *ticket* ya ndege ya *Qatar Airways,* Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kuwa Ofisi ya Bunge iliandaa tamasha la michezo na burudani lililofanyika siku ya jumamosi tarehe 27 Januari 2024 katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma kwa ufadhiri wa Benki ya Azania.

Aidha mdau wetu mwingie ambaye alikuwa ni Shirika la Ndege la *Qatar* alitoa zawadi ya *ticket* ya Ndege Daraja la biashara yaani *business class* kwa safari ya mshindi kwenda nchi yoyote duniani atakayoichagua na kurejea nchini. Hivyo Kamati ya Bunge Bonanza kwa kuzingatia vigezo walivyojipangia kupima ushiriki wa Wabunge na watumishi katika mabonanza yote manne yaliyofanyika kwa kushirikiana nami wanapenda kumtangaza Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko kuwa mshindi wa *ticket* hiyo, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumtakie kila la kheri katika safari yake Mheshimiwa kwenye safari atakayoenda na atataja yeye tarehe za kwenda na tarehe za kurejea, kwa hiyo, tunamtakia kila la kheri katika safari yake. *(Makofi)*

Hii tumeona tuitangaze hapa kwanza kwa ajili ya kuweka uwazi lakini pia kuwatia hamasa wengine kushiriki kwa sababu huko baadaye *ticket* zitakuwa nyingi, kwa hivyo wale ambao wangependa kujikuta mazingira aliyojikuta Mbunge mwenzetu basi washiriki vizuri kwenye michezo halafu mambo mazuri yanakuja. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge baada ya tangazo hilo sasa tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

MHE. EDWIN E. SWALLE: Mheshimiwa Spika, Hoja ya Dharura.

MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE: Mheshimiwa Spika, Hoja ya Dharura.

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Spika, Hoja ya Dharura.

SPIKA: Mbona inaonekana hoja zipo nyingi Wabunge watatu mmesimama, Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle.

HOJA YA DHARURA

MHE. EDWIN E. SWALLE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi, nimesimama hapa chini ya Kanuni ya 54, ya Kanuni za Kudumu za Bunge za mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, nasimama kuwasilisha kilio cha wananchi wa Jimbo langu la Lupembe mathalani Tarafa ya Lupembe ambayo ina kata saba, wananchi wangu wana hali mbaya sana. Hoja ni kwamba tangu mwaka jana mwezi Aprili wananchi wa Tarafa ya Lupembe ambao ni wakulima wa chai wanaidai kampuni ya *DL* ya nchi jirani zaidi ya milioni 600 na hawajalipwa mpaka leo zaidi ya miezi tisa sasa, madhara yake ni nini? Mwezi

wa kumi na mbili, Januari wananchi wengi wameshindwa kupeleka watoto shuleni kwa ajili ya masomo yao.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, huyu mwekezaji amewakopa wakulima wale wajasiliamali wenye Sheli za Mafuta na kuni fedha zaidi ya milioni 400 lakini juzi kuamkia jana mwekezaji huyu amefunga kiwanda wakulima wa chai hajawalipa na wajasiliamali aliowakopa fedha hajawalipa fedha yao, nimejaribu kufanya mawasiliano na watu wa Wizara ya Kilimo na Bodi ya Chai majibu ya kueleweka hayapo.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana Mheshimiwa Waziri wa kilimo alikuja Mkoani Njombe akaita wakulima na viongozi wao wa *AMCOS* mwekezaji huyu aliahidi kulipa ndani ya mwezi mmoja lakini mpaka leo hajalipa fedha, mwezi wa kwanza Bodi ya Chai imetuma watu lupembe akaahidi kulipa ndani ya wiki mbili mpaka leo hajalipa.

Mheshimiwa Spika, hali ni mbaya sana Lupembe wananchi hawa hawana sehemu ya kupeleka chai, kiwanda kimefungwa fedha wanadai na mwekezaji anasema anaondoka, sasa nilitaka nipate kauli ya Serikali hatima ya wananchi hawa ni nini? Waende wapi katika hali hii ambayo wanayo sasa na kama sipati majibu mazuri ya Serikali nitaomba kutoa hoja Wabunge wajadili tupate mwongozo wa bunge lako

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tuketi, sijaitoa hoja kwenu, sasa hapa wamesimama Wabunge watatu wote ni hoja ya dharura na inabidi kila hoja itazamwe pekee yake kwa sababu sijajua wanataka kusema nini au wote ni hoja hii ya chai? Mheshimiwa Mwenisongole ni hoja ya chai au hapana?

MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE: Mheshimiwa Spika, hapana.

SPIKA: Mheshimiwa Chege ni hoja ya chai au hapana?

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Spika, hapana

SPIKA: Haya, Waheshimiwa Wabunge amesimama Mheshimiwa Edwin Swalle akitupeleka kwenye Kanuni ya 54 kwamba kuna jambo la dharura na ameeleza hapa kwamba jambo hilo ambalo ameeleza kwa kifupi kabla sijampa nafasi kwa mujibu wa kanuni zetu akitaka kujua hatma ya Wananchi Kata ya Lupembe? Au Tarafa ya Lupembe?

MHE. EDWIN E. SWALLE: Tarafa nzima kata saba.

SPIKA: ...ambayo ina kata saba kwamba kuna changamoto ya malipo kati yao na mwekezaji ambaye amewekeza huko.

Sasa nilikuwa napitia hapa masharti ya Kanuni yetu ya 54 ambayo yanataka matumizi ya Kanuni ya 54 tutazame Kanuni ya 55 na inahusu masharti ya hiyo hoja ya dharura.

Sasa katika maelezo ya Mheshimiwa Mbunge amesema anataka kimsingi mambo mawili; la kwanza Serikali itoe kauli yake kuhusu jambo hili na wakati huo huo ametamani atoe hoja, kwa sababu hawezi kutoa hoja kabla sijampa nafasi kwa mujibu wa kanuni zetu.

Sasa kwa kulipima jambo hili namna alivyolieleza na wingi wa hawa watu ambao wanapata hii changamoto, kabla sijampa yeye nafasi tuimalize ile hoja yake ya kwanza ya kutaka Serikali inasema nini halafu nitajua nitoe hoja ama nisiitoe ili Bunge liweze kuishauri Serikali namna ya kwenda nalo hilo jambo. Sasa kwa sababu hoja inahusu Wizara ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza hoja aliyoisema Mheshimiwa Mbunge ni ya kweli, na sisi kama Wizara, Mheshimiwa Mbunge anafahamu, tangu juzi tumekuwa pamoja tukijadili na kufuatilia jambo hili, tumeshakaa mpaka na mwekezaji mwenyewe; jana Jijini Dar es Salaam Katibu Mkuu alijaribu kukaa na mwekezaji, kwa sababu nataka

Wabunge nataka mfahamu kwamba Kampuni ya *DL* ya Chai ni kampuni binafsi, haina ubia na sisi upande wa Serikali, ni mtu binafsi anayefanya biashara na wananchi wa Tarafa ya Lupembe kwenye zao la chai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo wajibu wetu sisi kama Serikali, moja tuliamua kumuita na kumwambia kwanza asifunge kiwanda na katika makubaliano ambayo tumekubaliana mpaka kufikia jana ni kwamba amesema ndani ya wiki hii atakuwa ameshafungua kile kiwanda ili kiweze kuendelea na utaratibu wa kununua chai ya watu, kwa sababu akifunga maana yake hata ile chai yenyewe iliyopo sasa hivi haitanunuliwa.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili, kwenye soko la chai duniani sasa hivi kuna changamoto ya bei ya soko duniani, *generally* kwenye bei ya chai duniani; na viwanda vingi vimekuwa vikifungwa, siyo cha *DL* pekee yake, hata ukienda Uganda zaidi ya viwanda vitano wamekuwa wafunga kwa sababu ya changamoto ya bei ya chai. Sasa sisi tunachotaka ni ku-*rescue* hili tatizo.

Moja, wakulima wa chai Lupembe walipwe deni lao; lakini pili mwekezaji aendelee na uzalishaji pale wa kununua chai ya wakulima wa Lupembe, na ndio kazi kubwa ambayo tunaendelea kuifanya sasa hivi. Mheshimiwa Mbunge analifahamu hili, hata jana alizungumza na Katibu Mkuu, jana alizungumza na mimi mwenyewe na vilevile tumeshakutana na mwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sisi tulichokuwa tunaomba kwamba kwa sababu tumeshakubaliana na mwekezaji kwamba ndani ya siku saba tangu alipofunga juzi mpaka kabla ya Jumanne atakuwa tayari ameshafungua kile kiwanda, tuone amefungua. Kwa sasa tunacho ki-*push* sisi ni yeye aweze sasa kuwalipa wale wakulima wa Tarafa ya Lupembe wanaolima zao la chai. Kwa hiyo, hayo ndiyo maelezo ya sisi Serikali mpaka hapa tulipofikia, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Sawa kabla sijarejea kwa Mbunge, ameeleza mambo ambayo wewe umeeleza jambo jipya. Wewe umeeleza kuhusu kufungua kiwanda, hoja ya Mbunge pamoja na kufunga kiwanda, lakini hoja yake kubwa ni wale wananchi kuwa na madeni, yaani kwamba mwekezaji anapaswa kuwalipa. Hizi siku saba ulizozitaja ni za kufungua kiwanda na kuwalipa wananchi wa Tarafa ya Lupembe ama ni kufungua tu kiwanda halafu mtaendelea na mazungumzo kwa ajili ya malipo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kama nilivyoeleza awali hapo kwamba cha kwanza tulichokubaliana, kwa sababu mtu amefunga kiwanda na anadaiwa na wakulima. Kwa hiyo, tukamwambia Hapana, tukubaliane afungue kiwanda ili sasa wakati amefungua aendelee na shughuli zake za uzalishaji na aendelee kuwalipa, kwa sababu yote mawili yanakwenda pamoja. Kwa hiyo, hiki ndicho ambacho tumekubaliana kwa sababu kiukweli yeye ndio alifanya biashara na wakulima na sisi wajibu wetu kama Serikali kwa sababu hii kampuni ni ya Kikenya, *DL Company* ni ya Kikenya na inamilikiwa na Mkenya na wala siyo Mtanzania.

SPIKA: Bodi ya Chai ina shughuli yoyote kwenye jambo hili au haina? Yaani ina jukumu lolote kwenye hili zoezi la wakulima kutokulipwa miezi tisa sijui mingapi?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, Bodi ya Chai…

SPIKA: Ina shughuli yoyote ama haina?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, ina shughuli, shughuli yake ni msimamizi mkuu wa shughuli za chai, ikiwemo kuhakikisha wakulima wanapata stahiki zao...

SPIKA: Serikali …

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: … kutoka kwa wawekezaji wa zao la chai.

SPIKA: Wakati huo huo Serikali haihusiki kabisa?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, sisi ndio tunayoisimamia Bodi ya Chai nchini. *(Kicheko/Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa hoja aliyoeleza Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Lupembe kuhusu wananchi wa Tarafa ya Lupembe ambao ni wakulima ni hoja nzito kwa kweli, kwa sababu wananchi wamehamasishwa kuingia kwenye kilimo cha chai na wengine walikuwa wameacha baada ya muda fulani, lakini wakarejeshwa tena kwenye kulima chai na sasa wamepata hii changamoto ambayo madeni ni ya muda mrefu. *(Makofi)*

Kwa kuwa Naibu Waziri hapa wakati ukijibu umesema pamoja na shughuli nyingine za Bodi ya Chai ni kuhakikisha mahusiano haya yanaenda kwa sura ambayo hawaonewi wakulima, na kwenye hili madam hawa hawajalipwa kwa hii miezi tisa, kwa kweli sisi tuwakabidhi ninyi Serikali, kwa sababu Bodi ya Chai siyo wakulima waliyoiweka, ni ninyi ndio mmeiweka Bodi ya Chai, na ilipaswa kufanya hii kazi mwanzo kabisa, kwa sababu wote tunajua lile zao la chai namna lilivyo. Kitendo tu cha kufunga siku ngapi kama chai ilitakiwa kuvunwa tayari ni hasara na huyu mwekezaji akienda kufungua hiki kiwanda maana yake ni madeni yanaongezeka juu ya madeni. Kwa hiyo, mazingira kidogo Bodi ya Chai lazima ifanye kazi yake kwenye jambo hili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa hoja hii inahusu mkataba kati ya wakulima na yule mwekezaji ambao Bodi ya Chai iliapaswa ishughulikie, mimi labda nitoe sasa kwa sababu sitaitoa hii hoja kama ya dharura pamoja na udharura wake, inakidhi vigezo vya kuwa dharura, lakini kisheria kwa sababu ni hoja inayohusu mkataba ambao hatuko nao hapa ndani, kwamba ni sehemu ya hoja ambayo sisi tutatakiwa sisi tuitolee maamuzi, kwa sababu baada ya mjadala itabidi tutoe maazimio. Sasa kwa sababu hatuwezi kufikia hiyo ngazi ya kuazimia mkataba ambao hatuko nao na hatujaweza kupata nafasi ya kuupitia na kujua una madhaifu gani, lakini hoja hapa tumeshaielewa kwamba kuna wananchi wa Tarafa ya Lupembe

wana hii changamoto ambayo Bodi ya Chai chini ya Wizara ifanye kazi yake kuhakikisha hawa watu wanalipwa pesa zao.

Sasa hizi siku za kufungua kiwanda ninyi endeleeni na kufungua kiwanda, lakini hili suala lishughulikiwe kwa sababu tusije tukajikuta tena mazingira ya kule nyuma zao la chai litaanza kushuka. Hii habari ya bei kupanda na kushuka miezi tisa sidhani kama bei ilishuka kwa wakati mmoja; na sitaki kuamini huyu mwekezaji hiyo chai sasa ya wakulima tangu aichukue hiyo miezi tisa yuko nayo pale kiwandani. Kwa hiyo, kama hayuko nayo kiwandani maana yake yeye ameuza na amepata pesa. Sasa ninyi na Bodi ya Chai kaangalieni ile chai ipo kiwandani? Ili kama ipo kiwandani wapewe wakulima watafute mteja. Kama haipo maana yake ameuza, awalipe. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa sababu ya hayo mambo kidogo tutakuwa tumefungwa kisheria sitaweza kuitoa hii hoja Waheshimiwa Wabunge ijadiliwe, lakini Serikali imeshatoa maelezo ya awali kuonesha kwamba wanalifahamu jambo hili, lakini ni kuweka mkazo kwa sura hiyo, kwa sababu tusingependa tuweke mazingira ambayo wawekezaji watakuwa wanajua kwamba wanaweza kujadiliwa na Bunge halafu tukafika mahali ambapo tutashindwa sasa kuisimamia Serikali, kwa sababu tutakuwa tumeingia kwenye utendaji ule ambao si kazi yetu, lakini ni kazi yetu kujali hoja za wananchi. Kwa maana hiyo tunaipelekea Serikali jambo hili na tunaamini lipatiwa ufumbuzi ndani ya muda mfupi ili wananchi wasipate athari hizo zaidi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge pole sana na litafanyiwa kazi kwa sura hiyo.

MHE. EDWIN E. SWALLE: Mwongoza wa Spika.

MWONGOZO WA SPIKA

SPIKA: Mheshimiwa Swalle.

MHE. EDWIN E. SWALLE: Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza nakushukuru sana kwa mawazo ambayo umeyatoa, lakini nilitaka

nipate mwongozo wako lile jambo ambalo tayari umeshalisema hapa awali.

Kwa kuwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo ameyatoa leo yametolewa pia mwaka jana (mwaka 2023) na hata kwenye maelezo yake ambayo ameyasema hapa hakuna ahadi yoyote kwamba hawa wakulima watalipwa lini? Sasa naomba mwongozo wako katika hali hii ya mkwamo hawa wananchi sasa wafanye nini? Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Haya, kwanza kwa sababu Mheshimiwa Waziri kwa maelezo aliyoyaeleza niondoe neno mkwamo, lakini kwamba watalipwa lini ndiyo maelezo niliyompa hapa, yeye na Bodi yake ya Chai wakafanye hiyo kazi ya kuzungumza na huyu mwekezaji, wananchi walipwe fedha zao. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, dharura nyingine imetokea, ni ya Mheshimiwa George Mwenisongole.

MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi, nimesimama hapa kwa Kanuni ya 54 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2023 nikiomba Bunge lako lisimamishe shughuli kujadili mustakabali wa ajira katika vyombo vyetu vya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Jeshi la Uhamiaji pamoja na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) walitangaza nafasi za ajira kwa vijana wote nchini, lakini katika hizo nafasi za ajira waliweka sharti ambalo mimi naliona ni la kibaguzi; kwamba yeyote anayetaka kuajiriwa kwenye vyombo vyetu hivyo vya ulinzi na usalama lazima apitie mafunzo katika Jeshi la Kujenga Taifa, lakini sasa hata hiyo nafasi ya kwenda huko JKT vijana wanaopata ni wachache na siyo wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo ukiangalia wanaomaliza kidato cha nne ni wanafunzi zaidi ya 500,000; wanaomaliza *form six* ni zaidi ya 200,000; wanaomaliza darasa la saba ni zaidi ya milioni moja na wote wangependa nafasi ya kuajiriwa katika

vyombo vya ulinzi na usalama. Sasa wanapoweka hilo sharti la kwamba lazima wapitie JKT linawanyima fursa vijana wetu wengi kupata nafasi ya kuijunga na JKT. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba ninukuu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 22(2) kinasema; "22.-(2) Kila raia anastahili fursa na haki sawa, kwa masharti ya usawa ya kushika nafasi yoyote ya kazi na shughuli yoyote iliyo chini ya Mamlaka ya nchi."

Mheshimiwa Spika, kufuatana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano mimi ninaona hili sharti linakinzana na Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na siyo haki kwa vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba Bunge lako lipate nafasi ya kuijadili na kuishauri namna gani nzuri ya Serikali ili kuondokana na hiyo kadhia ya vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwanza hoja haitolewi katika ngazi hii, lazima mimi niwe nimejiridhisha kwamba ni hoja ya dharura ili nimpe sasa nafasi ya kutoa hoja halafu aseme sasa anatoa hoja ndipo muunge mkono.

Waheshimiwa Wabunge, hili jambo si jambo jipya kuzungumziwa hapa Bungeni kuhusu vigezo vya ajira, si tu hizo za kwenye vyombo vyetu vya ulinzi na usalama lakini ajira yoyote inayoweka hicho kigezo cha JKT. Nadhani tulishawahi kuambiwa hapa na Serikali. Hayo matangazo yametoka lini Mheshimiwa Mbunge? Unayo hapo matangazo?

MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE: Mheshimiwa Spika, ninayo.

SPIKA: Hebu msaidizi niletee hayo matangazo, wakati huo huo Serikali haya maelekezo yalishawahi kutoka hapa ndani

kuhusu hiki kigezo na Serikali mlijibu kwamba hakitakuwepo. *(Makofi)*

Serikali hebu tupate maelezo, hiki kigezo ambacho kinaendelea kwenye matangazo wakati hapa ndani mliwahi kujibu kwamba hakitakuwepo kwa sababu nafasi za kwenda Jeshi la Kujenga Taifa hazitolewi kwa kila mtu. Nitoe nafasi kwenu Serikali kabla Bunge halijapewa nafasi ya kujadili hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, tuipokee hiyo hoja, lakini kwa msingi wa ajira kwenye vyombo vyetu vya ulinzi na usalama, kigezo muhimu sana ambacho tumekuwa tukizingatia ni uzalendo, lakini jambo lingine ambalo ni la muhimu pia kuzingatiwa wakati wa ajira za watu hawa pamoja na nia njema sana ya Mheshimiwa Mbunge juu ya kutokuwa na ubaguzi, lakini yapo masharti mengine ya kujiunga kwenye vyombo hivi ambavyo kwa namna yoyote ile yanaweza yasimchukue kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kwenye vyombo vya ulinzi na usalama shughuli za kijeshi tu zinazofanyika kule kwenye mafunzo haumtegemei mtu mwenye changamoto ya ulemavu kwa mfano kuingia huko hata kama angekuwa amepita JKT au hajapita JKT.

Kwa hiyo, kwa sababu umesema Bunge limeshatoa maelekezo kwamba kigezo hicho tusikiweke naomba tulichukue tutoe maelekezo kwa wakuu wa vyombo hivi kuzingatia maelekezo ya Bunge lako ili matangazo mengine yatakayotokea kigezo hicho kisijitokeze, nakushukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hii hoja iliyotolewa hapa na nimeletewa matangazo; tangazo moja linatoka kwa Kamishna Jenerali wa Magereza, limetolewa tarehe 9 Januari, 2024 na linacho hicho kigezo kinasema; "Awe amehitimu mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa au waliopo makambini."

Halafu tangazo lingine halijasema limetolewa lini, lakini linasema mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 20 Februari 2024, na hili linahusu Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nalo linasema; "Waombaji wawe wamepitia mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa." Haya na lingine hapa kuna ya Uhamiaji, tangazo la Uhamiaji la ajira limetolewa tarehe 30 Disemba; "Awe amehudhuria na kuhitimu mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa au Jeshi la Kujenga Uchumi, waliopo makambani au tayari amerudi uraiani."

Waheshimiwa Wabunge, nimempa nafasi hapa Mheshimiwa Naibu Waziri na ametoa maelezo, kwa maelezo aliyoyatoa yananilazimu Ofisi ifuatilie *Hansard* tulisema nini kama Bunge kuhusu jambo hili, kwa sababu huenda hatukutoa maelezo mahususi kwa hivyo wacha tujiridhishe. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa George Mwenisongole nakurudishia hizi karatasi zako, siku ya leo wasaidizi wangu watafuatilia Taarifa Rasmi za Bunge kuhusu jambo hili, tulitoa maelekezo gani ama tulitoa ushauri gani kwa upande wa Serikali, kwa sababu vyombo hivi watu wakishawachukua wao pia wanaouwezo wa kuwapeleka huko JKT, siyo lazima wawe wameenda kabla. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ukisema waende kabla ndiyo changamoto hii inajitokeza, lakini wao kwamba wawachukue wale wanaoweza kuwapeleka JKT ili wasiwe na hizo changamoto wanao uwezo huo. Kwa hiyo, hii itaondoa hii changamoto. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lakini kwa sababu hoja ni kwamba tayari Bunge lilishawahi kulisema hili jambo huko nyuma lazima nijiridhishe tulilisema kwa namna gani ili nisilitoe kwenu tujadili leo halafu tukasema jambo pengine tofauti na tulichosema mwanzo, ama kama mwanzo hatukusema basi tutalisema sasa baada ya hoja ya Mheshimiwa Mbunge, lakini nikishajiridhisha kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Kwa hiyo, Mheshimiwa utapewa nafasi kama tutakuwa hatukutoa maelekezo kamili, kama tulitoa maelekezo kamili

tutaikumbusha Serikali nini tuliagiza. Nadhani hiyo imeeleweka Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Jafari Chege.

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru; nimesimama kwa Kanuni namba 54 ya Kanuni za Kudumu za Bunge na mimi kuwasilisha jambo la dharura linahusiana na kukatika kwa mawasiliano ya barabara kwenye maeneo mengi nchini yanayotokana na kuvunjika kwa madaraja kutokana na mvua zilizonyesha, lakini kupeleka barabara nyingi hivi ninavyozungumza mpaka leo wananchi wengi maeneo mengi wanapata adha hii kubwa ya kusafirisha au kusafiri wao kutoka eneo moja kwenda eneo linguine, lakini si hivyo tu shughuli za kiuchumi kwenye maeneo mengi zimesimama kwa sababu barabara hizi kwa bahati mbaya au bahati nzuri zilikuwa ndizo zinakwenda maeneo ambayo kuna vyanzo vya kiuchumi za uendeshaji wa halmashauri, lakini na wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, lakini siyo hivyo tu hata shughuli za kijamii, juzi Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanachangia hapa kupitia Kamati ya USEMI wengi wametoa na ushahidi kwamba mahali pengine hata *ambulance* haziwezi kufika kwa ajili ya kuwachukua wagonjwa na kuna baadhi ya maeneo mengine hata magari ya dawa hayawezi kufika kwenda kuchukua au kupeleka dawa kwa ajili ya kutoa huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo mengine ambayo uharibifu huu umesababisha vifo na vifo hivi vinatokea wakati mwingine, wakati wananchi wana-*struggle* kutaka kuvuka kutoka eneo moja kwenda eneo lingine kutokana na kuvunjika kwa miundombinu, kwa haya yanasababisha leo nisimame kwa idhini yako kama utaridhia ili angalau niweze kutoa hoja ya dharura hasa tukizingatia hata kupitia Kamati ya USEMI fedha ambazo zimekwenda kwa ajili ya ujenzi ambazo zilitakiwa ziende *TARURA* kwa ajili ya ujenzi wa barabara imekwenda asilimia 10 peke yake.

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu tarehe 31 Januari tulipata maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ambaye alisema ndani

ya Bunge hili kwamba kabla ya Bunge kuahirishwa, fedha kwa ajili ya dharura ya utengenezaji wa barabara zitakuwa zimekwenda, mpaka leo hii tumebakiza siku moja hakuna fedha ambayo imekwenda mahali popote na wananchi wanaendelea kuteseka maeneo mengi nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa udharura huo naomba sasa nipate idhini yako kama ambavyo…

SPIKA: Haya Mheshimiwa Mbunge umeeleweka.

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Spika, kama utaniruhusu niweze kutoa hoja ili Wabunge wenzangu waweze kujadili hoja hii. Ahsante.

SPIKA: Umeeleweka. Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 54(3) na (4) na masharti yaliyowekwa kwenye Kanuni ya 55, Mheshimiwa Mbunge unapewa dakika tano ama kwa sababu umeshaeleza hauna haja ya kurejea yale yale lakini eleza sasa hoja yako uitoe kwa Bunge. *(Makofi)*

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimeeleza hapo awali na nimejaribu kueleza athari ambazo zinatukumba sisi wananchi wetu hayo maeneo tunayokwenda, na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha alitoa kauli hapa ndani ya Bunge hili ya kutuambia kabla ya Bunge kuahirishwa fedha hizi zitakuwa zimekwenda kwa ajili ya kunusuru na kuwasaidia wananchi wetu lakini mpaka leo kwenye maeneo yetu Majimbo mengi Wabunge hawajapata fedha hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo kwa kuokoa muda, naomba nitoe hoja sasa Wabunge waweze kusimama ili waniunge tuweze kujadili hoja hii. *(Makofi)*

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono lakini tutapata wachangiaji wachache kwa sababu muda wetu umekwenda kidogo kwa hiyo wachangiaji watakuwa wachache wa hoja hii. Sasa wengine mkae, wasimame wale wenye nia ya kuchangia na nitachagua wachache. Kwa hiyo wengine waliokuwa wanaunga mkono hoja wakae wabaki wale ambao wanataka kuchangia hoja. Ninyi simameni hivyo hivyo nitachagua wachache na tutakubaliana kwamba hao niliowachagua ndiyo hao hao.

Waheshimiwa Wabunge, wale waliopata nafasi ya kuzungumza leo Bungeni wakae. Ndiyo wale walioiuliza maswali ya nyongeza na swali la msingi wakae. Waliopata nafasi ya kuzungumza leo wakae, ndiyo lazima tutafute namna ya kupunguza watu.

Mheshimiwa Sophia, Mheshimiwa *Engineer* Chiwelesa, Mbunge wa Momba leo si ulipita hapa mbele kwa hiyo kaa Mheshimiwa. Mheshimiwa Kakunda, Mbunge wa Dar es Salaam naona umesimama na wewe kuna daraja limekatika? Ngoja hoja ya Mbunge inahusu barabara kutokupitika, kuna barabara haipitiki Kibamba? *(Kicheko)*

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Spika, nyingi sana.

SPIKA: Ahsante sana, haya Waheshimiwa tuketi.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Chiwelesa, Mheshimiwa Kakunda ajiandae, dakika tatu.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuanza kuchangia hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kabisa kwamba mtandao wa barabara nchini ni suala la muhimu sana kama Taifa, lakini katika bajeti ambayo ndugu zetu wa *TANROADS* waliomba shilingi trilioni tano kwa ajili ya kutengeneza barabara bajeti imewapa kidogo shilingi trilioni 1.5. Hii inaonesha jinsi gani kwamba Wizara hii

haipata fedha za kutosha ili kuweza kutengeneza pale inapotokea majanga kama ambavyo majanga ya sasa yametokea, hiyo ni moja.

Mheshimiwa Spika, pili; Taifa lazima iwe na fedha ya kujikimu pale tunapopata matatizo na majanga. Hatuwezi kuwa watu ambao tunasubiri tatizo litokee ndiyo tutafute fedha. Hii itufundishe kwamba tunahitaji kuwa na Kamati na tunajua tuna Wizara ipo inayoshughulikia majanga. Hivyo basi, tuhakikishe Wizara ya Fedha inapeleka kwenye Wizara husika ili majanga yanapotokea tutekeleze badala ya kuanza kutafuta fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna haja ya kupeleka fedha sasa na wananchi waweze kutengenezewa barabara zao. Tunafahamu katika Mkoa wa Mbeya ni Mkoa ambao unapeleka chakula katika Taifa hili katika ile Mikoa mitano bora. Leo hii baadhi ya barabara zimeharibika, wakulima wanashindwa kusafirisha mazao yao kwa sababu tu wameshindwa na mazao yameendelea kupanda bei kwa sababu yameshindwa kufika katika soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba Wizara husika ya Fedha ambayo iliahidi kwamba itapeleka fedha kwa wakati ingekuwa imekwishapeleka. Mara nyingi tunapozungumza katika Bunge lako lazima yatekelezwe. Tusiwe tunaongea kisiasa kwamba tutapeleka kabla ya kumaliza Bunge, Bunge linaisha kesho, Wabunge wa Majimbo wanasema pesa hazijaenda. Tunaomba kiti chako kitoe onyo kali na pesa zipelekwe madaraja yajengwe, barabara zirekebishwe, wananchi wawe salama na tuendelee kuendeleza Taifa letu, ahsante *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa *Engineer* Chiwelesa.

MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA: Mheshimiwa Spika, nami nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii. Kwanza kabisa kipekee nimpongeze sana mtoa hoja. Niliongelea hili jambo juzi, jana Waziri wa Fedha amejibu lakini majibu bado

hayajaridhisa kwa sababu kuna barabara ambazo tunasema zilifanyika kama nyongeza shilingi milioni 500 kila Jimbo.

Mheshimiwa Spika, halafu tukasema *TARURA so far,* barabara zilizokuwa zimetangazwa katika bajeti ya shilingi bilioni 808, *only 80 per cent* zimetangazwa lakini tunapoongea leo kuna baadhi ya Wakandarasi ambao wameshinda mikataba, wana *acceptance letters* lakini mikataba haijasainiwa na *TARURA only* kwa sababu *TARURA* hawana pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana tunataka kujua pesa ile iko wapi? Tukisikiliza hoja pamoja na kwamba mambo hayapitiki. Upande wa *TARURA* wamejitahidi hata kutangaza hizo barabara kwa wakati kwenye ile asilimia 80 lakini *so far* kuna watu wana *acceptance letter* hawajasaini mikataba. Ukiuliza ukifuatilia wanaambiwa tumeambiwa tusubiri hali ya fedha ndiyo tujibiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tunataka kama Bunge tusikie tutawabana *TARURA* hapa lakini Waziri wa Fedha yuko hapa atusaidie kama uzembe uko *TARURA* tujue leo, kama uzembe ni Wizara ya Fedha tujue leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zile barabara tulizoongezewa shilingi milioni 500 jana Waziri wa Fedha alisema ni *P4R,* sasa shilingi bilioni 350 hazikuwa zote zinaenda kwenye shilingi milioni 500 kama tulimuelewa Waziri wa TAMISEMI wakati ule. Ukichukua majimbo 264 ya uchaguzi ukazidisha mara shilingi milioni 500 ni karibu shilingi bilioni 132. Sasa kama tunatekeleza kwenye zile shilingi milioni 500 kila jimbo, hiyo *P4R* wengine ambao wako tayari na barabara ziko tayari ziweze kutekelezwa tutamaliza lini? Kwa sababu ujenzi wa barabara hupewi kilometa 20 au kilometa 10 ukaijenga ndani ya mwezi. Tumebakiza miezi minne tu bajeti hii iishe tuingie kwenye bajeti nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hata leo mtu akiwa *awarded* barabara *possibility* ya kumaliza zile 80% ambazo bado hazijafanyika, zije na hizi shilingi milioni 500 tulizoongezewa bado hazijafanyika, hizi barabara zinajengwa na watu na kuna *time*

frame ya kujenga barabara. Yaani hunyanyuki leo ukapeleka hela mwezi Mei ukategemea barabara iishe ndani ya mwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ninapomalizia vitu kama madaraja unapojenga *structures* hata kama mvua inanyesha vitu kama madaraja vinaweza vikajengwa wakati wa mvua kwa sababu mkandarasi anachofanya ata-*diverge* mto atajenga daraja akimaliza kujenga daraja ule mto ataurudisha. Kwa hiyo, kama hata pesa ingetolewa tu kwa ajili ya kujenga madaraja baadhi ya hali kule ingeweza kutengamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunataka kauli ya Serikali watuambie pesa inatoka lini tunaporudi Majimboni tukabanane na mameneja wa *TARURA* wa Wilaya zetu hatimaye wananchi wajue kwa sababu tunaenda kufanya mikutano tukawaambie wananchi tunaenda kwenye Bunge la Bajeti. Sasa unamwambiaje unakuja kuomba barabara za bajeti mpya wakati mwezi Julai taarifa uliyompelekea bado haijafanyika? Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Joseph George Kakunda atafuatiwa na Mheshimiwa Mbunge wa Kibamba, Mheshimiwa Lusinde ajiandae.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Spika, mimi namuunga mkono sana Mheshimiwa Chege kwa hoja yake kwa sababu ninaposimama hapa Mkoa wa Tabora umetengwa na Mkoa wa Mbeya kwa sababu barabara ya kutoka Tabora kwenda Mbeya katika eneo la Mbuga ya Ipembampazi imekatika sehemu sita, barabara ile haipitiki.

Mheshimiwa Spika, vilevile wakazi wangu wa Tarafa ya Kiwele wametengwa na Tarafa ya Sikonge kwa sababu Barabara hiyo haipitiki. Vilevile barabara ya kutoka Sikonge kwenda Kipili nayo haipitiki kwa sababu hiyo. Kwa hiyo tunahitaji fedha ziende haraka kwenye *TANROADS* lakini vile vile kwenye *TARURA* ili barabara ziweze kufunguka.

Mheshimiwa Spika, katika barabara ambazo zinasimamiwa na *TARURA* kati ya kilometa 900, kilometa 400 hazipitiki katika Jimbo langu. Kwa hiyo, mimi naomba sana tusisitize wala tusizungumze sana. Serikali ipeleke fedha haraka kwenye *TARURA* pamoja na *TANROADS* ili barabara zetu ziweze kupitika wananchi waweze kusafiri na kusafirisha mazao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Chege. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Issa Mtemvu atafuatiwa na Mheshimiwa Livingstone Lusinde, Mheshimiwa Kalogeris ajiandae.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza ninaunga mkono hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Chege na kwa wananchi wa Dar es Salaam wewe ni shahidi mvua hizi zinazoendelea zimeharibu kabisa barabara zilizopo lakini hata zile ambazo tulikuwa tunatarajia tuanze kuzitengeneza ziendelee kuwa vizuri na sasa hivi na zenyewe zimeharibika kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nikibeba msingi wa Dar es Salaam kwamba uchumi wetu ni barabara. Sisi hatupo kwenye uvuvi, hatupo kwenye kilimo ni barabara. Hali ya sasa wananchi wanashindwa hata kutoka kwenda kuendelea na shughuli zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nitumie nafasi hii kukumbuka sana kazi kubwa na nzuri aliyoifanya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan mwaka 2021/2022 kwa kuingiza ile shilingi 100 ya mafuta. Tukaongeza zaidi ya shilingi bilioni 350 tukaona kuna fedha zikaja kwenye majimbo na zikaleta hali nzuri kidogo lakini kipindi cha miaka miwili sasa hivi hakuna fedha zozote ambazo ni *material* zimekuja kusaidia barabara za mtandao wa zaidi ya kilometa 144,000 kwenye Nchi yetu ambayo ndiyo inabebwa na *TARURA,* kwa hiyo hali ya barabara ni mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatambua, kwa mfano Dar es Salaam mapato ni zaidi ya 85% yanatokea Dar es Salaam. Utalii hawezi

kufika Arusha, hawezi kufika huko kwenye mbuga zetu nyingine za Manyara na kadhalika kwenye madini lazima atue Da es Salaam kwanza. Sasa anaingia Dar es Salaam kutoka *Airport* mazingira yote kabisa hayana mvuto! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tuone Wizara ya Fedha imsaidie sana Mheshimiwa Rais kuona yale maelekezo katika Kamati zetu na Bunge lako Waziri aone umuhimu kwenye hili. Watenge fedha zinazohitajika zaidi ya shilingi bilioni 350 zielekee katika barabara hizi za ndani za *TARURA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukifika hivyo maeneo mengi ndani ya Jimbo la Kibamba kwa mfano maeneo ya Goba, Saranga, Kwembe, Msijani na Kibamba yenyewe. Hata maeneo ya Luguruni pale unanielewa nikisema hivyo hali ni mbaya sana. Kwa hiyo, niombe sana naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Chege lakini niombe Wizara ije iwe tayari kuungana na Wabunge hapa katika jambo hili la muhimu kabisa ili wananchi wetu waweze kuendelea na shughuli zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Livingstone Lusinde atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Kalogeris, Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota ajiandae.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kupata nafasi ya kuchangia hoja ya Mheshimiwa Chenge na kabla sijaenda mbali naiunga mkono…

SPIKA: Ngoja, ngoja anaitwa Mheshimiwa Jafari Chege.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Chege Mbunge wa Rorya, naiunga mkono hoja yake.

Mheshimiwa Spika, mimi ya kwangu ni mawili; jambo la kwanza Serikali ina vyombo ambavyo vinaitaarifu mapema Serikali kwamba kutakuwa na shida kwa mfano watu wa Hali ya

Hewa, wanaposema mwaka huu tanategemea kuwa na mvua nyingi tayari Serikali imeshapata taarifa kwamba barabara nyingi zitakatika. Kwa hiyo, huwezi ukasema kwamba Serikali haina habari, Serikali inayo habari ya kutosha kabisa kwamba tunaposema mwaka huu tuna mvua nyingi maana yake uharibifu wa barabara utakuwa mkubwa. Kwa hiyo Serikali inatenga bajeti yake kuhakikisha kwamba inakidhi yale mahitaji ya hali ya hewa waliyotutahadharisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili sisi Wabunge wa Vijijini madaraja yetu yakikatika na barabara zikikatika, namna ya kwenda kurudisha huduma kwa wananchi inachukua muda mrefu sana tofauti na Majimbo ya Mjini. Kwa hiyo tungeomba Serikali inavyothamini vilevile watu wa mijini ndiyo ithamini na watu wa vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na taabu sana halafu kuna madaraja sugu, yako madaraja kila mwaka lazima likatike. Sasa ujenzi wa maeneo yale si lazima uwe tofauti? Kwa mfano, kila siku tukisimama hapa tunazungumza habari ya Daraja la Manda limekatika, tunazungumza habari ya Daraja la Mlowa barabarani limekatika lakini ujenzi wake ukijengwa baada ya mwaka mmoja tena limekatika kama biskuti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tungeomba Mheshimiwa Waziri ayapitie yale madaraja sugu ambayo yana tabia ya kukatika kila mwaka wa mvua nyingi ili utengenezaji wake uwe imara zaidi. Waongeze namna ya kuyatengenza ili tusiwe tunatibu daraja hilo hilo linakula pesa nyingi matokeo yake kujenga ni daraja hilo hilo, mwakani unarudia daraja hilo hilo maana yake ujenzi pale haufuati taratibu za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo wakati nikiunga mkono hoja ya Mheshimiwa Chege naomba Serikali vilevile ihakiki madaraja ya vijijini, iangalie barabara za vijijini kama inavyoangalia barabara za mjini. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika...,

SPIKA: Ahsante sana; Mheshimiwa Innocent Kalogeris atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya ajiandae.

MHE. INNOCENT E. KALOGERIS: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi kuzungumza katika hoja ambayo iko mbele yetu imeletwa na Mheshimiwa Chege Mbunge wa Rorya.

Mheshimiwa Spika, kiuhalisia inawezekana kwa wale ambao wako kwenye majimbo ya mjini wanaweza kuwa hawaelewi nini athari ya ambayo wananchi wetu wanapata katika majimbo ya vijijini. Mimi leo hii mvua ambayo imepiga Dodoma zaidi ya masaa matano sikulala, kiuhalisia nilikuwa najua tu kuwa wananchi wangu huko wanaendelea kuteseka na bahati nzuri nilipopiga asubuhi nimeambiwa mvua imepiga lakini haijaendelea kuleta maafa makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiuhalisia nataka niombe tu Serikali iendelee kutenga fedha. Katika mazingira ya kawaida kuna wengine hapa wamezungumzia bajeti haijakwenda lakini kiuhalisia na kiuhakika hizi mvua za *El Nino* zilizojitokeza zimefanya maafa makubwa kwa wananchi wetu. Mfano, mmoja kwangu mimi tu leo hii ninapozungumza wananchi wa Kata ya Mngazi, Kijiji cha Vigolegole wanapata athari kubwa ya mafuriko kutokana na barabara kukatika na maji kuelekea kwenye wananchi wangu.

Mheshimiwa Spika, Meneja wa *TARURA* wa Wilaya ameomba kiasi cha shilingi bilioni tano kwa ajili ya marekebisho ambayo yamefanyika na mvua za *El Nino*. Kwa hiyo niombe tu Waziri wa Fedha, Waziri wa TAMISEMI angalieni hili jambo wananchi waweze kupita na maisha yaendelee kama kawaida.

Mheshimiwa Spika, vile vile kwenye upande wa *TANROADS* barabara kubwa juzi wakati nachangia taarifa ya Kamati ya Miundombinu, Barabara kubwa ya Bigwa – Kisaki imekatika zaidi ya mara tano wananchi wanashindwa kwenda, shughuli zao zinashindwa kwenda. Kwa hivyo tuombe tu Serikali angalieni wananchi wetu wa vijijini na wao wafurahie matunda ya uhuru.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, Serikali itupe maelekezo nini kinachotakiwa kuendelea kufanyika. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota atafuatiwa na Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, Mheshimiwa Constantine John Kanyasu ajiandae.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ambayo imewasilishwa mbele yetu na Mheshimiwa Jafari Chege Mbunge wa Rorya.

Mheshimiwa Spika, hali ya barabara zetu ni mbaya na katika maeneo mengi sasa hivi hayapitiki. Kama alivyosema Mjumbe aliyepita sisi wa Majimbo ya Vijijini lakini hata na wa Mjini athari ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano katika Mkoa wetu wa Mtwara sasa hivi kuna changamoto ya Daraja la Lukuledi. Mto Lukuledi umefurika na hakuna mawasiliano kati ya Nachingwea na Masasi. Siyo hivyo tu, jana tulipata maelezo kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Tunduru kwamba Daraja la Muhesi ambalo ni muunganiko kati ya Tunduru na Mkoa wa Mtwara nako kulikuwa na changamoto ya maji yanapita juu ya daraja na hata hivyo ililazimika kuzuia magari yasipite ili kuangalia ubora wa lie daraja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu barabara yetu ya ulinzi kati ya Tanzania na Msumbiji bado kuna changamoto ya mawasiliano kwa sababu nako vilevile kuna athari zimejitokeza. Mimi kwenye Jimbo langu la Nanyamba kuna daraja kubwa pale Mjini limekatika na hilo linaunganisha na Kitaya, kijiji ambacho kipo mpakani mwa Tanzania na Msumbiji, hivyo ninaiomba Serikali itoe fedha ya dharura kwa ajili ya matengenezo haya.

Mheshimiwa Spika, kinachoendelea sasa hii mameneja wa *TANROADS* na *TARURA* wameambiwa wapeleke makisio Wizarani halafu yaunganishwe lakini athari inaendelea kutokea kule. Ni muda muafaka fedha zitoke leo na si kesho, kama kuunganisha

wameshaunganisha tayari wameshapeleka TAMISEMI na wameshapeleka *TANROADS*. Kinachotakiwa ni fedha kutoka siyo kuunganisha kwa sababu athari ni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya atafuatiwa na Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mheshimiwa Deogratius Ndejembi ajiandae.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante, nami naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Chege. Ukweli ni kwamba barabara hasa za vijijini zina hali mbaya sana. Napenda kutoa mfano halisi, barabara ya kutoka Nyoni mpaka Mitomoni Eneo la Liparamba pale kulikuwa daraja lilijengwa lakini halikukamilika. Matokeo, yake mama mmoja alikuwa anajifungua watoto mapacha akashindwa kupelekwa hospitali. Gari ikabidi litafutwe upande mmoja lisimame sehemu moja na litoke upande mwingine lisimame, akafanikiwa kujifungua mtoto mmoja hapo hapo darajani, mwingine hakutoka. Baadaye walipomvusha kufika njiani yule mama akampoteza mtoto.

Mheshimiwa Spika, tunatambua jitihada za Serikali yetu, hilo halina ubishi, lakini kwa maendeleo na shida zilizopo hasa kwa barabara zinazopita Mwambao wakati mwingine mito ile inakuwa ni mikubwa, inajaza maji kiasi kwamba watoto wa shule utakuta siku tatu hawajaenda shule. Walimu wengine wanavuka, wanakufa.

Mheshimiwa Spika, tunaomba sana hii bajeti ambayo sisi wenyewe tulidhamiria angalau tuchangie kiasi fulani cha fedha kwenye mafuta ili iweze kusaidia maeneo hayo, basi zipelekwe ili iondoe hiyo dharura na pia kupata ufumbuzi wa kudumu hasa kwa barabara zote za *TARURA* na *TANROADS*, ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Ndejembi na Mheshimiwa Innocent Bashungwa, ajiandae.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nami naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Chege. Watu wakisikia Geita Mjini wanaweza wakafiri ni mjini na hakuna shida ya barabara. Geita Mjini inaundwa na kata 13. Kata tisa ziko vijijini. Watoto wa Bulela na Shiloleli hawaendi shule kwa sababu barabara zimekatika. Kinachotokea, barabara inajengwa ina kitambi, yaani inajengwa halafu daraja linainuka juu halafu huku kwenye barabara panakuwa chini. Kwa hiyo, mvua ikija maji yanapita kwenye barabara yanakwepa daraja. Sasa matokeo yake ni kwamba barabara nzima imekatika.

Mheshimiwa Spika, watoto wanaosoma kwenye Shule ya Emako hawawezi kwenda shuleni mpaka wapewe *escort* na walimu na wazazi. Kwa hiyo, barabara ya kutoka Geita kwenda Kakola - Kahama imekatika katikati na daraja halipitiki na barabara haipitiki. Ukiacha barabara za Bombambili na barabara za Matola ambako zote zile kuna vifusi viliwekwa tangu mwezi wa 10 wale wakandarasi hawakulipwa. Kwa hiyo, mvua zilipoanza wakasusia na wakaondoka na wenyewe barabara hazipitiki.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu Serikali inafanya kazi nzuri sana, lakini tunadhani hili jambo linahitaji dharura liweze kupatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

SPIA: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Deo Ndejembi atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Bashungwa na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, ajiandae.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI): Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kwa kukiri kwamba Waheshimiwa Wabunge wanachochangia ni kweli kuna changamoto ambazo zipo katika maeneo mbalimbali ya nchi hii. Changamoto hizi za barabara zimesababishwa na mvua kubwa za *El Nino* ambazo zinaendelea kunyesha hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto hizo, bado kuna jitihada kubwa sana ambazo zimefanywa na Serikali hii ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 taasisi yetu ya *TARURA* ilikuwa ina bajeti ya *emergence* ya shilingi bilioni 10 tu, lakini katika mwaka wa fedha wa 2023/2024 huu tuliopo sasa, *TARURA* iliidhinishiwa bajeti ya shilingi 21 kwa ajili ya dharura. Tayari fedha hiyo yote ya dharura Wizara ya Fedha imeshaileta kwa taasisi yetu *TARURA* na imeshatumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya mvua hizi zinazoendelea, mwezi Disemba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa aliielekeza taasisi yetu ya *TARURA* kuweza kufanya tathmini ya kina ya kuona athari ambayo imepatikana na mvua hizi ambazo zinaendelea kunyesha. Katika tathmini ile, ilionekana taasisi yetu ya *TARURA* inahitaji shilingi bilioni 65 ili kuweza kuendelea kutengeneza barabara zetu ziweze kupitika wakati wote hasa katika kipindi hiki ambacho mvua zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba isingekuwa kazi nzuri inayofanywa na *TARURA* katika miaka ya nyuma tangu ianzishwe taasisi hii mwaka 2017, kwa mvua hizi zinazoendelea hali ingekuwa mbaya zaidi. Ni kazi kubwa ambayo imefanywa na taasisi yetu ya *TARURA* na ni kazi kubwa ambayo Serikali hii ya Dkt. Samia Suluhu Hassan imekuja kuiongezea nguvu *TARURA*.

Mheshimiwa Spika, *TARURA* peke yake ilikuwa inapokea shilingi bilioni 226 tu kwenye bajeti yake, lakini tokea aingine madarakani Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, aliiongezea *TARURA* bajeti ya shilingi bilioni 810 ambayo ndiyo sasa tunaitekeleza. Hivi tunavyozungumza mpaka kufikia Disemba kama Taarifa ya Kamati ya Bunge ya TAMISEMI ilivyowasilishwa hapa na Mwenyekiti Londo, kweli bajeti ilikuwa bado fedha nyingi haijafika. Mpaka hapa niliposimama mbele ya Bunge lako Tukufu, zaidi ya shilingi bilioni 309 zimeshapokelewa kutoka kwa wenzetu wa Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, ni jana tu Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameelekeza shilingi bilioni 30 iweze kuletwa haraka *TARURA* kwa ajili ya kuweza kutekeleza na kutatua changamoto ambazo Waheshimiwa Wabunge wengi humu ndani wamezizungumza. Niwatoe mashaka, Serikali hii iko kazini na barabara hizi zitatengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameshatoa maelekezo baada ya kukaa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwamba ile shilingi bilioni 350 ya nyongeza kutoka kwenye ile 810 iliyopitishwa na Bunge iweze kuanza kutumika na kazi hizo zitangazwe. Yuko hapa atakuja kuzungumza yeye.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, tunakiri changamoto iliyopo, lakini changamoto hizi zinaenda kutatuliwa mara moja. Mtaona magreda na ardhi ikichimbwa katika majimbo yenu kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais wetu kipenzi Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, nimalizie. Nimtoe mashaka Mheshimiwa Mtemvu na Wabunge wote wa Mkoa wa Dar es Salaam. *DMDP II* tarehe 19 inaenda kuwa *signed* ambapo ni zaidi ya shilingi bilioni 850 kwa ajili ya kutengeneza barabara na miundombinu mbalimbali katika Mkoa wa Dar es Salaam kwa Mheshimiwa Mama Kilave, Temeke, kwa Mheshimiwa Chaurembo kwa Mheshimiwa Jerry Silaa, ukienda kwa Profesa Mkumbo na wengineo wote barabara hizi zinaenda kutengenezwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie hapo.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, kama utakumbuka, tulipata Mwongozo hapa nadhani wiki ile nyingine baada ya Wabunge wengi kuuliza maswali halafu ukataja wawili, watatu ukataja na kiasi cha pesa. Sasa hivi tena umejibu yote, ukarejea Dar es Salaam, ukaanza kumtaja mmoja mmoja na miradi iliyopo na pesa itakayopelekwa.

Hapa wamezungumza Wabunge wengi sana na wenyewe wangependa kusikia kwenye maeneo yao ni kiasi gani cha pesa kinakwenda? Sasa hapo kwa sababu Wabunge waliozungumza ni wengi na kwa kweli hapa makaratasi ninayo mengi ya Wabunge ambao waliomba kuzungumza imebidi niwakate. Wewe watoe wasiwasi Watanzania wote, siyo Dar es Salaam pekee, kwa sababu ukiwataja wao na pesa uliowatengea tutataka utaje Mbeya mkoa mzima umetenga ngapi? Utaje na majimbo yetu kama unavyowataja watu wa Dar es Salaam.

Kwa hiyo, tutoe hofu Watanzania wote, tunahitaji hizo pesa ulizozitaja, siyo wa Dar es Salaam peke yao.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI): Mheshimiwa Spika, sawa. Nikutoe hofu wewe pamoja na Wabunge wote na Watanzania kwa ujumla. Serikali hii ya Awamu ya Sita imewekeza fedha nyingi katika miundombinu ya barabara za mijini na vijijini. Ndiyo maana narejea niliyozungumza hapa kwamba *TARURA* ilikuwa inapokea shilingi bilioni 226 tu na sasa bajeti imekwenda shilingi bilioni 810.

SPIKA: Hiyo…

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI): Mheshimiwa Spika, hivi tunavyozungumza 350, Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameshatoa ruhusa kazi zitangazwe nchi nzima…

SPIKA: Mheshimiwa hiyo imeshaeleweka. Tulitaka tu utuambie na majimbo mengine. Ukiwataja Dar es Salaam na mikoa mingine pia inahitaji kutajwa. Ndiyo hoja iliyoko hapa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI): Mheshimiwa Spika, …

SPIKA: Kwa hiyo, kwa kuwa wewe umeshawataja Dar es Salaam na umeshataja kwa ujumla, nataka uliweke sawa, kwa sababu la sivyo utaombewa Mwongozo mwingine tena hapa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI): Mheshimiwa Spika, kwa Dar es Salaam mradi wa *DNDP* ni mradi mahususi kwa ajili ya Mkoa wa Dar es Salaam.

SPIKA: Haya, Morogoro.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI): Mheshimiwa Spika, Morogoro katika fedha hizi za bajeti ambazo nazitaja…

SPIKA: Ambazo ni ngapi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI): Mheshimiwa Spika, ambazo na wenyewe kuna Mradi wa *TACTIC* ambao upo kwenye majiji, manispaa, kuna halmashauri za miji na kadhalika.

SPIKA: Haya, unaulizwa Songwe?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI): Mheshimiwa Spika, kote, nchi nzima. *(Kicheko)*

SPIKA: Manyara!

MJUMBE FULANI: Morogoro vijijini?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI): Mheshimiwa Spika…

SPIKA: Haya, Mkoa wa Mara?

MJUMBE FULANI: Ifakara?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI): Mheshimiwa Spika, fedha kwa ujumla ni bajeti ya *TARURA* ya shilingi bilioni 810 ambayo itakwenda maeneo yote nchini.

MJUMBE FULANI: Kagera na Ngara?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI): Mheshimiwa Spika, kuna nyongeza ya shilingi bilioni 350 ambayo Wanambeya na mikoa mingine yote ambayo unawasikia Waheshimiwa Wabunge wanaitaja.

MJUMBE FULANI: Mtwara Mjini hujataja wewe! *(Kicheko)*

MJUMBE FULANI: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri unaona kuna Taarifa hapo inataka kuletwa.

MJUMBE FULANI: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

SPIKA: Ni hivi, sijaelewa ni wapi ambapo sijaeleweka. Kwa kuwa Wabunge waliochangia ni wengi na wote wana mahitaji katika maeneo yao, ukichagua wewe wa kuwataja wengine ukawaacha, wote wanaohitaji na wanataka wananchi wao wasikie kwamba ni pesa ngapi zimewekwa? Maadam wewe umeamua kutaja mkoa mmoja, nilikuwa nakuweka sawa, kwa sababu la sivyo utaombewa tena miongozo humu ndani.

Ukishasema pesa imetengwa kwa ajili ya wote, ukitaka kutaja *DMDP,* basi taja miradi yote iliyoko nchi hii ambayo inaenda kutengeneza huko, kwa sababu wengine sasa hapa, si unaona hata mimi nimemwuliza Mbunge wa Kibamba na wewe una shida kama wa Morogoro Vijijini? Sasa na wewe tena ukaenda huko huko, hapana. Wananchi wote wana haki sawa na mgao lazima na wao wapatiwe. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Innocent Bashungwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba na mtoa hoja ajiandae.

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja ambayo imeletwa mbele

yetu na Mheshimiwa Jafari Chege. Nakiri kama ilivyojadiliwa hapa, mvua za *El Nino* zimeleta dosari kubwa kwenye miundombinu ya barabara pamoja na madaraja. Faraja kubwa tuliyonayo ni kwamba Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Jemedari wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan haijawaacha peke yenu Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watanzania. Serikali kupitia Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu alizindua mpango wa dharura kwa Sekta zote na kutoa maelekezo kwamba kila sekta ijiandae kwa ajili ya kukabiliana na dosari ambazo zitajitokeza na Mvua za *El Nino*.

Mheshimiwa Spika, kila sekta tumejiandaa na kwa upande wa barabara na madaraja tulichokifanya na hata ukiangalia *Hansard,* nilielekeza wakati ule tunajiandaa na mvua za *El Nino* kwamba *Regional Managers wa TANROADS* wote wakishirikiana na Wizara pacha, TAMISEMI kwa maana ya *TARURA* wakague madaraja yote na kuzibua mifereji ili mvua zitakapoanza, basi zisilete athari kubwa kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mvua zimenyesha kubwa sana na maelekezo ya Serikali ambayo tunaendelea kuyasimamia ni kuweka mawasiliano ya barabara kwa kadiri inavyowezekana pale mawasiliano yanapokatika. Ninyi ni mashahidi, kwenye mikoa yetu na wilaya zetu kwenye upande wa barabara za *TANROADS* tumekuwa tukiwasiiliana kupitia Meneja wa Mikoa. Tunaenda kwenye maeneo ambayo mawasiliano yamekatika na kujaribu kulingana na mazingira yanavyoruhusu kurudisha mawasiliano ya Barabara.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyojadiliwa na Waheshimiwa Wabunge dosari zimekuwa kubwa, na tulichokifanya Wizara ya Ujenzi, tumefanya tathmini ya athari ya Mvua za *El Nino* mikoa yote na kubainisha hasara ya shilingi bilioni 200 ambayo imetokana na kuharibika kwa miundombinu ya barabara na madaraja. Kutokana na mvua kwa vile zinaendelea kunyesha, yapo masuala ya kitaalamu wahandisi mlioko humu mtaelewa. Kuna mambo ambayo tunaweza tukayafanya kurudisha mawasiliano ya barabra wakati mvua zinaendelea kunyesha.

Mheshimiwa Spika, yapo masuala ambayo inabidi tusubiri mvua zitakapokatika ili tuweze kuendelea na ujenzi kuweza kurudisha miundombinu hii kama ilivyokuwa kabla mvua haijanyesha. Tulichofanya kama nilivyosema ni tathmini ili tuweze kurudisha miundombinu hii kama ilivyokuwa, inahitajika kiasi gani? Jibu ni kwamba ni shilingi bilioni 200 zinahitajika.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Fedha tukaangalia, wakati tunaendelea na kurudisha mawasiliano kwa wananchi, mfuko wa *emergency* Serikali imeendelea kutupatia fedha na ndiyo maana *regional managers* unapowataka waende *site,* wakandarasi wanaenda na kufanya linalowezekana huku tukiendelea kusubiri mvua za *El Nino* ziishe ili tuweze kurudisha miundombinu hii kwa mpango wa kudumu kwa bajeti ya shilingi bilioni 200.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, naishukuru Serikali kupitia Wizara ya Fedha kwenye shilingi bilioni 200 tuliomba shilingi bilioni 66 tuendelee kutumia mfuko wa dharura kurudisha miundombinu hii wakati wa kipindi cha mvua. Mheshimiwa Mwigulu Waziri wa Fedha anaendelea kutuletea fedha ili *regional managers* wa *TANROADS* wanapohitaji kwenda ku-*respond* Waheshimiwa Wabunge mnapotupigia simu, mfuko huu wa fedha wa dharura uendelee kutoa huduma kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuendelea kuwaelekeza *Regional Managers* wa *TANROADS,* yapo maeneo ambayo kila mvua zinaponyesha kila mwaka huwa yana ukorofi ule ule. Kwa hiyo, nimeelekeza tusirudie hali hii kila mwaka na wakati tayari tumeshajua changamoto. Kwa mfano pale Mtanana, kila mwaka maji huwa yanavuka Barabara, lakini tumeenda pale, tumefanya usanifu wa kina Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan akatoa maelekezo, sasa hivi tuna mkandarasi anajenga kilometa sita.

Mheshimiwa Spika, sasa hata Mvua za *El Nino* zikinyesha kila mwezi au kila mwaka kwa namna ambavyo tunakwenda kujenga pale Mtanana kilometa sita tutainua barabara na kuijenga kwa

kilometa sita ili makalvat makubwa yapite chini ya barabara. Mvua zikinyesha ina maana mawasiliano ya barabara yanaendelea kuwepo. Tumebainisha maeneo kama hayo nchi nzima.

SPIKA: Haya, ahsante sana.

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wawe na subira, tumeshabainisha bajeti na Serikali ipo kazini, tutaendelea kujipanga ili kurudisha mawasiliano haya ya Barabara.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba na mtoa hoja ajiandae.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Nami nianzie kwa kusema kwamba Serikali inaungana na Wabunge kwenye hoja hii makini kabisa inayohusu kushughulikia miundombinu iliyoharibiwa na mvua. Hiki ambacho Bunge lako limekileta hapa kinaonesha tu ni kiasi gani Bunge hili ni Bunge la Watanzania. Ni Wabunge wanaoguswa na hoja za wananchi na Wabunge wanaofuatilia kila siku mambo yanayotokea majimboni mwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi kama Serikali tumeyaona haya mapema sana na Mheshimiwa Rais alitoa tamko katika moja ya siku za mwanzoni tu baada ya mvua kuwa zimeanza. Akatuelekeza Wizara tukatoa hizo fedha. Tumetoa fedha kwa mafungu kama ambavyo Naibu Waziri hapa amesema. Mwanzo tukatoa ile 21 iliyokuwemo na sasa tumetoa 30.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kinachojitokeza ni nini? Ukiachilia mbali mvua kubwa zilizonyesha, kinachojitokeza ni kwamba baada ya kuwa tumeshaongeza sana fedha kwenda kwenye Barabara, tumekuwa na barabara nyingi zenye urefu mkubwa. Maana yeke ulipokuja pia uharibifu,

uharibifu wake ni mkubwa kuliko barabara zilizokuwa na bajeti ya shilingi bilioni 200.

Mheshimiwa Spika, kinachojitokeza sasa hivi ambacho tunaumiza vichwa hapa na mwenzangu Waziri mwenye dhamana ya ujenzi na Waziri wa TAMISEMI, ni namna gani tutaongeza fedha kwa ajili ya matengenezo zinapotokea hizi dharura? Tumezitengeneza barabara ndiyo, lakini tunapokuwa na barabara ndefe zaidi, uharibifu unapotokea maana yake bajeti ya matengenezo na yenyewe ni kubwa zaidi. Kwa kipindi kirefu, hii miaka ambayo tumefanya hivi, tulikuwa tunafanya zaidi kufungua zile barabara.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, hata ninyi ni mashahidi, mtakubaliana kwamba katika kipindi cha miaka mitatu barabara za changarawe vijijini zilizofunguliwa ni ndefu sana. Leo hii mvua zilizonyesha isingekuwa bajeti hii ya takriban shilingi trilioni moja na bilioni 300 ambayo ni takribani shilingi trilioni tatu na kitu, tungekuwa tunaongelea kwamba mvua zimeharibu mashamba. Yaani zingekuwa zimeharibu mashamba tu, mapalio mapalio ambayo tusingeulizana hapa kwa sababu yangekuwa mashamba tu na mapalio, tusingeulizana kwamba barabara zimeharibika. Kwa urefu ule, ndiyo huo huo unaosababisha kwamba uharibifu leo uwe mkubwa sana. Sasa rai yangu…

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Spika, taarifa.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, rai yangu kwa Waheshimiwa Wabunge...

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kuna taarifa kutoka kwa Mbunge wa Momba, Mheshimiwa Condester.

TAARIFA

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Fedha anaeleza vizuri sana. Miongoni mwa hoja ambazo Wabunge waliochangia walizokuwa wanamwambia, swali letu kwanza tunawauliza hivi, pesa za bajeti

ambazo tulitenga kwenye mwaka huu wa Bajeti 2023/2024 ni shilingi bilioni 808. Mpaka sasa hivi Wizara wamepeleka pesa shilingi bilioni 89 ambayo ni sawa asilimia 12.

Mheshimiwa Spika, swali letu ni kwamba, anapoongelea upana wa barabara zimeongezeka, tunakubali hizo pesa kwanza tulizotenga ambazo sasa hivi ni mwezi wa pili tumebakisha mwezi wa tatu, wa nne, wa tano na wa sita tufunge bajeti, miezi minne kati ya miezi 12, kwa nini kwanza hajapeleka? Zingekuwa zimeenda kutengeneza hizo barabara?

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ana swali la msingi sana na mimi…

SPIKA: Mheshimiwa Waziri unaipokea taarifa hiyo iliyokuja kwa njia ya swali?

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa ya Mheshimiwa Mbunge, ana hoja ya msingi sana. Mimi siyo *engineer* Mheshimiwa Mbunge, ma-*engineer* wanatuambia hivi, kukitokea mvua kubwa zinaathiri kazi ya ujenzi, na sisi Wizara ya Fedha hatufanyi kazi tu ya kugawa fedha tu, tunalipia kazi zinazofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kazi zimesimama, Bunge lako ndiyo linalotuelekeza, likituelekeza tupeleke tu fedha Wizarani hata kama kazi haziendelei, nyinyi ndiyo mnaotusimamia hapa, lakini utaratibu wa ujenzi ni kwamba mvua kubwa zinaponyesha kazi nyingi zinasimama, zimeathirika, hata wakulima tu wanaathiriwa na mvua zikiwa nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tulishapeleka shilingi bilioni 300 na fedha ya *TARURA* iko zaidi ya shilingi bilioni 600, fedha zipo za TARURA, ni mfuko ziko *ring-fenced* lakini mvua zimeharibu. amesema pale.

Mheshimiwa Spika, katika kumalizia nasisitiza maagizo aliyoyatoa Mheshimiwa Rais, wataalam wetu, ma-*engineer* wetu na Mheshimiwa Lusinde, profesa, amesema pale na Mheshimiwa

Kanyasu umefika wakati wa kubadilisha utaratibu wetu tuliokuwa tunajenga barabara, twende kwenye kujenga barabara zinazodumu. Kwa utaratibu huu ambao tunajenga barabara nyingi sana, ndefu sana kama zitakuwa zinaharibika kuna siku tutakuja kupata *collapse* ya kila eneo na tutakuwa na kazi ngumu sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, angalau tuanze na maeneo korofi, yote tuyawekee barabara za kudumu ili mvua zikinyesha tuwe na uhakika. Waheshimiwa Wabunge nyinyi ni mashahidi, mnatoka kule vijijini, hakuna barabara yenye ujanja wa kustahimili maji. Barabara ya changarawe ikija mvua kubwa sana na barabara ikawa haina mifereji itasombwa tu. Tunaweza tukawa tunafanya kazi ya kupeleka fedha nyingi, ikija mvua moja kubwa inasomba fedha zile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nadhani ni wakati wa kuitikia agizo lile alilotoa Mheshimiwa Rais la kuangalia teknolojia mpya. Hata kama ni vijijini, tujenge barabara ambazo zinadumu ambazo zinaweza zikastahimili masuala haya ya mvua zinazokuja. Pia, zinazodumu zitupe fursa ya kupumua kidogo kuweza kutengeneza maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Bunge lako Tukufu lipokee, sisi kama Serikali hii ni *concern* kubwa sana na fedha tumetenga. Sasa hivi kwa kuwa baada ya mwezi mmoja tunakuja hapa Bungeni, hata hizi fedha tunazoongelea leo zilitokana na matatizo kama haya, tukakubaliana Bungeni tukaweka tozo ya mafuta tukaongeza bajeti.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tumeshaongea na mwenzangu hapa tunatengeneza fungu lingine ambalo litakuja kwa ajili ya *maintenance*, tunatengeneza, tutakuja kulitaja kwenye Bunge hili na tutaomba mtupitishie. Tuwe na fungu kubwa la *maintenance* ili barabara zikiharibika isisubiriwe kukata mafungu mengine ili kuweza kutengeneza barabara zilizoharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili tunaliangalia, tutaongeza bajeti ya *TARURA* na tutaongeza bajeti ya *TANROADS*. Pia,

tutaongeza ile ya *maintenance* ili barabara zinapoharibika kuwe na fedha ambazo zimetengwa, lakini la msingi sana….

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

WAZIRI WA FEDHA: ….na Waziri yuko hapa tuendelee kutengeneza barabara ambazo….

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

WAZIRI WA FEDHA: …zitakuwa na uimara zaidi ili kupunguza…

SPIKA: Nani mtoa taarifa?

WAZIRI WA FEDHA: …matatizo haya yanayojitokeza baada ya mvua kuwa zimenyesha. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kuchauka.

TAARIFA

ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, nataka kumpa taarifa Mheshimiwa Waziri, anasema vizuri sana. Labda mimi uniambie kwamba kwa sababu watabiri wa hali ya hewa walisema kutakuwa na mvua nyingi za *El Nino* ndiyo maana hizi fedha shilingi bilioni 800 hazikwenda *TARURA* walikuwa wanasubiri kipindi hiki cha maafa ndiyo wazipeleke. Kwa sababu bajeti ilipitishwa mwezi wa Saba mpaka Disemba hela haijaenda na mvua zimeanza Disemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, waseme labda kwamba walikuwa wanasubiri baada ya watu wa hali ya hewa kusema kutakuwa na mvua kubwa wakaacha ile hela wasubiri kuzileta leo. *(Makofi/Kicheko)*

SPIKA: Mheshimiwa Mwigulu, unapokea taarifa hiyo?

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, taarifa hii naipokea na mimi nitaomba tu hizi Kamati ambazo zinasimamia masuala ya barabara labda tufanye semina pia. Fedha haziendi shilingi bilioni 800 zote zinaenda *TARURA*, fedha zinakwenda kwa *certificate*.

SPIKA: Haya Mheshimiwa Waziri wa Fedha umeeleweka, swali, ngoja Mheshimiwa…

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, mvua za nchi hii hazianzi kwa siku moja zina majira tofauti tofauti…

SPIKA: Ngoja Mheshimiwa, mpaka sasa pesa zimeenda kiasi gani, za *TARURA*? *(Makofi)*

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, ni shilingi bilioni 300 na…wameshapokea shilingi bilioni 309 mpaka sasa na sasa hivi tumetoa *P4R* 350 na zenyewe tunatoa kwa *certificate* hivyo hivyo, zita kuwa 700. Tunaamini kazi inavyokamilika, mvua zikishaachia nafasi kidogo watamaliza kwa sababu wakandarasi wametapakaa nchi nzima. *(Kicheko)*

SPIKA: Ngoja, hii shilingi bilioni 309 ni sehemu ya fedha zinazopelekwa kwa dharura au hizi ni zile za bajeti halafu za dharura ni tofauti na hizi?

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, ni za bajeti ya kawaida, walizoomba za dharura ni kama shilingi bilioni 66 hivi, shilingi bilioni 21 wameshapokea na nadhani leo watapokea shilingi bilioni 30 kwenye ile shilingi bilioni 66.

SPIKA: Sawa ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge wale waliopata nafasi wote mmeshachangia sasa namkaribisha mtoa hoja ahitimishe hoja yake.

Mheshimiwa Jafari Chege.

JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote kwanza nachukua nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu ambao

wamepata nafasi ya kuchangia. Hata wale ambao walionyesha nia ya kuchangia lakini kwa sababu ya muda hawakupata nafasi hiyo. Naamini jambo hili linagusa Wabunge wote na kama muda ungekuwa unaruhusu naamini Wabunge karibu wote, asilimia 90 kama siyo asilimia 100 wangepata nafasi ya kuchangia changamoto hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee sana nachukua fursa hii kuwashukuru wale ambao wameweza kusema kwa niaba ya Wabunge wengine. Pia, nachukua nafasi hii kushukuru kwa majibu ya Serikali, kwa maana ya Waheshimiwa Mawaziri, kwa kupitia zile hoja ambazo zimezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge lakini na kusudio la mtoa hoja. Nachukua nafasi hii kuwashukuru kwa majibu mazuri kwa namna ambavyo wameweza kujibu.

Mheshimiwa Spika, hoja hapa kwanza naweka sawa sawa, barabara inagusa uchumi wa kila Mwananchi kwenye maeneo yote tunayotoka. Barabara pia ni sehemu ya kuimarisha na kujenga siasa ya maeneo yote tunayotoka. Pia, barabara pamoja na miundombinu mingine inatusaidia kwenye shughuli mbalimbali za kijamii kwa maana ya kwamba hakuna namna ambavyo unaweza kuzungumza barabara ukaiondoa bila kumgusa Mwananchi mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, tunavyozungumza hapa hatukatai na kama Waheshimiwa Wabunge wanavyochangia, tunaungana na kazi kubwa inayofanywa na Mheshimiwa Rais ya kuhangaika na kutafuta fedha kwa ajili ya kwenda kutengeneza barabara, hilo hatuna shaka nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuna shaka pia na fedha zinazotengwa kwenye bajeti mbalimbali ndani ya Bunge hili kwenda kwenye kurekebisha mambo mbalimbali kwenye sekta zingine pamoja na barabara hii. Changamoto yetu sisi ni pale ambapo tunatenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali na fedha ile haifiki kwa wakati, hii ndiyo changamoto inapokuja shida.

Mheshimiwa Spika, kwamba tumetenga fedha ndiyo na Serikali imeongeza fedha kutoka shilingi bilioni 300 anazosema kwenda shilingi bilioni 800 kwa ajili ya barabara lakini fedha hazifiki kwenye maeneo kwa wakati na hii ndiyo changamoto. Kwa hiyo, Waheshimiwa Mawaziri, hata tukizungumza kwa uzuri gani kwamba fedha imeongezeka kutoka shilingi bilioni 300 kwenda shilingi bilioni 800 na ushee. Kama haiendi kwa wananchi, bado haionekani na hatuwezi kupata matunda tunayokusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hoja yetu hapa ambacho tunataka Mheshimiwa Waziri atusaidie na kimsingi ndiyo itakuwa Azimio la mtoa hoja la kwanza; ni kuhakikisha angalau Waheshimiwa Mawaziri wa sekta pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Fedha shilingi bilioni 818 iliyotengwa kwa ajili ya kupelekwa hata kama siyo yote ihakikishe inakwenda kwa ajili ya ujenzi wa barabara ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakwenda robo ya pili ya bajeti, imekwenda asilimia 12 peke yake, tumebakiza mwezi mmoja tunakwenda kujadili bajeti ya awamu inayofuata lakini umepeleka asilimia 12 pekee yake. Hauwezi kutoa utetezi wa hoja hii kwa sababu ya mvua, tulikuwa tuna miezi sita ya utekelezaji, kuna wakandarasi wamekwishafanya kazi huko wanadai, ukirudi Mbunge ukiwaambia nyinyi mtaendelea kudai kwa sababu ya mvua, Wizara ya Fedha haikuleta fedha TAMISEMI mlipwe kwa sababu ya mvua hii inakuwa haikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha watusaidie kupeleka fedha huko ili angalau barabara hizi zitangazwe, wakandarasi walipwe na kazi iweze kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, Bunge hili linatazamwa na wananchi wote, Waziri wa Fedha alisimama hapa akatuahidi ndani ya Bunge hili na mimi hili ndiyo linanipa ukakasi, narudi kuwaambia nini wananchi. Kwamba fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya urekebishaji wa barabara wa dharura kabla ya Bunge hili kuahirishwa ambayo ni kesho, ndugu zangu wananchi mtulie zitakuwa zimefika maeneo yenu, ndiyo jibu ambalo limetoka.

Mheshimiwa Spika, ukizungumza leo na *TARURA* leo nimepiga simu hapa asubuhi kabla sijaleta hoja yangu. Mkurugenzi wa *TARURA* anasema fedha waliyoomba ni shilingi bilioni 131, fedha waliyopokea ndiyo hii ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI amesema, shilingi bilioni 21. Shilingi bilioni 130 na shilingi bilioni 21 angalia hiyo fedha huo ulinganifu wanakwenda kufanya dharura kwa barabara ipi? Wanaacha barabara ipi? Wanajenga daraja lipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, maana yake ninachosema, na hapo Mheshimiwa Waziri ameshaahidi ndani ya Bunge kwamba huko mnakokwenda ndugu zangu wananchi tulieni fedha hizi zinakwenda. Umetoa shilingi bilioni 21 imeshamalizika. Tunataka Mheshimiwa Waziri ukatusaidie hii fedha, Waziri wa Fedha atusaidie sana, tunajua anahangaika, shilingi bilioni 131 toa shilingi bilioni 21 fedha hii ahakikishe imekwenda kwa ajili angalau ya kukamilisha ungwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Azimio la tatu, kuna fedha ambayo ilizungumzwa ndani ya Bunge hili, ongezeko la shilingi bilioni 350 kutoka shilingi bilioni 818 kwenye bajeti, haipo. Yaani shilingi bilioni 18 yenyewe haijaenda, shilingi bilioni 350 haijaenda, tunasema kwamba tunasubiri mvua, zitakwenda lini hizi? Hili natamani sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa sekta waweze kutuambia.

Mheshimiwa Spika, la nne, wizara itusaidie kufanya tathmini ya barabara hizi ambazo kila mwaka zinatengenezwa. Barabara za udongo, kuna barabara ambazo kila mwaka zinapelekewa fedha zaidi ya shilingi milioni 100, shilingi milioni 20. Ukienda mwaka unaofuata shilingi milioni 100, shilingi milioni 20 mwaka unaofuata, wafanye tathmini, hakuna sababu ya kutengeneza hizi barabara kila mwaka za udongo. Wazibadilishe ziwe barabara za changarawe ili wapunguze fedha hizi kila mwaka zinakwenda zinamwaga pale na mwaka unaokuja tena mnamwaga fedha nyingine. Kwa hiyo, nafikiri hii Wizara ya sekta kwa maana ya TAMISEMI wafanye hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, ni Wizara ya Fedha pamoja na Wizara husika kuchukua tahadhari pale ambapo wenzetu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa wanapotoa tathmini ya maboresho au marekebisho ya hali ya hewa nchini. Kwa sababu nilitegemea lile lilipotoka tayari na sisi tungetenga fedha ya dharura moja kwa moja kwamba tunategemea hili litatokea, madaraja yatakatika, barabara hazitapitika, moja kwa moja fedha ya dharura ilitakiwa iende kwa sababu barabara zile kuharibika kwake zinamgusa mwananchi mmoja mmoja wa kule kijijini na Mwananchi wa maeneo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokutenga fedha na wakati tayari taasisi ya Serikali imetoa tathmini namna mvua inavyokwenda tunakuwa hatuwatendei haki wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa haya maazimio matano naomba kubwa kabisa ni kuhakikisha fedha zinakwenda ili na sisi tunapokwenda majimboni tuwe na jibu zuri la kuwaelewesha wananchi na wananchi wetu kimsingi watatuelewa kwa sababu fedha kama itakuwa imekuja lakini siyo kuwaambia kwamba fedha haijaenda kwa sababu ya mvua.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Sasa Waheshimiwa Wabunge kabla sijawahoji lazima tujue tunachofanya maamuzi ni kipi. Hebu niletee hayo Maazimio uliyonayo hapo. Wakati huohuo naomba ufafanuzi ili maazimio yetu yakae vizuri. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kama nimeelewa vizuri, maombi yaliyokufikia kutoka TAMISEMI kuhusu dharura ni shilingi bilioni 66, nimeelewa sawa sawa?

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, shilingi bilioni 66 ni *TANROADS* halafu shilingi bilioni 65 ni *TARURA*.

SPIKA: Ahaaa, shilingi bilioni 66 ni *TANROADS*?

WAZIRI WA FEDHA: *TANROADS*.

SPIKA: Halafu shilingi bilioni 65 ni *TARURA*?

WAZIRI WA FEDHA: *TARURA*.

SPIKA: Hizi shilingi bilioni 21 zimetolewa kwa nani?

WAZIRI WA FEDHA: Zimetolewa *TARURA*.

SPIKA: *TARURA* kati ya zile shilingi bilioni 65.

WAZIRI WA FEDHA: Shilingi bilioni 65

SPIKA: Halafu shilingi bilioni 30 zinazotoka leo ama kesho?

WAZIRI WA FEDHA: Shilingi bilioni 30 tunajaziliza *TARURA*.

SPIKA: Zinaelekea *TARURA*?

WAZIRI WA FEDHA: Ndiyo.

SPIKA: Kwa hiyo, *TARURA* jumla ya fedha zilizoombwa ni shilingi bilioni 65?

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, shilingi bilioni 65.

SPIKA: Ambazo zitakuwa zimetolewa mpaka kesho ni shilingi bilioni 51?

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, shilingi bilioni 51.

SPIKA: Ahsante, halafu *TANROADS* shilingi bilioni 66?

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, *TANROADS* shilingi bilioni 66.

SPIKA: Wao zimeshaanza kwenda ama bado?

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, kuna matatizo ya mambo ya vifungu ilikuwa itoke…*(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tusikilizane.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, ngoja tusikilizane, ilikuwa vifungu vya…

SPIKA: Hata hivyo, Mheshimiwa Chege samahani, nataka tuliweke Azimio letu vizuri. Mheshimiwa Chege, mwenye hoja, ile uliyosema shilingi bilioni 131 ulikuwa umechanganya za *TANROADS* na *TARURA* pamoja?

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Spika, ndiyo.

SPIKA: Haya, hoja yako ya msingi ilikuwa inahusu *TARURA* na *TANROADS* ama ilikuwa inahusu barabara za *TARURA*?

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Spika, barabara zote kuna baadhi ya maeneo *TANROADS* zimeharibika na kuna baadhi ya maeneo *TARURA* zimeharibika kwa hiyo ni barabara zote kwa ujumla wake. *(Makofi)*

SPIKA: Sasa hapa, kwa sababu kwanza hizi ni Wizara mbili tofauti. Sasa hii hoja yetu lazima tujue Azimio tunaazimia la sura gani. Hatuwezi kuazimia, yaani kama Bunge, tukaazimia maazimio ambayo utekelezaji wake kuna watu watakuwa wanavutana mahali.

Hoja yako ya mwanzoni kabisa uliyoisema kabla ya haya maazimio ilikuwa inahusu *TARURA* ama ilikuwa inahusu zote mbili? Hoja yako ya mwanzo kabisa.

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Spika, hoja yangu ya mwanzo kabisa nilikuwa nimejikita kwenye barabara kwa maana ya kwamba kuna baadhi ya barabara ambazo ni *TARURA* na baadhi ya barabara ambazo ni *TANROADS*.

SPIKA: Barabara zote?

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Spika, ndiyo barabara zote lakini nikawa nimetoa mfano zaidi kwenye barabara za *TARURA*.

SPIKA: Sawa imeeleweka. Mheshimiwa Waziri kama nimeelewa vizuri shilingi bilioni 309 zimeshatolewa kuelekea *TARURA* kati ya ile bajeti ambayo ilipitishwa na Bunge?

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, ndiyo hizo ni za bajeti ya kawaida.

SPIKA: Shilingi milioni 309?

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, shilingi milioni 309.

SPIKA: Halafu shilingi bilioni 350 ni zile ambazo zinategemea utendaji kazi wa zile shilingi bilioni 309?

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, hapana.

SPIKA: Si ndiyo hii umesema *P4R*?

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, hiyo ni nyongeza ni tofauti na bajeti. Ni tofauti na hizi ambazo kazi zinaendelea, hizo ni kazi mpya ambazo zitatangazwa majimboni na zitatoka kwa *certificate*.

SPIKA: Haya, Waheshimiwa Wabunge, Maazimio hapa yako matano. Ili Bunge tujue tunaamua kwenye jambo gani la kuiambia Serikali kabla sijatoa hoja kwenu kuhojiwa.

La kwanza, linasema fedha zilizopangwa na kutengwa na Serikali kwa *TARURA* ziende, shilingi bilioni 818. Kwa maelezo yaliyotolewa hapa na Mheshimiwa Waziri ni kwamba hizi fedha zimeshaenda shilingi bilioni 309 na zile za dharura ambayo ndiyo hoja ilikuwa hapo, hoja ya dharura ilikuwa inaongelea jambo la dharura ilikuwa haizungumzii utekelezaji wa bajeti. Lazima hapo tuelewane vizuri, ilikuwa inahusu dharura kwenye barabara sasa

hili la kwanza linaondoka kwa sababu linahusu kutengwa kwa fedha kwenye bajeti kwa hiyo, hili linakuwa halipo.

La pili, linasema fedha alizoahidi Mheshimiwa Waziri kwamba zitatoka fedha za dharura kabla ya Bunge hili kukamilika. Mheshimiwa Waziri hapo amesema shilingi bilioni 21 zilishaenda na shilingi bilioni 30 zinakwenda leo ama kesho?

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, *actually* hivi tunavyoongea nikiongeza taarifa kwa undani zaidi hizi ziko tayari *BOT* zinasubiri tu kwenda kwenye mfuko. *(Makofi)*

SPIKA: Haya, kwa hivyo katika shilingi bilioni 131 zilizokuwa zimeombwa shilingi bilioni 21 zishalipwa na shilingi bilioni 30 ziko njiani zinaenda kwenye barabara za *TARURA*. Kwa hiyo, ahadi ya Mheshimiwa Waziri maana yake imetekelezwa. Sasa cha kufanya, kwa sasabu leo ni Alhamis kesho ni Ijumaa, mchakato ule wa *BOT* kati ya leo na kesho nadhani baadhi ya halmashauri zitakuwa zimeshaanza kupata hizi pesa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kesho hapa ndani tutajiridhisha, watu wapige simu huko kwa wakurugenzi, wangapi zimeshafika ili hili tuwe tumeondokana nalo. *(Makofi)*

Haya, la tatu linahusu ongezeko la fedha shilingi bilioni 350 ziende, hili nalo shilingi bilioni 350 siyo fedha za dharura. Hizi ni fedha ambazo zinaenda maana yake ni utendaji kazi ule wa kawaida. Kazi zitangazwe watu wakafanyie kazi. Kwa hiyo, hili nalo hatuwezi kuazimia kama Bunge, watu wakafanye kazi kwa utaratibu wa kawaida.

Kufanya tathmini ya barabara za udongo kuanza kuwekwa changarawe ili zisiharibike halafu kuchukua tahadhari za waleta taarifa za kitaalam zinazotakiwa kutenga fedha mapema kwa ajili ya hili, sawa.

Sasa hili azimio letu hapa jamani hapa litatoka moja tu kati ya haya maazimio matano kwa sababu lingine ni utendaji wa kawaida wa Serikali. Namna ambavyo sisi tunakuwa, Serikali imeleta mapendekezo, sisi tumepitisha bajeti, kwa hiyo,

utekelezaji wa bajeti ni wa kawaida. Ufuatiliaji wake unakuja tutakapoanza mjadala wa kipindi cha Bunge letu la bajeti. Kwa sababu tunaangalia utekelezaji wa bajeti iliyopita na bajeti inayokuja.

Kwa hiyo, kwenye hoja ya Mheshimiwa Chege Azimio litakalotoka Bungeni linahusu shilingi bilioni 131, shilingi bilioni 66 za *TANROADS*, shilingi bilioni 65 za *TARURA*. Katika shilingi bilioni 65 za *TARURA* zitakuwa zimeshatoka shilingi bilioni 51. Kwa hiyo, maana yake wapo katika utekelezaji wa haraka zaidi kuliko upande wa *TANROADS*.

Kwa hiyo, Azimio litatoka moja na siyo matano kama alivyokuwa ameyapanga Mheshimiwa Mbunge. Ili twende na hoja yake ya msingi na iweze kuwa imefanyiwa kazi kwa mujibu wa Kanuni ya 54 na masharti yaliyowekwa kwenye Kanuni ya 55, lazima iwe ni ya dharura na iwe ni inahusu jambo mahususi ambalo haliwezi kufanyiwa kazi katika utaratibu wa kawaida. Yale yote yaliyo katika utaratibu wa kawaida Serikali itaendelea na utekelezaji wake ule wa kawaida.

Kwa hiyo Azimio la Bunge sasa litakuwa kwamba, Serikali ikamilishe utoaji wa fedha za dharura kama zilivyoombwa na *TANROADS* na *TARURA*. *(Makofi)*

Sasa haya mengine yaliyotolewa hapa kwamba ichukue tahadhari wakati wa Taarifa, haya haliwezi kuwa Azimio, kwamba wachukue tahadhari, kwa sababu Azimio lazima tuwe tunaweza kulipima, kama hatuwezi kulipima sasa kidogo itakuwa changamoto. Hii kufanya tathmini ya barabara, huu ni ushauri ambao Serikali mnapaswa kuuchukua. Kwa hiyo Azimio la Bunge ni hilo Serikali itoe fedha za dharura kama ambavyo nimeeleza hapo awali.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji kuhusu Azimio hilo la Bunge ili Serikali ijue ni nini inachokwenda kufanya.

Waheshimiwa Wabunge, wanaoafiki Azimio hilo nililolisema linalohusu Hoja ya Dharura ya Mheshimiwa Jafari Chege kuhusu

Barabara zilizoharibika hapa nchini zinazohusu *TARURA* na *TANROADS*. Wote mmeafiki, azimio limepita.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika, Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Azimio letu hilo tumeshalipitisha kwa hivyo Serikali imeshalisikia na itaenda kulifanyia kazi, pesa zilizoombwa na *TARURA* shilingi bilioni 65 zikamilishwe, lakini pia pesa zilizoombwa na *TANROADS* Serikali izipeleke.

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana, tumefika mwisho wa mjadala wetu kuhusu Azimio.

Mheshimiwa Musukuma, kuna Kanuni ilivyovunjwa, ni ipi? Nimekusikia unasema Mwongozo yaani kwamba kuna Kanuni, kuna jambo fulani hivi limefanyika hapa ambalo kikanuni unataka kujua linaruhusiwa ama haliruhusiwi, karibu.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, hapana hakuna Kanuni iliyovunjwa ila nilikuwa nataka kupata Mwongozo wako kwenye suala ambalo linaendelea la dharura.

SPIKA: Dharura nyingine? Dharura walipewa watu watatu waliokuwa wamesimama wakati huo walipopewa nafasi. Nikisema leo niruhusu dharura tu siku nzima, kuna hoja ziko mbele yetu…

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, mimi langu halihusu *TARURA*.

SPIKA: Hapana, siyo kuhusu *TARURA*, wameruhusiwa Wabunge watatu kuhusu Hoja za Dharura na wakati huo hukuwa umesimama Mheshimiwa Musukuma. Kwa hiyo, kwa Kanuni zetu zinataka mara baada ya Kipindi cha Maswali. Sasa kama kuna

hoja nyingine, unatumia Kanuni nyingine. Ukija na hii ya dharura, nimesharuhusu tatu na zinatosha kwa leo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania wa Mwaka 2024 *(The Law School of Tanzania (Amendment) Bill, 2024)*

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Muswada huo umesomwa kwa mara ya kwanza, Katibu.

NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ushindani wa Mwaka 2024 *(The Fair Competition (Amendment) Bill, 2024)*

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Muswada mwingine huo umesomwa kwa mara ya kwanza.

Katibu.

NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2024 *(The Social Security Laws (Amendments) Bill, 2024)*

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Muswada mwingine huo umesomwa kwa mara ya kwanza.

Katibu.

NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024)*

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Miswada hiyo imeshasomwa kwa mara ya kwanza; Miswada minne, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania wa Mwaka 2024 *(The Law School of Tanzania (Amendment) Bill, 2024),* Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria watashughulikia Muswada huu.

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ushindani wa Mwaka 2024 *(The Fair Competition (Amendment) Bill, 2024),* Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, itashughulikia Muswada huu.

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2024 *(The Social Security Laws (Amendments) Bill, 2024),* Kamati ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, watashughulikia Muswada huu.

Vilevile, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024),* Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria, watashughulikia Muswada huu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, Miswada hiyo imeelekezwa kwenye hizo Kamati ambazo nimezitaja, na sasa tunaendelea na utaratibu wetu.

Katibu.

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA KAMATI

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023
na
Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama ilivyo ada sasa namuita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali, Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, aje awasilishe Hoja ya Kamati yake; Mheshimiwa Mwenyekiti. *(Makofi)*

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa yetu ya *PAC*.

Mheshimiwa Spika, utangulizi; awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia zawadi ya uhai na hivyo kuwa na fursa ya kukutana hapa siku ya leo. Kwa heshima kubwa naomba kuwasilisha Taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya *PAC* zilizotekelezwa katika kipindi cha mwaka 2023. Naomba taarifa yangu yote iingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, katika kutimiza madhumuni hayo, taarifa hii inagusa uchambuzi wa Taarifa za Kaguzi za Kiufundi *(Technical Audits)* na Kaguzi za Ufanisi *(Perfomance Audits)* kama zilivyokaguliwa na *CAG* kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022. Vilevile taarifa hii inahusu ziara za ukaguzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo iliyotekelezwa na Serikali. Aidha, Taarifa hii imefafanua kuhusu mafunzo na semina za kuwajengea uwezo Wajumbe wa *PAC*.

Mheshimwa Spika, majukumu ya *PAC* yamebainishwa katika kifungu cha 13 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za

Bunge, Toleo la Februari, 2023. Kwa mujibu wa kifungu hicho, Kamati ina majukumu yafuatayo: -

(a) Kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma katika Wizara za Serikali na Mashirika ya Umma yaliyoainishwa katika Taarifa za CAG;

(b) Kufuatilia utekelezaji wa Mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati hii kuondoa matatizo yaliyobainika kwa mujibu wa kanuni hii; na

(c) Kutoa mapendekezo na ushauri kwa Wizara za Serikali na Mashirika ya Umma kuhusu matumizi mazuri ya fedha za umma ili kupunguza au kumaliza matumizi mabaya ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, msingi wa majukumu hayo unatokana na taarifa ya hesabu zilizokaguliwa na *CAG* kama ilivyobainishwa katika kifungu cha 15 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwezi Januari, 2023 hadi Februari, 2024, *PAC* ilitekeleza shughuli kuu nne kama ifuatavyo: -

(a) Kupitia na kuchambua Taarifa za Ukaguzi wa Ufanisi na Ukaguzi wa Kiufundi kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022;

(b) Ukaguzi wa Miradi mbalimbali ya Maendeleo inayotekelezwa na Serikali Kuu na Mashirika ya Umma;

(c) Kupitia na Kuchambua Ripoti za *CAG* kwa Ukaguzi wa Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022; na

(d) Mafunzo na Semina mbalimbali za kuwajengea uwezo Waheshimiwa Wahjumbe wa Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi wa ukaguzi wa ufanisi na kaguzi za kiufundi; kwa kipindi cha shughuli za Kamati cha kuanzia tarehe 15 Januari, 2024 hadi tarehe 25 Januari, 2024, Kamati ilijielekeza katika kupitia na kujadili Taarifa za Kiufundi *(Technical Audits)* na Kaguzi za Ufanisi *(Perfomance Audits)*. Taarifa hizi zilitokana na kaguzi zilizokuwa zimefanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanikiwa kupitia na kujadili jumla ya taarifa kumi na mbili za ukaguzi wa ufanisi na wa kiufundi. Aidha, Kamati ilifanya mahojiano na Maafisa Masuuli wanaosimamia mafungu husika yaliyoguswa na Taarifa hizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu matokeo ya uchambuzi wa Taarifa hizo kumi na mbili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu Taarifa ya Ukaguzi wa Kiufundi kuhusu Ujenzi wa Ukarabati wa Meli; Kamati ilipitia na kuchambua Taarifa ya Ukaguzi wa Kiufundi kuhusu Ujenzi na Ukarabati wa Meli na kubaini masuala yafuatayo:-

(a) Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi wakati huo ilianzisha mradi wa ujenzi wa meli bila ushahidi wa wazi wa uchunguzi wa awali. Hatua za awali za ujenzi huo zilikuwa za dharura na kusababisha kutokuwepo maandalizi ya kutosha;

(b) Kampuni ya Huduma za Meli haikufanya upembuzi yakinifu kwenye ujenzi wa meli mpya;

(c) Ujenzi wa meli ulianza bila kitanda cha kujengea meli *(slipway)* hivyo kusababisha Kampuni ya Huduma za Meli kuingia mikataba miwili ya ujenzi wa meli mpya na ujenzi wa kitanda cha kujengea meli *(slipway)* kwa wakati mmoja. Hali hii ilisababisha uhitaji wa ongezeko la muda wa kazi kwa miezi mitano ambao uliambatana na gharama ya dola za Marekani milioni 3.4 bila *VAT*.

(d) Vilevile ukaguzi ulibaini kuchelewa kukamilika kwa mradi kwa ujenzi wa meli ya MV Mwanza. Ongezeko la muda lilisababisha ongezeko kwa gharama za mradi kwa dola za Marekani milioni 7.9 kutoka kiwango kilichopangwa cha dola za Marekani milioni 39 hadi dola za Marekani milioni 46.6 bila kujumuisha *VAT*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Uondoshaji wa magari ya Serikali, hapa kuna kasheshe hapa.

Mheshimiwa Spika, naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu masuala yaliyobainika katika ukaguzi huo kama ifuatavyo:-

(a) Ukaguzi ulibaini kwamba jumla ya magari ya Serikali 547 yalikuwa yameegeshwa kwenye Karakana za Wakala wa Ufundi na Umeme *(TEMESA)* na katika baadhi ya taasisi za Serikali zilizotembelewa kwa ukaguzi;

(b) Baadhi ya taasisi za umma ziliondoa magari bila ya kutoa tangazo kwa wazi. Taasisi hizo ambazo hazikutoa tangazo ni Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, Halmashauri ya Jiji ya Tanga, Mahakama ya Tanzania, Wizara ya Afya, Wizara ya Fedha na Wakala wa Barabara;

(c) Uthamini wa magari 500 uliofanywa na Wizara ya Ujenzi ulifanyika kwa kuangalia gharama chache bila kuangalia gharama halisi iliyotumika wakati wa ununuzi, hivyo kuikosesha Serikali mapato ya takribani shilingi bilioni 2.7; na

(d) Kuchelewa kutoa vibali vya kukopesha na uondoshaji wa magari kwa muda wa takribani hadi siku 2226.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Mipango na Ujenzi wa Mifumo ya TEHAMA

Serikalini; naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu masuala matano yaliyobainika katika ukaguzi huo kama ifuatavyo: -

(a) Mapungufu katika Uaandaaji wa Miradi ya TEHAMA; mathalani Taarifa ya *CAG* ilibainisha kwamba asilimia 86 ya maandiko ya awali ya mradi *(concept notes)* kutoka kwenye Taasisi za Umma kuhusiana na Miradi ya TEHAMA yalikataliwa kwa sababu yalikuwa yana makosa au yalihitaji maboresho;

(b) Mapungufu katika ushirikishwaji wa wadau katika mchakato wa kuandaa mifumo ya TEHAMA Serikalini;

(c) Kulikuwa na ujumuishaji na ushirikiano mdogo wa mifumo iliyopo kwenye Taasisi za Umma, mazingira ya ndani yasiyo rafiki ya kuhifadhi mifumo na upatikanaji wa mifumo bila idhini ya Mamlaka ya Serikali Mtandao;

(d) Ufanisi duni kwenye majaribio ya mifumo ya TEHAMA; na

(e) Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, haikuwa na mfumo madhubuti wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa sera na mikakati mingine inayohusiana na TEHAMA ambayo ni pamoja na kupanga na kujenga mifumo ya TEHAMA ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Urasimishaji wa Makazi Yasiyopangwa; matokeo ya ukaguzi huu wa ufanisi kuhusu kupanga na kurasimisha makazi ni kama ifuatavyo: -

(a) Ukaguzi ulibaini kuwa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita yaani tangu 2015/2016 hadi 2020/2021, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, hazikujumuisha ipasavyo shughuli za urasimishaji kwenye mipango yao ya kimkakati na mipango ya mwaka;

(b) Ukaguzi ulibaini Mpango Mkakati wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2015/2016 mpaka 2020/2021 na 2021/2022 mpaka 2025/2026 ulibainisha kuwa TAMISEMI

haikutenga fedha katika bajeti yake ili kuwezesha shughuli za urasimishaji katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa; na

(c) Ukaguzi ulibaini kuwa hadi mwishoni wa mwaka wa fedha 2021/2022, jumla ya vipande vya ardhi milioni 1.1 kati ya kati ya vipande milioni 2.3 vilivyokuwa vimepangwa sawa na asilimia 49 tu ndivyo viliweza kupimwa na kuidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Taarifa ya Ukaguzi wa Kiufundi katika Ujenzi wa Shule za Sekondari chini ya Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari; masuala yaliyobainika katika ukaguzi huu ni kama ifuatavyo:-

(a) Katika hatua za kuainisha maeneo kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari hapakuwa na utaratibu wa kuandaa hati miliki ya maeneo yaliyochaguliwa kwa ajili ya ujenzi;

(b) Maeneo ya ujenzi 19 kati ya 24 yaliyotembelewa hayakuwa yamepimwa na kuandaliwa ramani ya ardhi ili kuweza kubainisha ukubwa halisi wa maeneo hayo;

(c) Shule za sekondari tatu kati ya 24 zilikuwa na matumizi ambayo hayakustahiki yenye thamani ya shilingi milioni 27.5;

(d) Kukosekana kwa baadhi ya michoro; na

(e) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilichelewa kukamilisha mchakato wa manunuzi ya msimamizi huru wa mradi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Taarifa ya Ukaguzi wa Kiufundi kuhusu udhibiti wa gharama za ujenzi kwa miradi inayotekelezwa na baadhi ya Taasisi za Umma; miradi mbalimbali ilikuwa na ongezeko kubwa kulinganisha na fedha yake ya awali. Kwa mfano, Mradi wa *Magomeni Quarter*, kiasi cha shilingi bilioni 20 hadi shilingi bilioni 52 ambapo ongezeko ni shilingi bilioni 32.20 sawa na ongezeko la asilimia 161.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa 711 Kawe, ongezeko lilifikia shilingi bilioni 31.50; *Morocco Square*, shilingi bilioni 30.11;

Hoteli ya Kitalii ya Nyota Tano Mwanza shilingi bilioni 20.65; na *DAWASA* yetu shilingi bilioni 11.98, hayo yote ni maongezeko.

Mheshimiwa Spika, sababu kubwa za kuongezeka kwa gharama ni maandalizi yasiyofaa, tafsiri isiyofaa ya mahitaji ya mteja kwenye usanifu na mahitaji maalum ya mradi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi katika Utekelezaji wa Mpango wa Usambazaji Umeme Vijijini; katika eneo hili ukaguzi ulibaini masuala yafuatayo: -

(a) Dosari katika upembuzi yakinifu uliofanywa na *REA*;

(b) Tafiti za jioteknolojia hazikufanyika ipasavyo katika kituo kidogo cha Mtera;

(c) Kuchelewa kuanza ujenzi wa miradi ya *BTIP-VEI* Kutokana na kutosainiwa kwa mikataba minne kati ya mitano;

(d) Kutokuwepo mipango ya usimamizi wa mazingira wakati wa utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya ukaguzi wa kiufundi katika udhibiti wa ubora wakati wa utekelezaji wa shughuli za ujenzi wa miradi ili kuzuia uchakavu mapema, hii ni miradi ya barabara tuliyokuwa tunazungumzia sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukaguzi huu wa kiufundi ulibainisha masuala muhimu yafuatayo:-

(a) Kati ya miradi nane ya barabara zilizokaguliwa miradi saba ilikuwa na mapungufu ya kiufundi katika usanifu.

(b) Mwongozo wa viwango vya barabara haujafanyiwa mapitio au kuboreshwa kwa takribani miaka 23.

(c) Miradi mitano kati ya nane iliyokaguliwa ilikuwa na washauri elekezi waliopatikana baada ya Mkandarasi kuanza kazi ambapo ni kinyume cha sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taarifa ya ukaguzi wa kiufundi katika Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Usafiri wa Mabasi yaendayo Haraka *(BRT)* awamu ya pili. Masuala yaliyobainika katika ukaguzi huu ni kama ifuatavyo:-

(a) Ucheleweshaji wa siku 326 katika kukamilisha mradi, wakati zamani ilipokwisha muda wake kulikuwa na kiasi cha shilingi bilioni 6.4 ambacho kilikuwa hakijarejeshwa kama sehemu ya malipo ya awali;

(b) Mabadiliko ya mawanda ya kazi kwa miradi ya Loti Namba Moja na Mbili ambayo yalisababisha kuzidi kwa gharama za mkataba kwa shilingi bilioni 7.03; na

(c) Kati ya Maafisa 11 walichaguliwa kama sampuli, Maafisa sita walikuwa hawana vibali vya kazi jambo ambalo ni kinyume na kanuni za ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taarifa ya ukaguzi wa ufanisi katika utekelezaji wa malengo ya maendeleo endelevu. Kwa muhtasari ukaguzi huu wa ufanisi hubainisha masuala yafuatayo:-

(a) Ujumuishaji hafifu wa malengo ya maendeleo endelevu katika Mipango ya Kitaifa ya Maendeleo ya Miaka mitano na Mipango Mikakati ya Wizara, Taasisi, Mikoa na Halmashauri nchini;

(b) Mbali na Kamati ya ufundi ya ngazi ya juu, Tanzania inahitaji kama timu ndogo ya kuratibu utekelezaji huo kwa kuzingatia takwimu za ajenda ya maendeleo, kuratibu maslahi ya wadau na juhudi zinazohusu masuala ya takwimu katika siku zijazo;

(c) Uwezeshaji mdogo kwa ajili ya shughuli za upatikanaji wa takwimu nchi; na

(d) Wizara ya Fedha na Mipango wakati huo kutoimarisha ukusanyaji wa kodi mbalimbali na kuwezesha mazingira kutambua vyanzo vipya vya mapato.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya ukaguzi wa ufanisi katika uendeshaji wa matengenezo ya miradi ya maji. Maelezo ya kina kuhusu matokeo ya ukaguzi huu ni kama ifuatavyo:-

(a) Katika mamlaka ya usambazaji maji mijini, Mamlaka nane zilizotembelewa ilibainika kuwa mamlaka tano zilikuwa na taratibu rasmi za uendeshaji maji huku mamlaka tatu zikiwa hazina taratibu rasmi za uendeshaji.

(b) Kwa miaka mitatu ya fedha iliyopita uzalishaji wa maji kwa mwaka ulikuwa chini ukilinganishwa na uwezo wa miundombinu ya usambazaji wa maji uliowekwa licha ya uhitaji mkubwa wa maji. *(Makofi)*

(c) Katika mamlaka nne kati ya nane zilizotembelewa kulikuwa na miundombinu ya usambazaji maji isiyofanya kazi ipasavyo.

(d) Ukusanyaji wa mapato kutoka kwa ankara za maji kilikuwa chini ukilinganisha na ankara za maji zilizotolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Taasisi mbalimbali za Serikali zilikuwa zinadaiwa takribani bilioni 43.3 hadi kufikia mwezi Mei, hii inafanya mamlaka hizi zishindwe kufanya kazi, bilioni 43 ni nyingi mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taarifa za ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo. Mapema mwezi Machi, 2023 Kamati ilifanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo ili kujiridhisha na thamani halisi ya fedha iliyotumika katika utekelezaji wa miradi hiyo. Ziara ilifanyika katika Mikoa ya Njombe, Iringa, Morogoro, Mtwara na Dar es Salaam. Maelezo ya kina kwa miradi iliyotembelewa inapatikana katika aya ya pili pointi mbili ya taarifa yetu kubwa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa taarifa za *CAG* kwa Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha unaishia tarehe 30 Juni, 2022. Mnamo tarehe 02

Novemba, 2023 Kamati ya *PAC* iliwasilisha taarifa yake Bungeni kuhusu uchambuzi wa taarifa za *CAG* kwa Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu lilipitia na kujadili taarifa ya Kamati inayohusu taarifa hizo za ukaguzi kwa muda wa siku tatu kuanzia tarehe 02 hadi 04 Novemba, 2023 ambapo Bunge lilipitisha jumla ya Maazimio ya Bunge kumi na nane (18).

Mheshimiwa Spika, Kamati itaendelea kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Maazimio hayo ya Bunge kuanzia mwezi Machi, 2024 ili kuhakikisha uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, mafunzo na Semina za kuwajenge uwezo Wajumbe. Katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari, 2023 hadi mwezi Februari, 2024 Kamati kwa idhini yako ilipatiwa mafunzo na Semina katika maeneo mbalimbali yalitolewa na Ofisi ya *CAG*, Ofisi ya Msajili wa Hazina, Taasisi mbalimbali za Serikali pamoja na Asasi za Kiraia zinazoangalia matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo. Mapendekezo ya Kamati yametolewa kwa kuzingatia dhima ya kaguzi za ufanisi na kaguzi za kiufundi ambazo kwa kiasi kikubwa ndizo zimechambuliwa katika taarifa hii. Kwa msingi huo mapendekezo ya Kamati yamejielekeza katika kuhakikisha kunakuwepo na tija, uwekevu na ufanisi katika matumizi ya fedha za umma. Naomba kuwasilisha mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukaguzi wa ufanisi katika usimamizi wa uondoshaji magari ya Serikali:-

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Serikali iandae mwongozo utakaotoa ukomo wa gari la Serikali kuegeshwa. Aidha, mwongozo huo utoe maelekezo bayana ya mchakato mzima wa uondoshaji magari hayo kwa uwazi na uthamini wake ili kupata gharama halisi na baada ya hapo maamuzi yatolewe

kuelekeza gari hilo kuondoshwa kwa kuuzwa au kukopeshwa Mtumishi; na

(b) Serikali ifanye mapitio ya Sheria zinazohusika na uthamini wa mali za Serikali ili kuondoa mgongano wa kisheria uliopo sasa wa uthamini wa magari ya Serikali, kufanywa na taasisi tofauti hali inayoleta mgongano wa kiutekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukaguzi wa ufanisi kwenye uendeshaji wa matengenezo ya Miradi ya Maji; Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Serikali ihuiwishe mpango kabambe *(master plan)* wa maji nchini ambao utaainisha miradi mikuu ya usambazi maji nchi nzima. Kupitia vyanzo vya uhakika kama vile maziwa na mabwawa ili kuwa na uhakika wa upatikanaji wa maji safi na salama kwa gharama nafuu na kwa kuzingatia thamani halisi ya fedha za umma. *(Makofi)*

(b) Serikali itoe tathimini ya kila mwaka ya asilimia anayofikiwa ya ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji *(percentage* ya *distribution)* inayokuwepo kwa kulinganisha na kilichopangwa katika mpango kabambe *(master plan)* ya maji.

(c) Serikali ihakikishe taasisi zote za umma zinazodaiwa ankara za madeni ya maji, zilipe madeni yake ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira hapa nchini zinafunga dira za malipo ya kabla *pre-paid meters* kwa taasisi zote za Serikali na binafsi zenye matumizi makubwa ya maji ili kuondoa madeni haya kulimbikizwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukaguzi wa ufanisi katika usimamizi wa Mipango na Ujenzi wa Mifumo ya TEHAMA Serikalini; Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Serikali ikamilishe mapema Sera ya TEHAMA Serikalini pamoja na kufanya tathmini ya mifumo yote ndani ya Serikali na kubaini mifumo yote ambayo haina tija kwa Serikali na kuchukua hatua madhubuti za kuiondoa; na

(b) Serikali ihakikishe kunakuwa na muungano wa Mifumo ya Serikali kati ya Taasisi moja na Taasisi nyingine au Sekta moja ni nyingine katika namna itakayorahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi bila vikwazo vyovyote vya kimfumo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukaguzi wa ufanisi na usimamizi wa urasimishaji wa makazi yasiyopangwa. Kwa kuwa Kamati imebaini uwepo wa mapungufu makubwa katika usimamizi na utekeleza mpango wa urasimishaji wa makazi yasiyofaa au yasiyopangwa. Bunge linaazimia ya kwamba:-

(a) Serikali ifanye tathmini ya kina ya sababu zilizochangia mpango wa urasimishaji makazi yasiyopangwa kushindwa kufikia malengo yaliyokusudiwa. *(Makofi)*

(b) Vilevile Serikali iandae mpango madhubuti na unaotekelezeka wa kurasimisha makazi yote yasiyopangwa nchini ili kuboresha utoaji wa huduma na kupata fedha za kuwahudumia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukaguzi wa ufanisi juu ya udhibiti wa vituo vya kutolea huduma ya afya vya binafsi na hiyari; Bunge linaazimia ya kwamba:-

(a) Serikali ihakikishe kunakuwepo na mfumo thabiti utakaounganisha Bodi zote zinazosimamia vituo vya afya binafsi na hiyari. *(Makofi)*

(b) Kuimarisha udhibiti na usimamizi wa vituo hivyo vya afya vya binafsi na hiyari, kwa kufanya hivyo thamani halisi ya fedha za umma iliyotumika kwenye usimamizi na udhibiti wa vituo itakuwa imepatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukaguzi wa kiufundi juu ya ujenzi wa shule chini ya Mradi wa *SEQUIP*; Bunge linaazimia ya kwamba:-

(a) Serikali ichukue hatua za makusudi kwa kuhakikisha kuwa miradi ya ujenzi wa shule inasimamiwa na watalam waliokidhi vigezo; na *(Makofi)*

(b) Serikali ifanye tathmini ya kina juu ya faida na hasara za mifumo au mfumo unaotumika kujenga shule za Sekondari nchini kwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukaguzi wa kiufundi katika udhibiti wa ubora wakati wa utekelezaji wa shughuli za ujenzi wa miradi ya barabara ili kuzuia uchakavu wa mapema; Bunge linaazimia ya kwamba:-

(a) Serikali ifanye mapitio ya utendaji wa wasimamizi wa miradi na washauri elekezi ambao wamesimamia miradi yenye mapungufu ya ubora, pamoja na ile yenye uchakavu wa mapema ili kubaini sababu za kuwa na usimamizi dhaifu pamoja na kuchukua hatua stahiki zitakazohimarisha usimamizi wa ujenzi wa barabara hizo.

(b) Aidha, Serikali ihuishe miongozo ya usanifu wa barabara ujenzi wake na usimamizi wake ili ikidhi vigezo vinavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukaguzi wa kiufundi katika udhibiti wa gharama za ujenzi wa majengo ya Serikali; Bunge linaazimia ya kwamba:-

(a) Serikali itoe mwongozo wa kudhibiti ongezeko la gharama za miradi pamoja na hilo kuwe na mfumo wa kuonyesha muda wa malipo wa mradi husika na taasisi zinazotakiwa kushughulikia malipo hayo ili kuondoa changamoto ya kuchelewa kukamilisha miradi; *(Makofi)*

(b) Serikali ihakikishe kunakuwepo mfumo utakaobainisha muda wa mradi, viashiria vya kuchelewa kwa mradi ili kuwe na tathmini ya taasisi nunuzi pamoja na Wizara ya Fedha kwa kuchelewesha miradi husika;

(c) Serikali ihakikishe inaweka mfumo wa kuhakikisha hatua zote za usanifu wa miradi zinafuatwa na taasisi nunuzi kabla ya kusainiwa kwa mikataba hiyo; na

(d) Kwa upande wa ujenzi wa miradi wa *Seven Eleven* Kawe, hili tulisikilize vizuri *CAG* afanye mapitio ya kina kuhusu mikataba na nyaraka zote zinazohusu upembuzi yakinifu wa mradi huo na kulitaarifu Bunge ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukaguzi wa kiufundi katika Ujenzi na Ukarabati wa Meli; Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Serikali iandae mipango ya muda mfupi na ya muda mrefu ya kuimarisha na kujenga uwezo wa kifedha na watalaam Kampuni ya Huduma ya Meli Nchini ili iweze kusimamia fanisi, uanzishwaji, upangaji, sanifu, utekelezaji na usimamizi wa miradi ya ujenzi ya ukarabati ya meli nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukarabati wa ufanisi katika utekelezaji maendeleo endelevu; Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Serikali ihakikishe kwa Wizara ya Fedha inaibua vyanzo mbadala vya mapato ambavyo vitachangia mapato ya ndani kupunguza utegemezi;

(b) Wizara ya Fedha ihakikishe mipango mikakati ya Wizara, Taasisi za Serikali, Sekretarieti ya Mikoa na Halmashauri za Serikali za Mitaa zinahuisha mipango mikakati yawe kwa wakati; na

(c) Tume ya Mipango iratibu kikamilifu utekelezaji wa mfumo kitaifa na uratibu wa malengo wa maendeleo endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi ya maendeleo iliyokaguliwa na Kamati mwezi Machi, 2023; Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Serikali iingie Mikataba Mipya ya Ujenzi wa Miradi pale tu inapokuwa na uhakika wa Bajeti na Fedha za Miradi husika ili kuepuka malipo ya riba kwa kuchelewa kulipa Wakandarasi ambayo imegharimu Taifa hili pesa nyingi sana kulipa riba. *(Makofi)*

(b) Tathmini ya utendaji wa kila mwaka ya Maafisa Masuuli wote ifanyike kwa kuongeza kigezo cha uwezo wa Afisa Masuuli katika kusimamia utekelezaji maridadi. Iwapo kunabainika dosari za kiusimamizi katika Miradi Afisa Masuuli husika achukuliwe hatua stahiki ili kuleta uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hitimisho, shukrani. Napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako makini na thabiti, uongozi wako umeuwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake bila vikwazo na kutoa maelekezo mengine mara kwa mara tunapoomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote wa Kamati yetu hii ya *PAC* kwa kufanya kazi kwa ufanisi na weledi mkubwa. Naomba majina yao wote ya Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya *PAC* yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Mwihambi, *Ndc* kwa uongozi wake thabiti na Sekretarieti ya Bunge ambayo imeratibu shughuli za Kamati kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho japo siyo kwa umuhimu. Kamati inatambua na kuthamini ushirikiano uliopata kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Wizara ya Fedha kupitia Mlipaji Mkuu wa Serikali, Mhasibu Mkuu wa Serikali, Msajili wa Hazina na Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali na Maafisa wote kwa ushirikiano waliotoa katika kuratibu majibu ya hoja za ukaguzi na mahojiano ya Kamati na Maafisa Masuuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI KWA MWAKA 2023 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

1.0 MAELEZO YA JUMLA

1.1 Utangulizi

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia zawadi ya uhai na hivyo kuwa na fursa ya kukutana hapa siku ya leo. Kwa heshima kubwa naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) zilizotekelezwa katika kipindi cha Mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, katika kutimiza madhumuni hayo, Taarifa hii inagusa uchambuzi wa Taarifa za Kaguzi za Kiufundi (Technical Audits) na Kaguzi za Ufanisi (Perfomance Audits) kama zilivyokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2022. Vilevile Taarifa hii inahusu ziara za ukaguzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali. Aidha Taarifa hii imefafanua kuhusu mafunzo na semina za kuwajengea uwezo Waheshimiwa Wajumbe zilizofanyika katika kipindi tunachokitolea Taarifa.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina na ufafanuzi kuhusu shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi chote hicho yamefafanuliwa katika Sehemu ya Pili ya Taarifa hii .

1.2 Muundo wa Taarifa

Mheshimiwa Spika, kwa madhumuni ya kurahisisha ufuatiliaji wa Taarifa hii, Taarifa hii imegawanyika katika Sehemu Kuu Tatu. Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla ikiwemo muundo wa taarifa, majukumu ya Kamati, msingi wa kazi za Kamati na muhtasari wa matokeo ya uchambuzi. Lengo la Sehemu hii ni kubainisha muktadha wa taarifa ili kuwezesha ufuatiliaji utakaosaidia kufanya uamuzi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi wa shughuli zilizotekelezwa na Kamati katika kipindi cha Mwezi Januari, 2023 hadi Februari, 2024.Katika Sehemu hii, Taarifa inafafanua mambo ya msingi kuhusu uchambuzi na kubainisha matokeo ya uchambuzi huo. Lengo la sehemu hii ni kuonesha dosari zilizobainika katika matumizi ya Fedha za Umma na kuweka msingi wa mtazamo wa Kamati kuhusu Matumizi ya Fedha za Umma kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022. Sehemu hii inajenga msingi wa Sehemu ya Tatu inayohusu Maoni na Mapendekezo.

1.3 Majukumu ya Kamati

Mheshimwa Spika, maudhui ya Taarifa hii yanahusu Matumizi ya Fedha za Umma kwenye Serikali Kuu na Mashirika ya Umma Nchini. Mambo hayo yanasimamiwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kama ilivyobainishwa katika Kifungu cha 13 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Kwa mujibu wa Kifungu hicho
Kamati ina majukumu yafuatayo: -

a) Kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma katika Wizara za Serikali na Mashirika ya Umma yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG);

b) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati ili kuondoa matatizo yaliyobainika kwa mujibu wa kanuni hii; na

c) Kutoa mapendekezo na ushauri kwa Wizara za Serikali na Mashirika ya Umma kuhusu matumizi mazuri ya fedha za umma ili kupunguza matumizi mabaya ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, Msingi wa majukumu hayo unatokana na Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kama ilivyobainishwa katika Kifungu cha 15 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

1.4 Njia zilizotumika Katika Utekelezaji wa Kazi za Kamati

Mheshimiwa Spika, Kanuni za Bunge Toleo la Februari, 2023 zimeweka masharti kwamba Taarifa yoyote ya Kamati inayoingia Bungeni, inatakiwa kubainisha njia zilizotumiwa na Kamati kufanya kazi inayotolewa Taarifa. Kwa msingi huo naomba kubainisha njia na mbinu zilizotumika na kuwezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba kuzitaja njia hizo kama ifuatavyo: -

a) Mapitio ya jumla ya Ripoti za CAG ili kubaini maeneo ya kuwekea mkazo na kukidhi masharti ya Ripoti hiyo ulikuwa msingi wa kazi za Kamati zilizopangwa kwenye Ratiba;

b) Kupokea Vidokezo (“briefs”) vya Ripoti za CAG kwa hoja za ukaguzi za mafungu yaliyopangwa kujadiliwa na Kamati kabla ya Kukutana na Afisa Masuuli anayehusika. Mbinu hii iliiwezesha Kamati kuzielewa hoja na wigo wa mahojiano na Afisa Masuuli kwa lengo la kupata undani wa tatizo la matumizi mabaya ya fedha za umma;

c) Mahojiano na maafisa masuuli kuhusu hoja za ukaguzi ili kupata undani wa matatizo ya matumizi ya fedha za umma na kubaini chimbuko la tatizo, wigo wa dosari na uwezekano wa kuepuka matumizi mabaya ya fedha za umma;

d) Uchambuzi wa kina wa Taarifa za Wakaguzi wa hesabu za Fungu linalohusika kwa pamoja na majibu ya Menejimenti za Taasisi, wizara au Shirika lililokaguliwa. Lengo ni kuelewa kwa kina muktadha wa hoja na matatizo ya matumizi mabaya ya fedha za Umma; na

e) Tafiti mbalimbali kuhusu masuala ya usimamizi wa fedha za umma. Lengo la njia hii ni kuona na kuutumia uzoefu wa jumla unaopatikana kwa tafiti hizo ili kutathmini maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma kama yalivyoainishwa na CAG.

Mheshimiwa Spika, njia na mbinu hizo ziliiwezesha Kamati kufanya uchambuzi wa kina kwa nia ya kulishauri Bunge kuhusu hatua za kuchukua. Mbinu hizo ziliendana na matumizi na marejeo ya miongozo ifuatayo: -

a) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 inayoonesha dhamana ambayo Serikali imepewa na wajibu wa Bunge kuisimamia na kuishauri Serikali ikiwemo eneo la matumizi ya fedha za umma;
b) Sheria ya Ukaguzi wa Umma, 2008 inayofafanua masharti muhimu kwa ajili ya kuwezesha ukaguzi, uandaaji wa Ripoti za CAG, uwasilishaji wake na hatimaye kujadiliwa na Kamati;
c) Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Sura 348 inayoweka miongozo ya matumizi ya fedha za umma na kusaidia kuamua iwapo kuna matumizi mabaya ya fedha za umma;
d) Sheria ya Bajeti, Sura ya 439, inayohusika na usimamizi wa matumizi ya Fedha za Umma kwa kuweka taratibu za utekelezaji wa bajeti na usimamizi wake;
e) Sheria ya Msajili wa Hazina Sura 370 inayogusa usimamizi wa matumizi ya Fedha za Umma katika mashirika ya umma;
f) Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410, inayoweka taratibu za kufuatwa wakati wa ununuzi wa bidhaa, huduma na kuingia mikataba kwa gharama ambazo zinahusisha matumizi ya fedha za umma;
g) Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu, Sura 286, inayosimamia weledi wa wahasibu na wakaguzi ili

kuwezesha kumbukumbu za kutumainiwa za fedha na usimamizi bora wa matumizi ya Fedha za
Umma;

h) Sheria ya Kinga Madaraka na Haki za Bunge, Sura 296 inayoliwezesha Bunge, Wabunge na Kamati za Bunge kupata stahili kutokana na madaraka yake na kupata ushahidi bila kukwama wakati wa kufuatilia matumizi ya fedha za umma; na
i) Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 zinazobainisha utaratibu wa Ripoti za CAG kuhusu matumizi ya fedha za umma kuwasilishwa Bungeni, kushughulikiwa na Kamati na hatimaye Kamati kutoa Taarifa hii.

1.5 Vigezo vya Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, uaandaji wa vigezo vya kuzingatiwa ni jambo muhimu katika uhakiki na tathmini yoyote. Suala la matumizi mabaya ya fedha za umma linaweza kubainika kutokana na vigezo vya matumizi ya fedha za umma. Aidha, uamuzi wa kuwahoji Maafisa Masuuli kutokana na Taarifa za CAG ni jambo lililohitaji kuwekewa vigezo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, baada ya kupokea Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Kamati ilitengeneza vigezo muhimu vya kuzingatia katika kutimiza majukumu yake ya Kikanuni. Vigezo hivyo vilitoa mwongozo wa uchaguzi wa mafungu ambayo yalipewa kipaumbele katika uchambuzi na mahojiano na Maafisa Masuuli.Aidha, vigezo hivyo vilisaidia katika kuchagua miradi ambayo ilitembelewa katika ziara za ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, vigezo vilivyozingatiwa wakati wa kuchagua vipaumbele katika utekelezaji wa shughuli za Kamati vilikuwa kama ifuatavyo: -

a) Uzito wa hoja ya ukaguzi kama ilivyoibuliwa na CAG;
b) Maslahi ya umma kuhusu hoja za fungu linalohusika;
c) Hali ya hati ya ukaguzi iliyotolewa kwa fungu linalohusika;
d) Kujirudia mara kwa mara kwa hoja husika katika Wizara, Idara, Wakala, Balozi au Mradi wa Maendeleo uliokaguliwa;

e) Kiwango cha fedha kinachohusika katika hoja za ukaguzi wa fungu linalohusika;
f) Kuleta uendelevu wa ufuatiliaji wa ushauri na maelekezo yaliyotolewa na Kamati kwa fungu husika kwa siku za nyuma;
g) Kutoa kipaumbele kwa sekta na taasisi za kimkakati (strategic sectors and parastatals) kwa kuzingatia utekelezaji wa malengo ya sasa ya Serikali;
h) Kutoa kipaumbele kwa kaguzi maalum (special audits) zilizofanyika hivi karibuni; na
i) Uzingatiaji wa kaguzi za ufanisi na kaguzi za kiufundi kwa mwaka husika.

Mheshimiwa Spika, vigezo hivyo viliisaidia Kamati kuendelea na mchakato wa kufuatilia matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia Ripoti za CAG. Nikiri kuwa vigezo hivyo vimeisadia Kamati kufikia lengo la kupitia na kuchambua taarifa nyingi na kubainisha maeneo yenye mapungufu katika matumizi ya fedha za umma.

SEHEMU YA PILI

2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI

Mheshimiwa Spika, kufuatia vigezo na mambo ya msingi niliyoyataja hapo awali, naomba sasa kutoa maelezo ya kina kuhusu shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2023 hadi Februari, 2024 kama ifuatavyo: -

2.1 Uchambuzi wa Taarifa za Ukaguzi wa Ufanisi na Kaguzi za Kiufundi

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha shughuli za Kamati cha kuanzia tarehe 15 Januari, 2024 hadi tarehe 25 Januari, 2024, Kamati ilijielekeza katika kupitia na kujadili Taarifa za Kaguzi za Kiufundi (Technical Audits) na Kaguzi za Ufanisi (Perfomance Audits). Taarifa hizi zilitokana na kaguzi zilizokuwa zimefanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanikiwa kupitia na kujadili jumla ya Taarifa kumi na mbili (12) za ukaguzi wa ufanisi na wa kiufundi. Aidha, Kamati ilipata fursa ya kufanya mahojiano na Maafisa Masuuli wanaosimamia mafungu husika yaliyoguswa na taarifa hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa nipende kukushukuru tena kwa kuipa fursa Kamati hii kupitia na kuchambua Taarifa za Ukaguzi wa Ufanisi na Ukaguzi wa Kiufundi. Hatua hii ni ya kipekee kwa Bunge letu ukilinganisha na Mabunge mengine katika ukanda wetu. Kaguzi hizi zinaenda mbali kwa kutoangalia masuala ya fedha peke yake bali kwa kuangalia ufanisi, tija na uwekevu mtawalia (efficiency, economy & effectiveness) respectively.

Mheshimiwa Spika, hatua hii ya uwajibikaji iliyofikiwa katika Bunge letu inathibitishwa na maelezo ya utangulizi ya Ndugu George C. Haule ambaye ni Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) aliyoyatoa mbele ya Kamati kuhusu umuhimu wa Taarifa hizi. Naomba kunukuu sehemu ya maelezo[1] yake kama ifuatavyo:- **Nukuu: "…Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, eneo la pili, ambalo Ofisi ya CAG, tungependa kuleta shukurani zetu za dhati kabisa. Ni kwahatua uliyoichukua wewe na Kamati yako ya kuzidi kuzijadili Taarifa za Ukaguzi wa Ufanisi na Kiufundi. Kwa kipindi cha miaka mitatu au minne sasa utaona kwamba Taarifa za Ukaguzi wa Ufanisi na Kiufundi zimekuwazikijadiliwa na Kamati yako na kwa kweli ni mijadala ambayo tunasema ni mizuri. Sisi ambao tunaenda kukutana na Wakaguliwa huko tunaona impact ya kile ambacho kinaendelea.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanazidi kutoa more attention kwetu na kuzidi kuhakikisha kwamba yale ambayo tunayaona wanayatilia maanani zaidi. Hasa ukichukulia kwamba tunakutana na Watendaji zaidi siyo wale Wahasibu pekee lakini Watendaji wenye fani tofauti tofauti. Kwa hiyo, kwa kweli kuna impact inaendelea. Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, upande wa sisi

[1] Rejea Uk. 1 wa Majadiliano Kamati, Taarifa Rasmi za Bunge Kikao cha Pili, Tarehe 16 Januari, 2024.

kwenye kukidhi vigezo vile vya Kimataifa vya Kikaguzi. Tunaonekana tumefika at least mwisho kabisa wa ile accountability loop. Kwamba Kamati zetu za Bunge zinakuwa nazo zimeshiriki kwenye mchakato wa Taarifa zetu…" Mwisho wa Nukuu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu matokeo ya uchambuzi wa Taarifa hizo kumi na mbili (12) kama ifuatavyo:-

2.1.1 Taarifa ya Ukaguzi wa Kiufundi Kuhusu Ujenzi na Ukarabati wa Meli

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipitia na kuchambua Taaarifa ya Ukaguzi wa Kiufundi Kuhusu Ujenzi na Ukarabati wa Meli. Lengo la jumla la Ukaguzi wa Kiufundi lilikuwa kutathmini kama Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) chini ya Wizara ya Uchukuzi ilisimamia ipasavyo ujenzi na ukarabati wa Meli hapa Nchini ili kuhakikisha thamani halisi ya fedha za umma inapatikana.

Mheshimiwa spika, ukaguzi huu ulihusisha ujenzi wa Meli ya MV Mwanza na ukarabati wa Meli za MV Umoja, MV Victoria na MT Sangara. Ukaguzi ulifanya ziara ya kuhakiki maeneo ya ujenzi na ukarabati wa Meli katika Mkoa wa Mwanza na Kigoma.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulihusisha kipindi cha miaka ya fedha kuanzia 2018/19 hadi Juni, 2021/22. Muda uliochaguliwa uliwawezesha wakaguzi kutathmini kama malengo yaliyokusudiwa yalikuwa yamefikiwa na kutoa hitimisho na mapendekezo kulingana na matokeo ya ukaguzi. Pia katika kipindi hiki kulikuwa na ufufuaji wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) kwa kutengewa bajeti ya ujenzi wa MV Mwanza na ukarabati wa Meli nne (4). Kwa hiyo, muda uliochaguliwa ulikuwa mwafaka kwa ajili ya kupata taarifa za kutosha kufanya tathmini ya Meli zinazojengwa na kukarabatiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu matokeo ya ukaguzi huo kama ifuatavyo: -

a) Ukaguzi ulibaini kuwa, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (MoWT) ilianzisha mradi wa ujenzi wa Meli bila ushahidi wa wazi wa uchunguzi wa awali. Hatua za awali za ujenzi huo zilikuwa za dharura na kusababisha kutokuwepo kwa maandalizi ya kutosha. Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) haikuandaa nyaraka inayoelezea mahitaji halisi kuhusu ukubwa wa mradi, mawanda ya mradi, manufaa na mahitaji. Mathalani kwa Meli ya MV Mwanza hatua hiyo ilisababisha mabadiliko ya vipimo ambapo kwa upande wa urefu ulibadilishwa ili kuwezesha meli kubeba abiria 1200 badala ya 600;

b) Kwa mujibu wa mapitio ya Majalada ya Mawasiliano na Ripoti za Utendaji, ukaguzi ulibaini kuwa, Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) haikufanya upembuzi yakinifu kwenye ujenzi wa Meli mpya. Usaili uliofanywa kwa Watumishi wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) ulibainisha kuwa, sababu yakutofanyika kwa upembuzi yakinifu ni kukosekana kwa uzoefu kwenye ujenzi wa Meli mpya hasa ikizingatiwa kuwa hii ndio mara ya kwanza Nchi kujenga Meli;

c) Uchambuzi wa Kamati ulibaini pia ujenzi wa Meli ulianza bila ya kitanda cha kujengea Meli (slipway) hivyo kusababisha Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) kuingia mikataba miwili (2) ya ujenzi wa Meli mpya na ujenzi wa kitanda cha kujengea Meli (slipway) kwa wakati mmoja. Ukaguzi ulibainisha kuwa sababu zilizopelekea Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) kuanza ujenzi wa Meli bila kukamilisha ujenzi wa kitanda cha kujengea Meli (slipway) ni uharaka uliokuwepo wa kutaka kukamilisha ujenzi wa Meli. Uamuzi wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) kuingia mikataba miwili (2) kwa wakati mmoja kulisababisha Kampuni kushindwa kukabidhi kitanda cha kujengea Meli (slipway) kwa mkandarasi wa ujenzi wa Meli mpya kwa wakati ili kuwezesha shughuli za kuweka uti wa mgongo wa Meli (keel laying). Hali hii ilisababisha uhitaji wa ongezeko la muda wa kazi kwa miezi mitano (5) ambao uliambatana na gharama ya **Dola za Marekani 3,426,251.84** (bila VAT);

d) Vilevile, ukaguzi ulibaini kuchelewa kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa Meli ya MV Mwanza. Ongezeko la muda lilisababisha kuongezeka kwa gharama za mradi kwa **Dola za Marekani 7,926,251.84** kutoka kiasi kilichopangwa cha **Dola za Marekani 39,000,000** hadi **Dola za Marekani 46,926,251.84** (bila kujumuisha VAT). Kuchelewa kukamilika kwa mradi pia kulizuia kufikiwa mapema kwa lengo la mradi la kuimarisha usafiri katika Ziwa Victoria;

e) Ukaguzi ulibaini pia mapungufu kadhaa katika ukarabati wa Meli ya MV Victoria.Mathalani Taarifa ya CAG inabainisha kwamba wataalamu kutoka Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) hawakushiriki katika jaribio la ubora wa mashine kiwandani (FAT)[2] kabla ya usimikwaji hasa jaribio la injini zinazotengenezwa na M/s STX Engine Co Ltd ya Korea Kusini. Hii ni kwa sababu, Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) haikuwa imetuma mtaalamu yeyote kushiriki katika zoezi hilo kwa sababu mkandarasi alikuwa na imani kubwa ya kiutendaji kwa M/s STX Engine Co Ltd ya Korea Kusini. Mapitio ya nyaraka za tarehe 31 Oktoba 2020 yalibainisha kuwa, baada ya Meli kufanya kazi kwa muda wa miezi mitatu (3), mapungufu kadhaa yalianza kuonekana yakiashiria udhaifu wa injini ya Meli. Kamati inaamini kwamba, endapo Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) ingehudhuria FAT, wangeweza kugundua mapungufu haya, hivyo yangefanyiwa kazi kabla ya vifaa kufika Tanzania;

f) Mapungufu katika usanifu wa mtambo mkuu wa kuendesha Meli ya MT. Sangara.Taarifa ya ukaguzi imebainisha kuwa, Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) ilipanga kufanya manunuzi na ufungaji wa injini kuu mbili (pacha) aina ya Caterpillar ambapo kila moja ilitakiwa kuwa na uwezo wa kasi ya juu ya fundo 11 (knots). Hata hivyo, wakati wa ziara ya Timu ya Wakaguzi iliyofanyika tarehe 9 Novemba, 2022 katika eneo la ukarabati wa Meli ya MT Sangara kando ya Bandari ya Kigoma, ilibainika kuwa, injini mbili (2) ambazo tayari zilikuwa zimewekwa kwenye Meli hiyo zilikuwa ni za

[2] FAT (Factory Acceptance Test).

upande mmoja (starboard). Hii ina maana kuwa, injini zote mbili (2) zingekuwa zinazunguka kwa mwelekeo mmoja ambapo ilikuwa ni kinyume na mahitaji ya mwajiri ambayo yalihitaji injini pacha ambazo ni "starboard na portside "; na

g) Kutofanyika shughuli za ufuatiliaji na tathmini ya kutosha katika ujenzi na ukarabati wa Meli. Dosari hii ilithibitishwa na uwepo wa taarifa zisizotosheleza ambapo ni ripoti mbili (2) tu kati ya ripoti zote zilizopaswa kutayarishwa kila Mwezi ziliwasilishwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, kwa kipindi chote cha utekelezaji wa ujenzi na ukarabati wa miradi ya Meli hizo. Pia, hapakuwa na mpango wa ufuatiliaji uliotayarishwa kuwezesha utekelezaji wa shughuli za ufuatiliaji.Hali hii ilisababishwa na ukosefu wa Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini kwa Miradi ya Ukarabati na Ujenzi wa Meli; na

h) Mwisho CAG alibainisha dosari kwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kuwateua Wajumbe wa Timu ya Ufundi wa Miradi husika bila Masharti ya Kazi (ToR).

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya CAG inayohusu ujenzi na ukarabati wa Meli, hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2023 matokeo ya uhakiki wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa ilibainisha kwamba,mapendekezo manne (4) yalikuwa yametekelezwa kikamilifu, mapendekezo mawili (2) yalikuwa katika hatua za awali za utekelezaji, mapendekezo saba (7) yalikuwa katika hatua nzuri ya utekelezaji na pendekezo moja (1) lilikuwa halijatekelezwa kabisa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya mahojiano ya kina na Katibu Mkuu Sekta ya Uchukuzi akiwa pamoja na Bodi na Menejimenti ya Kampuni ya Huduma za Meli. Mahojiano hayo yalifanyika siku ya tarehe 16 Januari,2024 na yalilenga kupata maelezo ya Serikali kuhusu mikakati ya kuondokana na mapungufu yaliyojitokeza katika ukaguzi husika wa kiufundi.

Mheshimiwa Spika,katika mahojiano hayo, uongozi wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) walikiri mbele ya Kamati kuwa ukaguzi

uliofanywa na CAG umekuwa nguzo kubwa kwa wao kufanya mabadiliko muhimu ya Kampuni.Walifafanua kuwa Kampuni ya MSCL ilikuwa imesitisha shughuli zake muda mrefu ikiwa ni pamoja na kuondolewa katika vitabu vya Serikali.

Mheshimiwa Spika,ufafanuzi wa Afisa Masuuli Wizara ya Uchukuzi ulibainisha kwamba, mapungufu mengi yaliyobainika katika ukaguzi huu yalitokana na takwa la ujenzi wa Meli kuanza kutekelezwa kabla Kampuni ya MSCL haijawa na uwezo wa kutosha. MSCL haikuwa na wahandisi wa kutosha (marine engineers), wataalamu wa manunuzi na wataalamu wa fedha.Hivyo wataalamu wengi waliazimwa kwa muda kutoka taasisi mbalimbali za Serikali kwa wakati huo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na dosari zilizobainika, Afisa Masuuli Uchukuzi aliifahamisha Kamati kuwa kwa mikataba mipya ya ujenzi wa Meli iliyoingiwa hivi karibuni na ile iliyoingiwa baada ya kipindi cha Uviko,dosari nyingi zimefanyiwa kazi kwa kuzingatia mapendekezo ya CAG.

Mheshimiwa Spika, hoja ya Kamati katika eneo hili ambayo itaendelea kufanyiwa kazi ni kuhusu ufuatiliaji wa mapendekezo ya ukaguzi kama yatatekelezwa kikamilifu. Aidha, hoja nyingine inahusu kuendelea kujenga uwezo wa MSCL ili kuhakikisha ujenzi wa Meli hapa Nchini unakuwa na tija na thamani ya fedha za umma inapatikana.

2.1.2 Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi Katika Usimamizi wa Uondoshaji wa Magari ya Serikali

Mheshimiwa Spika, mnamo mwaka 2009, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilitoa Mwongozo wa Uondoshaji wa Magari ya Serikali kwa njia ya kuwakopesha watumishi wa umma. Pia, Sheria ya Fedha za Umma Na.6 ya 2001 kama ilivyorekebishwa imeweka utaratibu wa uondoshaji wa mali za Serikali kwa njia ya mnada.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria hiyo, Wizara ya Fedha imepewa jukumu la kusimamia uondoaji wa mali za umma kwa kuzingatia uthamini sahihi wa magari hayo. Aidha, Ofisi ya Rais -

Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imepewa jukumu la kuidhinisha uondoshaji wa magari kwa kutoa mkopo au kuwauzia watumishi wa umma. Vilevile, Wizara ya Ujenzi inawajibika kufanya uthamini wa magari ya Serikali kabla ya kuidhinishwa kuondolewa kwa kuwakopesha au kuwauzia watumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la ukaguzi huu lilikuwa ni kutathmini kama Wizara ya Fedha na Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilisimamia kwa ufanisi uondoshaji wa Magari ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika ukaguzi huu, Wizara ya Fedha inahusika na uondoshaji wa magari kwa njia ya mnada na Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, inahusika na uondoshaji wa magari kwa njia ya kuwakopesha au kuwauzia watumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi huu ulihusisha Taasisi kumi (10) ambazo ni Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, Halmashauri ya Jiji ya Tanga, Mahakama ya Tanzania, Wizara ya Afya, Wizara ya Fedha, Wakala wa Barabara Tanzania, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Shirika la Utangazaji Tanzania na Shirika la Mawasiliano Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu masuala yaliyobainika katika ukaguzi huo kama ifuatavyo:-

2.1.2.1 Uwepo wa Magari ya Serikali 547 Ambayo Hayatumiki kwa Muda Mrefu

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulibaini kwamba jumla ya magari ya Serikali mia tano arobaini na saba (547) yalikuwa yameegeshwa kwenye Karakana za Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) na katika baadhi ya Taasisi za Serikali zilizotembelewa wakati wa ukaguzi. Aidha, baadhi ya magari yaliyotelekezwa hayakuwa kwenye mipango ya matengenezo au ya uondoshwaji. Ukaguzi ulibaini kuwa asilimia (43%) ya magari yalikuwa yameegeshwa kwenye Karakana za TEMESA kwa zaidi ya miaka mitatu (3)

kutokana na sababu mbalimbali kama vile ajali, matengenezo, maegesho, na kusubiri vibali vya uondoshaji.

Mheshimiwa Spika, uwepo wa magari mengi ya serikali yaliyoegeshwa kwa muda mrefu bila kutumika ulitokana na baadhi ya Taasisi kutofanya uhakiki wa hali za mali zake ili kufahamu kama ziondolewe au zitengenezwe. Kuwepo kwa magari mabovu ya Serikali ambayo yameegeshwa na hayatumiki kwa muda mrefu bila kuondoshwa kulikuwa na athari zifuatazo:-

a) Magari kuchakaa na kuharibika zaidi na kwa kasi hali inayopelekea kupungua kwa thamani ya magari haya pale ambapo Serikali itaamua kuyaondoa;
b) Madhumuni ya ununuzi wa magari hayafikiwi ipasavyo kwa sababu magari hayafanyi kazi kulingana na madhumuni yaliyokusudiwa;
c) Kuongezeka kwa gharama za matengenezo kutokana na uchakavu wa magari mabovu ambayo yamehifadhiwa na hayatumiki kwa muda mrefu; na
d) Upotevu wa rasilimali-fedha za umma.

2.1.2.2 Kutokuwepo kwa Uwazi wa Kutosha Katika Mchakato wa Uondoshaji wa Magari ya Serikali

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya CAG inabainisha kwamba ni Taasisi tatu (3) tu kati ya nane (8) zilizo tembelewa ambazo ziliondosha magari kwa kuwakopesha au kuwauzia watumishi wake zilitoa tangazo kwa watumishi. Taasisi ambazo hazikutoa tangazo ni Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, Halmashauri ya Jiji ya Tanga, Mahakama ya Tanzania, Wizara ya Afya, Wizara ya Fedha na Wakala wa Barabara. Dhumuni la kutoa tangazo la wazi lilikuwa ni kutoa fursa kwa kila mtumishi mwenye sifa na mwenye uhitaji wa gari kuweza kuwasilisha maombi ya kununua au kukopeshwa gari.

Mheshimiwa Spika, kutotolewa tangazo la wazi kulisibabisha baadhi ya watumishi kutopata fursa ya kuomba magari wakati huo na watumishi wengine waliweza kupata magari zaidi ya moja ndani ya kipindi kifupi.Hii inatokana na mwongozo uliopo, kutokumtaka Afisa Masuuli wa Taasisi husika kutoa tangazo pale

uondoshaji unapofanyika kwa kuwakopesha au kuwauzia watumishi wa umma. Aidha mwongozo uliopo haujaainisha idadi ya magari ambayo mtumishi mmoja anaweza kukopeshwa au kuuziwa na baada ya kipindi gani cha muda.

2.1.2.3 Dosari Katika Mchakato wa Uthaminishaji wa Magari ya Serikali Yanayouzwa au Kukopeshwa kwa Watumishi

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya CAG, mapitio ya taarifa za uthamini wa magari mia tano (500) uliofanywa na Wizara ya Ujenzi, ilibainika kuwa uthamini ulifanyika kwa kuangalia gharama (bei ya ununuzi, usafiri na bima hadi bandarini) iliyotumika wakati wa ununuzi na kutoa hali ya uchakavu.Ukaguzi ulibaini kuwa magari matano (5) yalithaminiwa kupita kiasi, matatu (3) yalithaminiwa kwa usahihi ambapo magari mia nne tisini na mbili (492), yalipunguzwa thamani ukilinganisha na thamani halisi wakati wa ununuzi.

Mheshimiwa Spika, dosari katika mchakato wa uthaminishaji wa magari ya Serikali kwa maeneo ambayo ukaguzi umefanyika unakadiriwa kuikosesha Serikali mapato ya takribani **shilingi bilioni 2.7**. Hali ya utofauti wa thamani iliyotumika kuuza magari ya Serikali iliyotumiwa na Wizara ya Ujenzi na iliyotumiwa na Wakaguzi ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 2.1 hapa chini:-

Jedwali Na 2.1: Hali ya utofauti wa uthaminishaji wa Magari

Idadi ya magari	Asilimia ya thamani halisi ya uthaminishaji (%)	Maelezo
5	(1) - (36)	Thamani iliongezwa
3	0	Ilikuwa sawa
310	10-100	Thamani ilipunguzwa
148	101-200	
34	201-836	

Chanzo: Taarifa ya CAG, Januari, 2024.

Mheshimiwa Spika, kama inavyonekana katika Jedwali Na.2.1 hapo juu, kulikuwa na dosari kwa Wizara ya Ujenzi kutohakiki kama bei ya gari, usafiri na bima (CIF) iliyokuwa inatumika wakati wa ukokotoaji wa thamani ya gari ndio halisi ukilinganisha na taarifa za gari wakati wa ununuzi zilizopo kwenye kanzidata ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, mapungufu ya mwongozo wa uthaminishaji wa magari ya Serikali wakati wa zoezi la uondoshaji yalithibitishwa pia kufuatia swali la Mhe. Esther Matiko, Mb Mjumbe wa Kamati alilouliza kwa CAG. Naomba kunukuu sehemu ya maelezo[3] ya swali lake kama ifuatavyo:-

Nukuu:- "...Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hii ya ukopeshaji. Ninataka tu nijue labda kuna miongozo like ambayo ina-set kuhusiana na hizo make za gari na mwaka kwa sababu kama inakuwa tu iko open tu hivi, a Landcruiser, irrespective of its condition inaweza hata ikawa disposed for five million shillings, six million shillings, three million shillings. Sasa nataka nijue, wakati wanafanya kaziwaliweza kuona kama kuna miongozo whatsoever. Kule kwingine wametueleza kwamba hata walikuwa hawaja-set muda wa vibali, yaani ile cycle ya power ya ku-dispose ilikuwa hamna, sasa hivi ndiyo wame-set three months. Mheshimiwa Mwenyekiti, je, huku sasa kwenye kukopeshana? Walikuta kuna mwongozo wowote? Hilo tu?..." Mwisho wa Nukuu.

Mheshimiwa Spika, majibu[4] ya Ndugu. George C. Haule ambaye ni Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yalikuwa kama ifuatavyo, naomba kunukuu:-

Nukuu:- "...Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kuna sehemu unaenda inasema kwamba, "Gari ya Serikali matumizi yake mwisho yake mwisho miaka mitano au likifika kilometa labda 200,000 au 250,0000." Then, sehemu nyingine inasema, "Gari likitaka kuondolewa, basi lithaminishwe kwanza". Kwa hiyo, ilikuwa inatoka kwenye vipande tofauti tofauti vya miongozo

[3] Rejea Ukurasa wa 11 wa Majadiliano ya Kamati,Taarifa Rasmi za Bunge Kikao cha Nne ,Tarehe 18 Januari, 2024.

[4] Rejea Ukurasa wa 11-12 wa Majadiliano ya Kamati,Taarifa Rasmi za Bunge Kikao cha Nne,Tarehe 18 Januari, 2024.

lakini kwenye ukaguzi tukasema kwamba, hili lilikuwa ni suala ambalo lingeweza kuwa na mwongozo mmoja.
Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ingeweza kusaidia kuhakikisha kwamba ina- harmonize kwenye Serikali nzima kuwa na utaratibu ambao unafanana wakati wa kuyaondoa haya magari. Kwa hiyo, ni eneo mojawapo ambalo tulikuwatunaona kwamba ni muhimu. Mwisho wa Nukuu.

2.1.2.4 Uthamini wa Magari Kutozingatia Gharama Halisi za Gari Inayouzwa au Kukopeshwa

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati katika Taarifa ya CAG ulibainisha kwamba tathmini ya magari kutoka Wizara ya Ujenzi haikuzingatia thamani ya awali wakati gari linanunuliwa, bali ilizingatia gharama za gari hadi linafika bandarini.

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida wakati wa ununuzi wa gari kunakuwa na gharama mbalimbali kama vile kodi ya ushuru wa forodha , kodi ya ongezeko la thamani(VAT), ushuru wa bidhaa, ada ya forodha, ushuru wa maendeleo ya reli na gharama ya usajili ambayo kwa kawaida huwa zaidi ya asilimia (50%) ya gharama za jumla za ununuzi wa gari. Kutokujumuishwa kwa gharama hizi kulipelekea thamani halisi ya magari kuwa ndogo na hivyo kusababisha magari kuondoshwa kwa thamani ndogo kuliko uhalisia.

Mheshimiwa Spika, mathalani kupitia mapitio ya thamani ya awali ya gari wakati yananunuliwa kwa magari ishirini na saba (27), ilibainika tofauti ya takribani asilimia (83%) kama uthamini wa magari hayo ishirini na saba (27) ungefanywa kwa kujumuisha gharama zote zilizoingiwa wakati wa ununuzi wa gari hilo. Matokeo ya hatua hiyo ni kupungua kwa thamani ya magari ambapo Serikali ingepata kiasi cha **shilingi 956,774,529.90** endapo magari hayo ishirini na saba (27) yangeuzwa kwa thamani halisi.

Mheshimiwa Spika, dosari za kutojumuisha gharama nyinginezo za gari wakati wa kuuza na kukopesha magari ya Serikali zilitokana na matumizi ya Mwongozo na Kanuni za Ukokotoaji za mwaka 1988, na ambao haujumuishi gharama zote zilizoingiwa wakati wa ununuzi wa gari. Aidha, Mthamini Mkuu wa Serikali hakuhusishwa

wakati wakufanya uthaminishwaji wa magari wakati wa uondoshaji, pamoja masharti ya Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathaminishaji Na.7 ya 2016[5].

2.1.2.5 Kuchelewa Kutoa Vibali vya Uondoshaji wa Magari kwa Mnada au Kukopesha

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya CAG imebainisha kwamba, Wizara ya Fedha ilikuwa inatumia takribani siku hamsini na saba (57) hadi siku elfu mbili mia mbili ishirini na sita (2226) kutoa idhini ya gari kuondoshwa. Pia, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ilikuwa inachukua kati ya siku nne (4) hadi siku elfu mbili na hamsini (2050) kutoa idhini. Uchelewashaji huu ulisababishwa na kutokuwa na muda uliowekwa kwenye kukamilisha utoaji wa vibali hivyo. Pia, zoezi hili halifanyiki kwa kutumia mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ambayo, ingeongeza ufanisi.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi wa kina wa matokeo ya ukaguzi huo wa ufanisi, Kamati ilikutana siku ya Alhamisi tarehe 18 Januari, 2024 ili kujadiliana na Maafisa Masuuli ambao Mafungu yao yalihusika na hoja za ukaguzi huo.Maafisa Masuuli waliohudhuria ni Afisa Masuuli Wizara ya Fedha, Afisa Masuuli OR – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Afisa Masuuli – TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, katika mapitio ya taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi, ilibainika kwamba jumla ya mapendekezo kumi (10) yalitolewa, ikiwa matano (5) kwa Wizara ya Fedha na matano (5) kwa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Baada ya kupitia majibu yaliyowalishwa mnamo Disemba, 2023, ilibainika kwamba Wizara ya Fedha ilipewa mapendekezo matano (5) ambapo mapendekezo manne (4) yako katika hatua nzuri za utekelezaji na pendekezo moja (1) lipo kwenye hatua za awali za utekelezaji. Aidha, kwa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora yalitolewa mapendekezo matano (5), ambapo

[5] Rejea masharti ya Kifungu cha 6(1)(a) cha Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathaminishaji Na.7 ya 2016

mapendekezo manne (4) yapo katika hatua nzuri za utekelezaji na moja (1) lipo kwenye hatua za awali za utekelezaji

Mheshimiwa Spika, katika kujibu hoja za ukaguzi huu, Afisa Masuuli OR – Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora aliifahamisha Kamati kuwa walitoa mwongozo kwa Taasisi za Serikali kwa barua ya tarehe 14 Februari, 2023 kuhusu uondoshaji wa magari ya Serikali.Mwongozo huo ulisisitiza suala la uwazi na kutenda haki katika mchakato wa uondoshaji wa magari ya
Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Afisa Masuuli Wizara ya Fedha aliifahamisha Kamati kuwa, ni sahihi kumekuwa na mapungufu katika mchakato wa uondoshaji wa magari ya Serikali.Sababu kubwa ilikuwa ni kutumia mfumo wa zamani (manual) ambao haukuwa na ufanisi. Hata hivyo Wizara ya Fedha kwa sasa wameunda mfumo wa Usimamizi wa Mali za Serikali (Government Assets Management System, GAMIS) ambao utaboresha shughuli za uondoshaji wa magari ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba kunukuu sehemu ya maelezo[6] ya Ndugu Jenifa Omolo,Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha aliyoyatoa mbele ya Kamati kufafanua kuwa, matumizi kamili ya mfumo wa GAMIS kwa "modules" zote yataondoa changamoto ya uondoshaji wa magari ya Serikali. Maelezo hayo ni kama ifuatavyo:-
Nukuu:- "...Mheshimiwa Mwenyekiti, pili hata uondoshaji kwa sababu tunaenda kwenye mfumo wa GAMIS, mfumo huu kwanza unaingiza asset zote za Serikali lakini pia mtu atakapokuwa anataka kufanya disposal hata kwa Mabalozi watakuwa wanatumia mfumo. Kwa hiyo, mchakato mzima ule wa disposal utakuwa umepungua na utakuwa umerahisishwa na suala la kucheleweshwa litakuwa limeisha kwa sababu mfumo utakuwa unafanya kazi…" Mwisho wa Nukuu.

Mheshimiwa Spika, changamoto hii ya uondoshaji wa magari ya Serikali haikuwa upande wa Serikali Kuu pekee bali pia katika

[6] Rejea Ukurasa wa 35 wa Majadiliano ya Kamati, Taarifa Rasmi za Bunge, Kikao cha Nne, Tarehe 18 Januari, 2024.

Mamlaka za Serikali za Mitaa. Naomba kunukuu sehemu ya maelezo ya Naibu Katibu Mkuu, OR – TAMISEMI Ndugu Rogatus Mativila akielezea kuhusu hoja hii na namna watakavyochukua hatua. Sehemu ya maelezo[7] hayo ni kama ifuatavyo:-

Nukuu:- "...Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni kweli nakubaliana kwamba taasisi na halmashauri zilizopo chini ya TAMISEMI, kuna hiyo changamoto ya kutokuwasilisha haraka mahitaji ya ku-dispose magari ambayo yameharibika kiasi kwamba hayawezi kutumika tena... Pia kukosa uwazi wa kukopesha watumishi...Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niseme tu kwamba sisi tunalichukua hili ili iwe pia ni sehemu ya maelekezo ya TAMISEMI kwenye halmashauri zetu zote na taasisi zingine kwamba, miongozo hii ambayo imetolewa ifuatwe na sisi tuweze kusimamia kwa karibu kuhakikisha kwamba miongozo hiyo inafuatwa namna ya ku-dispose magari, kukopesha watumishi au kutangazakuyauza kwa mnada..."

Mheshimiwa Spika, hoja ya Kamati katika eneo hili inabaki kwamba, changamoto tangu kuanzishwa kwa Mfumo wa GAMIS mwaka 2018, moduli ya uondoshaji wa magari ya Serikali bado haijaanza kutumika ipasavyo kwa takribani miaka mitano (5) sasa hivyo kupelekea mapungufu katika mchakato wa uondoshaji wa magari ya Serikali.

2.1.3 Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi Katika Usimamizi wa Mipango na Ujenzi wa Mifumo ya TEHAMA Serikalini

Mheshimiwa Spika, kwa lengo la kufikia dira ya 2025, Serikali ilitambua umuhimu wa kuboresha sera zake ambapo Sera ya Taifa ya TEHAMA iliundwa mwaka 2003, na kupitiwa mwaka 2016. Aidha, mipango mingine katika kuimarisha masuala ya TEHAMA ilitekelezwa ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa Wakala wa Serikali Mtandao mwaka 2012 na baadaye (mwaka 2019) ilibadilishwa na kuwa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa ajili ya kusimamia, kuratibu na kukuza uendeshaji wa huduma za Serikali mtandao, usimamizi wa data za kielektroniki na masuala mengine yanayohusiana na TEHAMA kwenye Taasisi za Umma.

[7] Rejea Ukurasa wa 47 wa Majadiliano ya Kamati,Taarifa Rasmi za Bunge, Kikao cha Nne, Tarehe 18 Januari, 2024.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi ambazo zimefanywa na Mamlaka ya Serikali Mtandao ikiwemo kuweka mikakati ambayo inalenga kuhakikisha kuwa kuna usimamizi mzuri wa upangaji na upatikanaji wa mifumo ya TEHAMA kwenye Taasisi za Umma, mipango ya Serikali mtandao imeendelea kukabiliana na changamoto ambazo zinahitaji ufumbuzi wa haraka na wa muda mrefu ili kuhakikisha utendaji wa Serikali unaboreshwa na kuendeshwa kwa urahisi na kwa viwango vya usalama wa Serikali Mtandao kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na kufichuliwa kwa miundombinu ya serikali ya TEHAMA. Vilevile, ongezeko la Vifaa vya TEHAMA limeongeza vitisho vya usalama na mashambulizi ya mitandaoni ambayo yanahatarisha au kusababisha hasara kwa mali na nyaraka za serikali. Kwa mujibu wa Ripoti ya Usalama wa Mitandao Tanzania ya mwaka 2017, Tanzania ilikadiriwa kupoteza **Dola za Marekani milioni 99.5** kila mwaka kutokana na mashambulizi ya kimtandao.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto zilizoainishwa hapo juu, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliamua kufanya ukaguzi katika usimamizi wa Mipango na Ujenzi wa Mifumo ya TEHAMA kama unavyofanywa na Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora pamoja na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) ili kubaini sababu zinazopelekea udhaifu uliobainishwa katika sekta ndogo ya Serikali Mtandao Nchini, na kutoa mapendekezo ambayo yataboresha utoaji wa huduma za Serikali Mtandao kwa Taasisi za Umma hapa Nchini.

Mheshimiwa Spika,naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu masuala makuu matano (5) yaliyobainika katika ukaguzi huo kama ifuatavyo:-

2.1.3.1 Mapungufu Katika Uaandaaji wa Miradi ya TEHAMA

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya CAG inabainisha kwamba, asilimia (86%) ya maandiko ya awali ya mradi (concept notes) kutoka kwenye Taasisi za Umma kuhusiana na miradi ya TEHAMA yalikataliwa kwa sababu yalikuwa yana makosa au yalihitaji

maboresho. Ukaguzi ulibaini kuwa maelezo mengi ya awali ya miradi yaliandaliwa kwa uharaka bila kuzingatia miongozo au kanuni za Serikali mtandao zilizopo.

Mheshimiwa Spika, vilevile taarifa ya ukaguzi ilifafanua kuwa, kati ya mwaka 2017 na 2022, jumla ya mapendekezo mia sita arobaini na tano (645) yalitolewa kama ushauri kwa Taasisi za Umma kutokana na maandiko ya miradi yaliyokuwa yamewasilishwa. Hata hivyo, ni mapendekezo arobaini na nne (44) ambayo ni sawa na asilimia saba (7%) yalitekelezwa kwa wakati na yaliyobaki yalicheleweshwa kwa nyakati tofauti. Kwa mfano, ukaguzi ulibaini kuwa asilimia themanini na tano (85) ya mashauri yaliyotolewa yalizidi kipindi cha siku sitini (60), pia kulikuwa na mapendekezo yaliyochukua zaidi ya miaka miwili (2) ili kupata maelezo ya ushauri.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi zaidi wa Kamati ulibaini kuwa sababu zilizopelekea mapungufu kwenye maandiko ya awali ya miradi mingi ya TEHAMA Serikalini ni ukosefu wa uelewa kwa watumishi na Taasisi za Umma kuhusu Kanuni za Serikali za Mtandao na Miongozo ya Maandalizi ya maandiko ya awali ya miradi ya TEHAMA pamoja na wajibu wa kushiriki wakati wa kuandaa mahitaji ya mifumo kabla ya kuanza manunuzi na ujenzi wa mifumo husika.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya ushiriki hafifu wa watumishi wenye wajibu na majukumu katika hatua zote za kupata mfumo ikiwa ni pamoja na maandalizi ya andiko la awali la mradi ulisababisha kuwepo kwa mifumo ya TEHAMA ambayo haikuweza kutoa huduma kwa wakati na ubora kama ilivyokusudiwa.

2.1.3.2 Ufanisi Katika Uaandaji wa Mifumo ya TEHAMA

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili uchambuzi wa Kamati katika taarifa ya ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na mapungufu katika ushirikishwaji wa wadau katika mchakato wa kuandaa mifumo ya TEHAMA Serikalini.Mathalani, taarifa inafafanua kwamba kiwango cha juu cha ushirikishwaji wa wadau kilibainika kwa EWURA na GPSA ikifuatiwa na TRA kwa asilimia (83%), (80%) na (62.5%) mtawalia. Kiwango cha chini cha ushirikishwaji wa wadau

kilibainika katika Wizara ya Kilimo na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) kwa asilimia (33%) na (37.5%) mtawalia.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili taarifa iliendelea kufafanua kwamba baadhi ya wadau walihusika kwa kiwango fulani wakati wa kukusanya mahitaji ya sehemu yake ya utendaji wa Taasisi au kwenye moduli. Hata hivyo,kuna sehemu nyingine zilibainika kushiriki kikamilifu katika mchakato wa kukusanya mahitaji ya kuboresha utendaji kazi wa Taasisi husika.

Mheshimiwa Spika, athari za kutohusisha wadau kulisababisha maandalizi ya mahitaji ya mtumiaji na mahitaji ya kiufundi ya mifumo kuwa duni. Uainishaji wa mahitaji ya mifumo yasiofaa yalisababisha kujenga au kusanifiwa kwa mifumo yenye mapungufu, ambayo ilipelekea kusanifiwa upya baada ya ununuzi wake. Kwa mfano, mifumo kumi na nne (14) ya TEHAMA kutoka Taasisi za Umma zilizotembelewa na wakaguzi ilikuwa imejengwa upya ili kukidhi mahitaji mapya ya mtumiaji.

2.1.3.3 Ufanisi Katika Ujenzi wa Mifumo ya TEHAMA

Mheshimiwa Spika,ukaguzi ulibaini kuwa, kulikuwa na ujumuishaji na ushirikiano mdogo wa mifumo iliyopo kwenye Taasisi za Umma, mazingira ya ndani yasiyo rafiki ya kuhifadhi mifumo, upatikanaji wa mifumo bila idhini ya Mamlaka ya Serikali Mtandao na uwezo mdogo wa ndani wa watumishi katika kujenga mifumo na kusimamia kikamilifu utendaji kazi wa mifumo husika.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya nyaraka za miradi yalibaini kuwa baadhi ya Taasisi za Umma hazikuwa na udhibiti madhubuti wakati wa hatua za awali za kuanzishwa kwa mradi kabla ya kuwasilisha mapendekezo ya mradi kwa Mamlaka ya Serikali Mtandao. Aidha, hatua tano (5) kati ya sita (6) muhimu za upatikanaji wa mradi, hazikusimamiwa vya kutosha na Mamlaka ya Serikali Mtandao, hivyo kuwa na athari za jumla katika kufuata Sheria ya Serikali Mtandao na Kanuni zake. Hatua hizo ni zoezi la uendeshaji wa manunuzi ya mifumo, uingiaji mikataba ya kazi za ujenzi, ujenzi wa mifumo husika, majaribio ya mifumo na makabidhiano ya mifumo**.**

Mheshimiwa Spika, vilevile ukaguzi ulibaini kuwa miongoni mwa mapungufu yaliyoripotiwa zaidi ni pamoja na utendaji kazi wa chini ya kiwango kutokana na mtandao kwa asilimia thelathini na mbili (32), kushindwa kwa mfumo kufanya kazi kutokana na mapungufu ya kiufundi ya utengenezaji wake na udhaifu mwingine wa kimfumo kwa asilimia kumi na nane (18%), maoni hasi ya kuhusu mifumo kwa asilimia kumi na sita (16) na asilimia kumi na moja (11%) ya mifumo ambayo ilitelekezwa na taasisi husika. Mapitio ya mifumo ya TEHAMA iliyoko katika Taasisi za Serikali zilizotembelewa na wakaguzi yalibaini kuwa asilimia sabini (70) ya mifumo iliyotengenezwa ilikuwa ikifanya kazi yenyewe bila kuwa na uwezo wa kuwasiliana na mifumo mingine ndani au nje ya Taasisi husika.

2.1.3.4 Ufanisi Katika Upatikanaji na Makabidhiano ya Mifumo

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili uchambuzi wa Kamati katika Taarifa ya CAG ulibaini kwamba, majibu ya majaribio na taarifa za Mifumo ya TEHAMA iliyopatikana au kutengenezwa yalibaini ufanisi duni kwenye majaribio ya mifumo ya TEHAMA. Mapitio ya nyaraka za majaribio yalibaini kuwa, Taasisi nyingi zilifanya majaribio ya mtumiaji, lakini, chache zilifanya majaribio ya muunganiko wa mifumo au moduli nyingine.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulihusisha Taasisi za Umma kumi na tatu (13) ambapo jumla ya mifumo sitini na nne (64) ya TEHAMA ilikaguliwa, ambayo kumi na tatu (13) ilitengenezwa na wataalamu wa ndani ya Taasisi husika, minne (4) ikiwa ni mifumo shirikishi ya Serikali na mifumo mingine arobaini na saba (47) ilinunuliwa au kutengenezwa na wataalamu wa nje ya Taasisi husika. Ukaguzi ulibaini kuwa, mifumo kumi na tatu (13) iliyotengenezwa na wataalamu wa ndani, ilifanyiwa majaribio ya kukubaliwa na watumiaji pekee na hakukufanyika majaribio mengine ya kimfumo. Aidha, ni mifumo miwili (2) pekee ambayo ilifanyiwa majaribio ya muunganiko na mifumo au moduli nyingine.

2.1.3.5 Mapungufu Katika Shughuli za Uratibu Katika Kujenga Mifumo ya TEHAMA Serikalini

Mheshimiwa Spika, mapitio ya kazi za ufuatiliaji katika Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora yalibaini kuwa, Wizara haikuwa na mfumo madhubuti wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa sera na mikakati mingine inayohusiana na TEHAMA ambayo ni pamoja na kupanga na kujenga mifumo ya TEHAMA ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulibaini kuwa, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa sasa ilikuwa inasimamia sera na miongozo iliyopitwa na wakati kuhusu mifumo ya TEHAMA. Mathalani, mapitio ya Taarifa za Utendaji kazi kuanzia mwaka 2017 hadi 2022 kutoka Wizarani, yalibainisha kuwa Wizara ilikuwa inategemea Mkakati wa Usalama Mtandaoni pamoja na Mwongozo wa Matumizi Bora ya TEHAMA Serikalini ambayo imetumika kwa zaidi ya miaka mitano (5) bila kufanyiwa mapitio.

Mheshimiwa Spika, kutofanyika kwa mapitio hayo kuliathiri usahihi wa miongozo hiyo katika kuongoza matumizi bora ya TEHAMA Serikalini pamoja na mapendekezo yake ya hatua na utendaji katika matumizi bora ya huduma na vifaa vya TEHAMA Serikalini. Aidha, Mkakati wa Usalama Mtandaoni uliendelea kuwa na mikakati, malengo na viashiria vya utendaji vilivyopitwa na wakati katika kukabili uvamizi na mashambulizi ya kimtandao.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi wa masuala hayo matano (5) yaliyobainika katika ukaguzi huu, mnamo tarehe 23 Januari 2024, Kamati ilikutana na Afisa Masuuli, OR – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao kujadili namna walivyotekeleza mapendekezo ya ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, katika mapendekezo kumi na mbili (12) yaliyotolewa, mapendekezo manne (4) sawa na asilimia (33%) yametekelezwa kikamilifu, mapendekezo matano (5) sawa na asilimia arobaini na mbili (42%) utekelezaji wake upo katika hatua nzuri, na mapendekezo matatu (3) sawa na asilimia ishirini

na tano (25%) utekelezaji wake upo katika hatua za awali. Hakuna pendekezo ambalo halikutekelezwa kabisa. Hali ya utekelezaji wa mapendekezo imechambuliwa katika Jedwali Na.2.2 Hapa chini:-

Jedwali Na 2.2: Kiwango cha utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi katika Ujenzi wa Mifumo ya TEHAMA

Eneo la Maboresho	Jumla ya Mapendekezo	Hali na Kiwango cha Utekelezaji			
		Idadi ya Mapendekezo Yaliyotekelez wa Kikamilifu	Idadi ya Mapendekeo yaliyo katika hatua za awali za Utekelezaji	Idadi ya Mapendekezo yaliyo katika hatua nzuri za utekelezaji	Idadi ya Mapendekezo Yasiyotekelezwa Kabisa
Mfumo wa Utendaji Kazi	3	2	1	0	0
Ufuatiliaji na Tathmini	1	0	1	0	0
Uanzishaji na Uendelezaji	1	0	0	1	0
Usimamizi wa Mawasiliano ya Kimfumo	2	0	0	2	0
Usimamizi wa Utekelezaji	3	2	0	1	0
Usimamizi Udhibiti Ubora	1	0	1	0	0
Usimamizi Rasilimali Watu	1	0	0	1	0
Jumla	**12**	**4**	**3**	**5**	**0**

Chanzo: Uchambuzi wa Kamati Kutokana na Taarifa ya Utekelezaji wa Mapendekezo Yaliyotolewa kwa Wakaguliwa, Januari, 2024.

Mheshimiwa spika,kama ufafanuzi unaonekana katika jedwali Na. 2.2 hapo juu, mapendekezo matatu (3), utekelezaji wake ulikuwa katika hatua za awali za utekelezaji. Katika kujibu hoja zinasohusu mapendekezo hayo ya ukaguzi, Afisa Masuuli Ofisi ya Rais-

Utumishi na Utawala Bora aliifahamisha kamati kuwa ujenzi wa mifumo ya TEHAMA unalenga kuboresha utendaji kazi wa Serikali.Alifafanua kwamba, Serikali ipo katika hatua za mwisho za maboresho ya mfumo wa utendaji kazi na inatarajiwa kabla ya mwaka huu wa fedha kuisha utakuwa umekamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa hoja inayohusu kusomana kwa mifumo, Afisa Masuuli OR- Utumishi na Utawala Bora aliifahamisha Kamati kuwa, kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali mtandao (eGA) hadi sasa taasisi 109 zimeunganishwa katika mfumo wa ubadilishanaji taarifa Serikalini. Vilvile hadi sasa mifumo 117 inayotumiwa na Serikali inasomana.

2.1.4 Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi Katika Usimamizi wa Urasimishaji wa Makazi Yasiyopangwa

Mheshimiwa Spika, urasimishaji wa makazi yasiyopangwa ni mchakato ambao Mamlaka za Upangaji Miji zinabainisha sehemu za ardhi ambazo hazijapangwa katika maeneo ya mijini na kupitia mchakato wa urasimishaji kwa kupanga, kupima na kutoa hati miliki (kumilikisha) kwa wahusika. Kupitia urasimishaji, maeneo yasiyopangwa huboreshwa na kuwezesha utoaji wa huduma za kijamii za msingi za miundombinu kama vile barabara, maji na huduma za umeme kwa jamii husika. Utaratibu wa urasimishaji hutolewa kupitia Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 na Sheria ya Mipango Miji ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, urasimishaji wa makazi yasiyopangwa unasimamiwa na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Ofisi ya Rais -TAMISEMI kupitia Mamlaka za Upangaji huanza kwa kufanya utambuzi wa maeneo yasiyopangwa katika maeneo ya mijini, kupanga na kupima na kisha Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi hutoa hati za umiliki kwa wahusika. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ina jukumu la kuandaa miongozo ya urasimishaji, kupitisha michoro ya urasimishaji iliyoandaliwa na Mamlaka za Upangaji, kuandaa hati za umiliki wa ardhi na kuzipeleka Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya kuzigawa kwa wahusika.

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la ukaguzi huu lilitokana na kuwepo kwa ongezeko la ukosefu wa fursa ya mapato ya Serikali yatokanayo na viwanja na makazi yasiyopimwa na kupangwa.Mathalani, kwa rejea ya hotuba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ya tarehe 10 Januari, 2021 ucheleweshaji wa urasimishaji na utoaji wa hati za umiliki kwa wananchi umeikosesha Serikali mapato ambayo yanatokana na malipo ya kodi za ardhi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na sababu hiyo, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliamua kufanya ukaguzi wa ufanisi katika Usimamizi wa Urasimishaji wa Makazi yasiyopangwa. Lengo la ukaguzi lilikuwa ni kubaini maeneo yenye mapungufu na kutoa mapendekezo ya kuboresha ili kuweza kufikia malengo yaliyokusudiwa. Ukaguzi ulihusisha kipindi cha miaka mitano (5) ya fedha cha kuanzia mwaka wa fedha 2017/18 hadi 2021/22. Kipindi hiki kilichaguliwa kwani ni kipindi ambacho Serikali ilianza kushirikisha makampuni binafsi katika urasimishaji wa makazi yasiyopangwa.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya ukaguzi huu wa ufanisi kuhusu kupanga na kurasimisha makazi ni kama ifuatavyo:-

a) Ukaguzi ulibaini kuwa, katika kipindi cha miaka mitano (5) iliyopita kutoka mwaka wa fedha 2015/16 hadi 2020/21, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, hazikujumuisha ipasavyo shughuli za urasimishaji kwenye mipango yao ya kimkakati na mipango ya mwaka. Aidha, Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi katika bajeti yake ya mwaka kwa ajili ya shughuli za maendeleo kwa miaka miwili (2) mfululizo yaani 2017/18 hadi 2018/19 haikutenga bajeti kwa ajili ya shughuli za urasimishaji. Kwa miaka mingine ya fedha kiwango cha juu cha bajeti kilitengwa katika mwaka wa fedha 2020/21 kilikuwa ni asilimia mbili (2) ya kiasi cha bajeti kwa ajili ya upangaji miji ambayo ni sawa na **shilingi milioni 80**;

b) Ukaguzi ulibaini Mpango Mkakati wa OR - TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2015/16-2020/21 na 2021/22-2025/26 ulibainisha kuwa, OR - TAMISEMI haikutenga fedha katika bajeti yake ili

kuwezesha shughuli za urasimishaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa miaka mitano (5) iliyopita
(2017/18 hadi 2021/22);

c) Ukaguzi ulibaini kuwa, hadi mwishoni mwa mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya vipande vya ardhi 1,137,437 kati ya 2,315,170 vilivyokuwa vimepangwa, sawa na asilimia (49%) ndio viliweza kupimwa na kuidhinishwa. Aidha, uchangiaji wa gharama za upimaji usiojitosheleza toka kwa wananchi kulichangia,kuchelewa kukamilisha upimaji na hivyo kuchelewesha zoezi la ukamilishaji wa utoaji hati za umiliki;

d) Ukaguzi ulibaini kuwa vipande 443,525 kati ya 1,137,437 ya vipande vya ardhi vilivyokuwa vimepimwa (sawa na 39%) vilitolewa ankara kwa ajili ya uandaji wa hati miliki. Hii ina maana kwamba asilimia (61%) ya wamiliki wote wa vipande vya ardhi vilivyopimwa hawakupewa ankara kwa ajili ya kulipia hati ili ziandaliwe. Hata hivyo, ni vipande 171,210 pekee kati ya 443,525 ambavyo wamiliki wake walipewa ankara kwa ajili ya uandaaji wa hati miliki, waliweza kuandaliwa hati. Hii inaonesha mwitikio mdogo wa wananchi kulipia gharama za hati, uliochangiwa na uhamasishaji wa wananchi usiotosheleza ili kutambua umuhimu wa kuchangia gharama za urasimishaji; na

e) Mapungufu ya kiuratibu katika shughuli za upimaji na urasimishaji kati ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na OR – TAMISEMI. Ukaguzi ulibaini kuwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na OR – TAMISEMI hazikuwa na utaratibu rasmi wa kuratibu shughuli za urasimishaji zinazotekelezwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Ofisi za Ardhi za Mikoa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na dosari zilizobainishwa hapo juu, CAG alitoa mapendekezo kadhaa ya utekelezaji kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na OR – TAMISEMI. Matokeo ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi yamebainisha kuwa mapendekezo ishirini na moja (21). Hata hivyo, hapakuwa na pendekezo lililotekelezwa kikamilifu. Aidha, mapendekezo tisa (9) kati ya ishirini na moja (21) yapo

katika hatua za awali za utekelezaji na zinazoridhisha, na mapendekezo matano (5) kati ya ishirini na moja (21) yapo katika hatua za awali za utekelezaji. Vilevile,matokeo ya ufuatiliaji yamebainisha kuwa mapendekezo saba (7) kati ya mapendekezo ishirini na moja (21) hayajatekelezwa kabisa.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 16 Januari, 2024, Kamati ilikutana na Afisa Masuuli Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Afisa Masuuli OR – TAMISEMI ili kujadili hoja za ukaguzi wa ufanisi ambazo hazijatekelezwa.Kwa hoja iliyohusu dosari za urasimishaji wa makazi, Afisa Masuuli Wizara ya ardhi aliifahamisha Kamati kuwa katika suala zima la urasimishaji katika Nchi yetu, halikufanyika vizuri toka tulipoanza ule mpango wa urasimishaji wa miaka kumi (10), kuanzia mwaka 2013 – 2023 na hasa katika upande wa viwanja.

Mheshimiwa Spika, Afisa Masuuli Ardhi aliendelea kufafanua kwamba, maboresho yaliyofanyika ili kutatua dosari zilizobainika ni pamoja kuandaa mwongozo wa kuhakikisha kwamba urasimishaji sasa ufanywe kwa mikataba ambayo inaingiwa katika yale maeneo ambayo walitumia kampuni. Aidha mwongozo unalekeza kuingiwa mikataba kati ya kampuni na ofisi za Wakurugenzi ili kudhibiti fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, kwa hoja zilizohusu upatikanaji wa bajeti kwa ajili ya urasimishaji wa makazi yasiyopangwa na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali, Afisa Masuuli Wizara ya Ardhi alitoa ufafanuzi wa Mpango wa Serikali wa " Land Tenure Improvement Programme' ambao utatatua changamoto ya kibajeti. Naomba kunukuu sehemu ya maelezo[8] ya Afisa Masuuli Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Ndugu Eng. Anthony Sanga aliyoyatoa mbele ya Kamati kuhusu hoja hiyo kama ifuatavyo:-
Nukuu:- "…Mheshimiwa Mwenyekiti, zile hati ambazo tulikuwa tunatarajia kuzipata katika muda huo ambao tumekosa kuzipata, basi tumeziingiza katika mradi. Katika mwaka huu tu wa fedha wa 2023/2024, jumla ya shilingi bilioni 16 zimepangwa ambapo viwanja laki tano vitapatiwa hati. Kwa hiyo, tunaamini katika huu

[8] Rejea Uk. 42 wa Majadiliano ya Kamati, Taarifa Rasmi za Bunge, Kikao cha Pili, Tarehe 16 Januari, 2024.

muda mfupi uliobaki mpaka mwaka 2025 kama Mjumbe ambavyo ameuliza, tutakuwa tumefanikiwa kupata viwanja vyenye hati jumla ya milioni mbili, kupitia mpango huu au mradi huu wa LTIP (Land Tenure Improvement Program).Mheshimiwa Mwenyekiti, ambapo sehemu kubwa ya fedha za mradi huu ambazo jumla ya fedha ya mradi ni dola milioni 150 lakini dola milioni 62 zimepangwa kwa ajili ya urasimishaji wamakazi holela Nchini na jumla ya hati milioni mbili zitapatikana kupitia mradi huu…" Mwisho wa Nukuu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo ya kina ya Afisa Masuuli Ardhi na Afisa Masuuli OR- TAMISEMI, Kamati ina hoja kuwa eneo hili la urasimishaji wa ardhi linaipotezea Serikali mapato. Kwa msingi huo Kamati imetoa pendekezo la maboresho katika sehumu ya tatu (3) ya Taarifa hii.

2.1.5 Taarifa ya Ukaguzi wa Kiufundi Katika Ujenzi wa Shule za Sekondari Chini ya Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP)

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kuboresha Ubora wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP)[9] unafadhiliwa kwa **Dola za Marekani milioni 500**. Mradi huu unafadhiliwa na Jumuiya ya Maendeleo ya Kimataifa (IDA)[10] na unalenga kuongeza ufikiaji wa elimu ya sekondari Nchini katika Halmashauri mia moja themanini na nne (184). Mradi huu unalenga kutoa mazingira mazuri ya kujifunzia kwa wasichana na kuboresha ukamilishaji wa elimu bora ya sekondari kwa wasichana na wavulana.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi chote cha mradi, inakadiriwa kuwa mradi utanufaisha moja kwa moja wanafunzi wapya na waliopo wapatao milioni 6.5 ambapo wasichana ni milioni 3.2 kati ya wanafunzi hao wote.

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la ukaguzi wa kiufundi lilikuwa ni kutathmini kama Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI) na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

[9] Secondary Education Quality Improvement Project (SEQUIP).

[10] The International Development Association (IDA).

zilisimamia ipasavyo ujenzi wa shule za sekondari unaotekelezwa chini ya Mradi wa Kuboresha Ubora wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP) ili kuhakikisha upatikanaji wa thamani ya fedha.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulihusisha ujenzi wa shule za sekondari za Kata na Mikoa Nchini katika Mikoa saba (7) ambayo ni Pwani, Lindi, Kagera,Tanga, Shinyanga, Songwe na Singida. Aidha, ukaguzi ulihusisha tathmini ya utekelezaji wa mradi katika vipengele sita vya mradi ambavyo ni uandaaji wa mipango, usanifu wa mradi, manunuzi, utekelezaji, usimamizi wa fedha, mazingira, na afya ya jamii, usalama na rasilimali watu.

Mheshimiwa Spika, mawanda ya ukaguzi huu yalizingatia pia miaka yote ya fedha chini ya utekelezaji wa mradi kuanzia mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2021/22. Kipindi hiki kilichaguliwa ili kuhusisha hatua zote za utekelezaji wa mradi. Pia, kilimuwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kupima kama malengo ya mradi aliyokusudiwa yamefikiwa au kuna uwezekano wa kufikiwa baada ya kukamilika kwa mradi.

Mheshimiwa Spika, masuala yaliyobainika katika ukaguzi huu ni kama ifuatavyo:-

a) Ukaguzi ulibaini kuwa, katika hatua za kuainisha maeneo kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari, hapakuwa na utaratibu wa kuandaa hati miliki ya maeneo yaliyochaguliwa kwa ajili ya ujenzi. Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa katika shule zote ishirini na nne (24) zilizotembelewa na Timu ya Wakaguzi, maeneo yake ya ujenzi hayakuwa na hati miliki.Kukosekana kwa taratibu za kuandaa hati za umiliki kulisababishwa na uharaka wa kutekeleza ujenzi wa shule za sekondari. Hivyo basi, miradi haikuwa na hati miliki hadi kufikia muda wa ukaguzi huu wa kiufundi hivyo maeneo ya shule yanakuwa katika hatari ya migogoro ya ardhi kutokana na ukosefu wa ushahidi wa umiliki wa ardhi husika kisheria;

b) Ukaguzi ulibaini kuwa maeneo ya ujenzi kumi na tisa (19) kati ya ishirini na nne (24) yaliyotembelewa hayakuwa yamepimwa na kuandaliwa ramani ya ardhi, ili kuweza kubainisha ukubwa halisi wa maeneo hayo. Aidha, hii ilichangiwa na Mamlaka za

Halmashauri kutokuweka kipaumbele katika upimaji wa ardhi kabla ya kupata ardhi na kabla ya kuanza kazi za ujenzi. Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa kutokana na kutokupima maeneo ya ujenzi na kuainisha ukubwa wake, baadhi ya shule zilijengwa katika maeneo madogo ambayo hayafikii ukubwa ulioanishwa kwenye ramani ya mradi. Kwa mfano, ujenzi wa shule katika Wilaya za Lushoto, Ikungi na Tunduma, miundombinu ya awamu ya kwanza iliyokuwa ikijengwa ilimaliza eneo lote la mradi hivyo kuashiria kuwa hakukuwa na nafasi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu kwa awamu zitakazofuta;

c) Ukaguzi ulibaini kuwa, **shilingi milioni 470** zilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari chini ya mradi wa SEQUIP. Fedha hizi zilikusudiwa kutumika kwa shughuli za ujenzi pekee na si vinginevyo.Hata hivyo, mapitio ya nyaraka za mradi na vocha za malipo ya ujenzi kwa shule ishirini na nne (24) za sekondari zilizotembelewa zilibainisha kuwa, shule za sekondari tatu (3) kati ya ishirini na nne (24) zilikuwa na matumizi ambayo hayakustahiki yenye thamani ya **shilingi 27,500,000**. Shule hizo na kiasi cha fedha ambacho kilitumika kwa matumizi yasiokusudiwa ni pamoja na shule ya Bagamoyo – Halmashauri ya Korogwe **(2,600,000)**, shule ya Ngome – Halmashauri ya Kilwa **(10,700,000)** na shule ya Namole – Halmashauri ya Tunduma **(14,200,000)**;

d) Kukosekana kwa baadhi ya michoro, na maelezo ya kina kulichangia mapungufu yafuatayo katika utekelezaji wa mradi wa SEQUIP:-

(i) Kutokujengwa kwa mifumo ya gesi katika maabara zilizokuwa zimejengwa; hii ilisababishwa na kukosekana kwa michoro ya mifumo hiyo;

(ii) Kutokuweka miundomimbu ya vyoo vya walemavu; na

(iii) Utofauti katika vifaa vilivyofungwa kwa ajili ya mifumo ya maji safi na maji taka; hii ilitokana na kukosekana kwa maelezo ya kina juu ya aina ya vifaa ambavyo

vingetumika, jambo ambalo lilipelekea kila watekelezaji kununua vifaa vya kampuni wanayoona inafaa.

e) Ukaguzi ulibainisha kuwa, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilichelewa kukamilisha mchakato wa manunuzi ya Mhakiki/Mdhibiti huru wa mradi kwa kutojumuisha manunuzi haya kwenye mpango wake wa ununuzi wa mwaka wa fedha 2020/21, ambapo makubaliano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na IDA yalifanyika.Ukaguzi ulibaini zaidi kwamba, kuchelewa kwa ununuzi wa Mhakiki/Mdhibiti Huru wa mradi kulitokana na ukosefu wa wazabuni wenye sifa na kupelekea kurudia kwa tangazo la ununuzi wa Mhakiki/Mdhibiti Huru wa mradi.Kutofuata makubaliano yaliyofanywa kati ya IDA na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kunaweza kusababisha usitishwaji wa Mkopo; na

f) Ukaguzi ulibaini kuwa timu zilizoundwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi hazikuwa na wataalamu wa ujenzi. Timu hizo ziliundwa na walimu na viongozi wengine wa Kijiji na Mtaa ambapo mradi unatekelezwa.Kutokana na timu hizo kukosa watu wenye utaalamu katika ujenzi, kazi za kila siku zilikuwa zikisimamiwa na walimu ambao hawakuwa na uwezo wa kubaini makosa ya kiufundi katika ujenzi uliokuwa ukitekelezwa. Aidha, wahandisi kutoka wilayani walitembelea miradi mara chache, hasa wakati ambapo mafundi walihitaji kulipwa, ili kuidhinisha malipo yao.

Mheshimiwa Spika, kutokana na matokeo ya ukaguzi huo, CAG alitoa mapendekezo ishirini (20) ambapo mapendekezo kumi na sita (16) yalitolewa kwa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na mapendekezo manne (4) yalitolewa kwa Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uhakiki wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa yalibainisha kuwa hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2023, pendekezo moja (1) kati ya ishirini (20) yaliyotolewa lilitekelezwa kikamilifu; mapendekezo kumi na nne (14) yalikuwa katika hatua za awali za utekelezaji, mapendekezo mawili (2) yalikuwa katika hatua nzuri za

utekelezaji, na mapendekezo matatu (3) yalikuwa hayajatekelezwa kabisa.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 17 Januari, 2024, Kamati ilikutana na Afisa Masuuli Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ili kupata ufafanuzi wa Serikali wa hatua zilizochukuliwa kutekeleza mapendekezo ya Taarifa ya Ukaguzi huu wa Kiufundi.

Mheshimiwa Spika, Afisa Masuuli Elimu aliifahamisha Kamati kuwa Serikali imekamilisha ujenzi wa shule mia nne arobaini na mbili (442) kati ya shule elfu moja (1000) zilizo ainishwa na mradi.Shule hizi zinatumika na umaliziaji wa vitu vichache kama uzio na vichomea taka unaendelea.Aidha, ailiifahamisha Kamati kuwa baadhi ya shule zimekamilika kwa wananchi wa maeneo husika kuchangia nguvu kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Afisa Masuuli Ofisi ya Rais-TAMISEMI aliifahamisha kamati kuwa ujenzi wa baadhi ya shule haujakamilika kutokana na sababu kwamba fedha iliyotolewa ilikuwa milioni mia nne sabini (470) kwa shule zote, hata hivyo, kutokana na sababu mbalimbali kama jiografia, gharama za vifaa vya ujenzi na gharama za usafirishaji kuwa tofauti kwa maeneo tofauti ya Nchi yetu ilipelekea baadhi ya shule nyingine kutokukamilika.Aidha Ofisi ya Rais-TAMISEMI ilifanya tathmini ya kina ya kiasi cha fedha kinacho hitajika ili kukamilisha shule zote ambazo hazijaisha na imeomba shilingi bilioni kumi na tisa (19,000,000,000) ili kukamilisha ujenzi

Mheshimiwa spika, pamoja na maelezo ya Serikali, hoja ya msingi ya Kamati inaendelea kubaki kwamba usimamizi wa ubora wa miradi iliyo jengwa kwa kutumia mfumo uliotumika, umesababisha mapungufu mbalimbali hasa kwenye ubora ikizingatiwa usimamizi wa wataalam ulikuwa ni mdogo. Hivyo,Kamati imetoa mapendekezo ya hatua za kuchukua kwa mapendekezo ambayo hayajakamilika utekelezaji wake.

2.1.6 Taarifa ya Ukaguzi wa Kiufundi Kuhusu Udhibiti wa Gharama za Ujenzi kwa Miradi Inayotekelezwa na Baadhi ya Taasisi za Umma

Mheshimiwa Spika, dhumuni la msingi la ukaguzi huu lililenga kufanya tathmini endapo Taasisi za Serikali zinadhibiti ipasavyo gharama wakati wa ujenzi wa majengo yanayomilikiwa na Serikali. Kwa msingi huo , ukaguzi ulilenga kutathmini taratibu na namna ambavyo gharama za ujenzi wa baadhi ya majengo ya Serikali zilidhibitiwa. Vilevile, ukaguzi huu ulifanya tathmini ya utoshelevu wa udhibiti wa gharama za ujenzi wa majengo ya Serikali katika hatua mbalimbali kuanzia upembuzi yakinifu hadi uuandaji wa gharama za mwisho na kufunga mikataba.

Mheshimiwa Spika, malengo mahsusi ya ukaguzi huu yalikuwa ni kama ifuatavyo:-

a) Kufanya tathmini ya kina iwapo kuna udhibiti wa gharama wakati wa upangaji wa ujenzi wa majengo yanayomilikiwa na Serikali;

b) Kubainisha endapo kulikuwa na udhibiti wa gharama wakati wa ununuzi wa wakandarasi, washauri elekezi, malighafi za ujenzi na manunuzi mengineyo na iwapo shughuli za manunuzi zilifanyika kwa kuzingatia taratibu na kanuni za manunuzi;

c) Kubainisha iwapo kulikuwa na utoshelevu wa nyaraka na taratibu za mikataba;

d) Kubainisha iwapo gharama za ujenzi wa majengo ya Serikali zinazingatia mikataba;

e) Kuchunguza endapo kulikuwa na udhibiti wa kutosha wa gharama wakati wa utekelezaji wa ujenzi wa majengo yanayomilikiwa na Serikali;

f) Kufanya mapitio ya kina iwapo udhibiti wa gharama katika hatua ya kukamilisha na kufunga ujenzi wa majengo ya Serikali ulifanyika ipasavyo; na

g) Kutathmini iwapo udhibiti wa gharama za huduma za mshauri elekezi zinazotolewa wakati wa ujenzi wa majengo yanayomilikiwa na Serikali ulifanyika ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi huu ulihusisha Taasisi za Umma tano (5) ambazo ni; Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (DAWASA) na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF).

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulihusisha majengo tisa (9) ambayo ni; Morocco Square (NHC), Victoria Place, 711 Kawe Residence Project, Mzizima Tower, Mwanza-Five Star Hoteli ya Kitalii, Maji House (DAWASA Yetu), PSSSF Commercial Complex -Sam Nujoma na PSSSF Kambarage Tower. Ukaguzi ulizingatia kuanzia uanzishwaji wa mradi, upangaji, ununuzi, utekelezaji na kukamilika kwa miradi ya majengo.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi huu ulihusisha miradi ya ujenzi wa majengo makubwa ya Serikali iliyotekelezwa katika kipindi cha Miaka sita (6) ya fedha kuanzia 2016/17 hadi 2021/22.Masuala yaliyobainika katika ukaguzi huo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mapitio ya takwimu za mikataba na taarifa za maendeleo ya miradi tisa (9) ya ujenzi wa majengo makubwa ya serikali yaliyokaguliwa imebaini kuwa, kulikuwa na mabadiliko ya gharama za ujenzi kutokana na sababu kadhaa zilizosababisha marekebisho ya bei za awali za mikataba. Bei za awali za mikataba na mabadiliko ya gharama zimefafanuliwa katika jedwali Na. 2.3 Hapa chini:-

Jedwali Na 2.3: Gharama za awali, zilizorekebishwa na za mwisho za mikataba kwa miradi ya ujenzi wa majengo ya Serikali zilizokaguliwa

Jina la Mradi	Gharama za Mikataba (Sh.Bilioni)	Mabadiliko ya Gharama za Mkataba (Sh. Bilioni)	Hesabu ya Mwisho 'final account' (Sh.Bilioni)	Ongezeko la Gharama (Sh. Bilioni)	% Ongezeko la Gharama (Bilioni)
Magomeni Quarters	20.0	52.20	Haipo	32.20	161
DAWASA Yetu	37.	48.98	Haipo	11.98	32
Mzizima (Loti 1 Ujenzi wa msingi, Loti 2 Ujenzi wa ghorofa la makazi, Lot 3 Ujenzi wa ghorofa la biashara)	12.81	11.81	11.81	(1)	-8
	79.36	79.36	Haipo	0	0
	141.17	141.17	Haipo	0	0
Hoteli ya Kitali ya Nyota tano-Mwanza	72.85	93.5	Haipo	20.65	28
Jengo la kibiashara la PSSSF Sam Nujoma	232.39	232.39	Haipo	0	0
Ghorofa la PSSSF KambarageDodoma	36.11	34.12	34.12	(1.99)	-5.51
Morocco Square	105.11	143.22	Haipo	38.11	36.26
Victoria Place	30.28	30.39	Haipo	0.11	0.36
711 Kawe	137.50	169.00	Haipo	31.50	22.91

Chanzo: ***Taarifa ya CAG kwa Kamati ya PAC Januari, 2024***.

Mheshimiwa Spika, Jedwali Na.2.3 linaonyesha kuwa, kuliidhinishwa ongezeko la gharama za ujenzi kwa miradi sita (6) kati ya tisa (9) iliyokaguliwa. Mradi wa magomeni quarter ulikuwa na ongezeko kubwa kulinganisha na fedha yake ya awali, kutoka kiasi cha **shilingi bilioni 20** hadi **shilingi bilioni 52.2** ambapo

ongezeko ni shilingi **bilioni 32.20** sawa 161% ya gharama ya awali ya mradi.Mradi wa Mzizima Loti 1 ulikamilika, na hesabu ya mwisho ilitayarishwa na gharama ya mwisho ilikuwa **shilingi bilioni 11.806** ikilinganishwa na gharama ya awali ya mkataba ya **shilingi bilioni 12.807**, inaonyesha punguzo la gharama la **shilingi bilioni 1.001** sawa na 8% ya gharama ya awali ya mkataba.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la gharama za miradi ya ujenzi wa majengo makubwa ya Serikali kama lilivyochambuliwa katika Jedwali Na. 2.3 linaendelea kuonekana katika miradi ya 711 – Kawe **(shilingi bilioni 31.50)**, Morocco Square **(shilingi bilioni 38.11)**, Hoteli ya Kitalii ya Nyota Tano Mwanza **(shilingi bilioni 20.65)** DAWASA yetu **(shilingi bilioni 11.98)**

Mheshimiwa Spika, taarifa ya ukaguzi imebainisha sababu kadhaa ambazo zinachangia ongezeko la gharama katika ujenzi wa majengo ya Serikali. Sababu hizo zinachangiwa na mambo ya ndani ya Taasisi na sababu nyingine ni za nje ya Taasisi. Sababu hizo kwa miradi yote sita (6) ambayo ilikuwa na ongezeko la gharama za ujenzi ni kama ifuatavyo:-

a) Maandalizi yasiyofaa na kutozingatia mahitaji ya mteja katika hatua za awali za mradi. Hii inasababisha mabadiliko wakati wa hatua ya usanifu na ujenzi;

b) Tafsiri isiyofaa ya mahitaji ya mteja kwenye usanifu na mahitaji maalum ya mradi. Hii ilisababisha tofauti wakati wa hatua za usanifu na ujenzi;

c) Nyaraka za zabuni zisizokamilika zilisababisha kuandaliwa kwa mikataba yenye mapungufu. Hii ilisababisha mabadiliko wakati wa hatua ya ujenzi ambapo baadhi ya kazi ambazo zilikosekana kwenye mkataba zilionekana kuwa muhimu kufanyika;

d) Kutolingana kwa nyaraka za mkataba hasa makadirio ya ujenzi, michoro na mahitaji maalum ya mradi. Kwa kuwa ujenzi wa majengo unazingatia michoro na mahitaji maalum palipotokea

mkanganyiko na makadilio ya ujenzi kazi zilipimwa upya na kupelekea gharama kuongezeka;

e) Makadirio yasiyo sahihi ya gharama za awali za mradi. Hii ilisababisha changamoto kwa sababu zabuni zilizopokelewa zilikuwa kubwa zaidi kuliko makadirio;

f) Makadirio ya chini ya gharama za kazi zinazofanywa na wakandarasi maalumu, mamlaka ya Serikali (prime costs) na fedha badilifu (provisional sums) katika mkataba. Hii ilisababisha gharama za ziada baada ya kupokea nukuu za juu kuliko gharama na kiasi kilichotolewa katika mkataba;

g) Makadirio ya chini ya fedha za dharura/tahadhari za mkataba. Hii iliongeza hatari ya kuongezeka kwa gharama kupita kiasi kwa kuwa hakukuwa na fedha za kutosha kwa ajili ya ongezeko hilo;

h) Marudio ya vitu kwenye makadirio ya ujenzi katika sehemu tofauti "Builders works and services section"; Hii ilisababisha gharama zisizo za lazima kwenye mradi;

i) Kujumuishwa kwa gharama zisizo za lazima kwenye mikataba ya ujenzi. Kwa mfano, malipo yaliyofanywa kwa safari za ukaguzi wa viwanda kwa wafanyikazi wasio na sifa;

j) Kuongeza gharama za mradi kwa kujumuisha manunuzi ya bidhaa zisizohusiana na kazi. Kwa mfano, ununuzi wa samani(furniture) hauhusiani na ununuzi wa kazi bali ulihusiana na ununuzi wa bidhaa;

k) Tafsiri isiyofaa na matumizi ya kifungu cha malipo ya awali katika mkataba. Hii ilisababisha malipo ya ziada ya malipo ya awali kwa mkandarasi mkuu;

l) Usimamizi usioridhisha na usiofaa wa vifungu vya mkataba vinavyohusiana na malipo ya huduma maalumu (special attendance) kwa wakandarasi wakuu kwa kazi za mkandarasi

mdogo. Hii ilisababisha malipo ya mahudhurio maalumu kwa wakandarasi wakuu bila vithibitisho;

m) Usimamizi usiofaa wa misamaha ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) katika tathmini za hati za malipo kwa wakandarasi. Hii ilisababisha malipo ya ziada kwa wakandarasi;

n) Usimamizi usiofaa wa muda wa mkataba uliopelekea kuongezeka kwa muda wa mradi. Zifuatazo ni sababu za ucheleweswaji wa mradi;

o) Ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi ndani ya muda uliowekwa katika mikataba. Hii ilizingatiwa kama sababu ya nje kwa sababu miradi yote ilifadhiliwa na Serikali;

p) Kuchelewa kupatikana kwa kibali cha ujenzi kulisababisha kuchelewa kuanza kwa kazi. Hii ilisababisha ongezeko la muda na gharama zinazohusiana na ongezeko la Muda; na

q) Kutimiza masharti yaliyowekwa na mtu wa tatu (third party) ya kujenga uwanja wa michezo na kuhamishwa kwa mashimo ya maji taka.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi zaidi wa Kamati katika sababu zilizochangia ongezeko la gharama katika miradi tisa (9) iliyokaguliwa ya kiasi cha **shilingi bilioni 113.78** ulibaini kwamba, usimamizi usiofaa wa muda wa mkataba ndio sababu kubwa iliyopelekea kuongezeka kwa muda na gharama za mradi. Ongezeko la muda limepelekea madai ya kifedha kutoka kwa wakandarasi juu ya madai ya fidia ya ongezeko la gharama, gharama za ziada kutokana na ongezeko la gharama za kazi za awali na matumizi ya kikokotoo cha marekebisho ya bei kwa mikataba isiyokuwa na mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, sababu ya pili iliyochangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka gharama za miradi ya ujenzi ilikuwa ni ukosefu wa fedha za kuwalipa wakandarasi ndani ya muda uliowekwa katika mikataba.Sababu hii ilisababisha madai ya riba kwa malipo

yaliyocheleweshwa na madai ya ongezeko la muda kama ilivyobainishwa katika miradi tisa (9) ya ujenzi iliyokaguliwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi wa kina wa taarifa ya ukaguzi na masuala yaliyobainika, Kamati ilikutana siku ya tarehe 18 Januari, 2024 ili kupata majibu ya Maafisa Masuuli walioguswa na hoja za ukaguzi huu. Katika kikao hicho Kamati ilipata maelezo kuhusu hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya ufuatiliaji yalibainisha kuwa mapendekezo thelathini na nne (34) yalitolewa kwa Taasisi zilizokuwa zinatekeleza miradi ya ujenzi wa majengo. Tathmini ilibainisha kuwa,mapendekezo kumi na tatu (13) yalikuwa yametekelezwa kikamilifu, mapendekezo nane (8) kati ya thelathini na nne (34) yapo katika hatua nzuri za utekelezaji, na mapendekezo nane (8) kati ya thelathini na nne (34) yapo katika hatua za awali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya mahojiano mahsusi na kila Afisa Masuuli aliyeguswa na ukaguzi huu. Mathalani kwa TBA wao waliifahamisha Kamati kuwa ujenzi wa majengo ya Magomeni Quarters ulitekelezwa kama agizo hivyo gharama zimeongezeka kwa sababu haukuwa umefanyiwa usanifu ipasavyo. Hata hivyo, katika kusisitiza masuala ya kuzingatia taratibu hata kama agizo limetolewa, naomba kunukuu sehemu ya mchango[11] wa Mhe. George Joseph Kakunda, Mjumbe wa Kamati kama ifuatavyo:-
Nukuu:- "...Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nieleze kwamba, Serikali iko makini sana kwenye maelekezo yake. Serikali imejiendesha kwa asilimia 80 kupitia standing orders. Sasa hii ya Magomeni Quarters hata kama lilikuwa ni tamko, na B. 13 ya standing order iko vizuri sana….Mheshimiwa Mwenyekiti,kwa bilioni ishirini alitakiwa arudi sasa kwenye utaratibu wa Serikali kwamba hapa mnahitaji feasibility study, tunahitaji usanifu, usanifu wa kina, usanifu wakina uta-inform gharama, tutafute mkandarasi gani? ajenge kama ni TBA alitakiwa awe engaged kwa mkataba…"
Mwisho wa Nukuu.

[11] Rejea Ukurasa wa 73 wa Majadiliano ya Kamati, Taarifa Rasmi za Bunge, Kikao cha Nne, Tarehe 18 Januari, 2024.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa jengo la Hoteli ya Nyota Tano linalojengwa na NSSF**,** maelezo ya ufafanuzi yalitolewa kwamba, gharama za ujenzi zimeongezeka kutokana na mradi huo kusimamishwa na Serikali mwaka 2016. Mradi ulisimamishwa na Serikali ili kutoa fursa ya Mamlaka za Udhibiti (BOT na PPRA) kufanya ukaguzi. Aidha, sababu nyingine iliyotolewa ilihusu ujenzi kuanza bila ya kuwa na Mwendeshaji wa Hoteli (Hotel Operator), hivyo Mwendeshaji alivyopatikana ameelekeza baadhi ya usanifu ufanyike upya kwa kadri ya mahitaji yake.Suala hili pia lilichangia ongezeko la gharama za mradi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Jengo la DAWASA, maelezo yalitolewa kwamba, DAWASA walikabidhiwa jengo hilo na Wizara ya Maji baada ya kutakiwa kuhama eneo lao la awali (Gerezani) ambalo lilipitiwa na ujenzi wa Reli ya SGR. Hivyo gharama za awali za ujenzi hazikuwa zimejumuisha gharama za samani **(shilingi bilioni 2.69)**. Hivyo walilazimika kuandaa mkataba wa nyongeza (addendum) ili kununua samani.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), kuhamishwa mradi wa Seven Eleven uliokuwa ujengwe Ngano lakini ukahamishwa kupelekwa Kawe kulisababisha ongezeko la gharama kwa **shilingi bilioni 16** na fidia ya **shilingi bilioni 31.5** alizolipwa mkandarasi kwa mradi kusimama kwa takribani miaka saba (7).

Mheshimiwa Spika, NHC waliifahamisha Kamati kuwa mwanzoni mwa mradi walifanya mikutano ya wadau (stakeholders engagement) na Taasisi kama TANESCO, TARURA na DAWASA ili kuangalia miundombinu itakayopita eneo la mradi. NHC waliendelea kufafanua kwamba, baadaye Benki ya Dunia walikuwa na mtizamo tofauti kuhusu eneo la Msimbazi na miundombinu inayotakiwa kujengwa hapo. Hivyo kwa miundombinu husika kutojengwa katika eneo hilo maana yake ingekuwa vigumu kwa ujenzi wa majengo ya biashara ya kuchukua familia 400.

Mheshimiwa Spika, NHC walifafanua kwamba kutokana na changamoto hizo za miundombinu ya majitaka katika eneo la

Ngano, Serikali iliwapatia eneo la Tanganyika Packers. Vilvile kwa hoja inayohusu kufanyika kwa upembuzi yakinifu, NHC waliifahamisha Kamati kuwa upembuzi yakinifu ulifanyika kwa mradi wakati unategemewa kujengwa eneo la Ngano na hata ulipohamishiwa eneo la Kawe.

Mheshimiwa Spika, naomba kunukuu sehemu ya maelezo[12] ya Mkurugenzi Mkuu wa NHC Ndugu Hamad Abdallah kwa Kamati kuhusu hoja ya kufanyika kwa upembuzi yakinifu wa mradi eneo la Kawe kama ifuatavyo:-

Nukuu:- "…Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, sidhani kama ilikuwa inaonesha nyaraka ambazo zilitakiwa sisi tuwapatie na tulizo wapatia moja wapo ikiwa ni Feasibility Study zote zipo kwenye documents na kama Kamati yako haikupata tuta-submit tena Taarifa yote kwa kina…Feasibility Study tulianza kufanya Feasibility Study ya eneo abla ya mradi na wakati wa kufanya Feasibility Study tulibaini soko lilkuwa zuri." Mwisho wa Nukuu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kulijitokeza kutofautiana kwa maelezo kati ya taarifa ya wakaguzi na ya NHC kuhusu kufanyika kwa upembuzi yakinifu kabla ya kuanza kwa mradi wa Kawe. Mathalani, CAG aliifahamisha Kamati kuwa mradi wa 711 Kawe Residents Project ulianza tarehe 7 Novemba, 2014 wakati upembuzi yakinifu ulikamilika Mwezi Juni,2015 ikiwa ni miezi (8) tangu kuanza kwa mradi. Hivyo, maelezo ya NHC na ya Wakaguzi yalikuwa yametofautiana kuhusu muda ambao upembuzi yakinifu ulifanyika, kukamilika na kuanza kwa mradi. Kwa msingi huo, Kamati imetoa pendekezo mahsusi katika eneo hili.

2.1.7 Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi Katika Utekelezaji wa Mpango wa Usambazaji Umeme Vijijini

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Tanzania iliingia mkataba na Serikali ya Swideni tarehe 30 Machi, 2016 kwa muda wa miaka mitano (5) ambao ulikuwa utekelezwe kuanzia mwaka 2015/16 hadi 2019/20. Wakati wa kusainiwa kwa mkataba huo, Serikali ya Swideni iliwakilishwa na Shirika la Maendeleo la Swideni (Sida) na Serikali ya Tanzania iliwakilishwa na Wizara ya Fedha (MoF).

[12] Rejea Ukurasa wa 113 wa Majadiliano ya Kamati, Taarifa Rasmi za Bunge, Kikao cha Nne, Tarehe 18 Januari, 2024.

Mheshimiwa Spika, kutokana na makubaliano hayo, kuanzia mwaka 2015 hadi 2019, Serikali kupitia Wakala wa Umeme Vijijini. (REA) ulitarajiwa kupokea ruzuku ya **SEK 600 milioni** (sawa na **Dola za Marekani milioni 72**) zilizoingizwa kwenye Mfuko wa Nishati Vijijini (REF[13]); na ruzuku kutoka DFID ya **paundi milioni 30** (sawa na **Dola za Marekani milioni 45** au **SEK milioni 390** iliyotengwa kusaidia uwekezaji wa kibinafsi katika nishati
jadidifu yaani "Green Mini-Grids" (GMGs); ambayo Swideni ilikubali kuisimamia kwa niaba ya Serikali ya Uingereza.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Swiden (Sida) liliona haja ya kufanya ukaguzi wa ufanisi (Value for Money Audit), ambao ulilenga kutathmini endapo REA imetekeleza mradi kwa tija, ufanisi au kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na matakwa hayo, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) ilipewa jukumu la kufanya ukaguzi wa ufanisi katika Utekelezaji wa Mpango wa Usambazaji Umeme Vijijini unaotekelezwa na REA na Taasisi nyinginezo. Ukaguzi wa Ufanisi ulifanyika katika programu hii ili kubaini maeneo yanayohitaji kuboreshwa zaidi katika shughuli za siku zijazo.

Mheshimiwa Spika, dhumuni kuu la ukaguzi lilikuwa ni kubaini kama REA inasimamia ipasavyo na kwa ufanisi utekelezaji wa programu ya kusambaza umeme vijijini ili kuhakikisha upatikanaji wa nishati endelevu na kuboresha maisha ya watu wa vijijini.Aidha kwa malengo mahususi ukaguzi ulijikita katika kuangalia masuala yafuatayo:-

a) Kutathmini iwapo mipango ya utekelezaji wa miradi ya usambazaji umeme vijijini ilifanyika ipasavyo;
b) Kuangalia endapo shughuli za ununuzi katika programu za kusambaza umeme vijijini zilifanyika kwa kuzingatia sheria na kanuni za manunuzi zilizoainishwa;
c) Kuangalia endapo mikataba ya miradi ya usambazaji umeme vijijini ilisimamiwa ipasavyo;
d) Kuangalia iwapo fedha za miradi ya usambazaji umeme vijijini zilisimamiwa ipasavyo kwa mujibu wa makubaliano ya fedha na miongozo ya fedha; na

[13] Rural Energy Fund

e) Kutathmini endapo mpango wa kusambaza umeme vijijini ulifikia matokeo yaliyokusudiwa ya kusambaza umeme vijijini ambayo yana mafanikio endelevu.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi huu ulihusisha vipengele vyote vitatu vya programu vilivyofadhiliwa na Sida, ambavyo ni; mradi wa ujazilishaji wa umeme maeneo ya vijijini (Densification Round IIA) ikiwa na mikataba sita (6) iliyosainiwa kati ya REA na wakandarasi;Mpango wa Usambazaji Umeme katika Vijiji vilivyopitiwa na Msongo mkubwa wa umeme (BTIP - VEI) ambapo mikataba mitano (5) ilisainiwa kati ya REA na wakandarasi; na Miradi ya Nishati Mbadala kwa maeneo yasiyo pitiwa na gridi ya Taifa (OFF GRID) ikiwa na mikataba kumi na tatu (13) ilisainiwa kati ya REA na Waendelezaji.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi huu ulihusisha nchi nzima, lakini ukaguzi ulitembelea mikoa kumi na nane (18) ambayo miradi ya umeme vijijini ilitekelezwa. Ukaguzi ulihusisha kipindi cha mwaka wa fedha wa kuanzia 2015/16 hadi 2019/20, kipindi ambacho miradi ya umeme vijijini ilitekelezwa kwa mujibu wa makubaliano yaliyosainiwa kati ya Sida na Serikali ya Tanzania. Hata hivyo, Ukaguzi ulijumuisha pia na taarifa za utekelezaji wa miradi kwa kipindi cha miaka ya fedha ya 2020/21 hadi 2022/23.

Mheshimiwa Spika, masuala muhimu yaliyobainika katika ukaguzi huu wa ufanisi katika maeneo yote manne (4) yaliyolengwa ni kama ifuatavyo:-

2.1.7.1 Matokeo ya Ukaguzi wa Usambazaji wa Umeme Katika Vijiji Vilivyopitiwa na Msongo Mkubwa Wa Umeme (BTIPVEI)

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili ukaguzi ulibainisha masuala yafuatayo:-

a) Ukaguzi ulibaini dosari katika upembuzi yakinifu uliofanywa na Wakala wa Umeme Vijijini (REA). REA ilifanya pembuzi yakinifu mbili (2) katika jumla ya vijiji mia moja arobaini na mbili (142). Aidha,utekelezaji wa mradi ulijumuisha vijiji vya ziada ambavyo havikujumuishwa katika pembuzi za awali.Mkoa wa Dodoma

ndio uliokuwa na asilimia kubwa zaidi (22%) ya vijiji ambavyo havikujumuishwa katika upembuzi yakinifu, ukifuatiwa na Mikoa ya Iringa (20%), Shinyanga (15%) na Singida (12%). Maafisa kutoka REA waliieleza timu ya ukaguzi kuwa, tofauti hii ilitokana na sababu kuwa wakati wa utekelezaji wa mradi baadhi ya vijiji vilikuwa vimepatiwa umeme kupitia mipango mikakati mingine ya TANESCO, hali iliyo sababisha kutojumuisha vijiji vingine; na

b) Ukaguzi ulibaini kuwa, tafiti za jioteknolojia hazikufanyika ipasavyo katika kituo kidogo cha Mtera. Licha ya miongozo inayosisitiza ulazima wa tafiti hizo kwa miradi hatarishi au inayotumia teknolojia ya juu zaidi. Ukosefu huu ulisababisha changamoto zisizotarajiwa wakati wa utekelezaji kama vile uwepo wa ardhi yenye miamba iliyohitaji mbinu maalum za uchimbaji.Kutokuwepo kwa taarifa ya kijioteknolojia kulisababisha kuongezwa kwa muda wa utekelezaji wa mradi kwa hadi miezi sita (6).

2.1.7.2 Matokeo ya Ukaguzi katika Usimamizi wa Utekelezaji wa Shughuli za Miradi ya BTIP-VEI

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili ukaguzi wa ufanisi ulibainisha masuala yafuatayo:-

a) Kuchelewa kuanza ujenzi wa miradi ya BTIP-VEI. Kutokuwepo kwa tarehe za kusainiwa kwa mikataba minne (4) kati ya mitano (5) kulikosababisha ucheleweshaji wa kuanza mradi kwa siku nane (8) hadi siku mia moja arobaini na sita (146) kutoka tarehe iliyolengwa yaani Aprili 17, 2017;
b) Ukaguzi ulibaini kuwa miradi ya BTIP-VEI ilichelewa kukamilika kwa miaka mitatu (3) na miezi tisa (9), mathalani katika mkataba wa kituo kidogo cha umeme cha Mtera (kipande cha 1) mkataba uliongezwa kwa miezi nane (8), kuanzia Machi 14, 2021 hadi Novemba 13, 2021;
c) Ukaguzi ulibaini kuwa mipango ya usimamizi wa mazingira na ripoti za usimamizi wa uzingatiaji wa masuala ya mazingira hazikuwepo wakati wa utekelezaji wa mradi;na
d) Mapitio ya taarifa za maendeleo na hati za makabidhiano ya mradi, yalibaini kuwa vifaa vya umeme tayari yaani UMETA

(ready- board) 24,178, ikiwa ni sawa na 68% ya viunganishi vilivyopangwa, vilikabidhiwa/hamishiwa Ofisi za TANESCO Singida mjini. Pamoja na uhamisho huu, haikufahamika iwapo TANESCO ilitumia vyema vifaa hivyo na kuwaunganisha wateja waliobaki.

2.1.7.3 Matokeo ya Mpango wa Ujazilizi Umeme Vijijini Mzunguko wa II A

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili ukaguzi ulibaini masuala muhimu kadhaa kama ifuatavyo:-

a) Mapungufu kadhaa katika kupanga mahitaji ya umeme kabla ya utekelezaji wa mradi. Katika hoja hii ukaguzi ulibaini kuwa mahitaji ya ujazilizi wa umeme yalipangwa mwaka 2016 lakini utekelezaji wa mradi ukafanyika mwaka 2020. Kwa msingi huo, mahitaji ya umeme yakawa yameongezeka ukilinganisha na hali halisi ya utekelezaji. Ongezeko la mawanda ya kazi lilisababisha ongezeko la gharama za mradi kwa kiasi cha **Dola za Marekani 3,485,931.01 (sawa na shilingi bilioni 8.05) na shilingi11,959,162,200.54**);

b) Ukaguzi ulibaini kuwa baadhi ya nyaya za umeme ziligusa jiwe ambalo linaweza kupata joto zaidi ya sentigredi 25 na kuathiri usambazaji wa umeme kalika mtandao huo. Jambo hili linaenda kinyume na mahitaji ya kiufundi (specifications) S01 ya TANESCO – ambayo yanaelekeza kuwa waya wa umeme unatakiwa kuwepo katika eneo lenye joto lisilozidi sentigredi 25;

c) Ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na ucheleweshaji wa kufanya malipo kwa mikataba yote sita (6). Muda wa wastani uliotumika kuandaa malipo kwa wakandarasi ulikuwa siku mia mbili sistini na nne (264) kutoka tarehe ya ombi la malipo na kufanya ucheleweshaji kufika siku mia mbili kumi na tisa (219) kutoka tarehe ya mwisho ya malipo (baada ya siku 45 tokea tarehe ya hati ya malipo);na

d) Ukaguzi ulibaini kuwa dhamana za malipo ya awali zilizowasilishwa na wakandarasi kwa mikataba yote sita (6) hazikuhuishwa baada ya kumalizika kwa muda wake.

2.1.7.4 Matokeo ya Ukaguzi katika Utekelezaji wa Miradi ya Gridi Ndogo kwa Kutumia Nishati Jadidifu

Mheshimiwa Spika, katika ukaguzi wa miradi ya gridi ndogo kwa kutumia nishati jadidifu, ukaguzi wa ufanisi katika REA ulibaini masuala yafuatayo:-

a) Mapungufu katika tathmini ya mahitaji ya kitaifa ya umeme kupitia gridi ndogo na hivyo kusabisha utoaji wa umeme wa gridi kubwa na gridi ndogo kwa mteja mmoja;

b) Ukaguzi ulibaini kutokuwepo kwa mipango madhubuti ya udhibiti wa ubora wa kazi na vifaa vilivyonunuliwa. Hii ni kwa sababu mkataba uliotayarishwa kwa waendelezaji haukujumuisha vigezo vya kiufundi (technical specifications) kwa kazi ya ujenzi na manunuzi ya vifaa vya ujenzi; na

c) Mapitio ya taarifa za uhakiki wa miradi pamoja na vyeti vya ukamilishaji wa miradi yalibainisha kuwa, miradi tisa (9) kati ya kumi na tatu (13) ilikuwa imekamilika, wakati miradi minne (4) iliyobaki ilikuwa bado inaendelea na ujenzi. Vilevile ukaguzi ulibaini kuwa, miradi iliyokamilika haikutamatishwa na kuanza kutumika kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kufanya mahojiano na Bodi na Menejimenti ya REA siku ya tarehe 20 Januari, 2024 ili kufanya tathmini ya hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi huu wa ufanisi. Matokeo ya ufuatiliaji yalibanisha kuwa jumla ya mapendekezo thelathini na moja (31) yalitolewa, ambapo mapendekezo nane (8) yalitekelezwa kikamilifu, mapendekezo ishirini na moja (21) yapo katika hatua za awali za utekelezaji. Aidha,matokeo ya tathmini yaliendelea kubainisha kuwa mapendekezo mawili (2) yalikuwa bado hayajaanza kutekelezwa.

2.1.8 Taarifa ya Ukaguzi wa Kiufundi Katika Udhibiti wa Ubora Wakati wa Utekelezaji wa Shughuli za Ujenzi wa Miradi ya Barabara ili Kuzuia Uchakavu wa Mapema

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ambazo zitadumu kwa muda mrefu huokoa rasilimali fedha za nchi ambazo zingetumika kukarabati barabara ambazo zimeharibika mapema kabla ya muda uliotarajiwa. Lengo la jumla la ukaguzi huu lilikuwa ni kutathmini kama ujenzi wa barabara zilizokaguliwa ulifanyika au umefanyika kwa ufanisi kwa kuzingatia vipengele vya ubora ili kuwezesha kudumu kwa muda uliokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, malengo mahsusi ya ukaguzi huu yalikuwa kutathmini iwapo Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS) alihakikisha masuala yafuatayo katika shughuli za ujenzi wa miradi ya barabara yanazingatiwa ipasavyo:-

a) Usanifu unafanyiwa mapitio kabla ya kuanza kazi za ujenzi wa barabara na iwapo ulifuatwa wakati wa utekelezaji;
b) Mipango ya udhibiti na uhakiki ubora iliandaliwa na kuwasilishwa kwa wahusika wa miradi kabla ya kuanza kutekelezwa;
c) Mbinu za kiufundi za ujenzi zilifuatwa wakati wa ujenzi;
d) Ukaguzi, majaribio ya uthibitisho na uthibitishaji wa kazi zilizofanyika ulifanyika ipasavyo na wasimamizi wa miradi ili kuhakikisha kwamba vifaa vya ujenzi, mbinu za ujenzi na muonekano wa kazi zilitimiza matakwa ya viwango na vigezo vya mkataba;
e) Uthibitisho kuwa kazi zilizofanyika zilizingatia miongozo ya usimamizi na mipango ya uhakiki ubora;
f) Majaribio ya kupima kazi za ujenzi yalifanyika kulingana na vigezo vilivyowekwa na miongozo ya viwango vya kazi za barabara; na
g) Matokeo ya majaribio ya kazi za ujenzi yalitafsiriwa kwa usahihi na hatua mahsusi kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi huu ulilenga pia kutathmini hatua za udhibiti wa ubora katika miradi ya barabara inayoendelea na iliyokamilika Nchini ili kuzuia uchakavu na uharibifu wa barabara mapema. Ukaguzi ulihusisha miradi minane (8) ya barabara

iliyotekelezwa na TANROADS kuanzia mwaka 2009 hadi 2022, kama inavyoonyeshwa kwenye Jedwali Na. 2.4 hapa chini.

Jedwali Na 2.4: Jina la barabara na urefu wake

Na.	Jina la Mradi	Urefu wa barabara katika (km)
1.	Ruangwa – Nanganga	49.3
2.	Bagamoyo – Msata	64.0
3.	Korogwe – Mkumbara	76.0
4.	Tanga – Pangani	50.0
5.	Loliondo – Mto Wa Mbu (Kipande cha barabara ya Waso hadi Sale)	49.0
6.	Dodoma – Iringa (kipande cha Dodoma – Fufu)	70.9
7.	Maswa –Mwigumbi	50.3
8.	Nzega – Tabora (kipande cha Puge – Tabora)	50.3
9.	Jumla	**459.8**

Chanzo: Taarifa ya CAG kwa Kamati, Januari, 2024.

Mheshimiwa Spika, Kama Jedwali Na. 2.4 hapo juu linavyobainisha, barabara zenye urefu wa kilometa 459 zilikaguliwa. Ukaguzi huu wa kiufundi ulibainisha masuala muhimu kama ifuatavyo:-

2.1.8.1 Mapungufu katika Mipango ya Ujenzi na Usanifu wa Miradi ya Barabara

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili CAG alibainisha dosari kadhaa katika mipango ya ujenzi na usanifu wa miradi ya barabara.Mapungufu hayo yalichangia ongezeko la gharama za miradi na kutokamilika miradi kwa wakati. Miongoni mwa mapungufu hayo yalijumuisha maeneo yafuatayo:-

a) Kati ya miradi nane (8) ya barabara zilizokaguliwa, miradi saba (7) ilionekana kuwa na mapungufu ya kiufundi katika usanifu, kama vile ujenzi wa mifereji ya maji katika maeneo ambayo sio sahihi, kujenga mifereji ya maji yenye uwezo mdogo na makadirio ya chini ya kiwango cha tabaka za barabara;

b) Nyaraka kuu ya kudhibiti ubora wa kazi za barabara Nchini ni Mwongozo wa Viwango vya Ujenzi wa Barabara zilizoandaliwa mwaka 2000 ambao ulitolewa na Wizara ya Ujenzi.Ukaguzi ulibaini kuwa, mwongozo huu wa viwango vya barabara haujafanyiwa mapitio au kuboreshwa kwa takribani miaka ishirini na tatu (23) iliyopita ili kurekebisha dosari na kasoro na kujumuisha mabadiliko yaliyojitokeza katika kipindi husika; na

c) Ukaguzi, ulibaini kuwa Mwongozo wa Usanifu wa Lami na Vifaa, wa mwaka 1999 haukuwa umehuishwa kwa miaka ishirini na tatu (23). Mwongozo huu hutumika kama mojawapo ya nyenzo wakati wa kuandaa ripoti za usanifu wa barabara, lakini maelezo yake yamepitwa na wakati, ambapo yalichangia uwepo wa usanifu wenye mapungufu wa barabara za lami ambazo hazikudumu kwa muda mrefu. Kwa mfano, maelezo ya mwongozo wa matabaka yaliyoimarishwa kwa saruji (C1 na C2) yalisababisha nyufa zinazotokana na kusinyaa (shrinkage cracks) ambazo ziliruhusu maji kuingia kwenye lami, na kusababisha uharibifu wa barabara.

2.1.8.2 Hoja za Ukaguzi Zilizohusu Manunuzi Kwenye Miradi ya Ujenzi wa Barabara

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo lilibainika kuwa na mapungufu katika miradi ya ujenzi wa barabara ni eneo la manunuzi. Hoja zilizobainika katika eneo hili ni kama ifuatavyo:-

a) Miradi mitano (5) kati ya nane (8) iliyokaguliwa ilikuwa na washauri elekezi waliopatikana baada ya mkandarasi kuanza kufanya kazi. Ucheleweshaji huo ulitokana na mpango wa manunuzi wa TANROADS usiojitosheleza. Kwa mfano, katika miradi ya barabara za Tanga - Pangani na Maswa - Mwigumbi, mshauri elekezi alipatikana miezi mitano (5) baada ya wakandarasi kuanza kufanya kazi. Hata hivyo hali hii haikuonekana katika miradi mingine iliyokaguliwa; na

b) Ukaguzi ulibaini sababu za kimfumo zinazoweza kusababisha udhaifu katika usimamizi wa ubora wa miradi ya barabara ikiwa ni pamoja na ushiriki wa Kitengo cha Ushauri wa Uhandisi (TECU) kama mshauri ambacho kiko chini ya TANROADS chenye jukumu la kusimamia miradi ya ujenzi ambayo TANROADS pia inasimamia. Kwa mujibu wa CAG hali hii inaweza kuibua migongano ya kimaslahi kuhusu uhuru wa TECU katika kuthibiti ubora.

2.1.8.3 Hoja za Ukaguzi Kuhusu Usimamizi wa Mikataba ya Ujenzi wa Barabara

Mheshimiwa Spika, katika eneo la usimamizi wa mikataba ya ujenzi wa barabara, taarifa ya ukaguzi ilibainisha hoja zifuatazo:-

a) Mapitio ya mikataba ya ujenzi pamoja na ripoti za maendeleo ya ujenzi yalibaini kwamba wafanyakazi muhimu kwenye mradi wapatao thelathini na moja (31) kati ya arobaini (40) ambao ni sawa na asilimia 77.5 katika miradi nane (8) ya barabara iliyokaguliwa hawakuwa wamesajiliwa kama wahandisi wataalamu na Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB). Jambo hili ni kinyume na matakwa ya kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Bodi ya Usajili wa Wahandisi; na

b) Kifungu cha 1408 (c) cha Kanuni za Viwango vya Ujenzi wa Barabara (2000), kinamtaka mkandarasi kumpa mshauri elekezi idadi ya wafanyakazi wa ziada kwa ajili ya kukagua, na kupima kazi.Ukaguzi ulibaini kuwa idadi ya wafanyakazi wa wakandarasi aliopewa mshauri elekezi katika kila mradi ilikuwa kati ya watano (5) hadi kumi na mbili (12). Pia ukaguzi ulibaini kuwa wafanyakazi waliohusika katika udhibiti wa ubora na

taratibu za uhakiki ubora wa miradi ya barabara walilipwa na mkandarasi, jambo ambalo liliibua wasiwasi kuhusu uhuru na uwezekano wa mgongano wa kimaslahi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana na Afisa Masuuli Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS) siku ya tarehe 22 Januari, 2024 ili kupata maelezo yake kuhusu utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi huu muhimu. Kupitia kikao hicho, Kamati ilifahamishwa kuwa CAG katika ukaguzi wake alitoa jumla ya mapendekezo kumi na tisa (19). Hadi kufikia Disemba 2023, jumla ya mapendekezo kumi na moja (11) yalikuwa katika hatua za utekelezaji na mapendekezo nane (8) yalikuwa bado hayajaanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hoja inayohusu madeni ya wakandarasi ambayo hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 yalikuwa **shilingi bilioni 701**, Afisa Masuuli Ujenzi alifafanua kwamba wamekuwa wakifanya vikao na Wizara ya Fedha Kuomba upatikanaji wa fedha za miradi kwa wakati. Hata hivyo ,katika eneo hili Kamati bado ina hoja kuwa kutokulipa madeni ya wakandarasi kwa wakati kunasababisha riba kubwa na gharama kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa mapungufu yaliyopo katika usimamizi wa miradi, Afisa Masuuli alikiri mbele ya Kamati uwepo wa changamoto hiyo kwa baadhi ya miradi. Aidha alitoa ufafanuzi kwamba, kwa sasa wanajenga uwezo wa wataalam wa ndani ili kuhakikisha miradi inasimamiwa ipasavyo.Hii ni pamoja na kuimarisha kitengo cha usimamizi wa miradi cha TANROADS hali ambayo itaisaidia kupunguza utegemezi wa washauri elekezi wa miradi kutoka nje ambao gharama zao zipo juu.

2.1.9 Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi Katika Usimamizi wa Vituo vya Afya vya Binafsi na vya Hiari

Mheshimiwa Spika, ukaguzi huu ulitathmini ikiwa Wizara ya Afya ina utaratibu madhubuti na mfumo bora wa usimamizi wa udhibiti wa utoaji wa huduma za afya zinazotolewa na vituo binafsi na vya hiari Nchini.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi huu ulilenga kuangalia utaratibu uliopo katika usajili wa vituo vya afya vya binafsi na hiari kama unafanya kazi vizuri; usimamizi shirikishi wa vituo vya afya vya binafsi na hiari kama unafanyika ipasavyo; ukaguzi wa vituo vya afya vya binafsi na hiari kama unafanyika ipasavyo na ukaguzi wa kimatibabu wa vituo vya afya vya binafsi na hiari kama unafanyika ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, vilevile ukaguzi huu ulizingatia kuangalia bei ya huduma za afya zinazotozwa na vituo vya afya vya binafsi na hiari kama vinasimamiwa ipasavyo na ushirikishwaji na utoaji wa taarifa kwa vituo vya afya vya binafsi na hiari kama unafanya kazi ipasavyo. Kwa muktadha huo,Wizara ya Afya, ndiyo ilikuwa mkaguliwa mkuu kwa sababu ndiyo yenye jukumu la kudhibiti vituo vya afya vya binafsi na vya hiari. Muda wa ukaguzi ulijumuisha miaka sita (6) kuanzia 2016/17 hadi 2021/22.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya ukaguzi huu wa ufanisi ni kama ifuatavyo:-

a) Ukaguzi huu ulichambua taarifa ya kiwango cha nyota cha vituo vya afya vya binafsi mia tano kumi na nne (518) kati ya vituo 1474 Nchini na kugundua kuwa ni asilimia 18 tu iliyofikia kiwango cha nyota tatu (3) na zaidi mpaka kufikia Juni 2022. Hivyo Wizara haikufikia malengo ya Mpango Mkakati wa Wizara (2016/17-2020/21) unaobainisha kuwa Wizara ya Afya ilipanga Kufikia ubora wa vituo vya afya wa nyota tatu (3) hadi tano (5) kwa asilimia 95;

b) Ukaguzi ulibaini kuwa Baraza la Famasia halikufanya mapitio ya uzingatiaji wa maduka ya dawa yaliyoambatanishwa katika vituo vya afya na viwango vya ubora wa utoaji huduma za dawa kuanzia mwaka 2016/17 hadi 2021/22, na hivyo hakukuwa na taarifa za idadi ya maduka ya dawa yenye sifa zinazotarajiwa;

c) Ukaguzi ulibaini baada ya kutembelea vituo vya afya vya binafsi, kwamba kati ya vituo 132 vilivyotembelewa, vituo 65

sawa na asilimia 49 viliendesha Maabara zao bila usajili kutoka Bodi ya Maabara ya Afya ya Binafsi;

d) Ukaguzi ulibaini kwamba kati ya vituo 132, vituo 32 sawa na asilimia 25 havikuhuisha leseni zao kama inavyotakiwa na kuendeshwa kwa leseni zilizokwisha muda wake;
e) Ukaguzi huu ulibaini, kupitia ziara zilizofanywa katika vituo vya afya ambapo kati ya Maabara 132 Maabara 65 sawa na asilimia 49, ziliendeshwa bila kuwa na wataalamu wa Maabara waliokidhi vigezo na kusajiliwa;

f) Ukaguzi wa mchakato wa usajili wa vituo vya huduma za afya binafsi Nchini Tanzania ulibaini kwamba muda wa kukamilisha usajili ulikuwa mrefu zaidi kuliko muda uliowekwa kisheria. Wastani wa muda uliotumika kwa usajili ulikuwa siku 283, ikilinganishwa na matakwa ya siku 14 yaliyowekwa kisheria. Tofauti za muda zilijitokeza kati ya Mikoa, kama vile Dar es Salaam (siku 191), Ruvuma (siku 288), Mwanza (siku 255), Mbeya (siku 319), Tabora (siku 270), Kilimanjaro (siku 389) na Dodoma (siku 269); na

g) Ukaguzi ulibaini kuwa Wizara ya Afya haikuhakikisha kuwa bei za matibabu zinawekwa wazi kwenye baadhi ya vituo vya afya vya binafsi na vya hiari. Aidha, ilibainika kuwa, bei za huduma za afya zilitofautiana kwenye vituo vya afya vya binafsi na hiari katika Mikoa yote. Katika Manispaa ya Tabora ni asilimia 20 tu ya vituo vya huduma za afya vilivyotembelewa viliweka bei za matibabu, huku vituo vya afya vya Dar es Salaam vikionekana kuwa na uwazi zaidi wa bei za matibabu ambapo asilimia 65 ya vituo vilivyotembelewa vilikuwa vimebandika bei hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana na Afisa Masuuli Wizara ya Afya siku ya tarehe 17 Januari, 2024 ili kupata maelezo ya Serikali kuhusu hatua iliyofikiwa ya kushughulikia hoja za ukaguzi husika. Afisa Masuuli alikiri uwepo wa mapungufu yaliyo bainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Alifafanua kwamba, baadhi ya dosari zinatokana na kasi ya ukuaji wa Sekta ya Afya Nchini hivyo mfumo uliopo sasa wa usimamizi kuwa na changamoto.

Mheshimiwa Spika, Afisa Masuuli Wizara ya Afya aliifahamisha Kamati kuwa mkakati wa muda mrefu wa kujibu dosari zilizobainishwa ni pamoja na kuunda chombo kitakachokuwa na jukumu la kusimamia na kudhibiti shughuli zote za sekta ya Afya Nchini. Kuanzishwa kwa chombo hiki kunatarajiwa kushughulikia tatizo kubwa la usimamizi na udhibiti wa huduma za Afya zinazotolewa na Vituo vya Binafsi na vya Hiari na pia vile vya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Afisa Masuuli aliendelea kufafanua kuwa, kwa sasa wanaendelea kuboresha mfumo uliopo wa TEHAMA ili kurahisisha kuweza kujua ni kitu gani kinafanyika wapi na kwa wakati gani kwa urahisi zaidi tofauti na ilivyo sasa vituo havijaunganishwa kwenye mfumo hivyo usimamizi wake unakuwa ni mgumu na hauna tija inayotarajiwa.

2.1.10 Taarifa ya Ukaguzi wa Kiufundi Katika Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) Awamu ya Pili

Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya usafiri wa mabasi yaendayo haraka (BRT) awamu ya pili katika mkoa wa Dar es Salaam unafanyika chini ya Loti namba mbili. Loti ya kwanza inajumuisha ujenzi wa miundombinu inayohusisha kilometa 20.3 za njia za mabasi yaendayo haraka. Njia hizi zinapita katikati ya barabara zinazotumiwa na vyombo vya usafiri vinavyotumia nishati (Motorised Traffic) pamoja na vile visivyotumia nishati (Non-Motorised Traffic) kwenye barabara ya Kilwa, sehemu za barabara ya Bandari, barabara ya Sokoine, na barabara ya Kawawa.

Mheshimiwa Spika, mradi unapita kutoka eneo la Mbagala katika Wilaya ya Temeke hadi katikati ya maeneo ya biashara katika Wilaya za Kinondoni na Ilala, ambapo unaunganisha na awamu ya kwanza ya mfumo wa BRT, Kariakoo na vituo vya vivuko vya kuelekea Zanzibar. Loti ya pili inajumuisha ujenzi wa majengo, ikiwa ni pamoja na kituo kikuu cha mabasi yaendayo haraka cha Mbagala, vituo viwili vya mabasi vya ukubwa wa wastani, na vituo vidogo vitano (5) katika maeneo tofauti.Mradi huo unatarajiwa kunufaisha watu wapatao milioni 1.2 sawa na 25% ya

wakazi wa Jiji la Dar es Salaam. Wanufaika wengine ni pamoja na watumiaji wa njia kuu za barabara zinazounganisha jiji kama vile barabara za Mandela na Nyerere.

Mheshimiwa Spika, gharama zilizokadiriwa za mradi baada ya kutozwa kodi ni **Dola za Marekani milioni 159.32** (sawa na **Tsh. bilioni 285.1**). Mradi ulifadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB = 61.1%), Mfuko wa Kukua Pamoja wa Afrika (AGTF = 27.8%), na Serikali ya Tanzania (GoT = 11.1%). Awali, ilipangwa kwamba mradi ungekamilika katika kipindi cha miaka minne (2016-2020). Hata hivyo, kutokana na kucheleweshwa kwa hatua za usanifu na ununuzi, tarehe ya kukamilisha mkataba kwa Loti ya kwanza ilikuwa tarehe 5 Mei, 2022, na kwa Loti ya pili ilikuwa tarehe 28 Februari, 2021.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa kufanya Ukaguzi wa Kiufundi ulitokana na sababu mbalimbali kama vile umuhimu wake kwa Taifa na kiasi cha fedha kinachotumika na mchango wake katika kufanikisha malengo ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, lengo la kaguzi lilikuwa ni kutathmini iwapo ujenzi wa mradi wa miundombinu ya barabara ya mabasi yaendayo haraka Dar es Salaam (BRT), Awamu ya pili umetekelezwa kwa ufanisi kwa kuzingatia muda, gharama, ubora, na mawanda, ili kurahisisha kufikia malengo yaliyokusudiwa ya mradi. Pia, Ukaguzi wa Kiufundi ulitathmini ufanisi wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika Ukaguzi wa Kiufundi uliotangulia kuhusu mradi huo.

Mheshimiwa Spika, Timu ya Ukaguzi ilifuatilia kazi zilizotekelezwa katika kipindi cha miaka sita (6) iliyopita kuanzia 2016/17 ambacho ndio kipindi TANROADS ilianza kutekeleza mradi hadi 2021/22 ambapo mradi ulikuwa unaendelea kutekelezwa. Ukaguzi ulizingatia sehemu mbili (2) za ujenzi ambazo ni kazi za barabara na kazi za majengo. Kwa ujumla, ukaguzi ulilenga kwenye hatua ya sasa ya utekelezaji wa mradi na kutoa tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi uliopita.

Mheshimiwa Spika, masuala yaliyobainika katika ukaguzi huu ni kama ifuatavyo:-

a) Ukaguzi ulibaini ucheleweshaji wa siku 326 katika kukamilisha mradi, ambao umerefushwa kutoka tarehe ya awali ya kukamilika kwa mradi 5 Mei 2022 hadi tarehe 27 Machi 2023. Aidha, wakati wa ukaguzi, maendeleo ya mradi kwa upande wa Loti 2 yalikuwa 100%; na kwa Loti ya 1 yalikuwa 80.09% ikilinganishwa na 86.11% iliyopangwa kwa wakati huo, ikionesha kuchelewa kwa 6.02%. Sababu zilizochangia ucheleweshaji huu kwa Loti 1, ilikuwa ni pamoja na kuchelewa kwa malipo kwa mkandarasi, kuchelewa kwa makabidhiano ya eneo la kazi kwa mkandarasi na ongezeko la kazi za ziada katika mchanganuo wa kazi (BOQ);

b) Ukaguzi ulibaini kuwa dhamana ya malipo ya awali ilifikia ukomo tangu tarehe 30 Disemba 2020, mpaka wakati wa ukaguzi huu Novemba 2022 dhamana hiyo ilikuwa haijahuishwa licha ya mkandarasi kukumbushwa na TANROADS. Wakati dhamana ilipokwisha muda wake, kulikuwa na kiasi cha **Sh. 6,392,778,506.57** ambacho kilikuwa hakijarejeshwa kama sehemu ya malipo ya awali, hii ilkuwa kinyume na masharti ya mkataba[14];

c) Ukaguzi ulibaini mabadiliko ya mawanda ya kazi kwa miradi ya Loti ya kwanza na ya pili (2) ambayo yalisababisha kuzidi kwa gharama za mkataba wa ushauri wa awali kwa 107% na 67% kila moja (mtawalia). Gharama kwa Loti ya kwanza iliongezeka kwa jumla ya **shilingi 7,031,346,281.94** kutokana na nyongeza nne; na

d) Wakati wa mapitio ya nyaraka za maafisa wa ngazi ya juu wa mkandarasi (Sinohydro Corporation Limited) kuhusiana na Loti ya kwanza, ukaguzi ulibaini kuwa kati ya maafisa kumi na moja (11) waliochaguliwa kama sampuli, maafisa

sita (6) walikuwa wanafanya kazi bila vibali vya kazi, jambo ambalo ni kinyume na kanuni za ajira[15].

Mheshimiwa Spika, Kamati iliomba kupata maelezo ya Afisa Masuuli TANROADS kuhusu hali halisi ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi. Matokeo ya uhakiki wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa yanaonesha kuwa hadi kufikia tarehe 3 Januari, 2023, pendekezo moja (1) lilikuwa halijatekelezwa na mapendekezo kumi na moja (11) yalikuwa katika hatua za awali za utekelezaji na mapendekezo mawili (2) yalikuwa yametekelezwa.

Mheshimiwa Spika, pendekezo ambalo halijatekelezwa linahusu masharti ya mkataba ambapo mkandarasi alitakiwa kuleta vifaa vyote kwenye ofisi ya mshauri mwelekezi. Hata hivyo ukaguzi haukupata nyaraka za uthibitisho wa baadhi ya vifaa ambavyo mkandarasi alitakiwa kuviwasilisha kwenye ofisi ya mshauri mwelekezi wa mradi.

2.1.11 Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi Katika Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu Nchini

Mheshimiwa Spika, mnamo Mwaka 2015, Tanzania ilipitisha Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ambayo yalikuwa na shabaha 169 za matarajio kufanikisha Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDGs). Ikiwa ni miongoni mwa nchi iliyotia saini Ajenda ya 2030, Tanzania ilichukua hatua za kuhuisha Ajenda hiyo katika muktadha wa kitaifa kwa kuimarisha malengo na shabaha katika mfumo wake wa mipango ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, wakati wa upitishaji wa Ajenda ya 2030, Tanzania ilikuwa katika maandalizi ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP II) hivyo ajenda hiyo

[14] Rejea masharti ya Kifungu cha 14.2 cha Masharti Jumla ya Mkataba kinachotaka mkandarasi kuhakikisha kuwa dhamana inabaki halali na inatekelezeka hadi fidia ya malipo ya awali itakapokuwa imelipwa.

[15] Kifungu cha 9(2) (a) cha Kanuni za Ajira za Wasio Raia ya mwaka 2015 kinazuia kuajiri mtu ambae si raia mpaka awe anamiliki kibali halali cha kazi ambayo inatambulika.

ilihuishwa katika mpango huo. Malengo yote 17 yalijumuishwa kutoa dira ya utekelezaji wa mipango ya Serikali, Mashirika ya Kimataifa, Mashirika ya Kiraia na Taasisi nyingine katika miaka 15 kuanzia Mwaka 2016 hadi Mwaka 2030.

Mheshimiwa Spika, dhumuni la ukaguzi huu ilikuwa ni kutathmini iwapo Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zilisimamia ipasavyo utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu kupitia mipango ya kitaifa hadi utekelezaji katika ngazi za chini za Serikali.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulijikita katika kipindi cha miaka sita (6) ya fedha kuanzia Julai 2016/17 hadi Juni 2021/22. Kipindi hiki kilichaguliwa ili kutoa mwenendo wa utendaji katika utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu Nchini kuanzia Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 - 2020/21) na Mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26).

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari ukaguzi huu wa ufanisi ulibaini masuala yafuatayo:-

a) Kutojitosheleza na ujumuishaji hafifu wa malengo ya maendeleo endelevu katika mipango ya taifa ya maendeleo ya miaka mitano na mipango mikakati ya Wizara, Taasisi, Mikoa na Halmashauri Nchini. Mathalani ukaguzi ulibaini hapakuwa na Sekretarieti ya Mkoa hata moja (1) kati ya sita (6) zilizotembelewa ambazo ziliandaa Mipango Mikakati yao kwa wakati na uzinduzi wa Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Juni 2016. Vilevile, Sekretarieti mbili (2) kati ya sita (6) za Mikoa zilizotembelewa zilifanya mapitio ya mipango mikakati yao baada ya uzinduzi wa Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo.Hii ilionesha kuwa mipango mikakati haikujumuisha vipaumbele vya Mpango wa Taifa wa Maendeleo;

b) Ukaguzi ulibaini kuwa, mbali na Kamati ya Ufundi ya Ngazi ya Juu, Tanzania inahitaji uratibu wa utekelezaji kwa kuzingatia takwimu za ajenda ya maendeleo ikifanya kazi kama kamati

ndogo ya Kamati ya Ufundi ya Ngazi ya Juu, kuratibu maslahi ya wadau na juhudi zinazohusu masuala ya takwimu katika siku zijazo;

c) Ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na uwezeshaji mdogo kwa ajili ya shughuli za upatikanaji wa takwimu Nchini.Bajeti zilizotengwa za shughuli ziliwekewa ukomo na pia zilikuwa katika hatari ya kupunguzwa wakati wa upungufu wa Fedha;

d) Wizara ya Fedha na Mipango ilitakiwa kuimarisha ukusanyaji wa kodi mbalimbali na kuwezesha mazingira ya kutambua vyanzo vipya vya mapato. Ukaguzi ulibaini kuwa, kulikuwa na upungufu wa rasilimali fedha ya kutosha kufadhili utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano;

e) Ukaguzi ulibaini kuwa vyanzo vipya vya mapato vya ndani ya nchi vilianzishwa ikiwa ni pamoja na dhamana za manispaa, dhamana za uraia na uhamiaji, dhamana za uhifadhi wa mazingira, ufadhili wa msongamano (crowd funding), miradi ya Mfuko wa Fedha, vyombo mbalimbali vya usawa na bima na dhamana ya Kiislamu (Sukuk) na Mfuko wa Maliasili (NRF). Hata hivyo, vyanzo hivyo havikutoa mchango wa kutosha kutekeleza malengo endelevu hapa Nchini; na

f) Dosari kadhaa zilibainika katika mfumo wa tathmini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa malengo endelevu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kubainisha hoja muhimu zilizotokana na ukaguzi huu, CAG alihitimisha hoja yake kwa kubainisha matokeo ya dosari hizo za kiutekelezaji. Naomba kunukuu sehemu ya maelezo yake katika ukurasa wa 13 wa Taarifa yake kwa Kamati kama ifuatavyo:-

Nukuu: "...Kwa hiyo, uzalishaji wa takwimu usioridhisha; Uratibu na ushirikiano kati ya mashirika ya utekelezaji na wadau umepelekea mapungufu na kiwango cha chini cha mwenendo wa utekelezaji wa malengo yote 17 ifikapo Mwaka 2030. Hii ina athari ya moja kwa moja kwa mafanikio ya hatua za Mpango wa Pili na wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano kuhusiana na kanuni ya ufanisi, tija na uwekevu. Hii inaweza pia

kusababisha hatari katika mafanikio ya mikakati na nguzo kuu za Mpango wa Pili na wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambazo ni viwanda, maendeleo ya binadamu, na ufanisi wa utekelezaji..." Mwisho wa Nukuu.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi unatambua juhudi za Wizara ya Fedha ,Wizara ya Uwekezaji, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, na Ofisi ya Waziri Mkuu katika kuboresha utekelezaji wa malengo ya maendeleo endelevu Nchini. Hata hivyo, hatua zaidi bado zinahitajika ili kuboresha eneo hili zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana siku ya tarehe 08 Februari, 2024 ili kupata maelezo ya Serikali kuhusu utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi huu wa ufanisi. Maafisa Masuuli walioshiriki kikao hicho ni Afisa Masuuli Fungu 21 – Wizara ya Fedha, Afisa Masuuli OR – TAMISEMI, Afisa Masuuli Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Afisa Masuuli Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Spika, ufafanuzi wa hoja kadhaa za CAG ulitolewa. Mathalani, kwa hoja ya uhuishaji wa malengo ya maendeleo endelevu katika mipango ya taifa ya maendeleo ya miaka mitano (5) na mipango mikakati ya Wizara, Taasisi, Mikoa na Halmashauri Nchini;Afisa Masuuli Ofisi ya Rais TAMISEMI aliifahamisha Kamati kuwa Mikoa ishirini na nne (24) imehuisha Mipango mikakati yake isipokuwa Mikoa miwili (2) ambayo ni Singida na Kigoma. Aidha Halmashauri mia moja na sitini na tatu (163) zimehuisha mipango yake na malengo ya maendeleo endelevu.Matarajio ya Ofisi ya Rais TAMISEMI ni kuwa ifikapo Machi 2024, Sekretarieti za Mikoa zote na Halmashauri zote ziwe zimehuisha mipango mikakati yao na malengo ya maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Spika, vilevile ufafanuzi uliendelea kutolewa kwamba,Serikali imeanzisha kitengo cha ufuatiliaji na tathmini (Monitoring and Evaluation) kwenye kila Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa hivyo inatarajiwa kuanzia Mwezi wa saba (7), 2024 vitengo hivi vitapewa bajeti,hii itawezesha upatikanaji wa takwimu kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa hoja inayohusu upatikanaji wa takwimu katika kufanya tathmini;Mtakwimu Mkuu wa Serikali alifafanua kwamba ni kweli kulikuwa na asilimia 39 ya upatikanaji wa takwimu kabla ya zoezi la Sensa ya Watu na Makazi. Hata hivyo, baada ya zoezi la Sensa ya Watu na Makazi, takwimu za viashiria imepanda hadi kufikia asilimia 61.

Mheshimiwa Spika, kwa hoja inayohusu ukusanyaji wa mapato; Afisa Masuuli Wizara ya Fedha alifafanua kuwa wanashirikisha wadau kupitia vyanzo vya kodi vilivyopo ili kuhakikisha vinakuwa na ufanisi katika ukusanyaji wa mapato na vyanzo vilivyopo vinakuwa na tija kwa Serikali na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo ya kina ya Serikali, Kamati iilifanya tathmini ya maelezo hayo ukilinganisha na hoja za ukaguzi na umuhimu wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi. Hivyo basi, Kamati imeboresha mapendekezo yake kuhusu ukaguzi huu kama yanavyoonekana katika Sehemu ya Tatu ya Taarifa hii.

2.1.12 Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi Katika Uendeshaji na Matengenezo ya Miradi ya Maji

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Tanzania imeweka kipaumbele katika upanuzi wa miradi ya miundombinu ya maji. Hii inafanywa ili kukidhi mahitaji ya maji yanayoongezeka Nchini kutokana na ukuaji wa miji na ongezeko la watu. Malengo ya serikali ifikapo Mwaka 2025 ni kufikia asilimia 95 na asilimia 85 ya huduma za maji mijini na vijijini mtawalia. Ili kufikia lengo hilo, Serikali imeongeza uwekezaji katika Sekta ya Maji katika kipindi cha miaka kumi (10) iliyopita kutoka **shilingi bilioni 563.1** hadi **shilingi bilioni 705** katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2020/21.

Mheshimiwa Spika, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anafafanua kwamba, pamoja na maboresho na kasi ya upanuzi wa miundombinu hiyo, msisitizo upo zaidi kwenye ujenzi wa miundombinu mipya ukilinganisha na matengenezo ya miundombinu iliyojengwa hapo awali. Kutokana na hatua hiyo, kumekuwa na kupungua kwa uwezo wa usambazaji maji wa

miundombinu ya maji iliyojengwa na kuongeza hatari ya kushindwa kutoa huduma endelevu ya maji.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya CAG inaendlea kubainisha kwamba,kutofanyika kwa matengenezo ya kutosha, kumesababisha uchakavu wa miundombinu ya maji. Matokeo yake, kipindi cha matumizi kilichotarajiwa hakiwezi kufikiwa huku gharama za ujenzi mpya zikiwa zimeongezeka. Kwa msingi huo, kuna hitaji kubwa la kuwa na mkakati wa usimamizi wa kutosha wa usambazaji maji na matengenezo ya mitambo ya maji kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi huu ulilenga kutathmini iwapo Wizara ya Maji kupitia Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) na Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mijini, zinaendesha na kutengeneza miradi ya usambazaji maji kwa ufanisi ili kuhakikisha kunakuwa na huduma endelevu.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulijikita katika uendeshaji wa miundombinu ya usambazaji maji ambapo ukaguzi ulilenga katika masuala mahsusi kama vile; mipango na ratiba iliyoandaliwa, uchukuaji wa maji kutoka kwenye chanzo, mchakato wa bili na ukusanyaji wa mapato, usafirishaji wa maji kutoka kwenye chanzo (njia kuu na mfumo wa usambazaji), shughuli za kusafisha maji, shughuli za kuhifadhi maji, kupima mita za maji zinazotolewa kwa wateja; na mchakato wa bili na ukusanyaji wa mapato mijini na vijijini.

Mheshimiwa Spika, vilevile ukaguzi huu uliangalia katika eneo la matengenezo ya mitandao ya usambazaji maji, lengo lilikuwa kuangalia aina zote za shughuli za matengenezo,yaani, matengenezo ya kuzuia, kurekebisha na utendaji. Kwa aina zote za matengenezo, lengo lilikuwa ni kuangalia masuala mahsusi kama vile mipango ya matengenezo, ufuatiliaji wa mtandao wa usambazaji maji, ukarabati au uingizwaji wa sehemu mbalimbali za miundombinu ya usambazaji wa maji, orodha ya sehemu zilizoathirika na zana zinazohitajika kwa ukarabati, kusafisha mfumo na upakaji mafuta kwenye mitambo kwa maeneo ya mijini na vijijini.

Mheshimiwa Spika, mawanda ya ukaguzi yalijumuisha miaka mitatu ya fedha (2019/20 hadi 2021/22) ili kupata hitimisho la ukaguzi na mapendekezo ya kutosha kulingana na mwenendo wa utendaji. Pia, hiki ndicho kipindi ambacho RUWASA ilianzishwa (2019), hivyo utendaji wake ulipimwa kwa kuzingatia muda ilipoanzishwa.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi huu umebainisha maeneo matatu (3) ambayo yanahitaji kuboreshwa. Maeneo hayo ambayo yanahitaji maboresho ni pamoja na; uendeshaji wa skimu za usambazaji maji zilizoanzishwa Nchini; matengenezo ya skimu za usambazaji maji zilizoanzishwa Nchini; na namna Wizara ya Maji inavyosimamia utendaji wa Mamlaka za Maji na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Maelezo ya kina kuhusu matokeo ya ukaguzi huo ni kama ifuatavyo:-

a) Matokeo ya Ukaguzi kuhusu Uendeshaji na Utengenezaji wa Miradi ya Usambazaji Maji Mijini

Katika eneo hili kulibainika masuala kadhaa kama ifuatavyo:-

(i) Mamlaka za Usambazaji Maji Mijini nane (8) zilizotembelewa,ilibainika kuwa, Mamlaka tano (5) zilikuwa na taratibu rasmi za uendeshaji huku tatu (3) zikiendeshwa bila kuwa na taratibu rasmi za uendeshaji zilizopaswa kufuatwa kwenye skimu ya maji husika. Hii ilitokana na ukosefu wa ufuatiliaji na mpango wa uhamasishaji , jambo ambalo ilikuwa linakiuka Mwongozo wa Uendeshaji na Matengenezo wa Wizara ya Maji[16];

(ii) Ukaguzi ulibaini kuwa, kwa miaka mitatu (3) ya fedha iliyopita, uzalishaji wa maji kwa Mwaka ulikuwa chini ukilinganisha na uwezo wa miundombinu ya usambazaji wa maji iliyowekwa licha ya kuwa mahitaji ya maji hayakufikiwa. Hii ilidhihirika pia kwa Mamlaka nane (8) za Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Mijini zilizotembelewa kama inavyofanunuliwa kwenye **Kielelezo Na. 2.1 hapa chini:-**

[16] Rejea Kifungu cha 4.2 cha Mwongozo wa Uendeshaji na Matengenezo wa Wizara ya Maji.

Kielelezo Na. 2.1: Uwezo wa Uzalishaji wa Mamlaka



Kielelezo Na. 2.1 kinaonyesha kuwa, kati ya Mamlaka nane (8) za Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Mijini zilizotembelewa, Mamlaka moja (1) tu (DUWASA) iliyotumia uwezo uliowekwa kwa asilimia 100. DAWASA na MWAUWASA pia zilibainika kuwa na matumizi ya juu kiasi ya uwezo uliowekwa wa asilimia 78.5 na asilimia 61.8 mtawalia. Aidha, LUWASA ilibainika kuwa na uwezo mdogo zaidi wa matumizi kati ya mamlaka zilizotembelewa ikiwa na uwezo wa kutumia asilimia 22.6 tu ya uwezo wake;

(iii) Katika mamlaka nne (4) kati ya nane (8) zilizotembelewa kulikuwa na miundombinu ya usambazaji maji isiyofanya kazi ipasavyo.Katika Mamlaka ya Maji Lindi Mjini, visima vinne (4) kati ya nane (8) vya mradi wa Nga'apa vyenye uwezo wa kuzalisha maji takribani mita za ujazo 2,856 havikuwa vinafanya kazi. Hali kadhalika, wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa katika Mamlaka za Maji Dar es Salaam na Bukoba mjini, pampu ya akiba ya kuvuta maji kutoka kwenye chanzo cha Ruvu Juu kwa Dar es salaam na chanzo cha Bunena kwa Bukoba Mjini zilikuwa hazifanyi kazi mtawalia kutokana na kuharibika kwa mota;

(iv) Ukaguzi ulibaini kiasi cha ukusanyaji wa mapato kutoka kwa ankara za maji kilikuwa chini ukilinganisha na ankara za maji zilizotolewa kama inavoonyeshwa kwenye **Kielelezo Na. 2.2.** hapa chini:-

Kielelezo Na. 2.ielelezo Na.2.2: Asilimia za 2: Asilimia za Ukusanyaji Mapato Ukusanyaji Mapato kwenye Ankara



Kielelezo Na. 2.2 kinaonesha kuwa, Mamlaka za Maji 3 kati ya 8 zilizotembelewa zilikusanya mapato kutoka kiasi kilichodaiwa kwa zaidi ya 100%. Pia, Mamlaka za Maji 5 kati ya 8 zilizotembelewa zilikusanya chini ya 100% kutoka kwenye kiasi kilichokuwa kinadaiwa.Pamoja na makusanyo ya jumla kutoka kwenye ankara zilizotolewa kuwa zaidi ya 80% katika Mamlaka zote 8 zilizotembelewa, makusanyo halisi kutoka ankara ya Mwaka husika yalikuwa chini ya asilimia iliyooneshwa. Hii ilitokana na ukweli kwamba, makusanyo hayo yalijumuisha makusanyo ya madeni ya miaka iliyopita; na

(v) Ukaguzi ulibaini kuwa, kwa mwaka wa fedha 2019/20, Taasisi mbalimbali za Serikali zilikuwa zinadaiwa takribani **shilingi bilioni 43.3** hadi kufikia Mwezi Mei, 2020. Wastani wa madeni kwa Mwaka ya mamlaka 8 zilizotembelewa ilikuwa ni **shilingi bilioni 31.7** kuanzia 2019/20 hadi 2021/22. Mamlaka ya Maji Dar es Salaam ilikuwa na wastani wa madeni ya Ankara za maji kwa Mwaka ni **shilingi bilioni 11.309**. Kiasi kidogo cha madeni ya maji kilikuwa ni **shilingi milioni 119** kwenye Mamlaka ya Maji LUWASA.

b) Matokeo ya Ukaguzi Kuhusu Matengenezo ya miundombinu Katika Skimu za Maji

(i) Ukaguzi ulibaini kuwa, katika mamlaka zote nane (8), kulikuwa na mapungufu katika mipango ya matengenezo ya kila Mwaka/mara kwa mara ambayo yangehakikisha

matengenezo endelevu ya vifaa vya maji vilivyowekwa kwenye skimu mbalimbali za usambazaji maji;

(ii) Ukaguzi ulibaini kuwa, kwa Mamlaka za Maji nane (8) zilizotembelewa, tano (5) zilikuwa na rekodi za matengenezo ya miundombinu ya usambazaji maji wakati Mamlaka tatu (3) hazikuwa na kumbukumbu za matengenezo;

(iii) Ukaguzi ulibaini kuwa, Mamlaka 6 kati ya 8 zilizotembelewa, zilikuwa na mifumo ya kufuatilia utendaji wa mtandao wa usambazaji maji wakati Mamlaka mbili (2) hazikuwa na mfumo huo. Kati ya Mamlaka sita (6) zilizokuwa na mfumo wa usimamizi ni moja (1) tu (DAWASA) iliyokuwa ikifanya kazi kwa ufanisi huku tano (5) zikibainika kuwa na kasoro.Kutokana na kukosekana au kuharibika kwa mfumo wa usimamizi wa taarifa katika Mamlaka za Maji zilizotembelewa;

(iv) Ukaguzi ulibaini dosari katika ukaguzi wa mitandao ya usambazaji maji katika Mamlaka nane (8) zilizotembelewa.Hali hii inaweza kusababisha gharama kubwa za matengenezo au ubadilishwaji wa sehemu ambazo hazikukaguliwa na kurekebishwa kwa wakati;

(v) Ukaguzi ulibaini kuwa, kwa Mwaka wa Fedha 2019/20, 2020/21 na 2021/22 ni Mamlaka ya Maji Moshi Mjini pekee kati ya Mamlaka 8 haikuvuka ukomo wa kiwango cha maji yanayopotea ambacho ni 20%. Hili lilitokea Mwaka 2020/21 pekee huku katika miaka mingine kiwango cha upotevu wa maji kikiwa zaidi ya 20%. Upotevu wa maji ulisababishwa na mambo kama wizi wa maji, na dira za maji kushindwa kusoma kwa usahihi maji yanayotumika. Pia, upotevu wa maji ulitokana na changamoto za miundombinu kama vile kupasuka kwa mabomba; na Kutokana na upotevu wa maji zaidi ya kiwango kinachoruhusiwa cha 20%, Mamlaka nane (8) zilizotembelewa, kwa ujumla, zilipoteza takribani wastani wa kiasi cha **shilingi bilioni 57.2** kwa mwaka wa fedha 2019/20 na **shilingi bilioni 60.94** kwa mwaka wa fedha

2020/21 ambazo zingepatikana kutokana na ankara za maji kama upotevu wa maji ungedhibitiwa ipasavyo.

c) Matokeo ya Ukaguzi Uendeshaji na Utengenezaji wa Miradi ya Usambazaji Maji Vijijini

Katika eneo la uendeshaji na matengenezo ya miradi ya usambazaji maji vijijini, taarifa ya ukaguzi ilibainisha masuala yafuatayo:-

(i) Ukaguzi ulibaini kuwa, katika skimu 19 za usambazaji maji zilizotembelewa, wasimamizi wa uendeshaji hawakuwa na miongozo ya kuendesha mitambo na miundombinu iliyopo katika skimu zao ili kuweza kuhakikisha kuwa miundombinu ya usambazaji maji inaendeshwa katika utaratibu maalum;

(ii) Ukaguzi ulibaini kuwa, katika jumuiya za watoa huduma ngazi ya jamii (CBWSOs) 19 zilizotembelewa, hazikuwa na mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa madeni ya maji. Pia, Jumuiya 3 kati ya 19 hazikuwa zimefungwa dira za kusoma maji kwa wateja wao na Jumuiya zingine 16 zilikuwa hazijafunga dira kwa wateja wao kati ya 7% hadi 89%. Vilevile ilibainika kuwa, kwa Jumuiya zote 19 zilizotembelewa, hakukuwa na dira ya kupima wingi wa maji ili kujua kiwango cha maji kinachozalishwa na kinachosambazwa kwa wateja;

(iii) Ukaguzi ulibaini kuwa skimu 17 kati ya 19 zilizotembelewa hazikuwa na utaratibu wa kupima ubora wa maji yanayosambazwa kwa jamii husika. Skimu 2 za LawateFuka na Makiwaru-Magadini ndiyo zilizokuwa zinapima ubora wa maji kila baada ya miezi mitatu (3) kwa kutumia maabara za nje;na

(iv) Ukaguzi ulibaini kuwa skimu 12 kati ya 19 zilizotembelewa ambazo ni sawa na asilimia 63 zilikuwa zinaendeshwa na watu wasio na vigezo vilivyoainishwa kwenye Sheria Na. 5 ya Mwaka 2019, ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira ambayo imeainisha kuwa timu ya uendeshaji wa Skimu za maji vijijini inapaswa kuundwa na msimamizi ambaye anatakiwa kuwa na cheti cha ufundi kuanzia kiwango cha

NTA Daraja la 3, mwekahazina ambaye anapaswa kuwa na cheti cha uhasibu kuanzia kiwango cha NTA daraja la 3 na kuendelea, pamoja na taaluma nyingine ambayo itaonekana inafaa kutokana na aina ya Skimu.

d) Matengenezo ya Miundombinu Katika Skimu za Usambazaji Maji Vijijini

(i) Ukaguzi ulibaini kwamba, katika skimu 19 za usambazaji maji vijijini zilizotembelewa, kulikuwa na dosari katika taarifa ya matengenezo yaliyofanyika kwenye mitambo na miundombinu mingine iliyopo katika skimu husika. Kutokana na hilo ilikuwa ni vigumu kwa wasimamizi wa skimu za maji kuweza kufanya tathmini ya utendaji kazi wa mtambo husika na kuchukua hatua stahiki;

(ii) Ukaguzi ulibaini kuwa skimu za usambazaji maji vijijini zilizotembelewa kulikuwa na mapungufu katika ratiba na mpango wa matengenezo katika miundombinu ya usambazaji maji ambao ungewezesha kufanyika matengenezo ya mara kwa mara pasipo kusubiri kuharibika kwa mtambo au miundombinu husika;na

(iii) Ukaguzi ulibaini kuwa Jumuiya za Watoa Huduma za Maji Vijijini (CBWSOs) hazikuwa na utaratibu ambao ungewawezesha kujua kiwango cha maji yanayopotea katika skimu za usambazaji maji vijijini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo ya kina kuhusu hoja za ukaguzi zilizojitokeza katika maeneo mbalimbali yanayohusu uendeshaji na utengenezaji wa miradi ya maji, Kamati ilikutana na Afisa Masuuli Wizara ya Maji. Kikao hicho kilifanyika tarehe 24 Januari, 2024 kikiwa na lengo la kupokea na kujadili maelezo ya Afisa Masuuli kuhusu utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika taarifa ya ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya ufuatiliaji yameonesha kuwa kati ya mapendekezo kumi na saba (17) yaliyotolewa, pendekezo moja (1) limetekelezwa kikamilifu, mapendekezo mawili (2) yapo

katika hatua nzuri za utekelezaji, na mapendekezo kumi na nne (14) yapo katika hatua za awali za utekelezaji. Jedwali Na. 2.5 linaainisha hali ya utekelezaji kwa kila mkaguliwa:-

Jedwali Na 2.5: Hali ya ujumla ya utekelezaji wa Mapendekezo

Taasisi Kaguliwa	Idadi ya Mapendekezo yaliyotolewa	Hali na kiwango cha utekelezaji			
		Idadi ya Mapendekezo Yaliyotekelezwa Kikamilifu	Idadi ya Mapendekezo yaliyo katika hatua za awali za Utekelezaji	Idadi ya Mapendekezo yaliyo katika hatua nzuri za Utekelezaji	Idadi ya Mapendekezo Yasiyotekelezwa Kabisa
Wizara ya Maji	09	**0**	9	0	**0**
Wakala wa Maji Vijijini	08	1	**5**	**2**	**0**
Jumla	**17**	**1**	**14**	**2**	**0**

Chanzo: Uchambuzi wa Taarifa ya CAG kwa Kamati Januari, 2024.

Mheshimiwa Spika, Jedwali 2.5 hapo juu linatoa mchanganuo wa utekelezaji wa mapendekezo yote kumi na saba (17) yaliyotolewa kwa Wizara ya Maji na RUWASA. Kwa ujumla, katika mapendekezo kumi na saba (17) yaliyotolewa, pendekezo moja (1) limetekelezwa kikamilifu, mapendekezo mawili (2) yapo katika hatua nzuri za utekelezaji, na mapendekezo kumi na nne (14) yapo katika hatua za awali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, katika hatua ya mjadala, Afisa Masuuli alitoa ufafanuzi kuhusu hoja kadhaa za CAG na Kamati. Mathalani, kwa hoja ya skimu za maji kutokuwa na miundo mbinu ya kutibu maji alikiri changamoto hiyo. Miradi mingi iliyokuwa na changamoto hiyo ni ile iliyotekelezwa kabla ya RUWASA kuanzishwa (2009), hivyo kwa miradi mipya ambayo inatekelezwa chini ya RUWASA, wamezingatia utengenezaji wa miundombinu ya kutibu maji. Aidha, Afisa Masuuli aliithibitishia Kamati uwepo wa Mwongozo wa kutibu maji ambao umeanza kufanya kazi kuanzia mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, kwa hoja inayohusu upotevu wa maji, Afisa Masuuli aliifahamisha Kamati kuwa wameanza kufunga dira za maji za malipo ya kabla kwa watumiaji wakubwa wa maji na Taasisi za Serikali. Aidha, Mamlaka za Maji zinasimamiwa ipasavyo kufanya matengenezo ya mabomba yaliyopasuka na matumizi ya teknolojia katika kudhibiti upotevu wa maji. Mathalani kwa Mkoa wa Dar es Salaam,asilimia ya maji yanayopotea imeshuka kutoka asilimia 41 wakati ukaguzi huu unakamilika (2022) hadi asilimia 37.9 kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, Afisa Masuuli aliifahamisha Kamati kuwa dira zote za maji zinazotumika hapa nchini kwa sasa zinapitia zoezi la upimaji wa ufanisi wake kwa kipindi cha miezi sita (6) kabla ya kuruhusiwa kufungwa kwa wateja. Lengo la hatua hii ni kuepuka ufungaji wa dira za maji zenye mapungufu kama ilivyowahi kutokea hapo awali ambazo zilichangia upotevu wa maji na mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya Afisa Masuuli Wizara ya Maji yataendelea kufanyiwa uhakiki na CAG kwa kaguzi zijazo na kuwasilishwa mbele ya Kamati. Aidha, Kamati imetoa mapendekezo ya maboresho katika Sehemu ya Tatu ya Taarifa hii kwa hoja ambazo ziliibuliwa na CAG na zinahitaji kufanyiwa kazi.

2.2 Taarifa za Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, mapema Mwezi Machi, 2023, Kamati ilifanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo ili kujiridhisha na thamani halisi ya fedha iliyotumika katika utekelezaji wa miradi hiyo. Ziara zilifanyika katika Mikoa ya Njombe, Iringa, Morogoro, Mtwara na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, miradi iliyotembelewa ni pamoja na mradi wa "backbone transmission investment" Awamu ya Pili unaohusu ujenzi wa kituo cha kupoza umeme uliopo Iringa, Mradi wa Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Njombe, mradi wa Kiwanja cha Ndege cha Iringa,mradi wa kuchakata na kusafirisha gesi asilia eneo la Madimba Mtwara na mradi wa ujenzi wa Reli ya kisasa SGR LOT 1 (Kipande cha Dar es salaam-Morogoro).

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati ilipata fursa ya kutembelea na kukagua mradi wa usambazaji gesi majumbani, Mtwara Mjini, mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Kanda ya Mtwara,mradi wa ujenzi wa nyumba za ghorofa kwa watumishi wa umma Temeke na miradi ya maboresho ya miundombinu ya barabara inayotekelezwa chini ya mradi mkubwa wa "Dar es salaam Metropolitan Development Project" (DMDP).

Mheshimiwa Spika, miradi mingine ilikuwa ni pamoja na ujenzi wa Barabara ya mwendokasi kutoka kati kati ya Jiji la Dar es Salaam kuelekea Gongo la mboto Dar es salaam, uchimbaji wa visima vya maji eneo la Kigamboni, ujenzi wa skimu ya umwagiliaji shamba la mbegu la Kilangali Mkoani Morogoro, ujenzi wa mabweni mawili katika chuo cha ualimu wa ufundi stadi Morogoro, uboreshaji wa mtandao wa usambazi huduma ya maji wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Njombe (NJUWASA) na ujenzi wa kiwanda cha dawa na vifaa tiba cha Idofi unaotekelezwa na Bodi ya Madawa Tanzania (MSD).

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia majukumu ya msingi ya Kamati hii kama yalivyoainishwa katika Kifungu cha 13 (a) hadi (c) cha Kanuni za Bunge Toleo la Februari , 2023, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuhusu hali halisi ya miradi iliyokaguliwa. Maelezo ya kina kwa kila mradi uliotembelewa na kukaguliwa ni kama ifuatavyo: -

2.2.1 Mradi wa Njia ya Usafirishaji Umeme (Backbone Transmission Investment) Awamu ya Pili - Iringa

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kukagua mradi huu unaotekelezwa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) katika Mkoa wa Iringa. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za mkopo kiasi cha **Dola za Marekani milioni 48,477,264** (ikijumlisha **shilingi 1,438,959,549** kutoka Serikali ya Tanzania kupitia TANESCO) ambapo pesa zote zilikuwa zimetumika katika kutekeleza mradi.

Mheshimiwa Spika,changamoto zilizobainika wakati wa utekelezaji wa mradi ni pamoja na kuchelewa kupatikana kwa msamaha wa kodi katika utekelezaji wa mradi, dhamana ya

utendaji (performance security) kutokidhi kipindi cha matazamio ya mradi (defective period) na utekelezaji wenye mapungufu katika kazi za saruji (concrete works).

2.2.2 Mradi wa Uchimbaji Visima Kigamboni Dar es Salaam

Mheshimiwa Spika, mradi wa uchimbaji wa visima virefu vya maji katika eneo la Kigamboni Dar es Salaam unatekelezwa na Serikali kupitia Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA). Mradi huu unahusisha uchimbaji wa visima 7 kati ya visima 11 vilivyochimbwa na mkandarasi JV Serengeti na NSPT ltd.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa visima virefu umewezesha ongezeko la uzalishaji wa maji kiasi cha lita millioni 70 kwa siku na hivyo kufanya uwezo wa uzalishaji maji kutoka vyanzo vya DAWASA kufikia lita millioni 590 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, mradi huu unatekelezwa kwa fedha kutoka Serikali kuu na fedha za mapato ya ndani ya DAWASA ambapo gharama ya jumla ya mradi ni **shillingi bilioni 31.42**, kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 23.09** zimetolewa na Serikali kuu na **shilingi bilioni 8.33** zinatolewa na DAWASA.

Mheshimiwa Spika, hadi Kamati inahitimisha ziara yake Mwezi Machi, 2023, changamoto zilizobainika katika mradi huo ni kuchelewa kukamilika kwa mradi kwa wakati hivyo kuongeza gharama za mradi kutoka **shilingi bilioni 18.48** hadi **shilingi bilioni 26.45**.Vilevile kulikuwa na changamoto ya utoaji wa fedha usiotosheleza kwa Serikali kwa ajili ya mradi wa uchimbaji wa visima katika eneo la Kimbiji kwani hadi kufikia Mwezi Juni,2022 Serikali ilikuwa imetoa **shilingi bilioni 11.8** kati ya **shilingi bilioni 23.09**.

2.2.3 Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Kanda Mtwara

Mheshimiwa Spika, fedha zilizotumika kwenye mradi huu ni **shilingi bilioni 15.81**. Mchanganuo wa malipo yaliyofanyika ulibainisha kuwa mshauri mwelekezi hadi Mwezi Mei,2021 alilipwa **shilingi 576,662,61.26** na mkandarasi hadi Mwezi Juni,2021 alilipwa

shilingi bilioni 15.15 hivyo kufanya jumla ya fedha zilizolipwa hadi Juni,2021 kuwa **shilingi bilioni 15.73**.

Mheshimiwa Spika,changamoto za mradi huu ni pamoja na dosari katika upembuzi yakinifu, mipango ya bajeti kwa mradi isiyojitosheleza,mapungufu katika usanifu na vielelezo vya kitaalamu (specifications), kutofanyika tathmini ya mazingira na makadirio ya gharama za ujenzi (BoQs) kutojitosheleza.

2.2.4 Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Mwendo Kasi Kutoka Katikati ya Jiji la Dar Es Salaam Kuelekea Gongo la Mboto

Mheshimiwa Spika, fedha za malipo yaliyoidhinishwa na kufanyika kwa kipande cha kwanza hadi Mwezi Machi 2023 kiasi cha **shilingi 39,425,985,133.56**.Kiasi hiki cha pesa kinajumuisha malipo ya awali (advance payment) ya **shilingi 34,749,618,016.34** na malipo ya kwanza yanayohusiana na kazi iliyofanyika ni **shilingi 4,676,367,117.22** .

Mheshimiwa Spika, changamoto zilizobainika katika mradi huu ni kuchelewa kuanza ujenzi (LOT II) kutokana na changamoto ya upatikanaji wa eneo la ujenzi wa karakana(depot), kubadilishwa kwa eneo lililotolewa na DART kwa ajili ya ujenzi wa karakana mara kwa mara ikiwa ni kutoka eneo la awali Gongo la mboto ambalo lilitwaliwa na TRC kupitia mradi wa SGR. Changamoto nyingine ni kuisha kwa muda wa mkopo "credit period" ambao ulianza tarehe 13 Juni, 2017 ulitegemewa kuisha tarehe 31 Disemba, 2023.

2.2.5 Mradi wa Kuchakata na Kusafirisha Gesi Mtwara

Mheshimiwa Spika,Fedha za mradi huu mfadhili ni Serikali ya Tanzania kupitia mkopo kutoka EXIM BANK kiasi cha **Dola za Marekani bilioni 1.195** (**shilingi za Tanzania trilioni 2.30**) na mkopo huu utalipwa kwa miaka 13 (miezi 156).

Mheshimiwa Spika, changamoto zilizobainika kwenye mradi huu ni utegemezi wa wataalamu wa kigeni kwa ajili ya ukarabati na matengenezo ya miundombinu ya gesi, kutofanyika kwa usafishaji

wa ndani ya boma la gesi(pigging), ucheleweshaji wa ununuzi wa mfumo wa kidigitali wa usimamizi wa ukarabati wa miundombinu ya gesi asilia (computerized maintainance management system-CMMS) na kutu kwenye miundombinu ya gesi haidhibitiwi ipasavyo.

2.2.6 Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Ghorofa kwa Watumishi wa Umma Temeke Quarter

Mheshimiwa Spika,mradi huu unatekelezwa na Wakala wa Majengo Tanzania(TBA) na kugharamikiwa na Serikali ya Tanzania kwa gharama ya **shilingi 21,369,222667.91** kwa jengo moja ikiwa ni gharama ya ujenzi na huduma ya ushauri.Mradi huu ulitengewa bajeti ya **shilingi bilioni 5,128,986,000** ambapo kiasi cha **shilingi 4,300,000,000** kilikuwa kimepokelewa hadi Mwezi Machi,2023 kwa ajili ya kutekeleza mradi.

Mheshimiwa Spika,mapungufu yaliyojitokeza kwenye mradi ni kupangwa kutekelezwa kwa miaka miwili (2022/23 na 2023/24) lakini fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 ni **shilingi 5,128,986,000** tu sawa na asilimia 24 ya jumla ya gharama ya mradi.

Mheshimiwa Spika, vilevile wakati Kamati inatembelea mradi huu ilibainika kuwa, mradi ulianza kabla ya kufanyika kwa tathmini ya athari ya mazingira na ya jamii "Environmental and Social Impact Asessment"(ESIA), mradi haukuwa umesajiliwa na Bodi ya Usajili wa Wahandisi(ERB) pamoja na Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majengo (AQRB) kinyume na matakwa ya Sheria[17].

2.2.7 Mradi wa Kiwanda cha Dawa cha Idofi,Unaotekelezwa na Bodi ya Madawa Tanzania (MSD)

Mheshimiwa Spika, hadi Kamati inatembelea mradi huu Mwezi Machi, 2023 mradi huu ulikuwa haujaanza uzalishaji na upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.Fedha zilizotumika kwenye mradi huu ni jumla **shilingi bilioni 16,957,183,331.31** kwa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni,2021.

[17] Rejea Sheria ya Wahandisi Namba 15 ya Mwaka 1997.

Mheshimiwa Spika,mapungufu yaliyobainishwa kwenye mradi huu ni kuanzishwa kwa kiwanda cha Idofi na ununuzi wa malighafi za kuzalisha bidhaa kabla ya jengo la kuhifadhi mashine hiyo kukamilika. Vilevile mradi huu ulianza bila ya kuwa na mpango endelevu wa kibiashara wa kupata malighafi za kiwandani.

2.2.8 Mradi wa Dar es salaam Metropolitan Development Project (DMDP)

Mheshimiwa Spika,gharama za mradi ni **Dola za Marekani milioni 330.30** ambapo Benki ya Dunia imetoa **Dola za Marekani milioni 300**,Shirika la Maendeleo la Nordic limetoa **Dola za Marekani milioni 5** na gharama zilizobaki **Dola za Marekani milioni 25.30** zilitolewa na Serikali kama fidia kwa watu waliotakiwa kupisha maeneo ya utekekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Spika,changamoto iliyobainika katika mradi huu ni kuchelewa kukamilika hivyo kulazimu muda wa nyongeza wa miezi 11 kutoka miezi 15 ya mkataba hadi miezi 26 . Sababu kubwa ya kuchelwa miradi ya DMDP ilitokana na ucheleweshwaji wa malipo kwa mkandarasi kwa siku 33 hadi 295 kinyume na masharti ya mkataba. Vilevile kulikuwa na dosari kwa cheti cha kumaliza na kukabidhi kazi (completion certificate) kutolewa tarehe 31/8/2021 kabla mkandarasi hajaanza wala kumaliza kazi zote alizolipwa ndani ya mkataba.

2.2.9 Mradi wa Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Iringa

Mheshimiwa Spika, hadi Mwezi Machi 2023, mkandarasi alikuwa amewasilisha hati za madai Na 1 hadi 12 zenye thamani ya **shilingi bilioni 26,382,225,563.25** na alikuwa ameshalipwa **shilingi bilioni 14,725,868,868.17** ambazo ni madai ya hati Na 1 hadi 7.Hivyo kwa wakati huo, mkandarasi alikuwa anadai **shilingi bilioni 11,656,356,698.08** ambazo ni hati za madai Na. 8 hadi Na. 12.

Mheshimiwa Spika,changamoto kwenye mradi huu ni kucheleweshwa kwa malipo ya mkandarasi zaidi ya siku 28 kama mkataba unavyoelekeza, hivyo kusababisha Serikali kulipa riba ya **shilingi milioni 983,578,900** (hati Na. 1 hadi 10), Serikali inadaiwa

jumla ya riba **shilingi milioni 223,651,810.19** . Vilvile kulikuwa na madai ya wananchi kutokana na kuchelewa malipo ya fidia kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na.5 (1999). Aidha, mapungufu katika upembuzi na usanifu wa mradi yamesababisha kuongezeka kwa gharama za mradi kwa asilimia 55 hadi kufikia **shilingi bilioni 63,742,748,090**.

2.2.10 Mradi wa Ununuzi na Usimikaji wa Rada 16 "Nodes HPC Cluster with 1536 Cores and 2 Master codes" kwa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA)

Mheshimiwa Spika,lengo la mradi huu ni kuboresha utabiri kwa kutumia mifumo ya kisasa ya kompyuta zenye uwezo mkubwa kwa ajili ya kulinda maisha na mali na kuongeza ufanisi kwa sekta za kiuchumi na kijamii zinazotegemea huduma za hali ya hewa. Gharama za mradi huu ni **shilingi bilioni 2,496,558,695.71.**

Mheshimiwa Spika,changamoto katika mradi huu zilikuwepo siku za nyuma ikiwa ni pamoja na mzalishaji kuwa na uhaba wa vifaa kama vile ICs,SSD,RAID,SSDs,DRAM memory and CPUs na zuio lililokuwepo la kusafiri Kwenda kwenye baadhi ya nchi lililosababisha kubadilisha ratiba ya mafunzo ya wataalamu. Vilvile CAG alibainisha malipo ya kiasi cha **shilingi milioni 118,384,353.92** kwa ajili ya huduma saidizi za kiufundi (technical support service) kilikuwa kimelipwa kabla ya kazi za mkataba kukamilika.

2.2.11 Mradi wa ujenzi wa Umwagiliaji Shamba la Mbegu la Kilangali

Mheshimiwa Spika,Wizara ya Fedha ilipokea fedha kutoka Benki ya Dunia na Serikali ya Tanzania kwa ajili ya shughuli za ukarabati na upanuzi wa shamba la mbegu la kilangali katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa kwa Mwaka wa Fedha 2017/18 na kiasi halisi cha mkataba ni **shilingi bilioni 5,428,692,298.92.**

Mheshimiwa Spika,changamoto iliyoibuliwa kwenye mradi huu ni Pamoja na mradi kuchelewa kukamilika kwa wakati uliopangwa, udhibiti usioridhisha wa gharama wakati wa ujenzi wa mradi na mapungufu katika udhibiti wa ubora.

2.2.12 Mradi wa REA Awamu ya Pili Kwa Baadhi ya Vijiji vya Mkoa Iringa

Mheshimiwa Spika, mawanda ya mradi huu yalihusisha ujenzi wa kilometa 341.3 za njia za msongo wa kati (MV line), kilometa 39 msongo mdogo (LV line) na uungwanishaji wa wateja wa awali wa njia moja 707 na njia tatu 54 na kupelekea umeme kwenye vijiji 39.

Mheshimiwa Spika, gharama za mkataba (zimejumuisha VAT) **shilingi 13,457,669,012.29**, gharama za mkataba zilizorejewa **shilingi 15,670,864,914.73**. Hadi kufikia Januari, 2023 kiasi kilicholipwa ukiondoa kiasi cha bakizo la kipindi cha matazamio ni **shilingi 5,731,414,404.33** sawa na asilimia 38 ya fedha zote za mkataba.

Mheshimiwa Spika, changamoto zilizokuwa zinaukabili mradi huu wakati wa ukaguzi Mwezi Machi, 2023 ilikuwa ni kuchelewa manunuzi na kuwasili kwa vifaa vya kutekelezea mradi vinavyotoka nje ya nchi uliosababishwa na ongezeko la bei za vifaa kwenye soko la Dunia (aluminium, copper, and steel). Vilvile, kuchelewa kufika kwa vifaa hasa vinavyoagizwa kutoka nje ya nchi kutokana na ugumu wa uzalishaji na usafirishaji wa vifaa hivyo uliosababishwa na mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO 19.

2.2.13 Uboreshaji wa Barabara ya Njombe – Moronga (53.9 Km)

Mheshimiwa Spika, Serikali ilianza utekelezaji wa mradi huu kwa kufanya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina uandaaji wa nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwago cha lami ambao ulifanywa mwaka 2014 na kampuni ya kihandisi ya M/S crown TECH-consult ltd ya Tanzania kwa gharama ya **shilingi 505,100,000.**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuchelewa kwa malipo ya mkandarasi kwa zaidi ya siku 28 kama ilivyokubaliwa kwenye mkataba hivyo kusababisha Serikali kulipa riba jumla ya shilingi **5,319,489,284.22** (kuanzia hati namba 2 hadi namba 18). Vilvile mradi ulikuwa unakabiliwa na changamoto ya kutokamilika kwa malipo ya fidia kwa wananchi 31 walioathirika na mradi ya **shilingi**

622,584,553 katika maeneo ya Ramadhani, Makete, Ndulamo, Usungilo na kisinga kwa kipindi cha miezi sita toka "valuation" kukamilika tarehe 29 Agosti 2022.

2.2.14 Mradi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe

Mheshimiwa Spika, mradi huu ulikuwa umekamilika kwa asilimia 96 na tayari majengo yanatoa huduma kama ambavyo imekusudiwa. Hata hivyo, jingo la chumba cha kuhifadhia maiti na baadhi ya kazi za nje (walk ways na prevements) zilitarajiwa kukamilika tarehe 30.03.2023 baada ya kufanya installation ya majokofu.

Mheshimiwa Spika, changamoto zilizobainika katika utekelezaji wa mradi huu ni pamoja na kupokea fedha za mradi kidogo kidogo kutoka Serikalini, kuongezeka kwa kazi nje ya mkataba ambazo ni miundombinu (umeme,viyoyozi,lifti,vifaa vya moto na tehama),ujenzi wa mochwari na jengo la damu salama na hali ya hewa ya mvua hivyo kutahiri utekelezaji wa mradi ndani ya muda uliopangwa.

2.2.15 Mradi wa Usambazaji Maji Njombe Mjini

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2021, taarifa ya fedha za Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Njombe (NJUWASA) ikiwa ni pamoja na mradi huu zilipata hati safi. Aidha, hadi Kamati inatembelea Njombe, mradi huu ulikuwa umekamilika na na kutoa huduma kwa wanufaika na Jumla ya gharama zilizotumika ni **Dola Marekani 415,895,529.17.**

2.2.16 Mradi wa Skimu ya Umwagiliaji Msolwa – Ujamaa

Mheshimiwa Spika, mradi huu unatekelezwa na Wizara ya Kilimo baada ya kupokea fedha kutoka Benki ya Dunia. Shughuli zinazotekelezwa ni ukarabati na upanuzi wa skimu ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, dosari zilizobainika katika mradi huu ni pamoja na upembuzi yakinifu usiojitosheleza ambapo, taarifa ya utafiti ya maji, uchunguzi wa topografia, taarifa ya nyanja ya uhandisi na tathmini ya mazingira hazikujumuishwa wakati wa kuanza mradi. Vilevile kulikuwa muda wa kukamilisha mradi uliongezeka kwa siku

180 sababu kubwa ni udhaifu wa wakandarasi na kuchelewa malipo kwa wakandarasi.

2.2.17 Ujenzi wa Mabweni ya Walimu Tarajali, VETA – Morogoro

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Mwezi Machi, 2023, jumla ya fedha zilizolipwa kwa mradi huu ni **shilingi 1,087,541,584.16.** Changamoto za mradi zilizobainika ilikuwa ni pamoja na kuchelewa malipo kwa mkandarasi kati ya siku 75 hadi 186. Hii ilisababisha kuchelewa kukamilika kwa mradi kwa muda wa miaka mitatu na miezi minne (kuanzia 13 septemba 2019 hadi tarehe ya kumaliza ujenzi 30 januari 2023).

2.2.18 Mradi wa Usambazaji Gesi Majumbani Mtwara – Mjini

Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusisha ujenzi wa miundombinu ya gesi awamu ya kwanza kwa gharama ya **shilingi 3,200,000,000** sawa na kiasi cha fedha kilichotengwa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021. Wanufaika wa mradi huu ni wananchi wa Mkoa wa Mtwara na taasisi zote zilizopo ndani ya mkoa wa Mtwara.

2.3 Uchambuzi wa Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha Ulioishia Tarehe 30 Juni, 2022

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 02 Novemba, 2023 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) iliwasilisha Taarifa yake Bungeni kuhusu uchambuzi wa Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha Kamati cha Mwezi Agosti 2023 hadi Novemba 2023, shughuli za Kamati zilijielekeza katika kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Wizara na Mashirika ya Umma kama yalivyobainishwa katika Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa

Hesabu za Serikali (CAG) kwa Mwaka wa Fedha unaoshia tarehe 30 Juni, 2022. Aidha, shughuli hizo zilikusudia kufuatilia utekelezaji wa maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kwa nyakati tofauti kwa kipindi chote cha Mwaka 2022 hadi 2023.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, kwa Mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022, kwa upande wa Serikali Kuu, CAG alikagua na kutoa Hati za ukaguzi kwa Wizara na Idara za Serikali 65, Balozi 43, Sekretarieti za Mikoa 26,Wakala 30 na Mifuko Maalumu 16. Aidha, katika kundi hilo la Serikali Kuu, Kaguzi za Vyama vya Siasa 19, Hospitali za Rufaa na Maalumu 34 na Taasisi nyinginezo 129 zilifanyika na kukamilika. Zaidi ya hayo, ukaguzi ulijumuisha Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Hesabu Jumuifu za Taifa (consolidated accounts) na ukaguzi wa awali wa mafao ya wastaafu kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2022.

Mheshimiwa Spika, katika ngazi ya Kamati, Kamati ilifanikiwa kuchambua na kujadili taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za mafungu 18 ya Serikali Kuu, Mashirika ya Umma 39, Taasisi zinazojitegemea 10 na Mifuko Maalumu 13.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu lilipitia na kujadili Taarifa ya Kamati inayohusu Taarifa hizo za ukaguzi kwa muda wa siku tatu (3) kuanzia tarehe 02 Novemba, 2023 hadi tarehe 04 Novemba, 2023. Baada ya mjadala Bungeni, Bunge lilipitisha jumla ya Maazimio ya Bunge kumi na nane (18).

Mheshimiwa Spika, Kamati itaendelea kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Maazimio hayo ya Bunge kuanzia Mwezi Machi, 2024 ili kuhakikisha uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma. Kamati ina imani kwamba Bunge litapata fursa ya kujadili tena hali halisi ya utekelezaji wa Maazimio hayo ya Bunge kabla ya kukamilika kwa Mkutano wa Bunge la Bajeti.

2.4 Mafunzo na Semina za Kuwajengea Uwezo Wajumbe

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukurani za dhati kwako wewe binafsi kwa kutoa idhini kwa Kamati ya PAC kupatiwa mafunzo na semina mbalimbali kwa ajili ya kuongeza uelewa, ufanisi na uwezo wa wajumbe katika kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma. Aidha, napenda kuishukuru Ofisi ya Katibu wa Bunge kwa kufanya uratibu na kuwezesha kufanyika kwa shughuli hizo za mafunzo na semina.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Mwezi Januari, 2023 hadi Mwezi Februari, 2024 Kamati kwa idhini yako ilifanikiwa kupatiwa mafunzo na semina katika maeneo tisa (9). Mafunzo na Semina hizo yalitolewa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Msajili wa Hazina, Taasisi mbalimbali za Serikali pamoja na Asasi za Kiraia zinazoangalia matumizi ya fedha za umma. Mafunzo na Semina hizo ziliweka msisitizo katika maeneo yafuatayo:-

a) Uchambuzi wa Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

b) Kuongeza uelewa kuhusuhati mbalimbali za ukaguzi zinazotolewa katika Ripoti za CAG;

c) Kujenga na kuongeza uelewa kuhusu kaguzi mbalimbali zinazofanywa na CAG;

d) Kujenga na kuongeza uelewa kuhusu uwazi na uwajibikaji katika kusimamia matumizi ya fedha za umma;

e) Kujenga na kuongeza uelewa kuhusu wajibu wa Mkaguzi Mkuu wa Ndani katika kuimarisha uwajibikaji, usimamizi wa fedha na utawala bora; na

f) Kujenga na kuongeza uelewa kuhusu shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Taasisi na Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Spika, mafunzo haya yameendelea kuwa nguzo kubwa katika kufanikisha majukumu ya Kamati ya PAC. Waheshimiwa Wajumbe waliongeza weledi katika shughuli za uchambuzi wa Taarifa za CAG hivyo kuongeza ufanisi katika kutimiza majukumu yao ya Kikanuni.

Mheshimiwa Spika, Kamati inategemea kuendelea kupata mafunzo kama hayo na mengine kwa mawanda mapana zaidi ili kuendelea kuboresha utendaji kazi wa Kamati na Bunge kwa ufanisi na weledi mkubwa.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

3.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii imefafanua kwa kina shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kwa kipindi cha Mwezi Januari 2023 hadi Februari, 2024. Shughuli hizo zinajumuisha, uchambuzi wa Taarifa za CAG kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022, ukaguzi wa miradi ya maendeleo na mafunzo na semina za kuwajengea uwezo Waheshimiwa Wajumbe. Kwa kuzingatia utekelezaji wa shughuli zote hizo, Kamati ina maoni na mapendekezo kama ifuatavyo: -

3.2 Maoni

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati yamezingatia jukumu la Bunge kuwa chombo mahsusi cha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma. Kwa mantiki hiyo, Kamati ina maoni ya ujumla yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni ya jumla kuwa Bunge linabaki kuwa na dhima kubwa ya kusimamia uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma. Na kutokana na dhima hiyo, ni maoni ya Kamati kuwa kunahitajika maboresho katika mifumo ya udhibiti katika usimamizi wa fedha za umma ikiwa ni pamoja na kuendelea kuboresha Sheria na Kanuni zinazosimamia fedha za umma ili kuongeza hatua za kiuwajibikaji.Sheria na Kanuni za usimamizi wa fedha za umma ziendelee kuboreshwa ili

kuhakikisha Maafisa Masuuli wanawajibika ipasavyo kwa hatua wanazochukua au kutochukua kwa rasilimali zilizowekwa chini ya uangalizi wao.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati ina maoni kwamba bado kuna changamoto kadhaa katika usimamizi wa mikataba kwa baadhi ya Taasisi za Serikali hali inayochangia upotevu wa fedha za umma. Eneo hili linatakiwa kuangaliwa kwa makini na kusimamiwa ipasavyo, kwani katika utekelezaji wa shughuli zake Kamati imekutana na changamoto kubwa ya matumizi ya fedha za umma kwenye usimamizi wenye dosari wa mikataba katika hatua zote za uingiaji, usimamizi na ufungaji wa mikataba.

3.3 Mapendekezo

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Kamati yametolewa kwa kuzingatia dhima ya Kaguzi za Ufanisi na Kaguzi za Kiufundi ambazo kwa kiasi kikubwa ndizo zimechambuliwa katika Taarifa hii. Kwa msingi huo, mapendekezo ya Kamati yamejielekeza katika kuhakikisha kunakuwepo na tija, uwekevu na ufanisi mtawalia katika matumizi ya fedha za umma. Naomba kuwasilisha mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

3.3.1 Kuhusu Ukaguzi wa Ufanisi Katika Usimamizi wa Uondoshaji wa Magari ya Serikali

KWA KUWA, Taarifa ya CAG imebainisha uwepo wa magari mengi ya Serikali yaliyoegeshwa kwenye Karakana na Taasisi za Umma kwa muda mrefu yakisubiri kutengenezwa au kibali cha uondoshwaji kwa yale yaliyotumika zaidi ya miaka mitano (5). Vilevile Taarifa imethibitisha ukosefu wa uwazi na uthamini usio halisia kwenye mchakato wa uondoshaji wa magari kwa kuwakopesha au kuwauzia watumishi wa umma;

NA KWA KUWA, Hali hiyo imepelekea magari hayo kuendelea kuchakaa na kutotumika kwa lengo lililokusudiwa. Aidha,hali hiyo imesababisha Serikali kukosa mapato kusudiwa kutokana na kuuzwa au kukopeshwa magari hayo kwa thamani ambayo haina uhalisia. Vilevile, kukosa uwazi wakati wa uuzaji wa magari

hayo kumesababisha wafanyakazi wachache kufaidika na magari hayo yanayoondoshwa;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

a) Serikali iandae mwongozo utakao toa ukomo wa gari la Serikali kuegeshwa. Aidha, mwongozo huo utoe maelekezo bayana ya mchakato mzima wa uondoshaji magari hayo kwa uwazi na uthamini wake ili kupata gharama halisi na baada ya hapo maamuzi yatolewe kuelekeza gari hilo kuondoshwa kwa kuuzwa au kukopeshwa mtumishi; na

b) Serikali ifanye mapitio ya Sheria zinazohusika na uthamini wa mali za Serikali ili kuondoa mgongano wa kisheria uliopo sasa wa uthamini wa magari ya Serikali kufanywa na Taasisi tofauti hali inayoleta mgongano wa kiutekelezaji.

3.3.2 Kuhusu Ukaguzi wa Ufanisi Kwenye Uendeshaji na Matengenezo ya Miradi ya Maji

KWA KUWA, Kupitia uchambuzi wa Taarifa ya CAG katika ukaguzi wa uendeshaji na matengenezo ya miradi ya maji ilibainika uwepo wa mapungufu kadhaa katika usanifu, usimamizi, na utekelezaji wa miradi ya maji Nchini. Pia, ilibainika kuwa mpango wa usambazaji wa maji Nchini bado haujaakisi ipasavyo matumizi ya vyanzo vyote vilivyopo vya maji ili kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa maji Nchini. Vilevile, ilibainika kuwepo kwa miradi mingi midogo midogo isiyo na vyanzo madhubuti na ambayo uendelevu wake sio wa kudumu.Taarifa ya ukaguzi iliendelea kubainisha uwepo wa madeni makubwa kwa Taasisi za Serikali ambazo hazilipii huduma ya maji wanayopewa na Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira Nchini.

NA KWA KUWA, Mapungufu hayo yote kwa ujumla wake yanasabaisha kutopatikana thamani halisi ya fedha za umma kwa uwekezaji mkubwa unaofanywa na Serikali katika Sekta ya Maji. Aidha, athari zilizobainika za kutolipa madeni ya maji kwa wakati kwa Taasisi za Serikali ni kukosekana kwa fedha kwa ajili ya uendeshaji wa Mamlaka husika za Maji hivyo kusababisha

Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira kuendelea kutegemea ruzuku za uendeshaji wa Mamlaka husika toka Serikali Kuu;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

a) Serikali ihuishe Mpango Kabambe (Master Plan) wa maji Nchini ambao utaainisha miradi mikuu ya usambazaji maji nchi nzima kupitia vyanzo vya uhakika kama vile Maziwa na Mabwawa ili kuwa na uhakika wa upatikanaji wa maji safi na salama kwa gharama nafuu na kwa kuzingatia thamani halisi ya fedha za umma;

b) Serikali itoe tathmini ya kila mwaka ya asilimia iliyofikiwa ya ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji (percantage distribution network) kwa kulinganisha na kilichopangwa katika mpango kabambe (master plan) ya maji; na

c) Serikali ihakikishe, Taasisi zote za Umma zinazodaiwa ankara za madeni ya maji zilipe madeni yake ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira hapa nchini zinafunga dira za malipo ya kabla (pre – paid meters) kwa Taasisi zote za Serikali na watu wote wenye matumizi makubwa ya maji.

3.3.3 Kuhusu Ukaguzi wa Ufanisi Katika Usimamizi wa Mipango na Ujenzi wa Mifumo ya TEHAMA Serikalini

KWA KUWA, Kamati imebaini uwepo wa mapungufu katika usimamizi na udhibiti wa mipango na ujenzi wa mifumo ya TEHEMA Serikalini;

NA KWA KUWA, Hali hiyo imepelekea kuwepo kwa mifumo mingi ndani ya Serikali ambayo haina tija kwa Serikali ikiwa imejengwa kwa gharama kubwa pasipokuwa na manufaa yaliyotarajiwa kwa Serikali. Aidha, kutokana na udhaifu huo katika udhibiti wa ujenzi wa mifumo, Serikali imejikuta ikiwa na mifumo mingi kwa Taasisi na Sekta tofauti za Umma ambayo haisomani na hivyo

kupunguza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi pamoja na Taasisi nyingine za Serikali;

KWA HIYO BASI, Bunge liaanzimia kwamba;

a) Serikali ikamilishe mapema Sera ya TEHAMA Serikalini pamoja na kufanya tathmini ya mifumo yote ndani ya Serikali na kubaini mifumo yote ambayo haina tija kwa Serikali na kuchukua hatua madhubuti za kuiondoa; na

b) Serikali ihakikishe kunakuwa na muunganiko wa mifumo ya Serikali kati ya Taasisi moja na Taasisi nyingine au Sekta moja na nyingine katika namna itakayorahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi bila vikwazo vyovyote vya kimfumo.

3.3.4 Kuhusu Ukaguzi wa Ufanisi wa Usimamizi wa Urasimishaji wa Makazi Yasiyopangwa

KWA KUWA, Kamati imebaini uwepo wa mapungufu katika usimamizi na utekelezaji wa mpango wa urasimishaji wa makazi yasiyopangwa;

NA KWA KUWA, Mapungufu yaliyobainishwa katika taarifa ya ukaguzi iliyopitiwa na kujadiliwa na Kamati yamesababisha kushindwa kupima na kurasimisha sehemu kubwa ya vipande vya ardhi kama ilivyopangwa hivyo kuikosesha Serikali mapato stahiki;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba;
Serikali ifanye tathmini ya kina ya sababu zilizochangia mpango wa urasimishaji makazi yasiyopangwa kushindwa kufikia malengo yaliyokusudiwa. Vilevile, Serikali iandae mpango madhubuti na unaotekelezeka wa kurasimisha makazi yote yasiyopangwa Nchini ili kuboresha utoaji wa huduma na kupata fedha za kuwahudumia wananchi.

3.3.5 Kuhusu Ukaguzi wa Ufanisi Juu ya Udhibiti wa Vituo vya Kutolea Huduma ya Afya vya Binafsi na Hiari

KWA KUWA, Uchambuzi wa Kamati katika Taarifa ya CAG Kuhusu Udhibiti wa Vituo vya Kutolea Huduma ya Afya vya Binafsi na Hiari

umebainisha uwepo wa mapungufu katika udhibiti na usimamizi madhubuti wa vituo hivi katika maeneo ya usajili, usimamizi shirikishi, ukaguzi, tathmini za huduma na udhibiti wa bei;

NA KWA KUWA, Dosari hizo zimepelekea vituo hivyo kutokutoa huduma bora za afya ambazo zinatarajiwa kutolewa na vituo vya afya binafsi na hiari ambayo imechangiwa na kuwepo kwa muingiliano wa majukumu ya bodi na mabaraza ya usimamizi wa huduma ya afya. Aidha, dosari hizo zimesababisha kuwepo kwa gharama tofauti tofauti za huduma za afya bila kuwepo kwa bei elekezi katika huduma husika. Mapungufu haya yote yanachangia kutopatikana thamani halisi ya fedha za umma zinazoelekezwa kwenye vyombo vya udhibiti wa huduma za afya hapa Nchini;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba;
Serikali ihakikishe kunakuwepo mfumo thabiti utakaounganisha Bodi zote zinazosimamia vituo vya afya binafsi na hiari ili kuimarisha udhibiti na usimamizi wa vituo hivyo vya afya vya binafsi na hiari.Kwa kufanya hivyo,thamani halisi ya fedha za umma inayotumika kwenye usimamizi na udhibiti wa vituo itakuwa imepatikana.

3.3.6 Kuhusu Ukaguzi wa Kiufundi Juu ya Ujenzi wa Shule Chini ya Mradi wa "SEQUIP"

KWA KUWA, Kamati imebaini mapungufu kadhaa ikiwemo kukosekana kwa usimamizi uliojitosheleza wa ujenzi wa shule za Sekondari chini ya mradi wa SEQUIP kwa kutumia mafundi 'Local Fundi';

NA KWA KUWA, Athari zinazotokana na dosari zilizobainishwa hapo juu ni pamoja na kutokuwepo kwa ubora kwa baadhi ya miundombinu ya shule zilizojengwa. Vilevile,dosari hizo hupelekea kukosa uhakika wa uendelevu (sustainability) wa majengo yaliyojengwa kwa kipindi kilichotarajiwa/kilichopangwa;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba;

a) Serikali ichukue hatua za makusudi kwa kuhakikisha kuwa miradi ya ujenzi wa shule inasimamiwa na wataalamu waliokidhi vigezo, ikiwa ni pamoja na kuandaa na kutumia miongozo madhubuti yenye kutoa miongozo sahihi juu ya usimamizi, ubora, upatikanaji wa mafundi na ukamilishaji kwa wakati miradi hii; na

b) Serikali ifanye tathmini ya kina juu ya faida na hasara za mfumo huu unaotumika kujenga shule za sekondari Nchini kwa sasa.

3.3.7 Kuhusu Ukaguzi wa Kiufundi Katika Udhibiti wa Ubora Wakati wa Utekelezaji wa Shughuli za Ujenzi wa Miradi ya Barabara ili Kuzuia Uchakavu wa Mapema

KWA KUWA, Kamati imebaini uwepo wa mapungufu katika usimamizi wa ubora katika ujenzi wa baadhi ya miradi ya barabara zilizoko chini ya Wakala wa Barabara Tanzania;

NA KWA KUWA, Hali hiyo imesababisha kujengwa kwa baadhi ya barabara zenye changamoto za ubora hivyo kupelekea baadhi ya barabara hizo kuwa na uchakavu wa mapema kabla ya wakati uliotarajiwa wakati wa usanifu wa barabara hizo. Aidha, Serikali imekuwa ikipoteza fedha nyingi kutokana na kurudiwa kwa kazi za ujenzi wa barabara au kufanya matengenezo makubwa ya barabara hizohizo zilizojengwa kwa gharama kubwa za fedha za walipa kodi;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba;
Serikali ifanye mapitio ya utendaji wa wasimamizi wa miradi na washauri elekezi ambao wamesimamia miradi yenye mapungufu ya ubora pamoja na ile yenye uchakavu wa mapema ili kubaini sababu za kuwa na usimamizi dhaifu pamoja na kuchukua hatua stahiki zitakazoimarisha usimamizi wa ujenzi wa barabara hizo. Aidha, Serikali inatakiwa kuhuisha miongozo ya usanifu wa barabara,ujenzi wake na usimamizi wake ili kuhakikisha miongozo hiyo inakidhi vigezo na mahitaji ya sasa ya ubora.

3.3.8 Kuhusu Ukaguzi wa Kiufundi Katika Udhibiti wa Gharama za Ujenzi wa Majengo ya Serikali

KWA KUWA, Kamati imebaini uwepo wa ongezeko la gharama za miradi ya ujenzi wa majengo ya Serikali. Sababu za ongezeko hilo ni malipo ya riba zitokanazo na kucheleweshwa malipo kwa wakandarasi sambamba na malipo ya fidia kwa wakandarasi zitokanazo na kuchelewa kukamilika kwa miradi kwa mujibu wa mikataba husika. Pia, dosari katika upangaji na usanifu wa miradi imepelekea mabadiliko ya kazi na kuchangia katika ongezeko la gharama za miradi;

NA KWA KUWA, mapungufu yote hayo yaliyobainishwa na CAG yanasababisha matumizi mabaya ya fedha za umma;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba;

a) Serikali itoe mwongozo wa kudhibiti ongezeko la gharama za miradi pamoja na hilo kuwe na mfumo wa kuonesha muda wa malipo kwa mradi husika na taasisi zinazo takiwa kushugulikia malipo hayo ili kuondoa changamoto ya kuchelewa kukamilika miradi;

b) Serikali ihakikishe kunakuwepo mfumo utakao bainisha muda wa mradi, viashiria vya kuchelewa kwa mradi ili kuwe na tathmini ya taasisi nunuzi pamoja na Wizara ya Fedha kwa kuchelewesha mradi husika;

c) Serikali ihakikishe inaweka mfumo wa kuhakikisha hatua zote za usanifu wa miradi zinafuatwa na taasisi nunuzi kabla ya kusainiwa kwa mikataba; na

d) Kwa upande wa ujenzi wa mradi wa 711, Kawe, CAG afanye mapitio ya kina kuhusu mikataba na nyaraka zote zinazohusu upembuzi yakinifu (feasability study) wa mradi huo na kulitaarifu Bunge ipasavyo.

3.3.9 Kuhusu Ukaguzi wa Kiufundi Katika Ujenzi na Ukarabati wa Meli

KWA KUWA, Kamati imebaini kuwa, Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) iliwahi kuwa katika hali mbaya ya kifedha na kiutendaji kwa kukosa wataalamu wenye ujuzi na fedha za kutekeleza miradi ya ukarabati na ujenzi wa Meli katika Maziwa na Bahari. Hali hii ilisababisha shughuli za ukarabati na ujenzi wa Meli zilizofanyika hapo awali kuwa na mapungufu kadhaa;

NA KWA KUWA,Mapungufu hayo yalisababisha ujenzi na ukarabati wa Meli kutokamilika kwa wakati hivyo kuathiri thamani halisi ya matumizi ya fedha za umma;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba;
Serikali iandae mipango ya muda mfupi na ya muda mrefu ya kuiimarisha na kuijengea uwezo wa kifedha na wataalamu Kampuni ya Huduma za Meli Nchini ili iweze kutekeleza na kusimamia kiufanisi uanzishwaji, upangaji, usanifu, utekelezaji na usimamizi wa miradi ya ujenzi na ukarabati wa Meli Nchini. Maboresho haya yatasaidia kuimarisha sekta ya uchukuzi na uchumi wa nchi yetu kutokana na nchi yetu kuwa na mahitaji makubwa ya ukarabati na ujenzi wa Meli hasa za kubeba abiria, mizigo na mafuta.

3.3.10 Kuhusu Ukaguzi wa Ufanisi Katika Utekelezaji wa Maendeleo Endelevu Nchini

KWA KUWA, Kamati imebaini mapungufu katika ukusanyaji wa rasilimali, uratibu na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu Nchini;

NA KWA KUWA,Mapungufu katika mfumo wa uratibu yamesababisha kushindwa kuleta matokeo chanya hasa kuwaleta wadau kujadili changamoto pamoja na sera hali ambayo itasababisha Nchi yetu kushindwa kufikia shabaha ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu Nchini;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba;

a) Serikali ihakikishe kuwa, Wizara ya Fedha inaibua vyanzo mbadala vya mapato ambavyo vitachangia mapato ya ndani na kupunguza utegemezi katika utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu Nchini;

b) Wizara ya Fedha ihakikishe Mipango Mikakati ya Wizara, Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Serikali za Mitaa zinahuisha mipango mikakati yao kwa wakati; na

c) Tume ya Mipango iratibu kikamilifu utekelezaji wa mfumo wa kitaifa wa uratibu wa malengo ya maendeleo endelevu. Vilevile, Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Wizara ya Fedha na Ofisi ya Rais - TAMISEMI zihakikishe upatikanaji wa Takwimu bora kwa wakati kwa ajili ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mipango iliyohuisha Malengo ya Maendeleo Endelevu.

3.3.11 Kuhusu Miradi ya Maendeleo Iliyokaguliwa na Kamati Mwezi Machi, 2023

KWA KUWA, Kamati ilibaini dosari kadhaa katika miradi ya maendeleo iliyotembelewa na kukaguliwa na Kamati Mwezi Machi, 2023. Dosari hizo ni pamoja na usanifu usiojitosheleza wa baadhi ya miradi, baadhi ya miradi kutokamilika kwa wakati, ongezeko la gharama kwa baadhi ya miradi, kuchelewa malipo kwa wakandarasi na usimamizi hafifu wa baadhi ya miradi;

NA KWA KUWA, Dosari hizo kwa ujumla wake zimesababisha kutopatikana thamani halisi ya fedha za umma iliyotumika kwenye baadhi ya miradi husika. Aidha kwa baadhi ya miradi kumekuwa na viashiria vya matumizi mabaya ya fedha za umma;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba;

a) Serikali iingie mikataba mipya ya ujenzi wa miradi pale tu inapokuwa na uhakika wa bajeti na fedha za miradi husika ili kuepuka malipo ya riba kwa kuchelewa kulipa wakandarasi kwa wakati; na

b) Tathmini ya Utendaji wa kila Mwaka ya Maafisa Masuuli wote ifanyike kwa kuongeza kigezo cha uwezo wa Afisa Masuuli katika kusimamia utekelezaji wa miradi. Iwapo kunabainika dosari za kiusimamizi katika miradi, Afisa Masuuli husika achukuliwe hatua stahiki ili kuleta uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma.

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

4.1 Shukurani

Mheshimiwa Spika, Napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako makini na thabiti. Uongozi wako umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi uliotarajiwa kwa kutoa maelekezo na miongozo kila mara ulipoombwa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa ufanisi na weledi mkubwa. Naomba majina ya Waheshimiwa Wabunge Wajumbe wa PAC majina yao yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, Naomba kuwatambua Waheshimiwa Wajumbe hao kama ifuatavyo: -

1) Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mb – **Mwenyekiti**
2) Mhe.Japheti Ngailonga Hasunga, Mb – **M/Mwenyekiti**
3) Mhe. Eng. Isack Aloyce Kamwele, Mb
4) Mhe. Joseph George Kakunda, Mb
5) Mhe. Geoffrey Idelphonce Mwambe, Mb
6) Mhe. Simon Songe Lusengekile, Mb
7) Mhe. Anton Albert Mwantona, Mb
8) Mhe. Kiswaga Boniventura Destery, Mb
9) Mhe. Juma Othman Hija, Mb
10) Mhe. Idarus Faina Ravia, Mb
11) Mhe.Jacqueline Ngonyani Msongozi Mb
12) Mhe.Janeth Maurice Masaburi, Mb
13) Mhe.Esther Nicholas Matiko, Mb

14) Mhe. Anatropia Lwehikila Theonest, Mb
15) Mhe.Condester Michael Sichalwe, Mb
16) Mhe.Nancy Hassan Nyalusi, Mb
17) Mhe. Daudi Protas Venant, Mb
18) Mhe. Issa Jumanne Mtemvu, Mb
19) Mhe. Bakar Hamad Bakar, Mb
20) Mhe. Emmanuel Lekishon Shangai, Mb

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Mwihambi,ndc kwa uongozi wake thabiti wa Sekretarieti ya Bunge ambayo imeratibu shughuli za Kamati kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho japo sio kwa umuhimu, Kamati inatambua na kuthamini ushirikiano mkubwa ilioupata kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) na kwa namna ya kipekee kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Ndugu Charles Kichere. Aidha naishukuru Wizara ya Fedha kupitia Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG), Mhasibu Mkuu wa Serikali (AcGen), Msajili wa Hazina (TR) na Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali (DGAM) na Maafisa wao wote kwa ushirikiano waliotoa katika kuratibu majibu ya hoja za ukaguzi na mahojiano ya Kamati na Maafisa Masuuli.

4.2 Hoja

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Naomba kutoa Hoja.

Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, MB
MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC)
15 Februari, 2024

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.
(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana.

Ahsante sana Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge kwa kutuletea taarifa ya Kamati ya Shughuli ambazo mmezifanya ndani ya mwaka mzima, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mwenyekiti mwingine kuja kuwasilisha hoja ya Kamati, wapo wageni ambao wameingia baada ya kuwa tumeshatangaza lile tangazo la wageni wengine.

Tunao wageni 103 wa Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana ambaye ni Waziri wa Katiba na Sheria, hawa ni Mabalozi wa Sauti ya Wapinga Rushwa *(ACVF Ambassadors)* sijui ni wepi? Ooh, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 45 wa Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo ambao ni Wajumbe wa Bodi ya Uongozi wa Shule ya Sekondari Afrika Amini kutoka Usa River - Meru, Mkoa wa Arusha, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni 48 wa Mheshimiwa Rose Busiga ambao ni Wajumbe wa Umoja wa Wanawake Tanzania kutoka Wilaya ya Mbogwe, Mkoa wa Geita, wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Mbogwe, Mheshimiwa Sakina Mohamed, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimuite sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Halima James Mdee, aje awasilishe hoja ya Kamati. *(Makofi)*

MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati inayoshughulika na Hesabu za Serikali za Mitaa, naomba kutoa taarifa ya shughuli za Kamati za mwaka 2023 ambayo inatolewa chini ya Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za mwaka 2023. Naomba taarifa yote ya Kamati iingie kama ambavyo imewasilishwa nitakachokisoma hapa ni *summary* tu ya taarifa yetu.

Mheshimiwa Spika, utangulizi. Napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai, afya njema na fursa ya kukutana leo ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, kuhusu shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2023 hadi 2024 ili iweze kujadiliwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Uchambuzi wa Matokeo ya Utekelezaji, baada ya uchambuzi wa kina wa Taarifa za Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, mnamo tarehe 2 Novemba, 2023, Kamati ilipata fursa ya kipekee ya kuwasilisha kwenye Bunge lako Tukufu, taarifa yenye jumla ya mapendekezo 13.

Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo pamoja na mapendekezo yake ilijadiliwa kwa kina na Bunge na hatimaye kupatikana kwa Maazimio ya Bunge ambayo Serikali ilielekezwa na Bunge kuyafanyia kazi. Ni matarajio yetu Serikali imeyabeba kwa uzito wake yale maazimio ambayo Bunge hili lilipitisha mwezi Novemba na imeanza kuyafanyia kazi maazimio husika.

Mheshimiwa Spika, uwasilishaji wa taarifa katika Mkutano huu wa Bunge…

SPIKA: Mwenyekiti, hebu subiri kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, mnaozungumza tafadhali tumieni sauti ya chini ili Mwenyekiti asikike kusudi muweze kuchangia hoja mkiwa mmesikia Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti endelea.

MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, uwasilishaji wa Taarifa

ya Kamati katika Mkutano huu wa Bunge utajikita zaidi kwenye eneo la *Force Account* kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, chimbuko la *Force Account*. *Force Account* ni mchakato ambapo kazi zinafanywa na Idara au Wakala wa Umma kwa kutumia wafanyakazi wake na vifaa ama kwa ushirikiano na taasisi nyingine yoyote ya umma au binafsi. Kifungu cha 64(5) cha Sheria ya Ununuzi ya Umma ya Mwaka 2011 na Kanuni ya 167 (1) ya Kanuni ya Ununuzi wa Umma, 2013 *GN* Na. 446 kama ilivyorekebishwa, inaainisha masharti yanayoweza kuhalalisha matumizi ya *Force Account*.

Mheshimiwa Spika, tunatambua kuwa Bunge lako Tukufu lilipitisha sheria mpya ya ununuzi ya umma. Taarifa yetu inafanya rejea ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011 na marekebisho yake mbalimbali kwa kuwa ndiyo sheria iliyotumika wakati wa ukaguzi wa Hesabu za Halmashauri kwa Mwaka wa Fedha Ulioishia Tarehe 30 Juni, 2022.

Mheshimiwa Spika, sababu za Kutumia Force Account. Kifungu cha 64 (5) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011 na Kanuni zake za mwaka 2013 kama zilivyorekebishwa pamoja na Mwongozo wa *PPRA* uliotolewa Tarehe 22 Mei, 2020, imeeleza mazingira yanayolazimu Taasisi Nunuzi kutumia njia ya *Force Account* katika utekelezaji wa miradi mbalimbali. Mazingira hayo ni kama yafuatavyo: -

(i) Itumike kwenye kazi ndogo, zilizotawanyika na ziko katika eneo la mbali ambalo kampuni za ujenzi zilizohitimu haziwezi kutoa zabuni kwa bei nzuri;

(ii) Kazi zinatakiwa zifanyike bila kutatiza au kukwamisha shughuli zinazoendelea;

(iii) Kunapotokea jambo la dharura ambalo linahitaji utekelezaji na uangalizi wa haraka;

(iv) Madhara yasiyoweza kuzuilika katika kukwamisha kazi hubebwa na vyombo vya ununuzi vya mamlaka ya umma *(procuring entities)* kuliko kwa mkandarasi;

(v) Taasisi nunuzi ina wafanyakazi wenye sifa zinazotambuliwa na vyombo husika vya kitaaluma ili kutekeleza na kusimamia kazi zinazohitajika;

(vi) Matengenezo au ujenzi ni sehemu ya shughuli za kawaida za taasisi nunuzi.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu ulianza kutoka mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, ili kulisaidia Bunge lako kupata uelewa mpana wa utekelezaji wa miradi kwa kutumia utaratibu wa *Force Account* na hatimaye kuweza kuishauri Serikali, kufanya maboresho pale yanapohitajika na kusahihisha pale ambapo upo upungufu, katika kipindi cha tarehe 15 na 24 Januari, 2024, Kamati ilikutana na kufanya mahojiano na Halmashauri 21. Halmashauri hizo ni zifuatazo: Halmashauri ya Nzega, Uyui, Kaliua, Tanganyika, Mpimbwe, Mpanda, Nsimbo, Mlele, Lindi, Nachingwea, Mtama, Kilwa, Newala, Nanyumbu, Mji Masasi, Mlimba, Ulanga, Malinyi, Mvomero, Morogoro, na mwisho Namtumbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi wa taarifa hizi, Serikali ilifikia uamuzi wa kutumia njia ya *Force Account* ili kupunguza gharama za ujenzi. Njia hii imetumika katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa shule, hospitali, vituo vya afya, zahanati na majengo ya ofisi za Makao Makuu ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, *CAG* alishafanya ukaguzi wa ufanisi kuhusu ufuatiliaji na usimamizi wa miradi iliyotekelezwa kwa kutumia njia ya *Force Account* katika sekta ya elimu katika kipindi cha mwaka 2016/2017 hadi 2019/2020. Ripoti hii ilitoka mwezi Machi, 2021.

Mheshimiwa Spika, katika ripoti hiyo, upungufu kadhaa ulibainika ikiwa ni pamoja na usimamizi hafifu wa miradi wa mamlaka zinazohusika, rasilimali finyu ya kuweza kusimamia miradi husika, gharama kubwa za mafundi ujenzi, kutozingatiwa kwa muda wa utekelezaji na uimara wa miradi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya mahojiano na halmashauri 21 tulizozizungumza hapo juu, upungufu ufuatao ulibainika: -

Mheshimiwa Spika, gharama za utekelezaji wa miradi zisizoakisi uhalisia. Dhamira ya Serikali ya kutumia njia ya *Force Account* ni kupunguza gharama za utekelezaji wa miradi. Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati umebaini kukosekana kwa thamani halisi ya gharama za utekelezaji wa miradi kwa kuwa taarifa nyingi zilizowasilishwa mbele ya Kamati zimeonesha kuongezeka kwa gharama za miradi katika miradi mingi tofauti na gharama zilizoainishwa na *BOQ*. Ufafanuzi umeainishwa katika jedwali Na.3 tutalifikia huko mbele na mtasikia.

Mheshimiwa Spika, aidha, kumekuwa na tatizo la kutojumuishwa kwa gharama za usimamizi na ufuatiliaji zinazotumika na Halmashauri wakati wa utekelezaji wa miradi kwa njia ya *Force Account*. Vile vile gharama za kutekeleza miradi kwa njia ya *Force Account* haitolewi kulingana na uhalisia wa mazingira ya halmashauri inayotekeleza mradi na bei halisi zinazopatikana katika maeneo hayo. Halmashauri zote nchini zimekuwa zikipewa kiasi sawa cha fedha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upungufu wa wataalamu wa kada ya Uhandisi, Ukadiriaji Ujenzi na Usanifu Majengo katika Halmashauri. Sheria ya Ununuzi wa Umma, Kanuni zake na Miongozo yake imeelekeza kuwa, utekelezaji wa miradi ya *Force Account* unahitaji uwepo wa wataalamu ili kuhakikisha miradi inasimamiwa kwa weledi na kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa. Kamati imebaini kuwepo kwa upungufu mkubwa wa wataalamu wanaohitajika katika usimamizi wa miradi kama wahandisi, wakadiriaji Ujenzi na wasanifu Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika, ripoti ya *CAG* ya Ukaguzi wa Ufanisi wa *Force Account* iliyorejewa ilionesha kwamba, hadi kufikia mwezi Mei, 2019 kulikuwa na wataalamu wenye sifa 213 tu kati ya 859 wanaohitajika sawa na 24.8% tu. Upungufu huu ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na uanzishwaji wa *TARURA* ambapo wahandisi 419, sawa na 66.2% kati ya wahandisi 632 waliokuwepo kwenye Halmashauri na Ofisi ya Rais, TAMISEMI walihamishiwa *TARURA* ombwe ambalo Serikali halijazibwa mpaka sasa. Kukosekana kwa wataalamu wanaohitajika, imelazimika kutumia watumishi wa kada ya elimu na afya kusimamia miradi ya ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa idadi ya Wahandisi, Wakadiriaji Ujenzi na Wasanifu wa Majengo waliopo katika mikoa mitano ni kama inavyoonekana katika jedwali hili. Hapa nitafanya uchambuzi wa wataalam katika halmashauri dhidi ya idadi ya miradi ya *Force Account* waliotakiwa kuisimamia.

Mheshimiwa Spika, tukianza na Halmashauri ya Wilaya ya Madaba *DC* wana Wahandisi wawili, Mkadiriaji Ujenzi mmoja, idadi ya miradi ya kusimamia ni 62. Namtumbo *DC* ina Wahandisi wawili, Mkadiriaji Ujenzi mmoja, Msanifu wa Majengo mmoja na wanatakiwa kusimamia miradi 143. Katika Mkoa mzima wa Ruvuma kwa ajili ya muda, natoa mifano michache, kuna Wahandisi 14, Wakadiriaji Ujenzi sita, Wasanifu wa Majengo watatu, wanasimamia miradi 372. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Lindi; Ruangwa *DC* Wahandisi watatu, Wakadiriaji Ujenzi mmoja. Miradi ya *Force Account* anayotakiwa kusimamia ni 140. Liwale *DC* Mhandisi mmoja, Mkadiriaji Ujenzi mmoja, miradi ya *Force Account* 91. Kilwa *DC* Wahandisi nane, Mkadiriaji Ujenzi mmoja, miradi 157. Halafu mnategemea miujiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tabora, Kaliua kuna Wahandisi wawili, Wakadiriaji Ujenzi mmoja, Wasanifu wa Majengo wawili, Miradi ya *Force Account* 141. Nzega kwa Mheshimiwa kaka yangu, yule mwingine lakini siyo huyu; Mhandisi mmoja, Wakadiriaji Ujenzi mmoja, miradi 115. Uyui Wahandisi wawili, Mkadiriaji Ujenzi mmoja,

miradi 119. Mkoa mzima wa Tabora una Wahandisi 19, Wakadiriaji Ujenzi ni watano, Wasanifu majengo watatu, wanatakiwa wasimamie miradi ya *Force Account* 812. Mnategemea kutatokea miujiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Tanganyika, Ma-*engineer* wanane, Wakadiriaji Ujenzi mmoja, miradi 169. Mpanda hali kadhalika Ma-*engineer* wanne, Mkadiriaji Ujenzi mmoja, miradi 169. Suala hili lipo kwenye Nyasa *DC,* Masasi, Mtwara, na hii ni *sampling*, halmashauri 21 zinatoa *reflection* ya halmashauri nyingine 184. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jumla kuu kwenye hizi halmashauri zote zenye mikoa mitano, Wahandisi 79, Wakadiriaji Ujenzi 24, Wasanifu wa Majengo saba, miradi ya *Force Account* 3,167.

Mheshimiwa Spika, kutofanyika kwa tathmini ya mahitaji ya miundombinu muhimu kabla ya utekelezaji wa miradi. Kabla ya utekelezaji wa mradi wowote inatakiwa kufanyika tathimini ya kina juu ya mahitaji ya miundombinu muhimu katika eneo la mradi kama miundombinu ya barabara, maji na umeme. Kwa ufupi Kamati imebaini kuwa, Taasisi na Idara za Serikali haziwasiliani, hazishirikiani na kutokuwa na mpango wa pamoja wa utekelezaji wa miradi. Hakuna *connectivity*. Nilisema *last time,* Serikali ni moja haizungumzi, kila mmoja anafanya lake, matokeo yake miradi inakwama.

Mheshimiwa Spika, ubora usiokidhi vigezo VYa miradi inayotekelezwa kwa *Force Account*. Mwongozo kuhusu usimamizi wa mali za Serikali na marekebisho yake ya mwaka 2019 uliotolewa na Wizara ya Fedha, umefafanua kuhusu muda wa matumizi wa mali za Serikali ikiwemo majengo, mashine na vifaa. Mchanganuo huo kwa mujibu wa kiambatisho Na. 3 cha Mwongozo huo ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 2.

Mheshimiwa Spika, jedwali Na. 2 linasema hivi, nyumba ya Makazi inatakiwa iishi miaka 50, shule inatakiwa iishi miaka 75, Hospitali inatakiwa iishi miaka 60, ofisi inatakiwa iishi miaka 50,

mashine miaka 15, samani miaka mitano, vifaa vya ofisi miaka mitano, na mambo mengine mengi.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi uliofanywa na *CAG* katika miradi iliyotekelezwa kwa njia ya *Force Account,* umebaini ubora hafifu wa miradi hiyo, hali ambayo inatishia kutotimiza umri ambao upo kwa mujibu wa takwa la kisheria la kuishi kwa mujibu wa mali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, ukiukwaji wa hatua za kitaalamu za ujenzi. Miradi mingi imejengwa bila ya kuzingatia hatua za kitaalamu za ujenzi kutokana na uharaka wa kukamilisha miradi husika, ili kuwahi muda wa mwisho wa utekelezaji uliowekwa. Hali inayopelekea kukiuka hatua muhimu za ujenzi na kupelekea miradi kukosa ubora.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi uliofanywa na *CAG* katika baadhi ya miradi umebaini baadhi ya majengo kuweka nyufa kabla ya kukamilika, milango na madirisha kudondoka, marumaru kupasuka na kuweka vishimo na baadhi ya kuta za madarasa kusagika. Upungufu huu unatokana na ukiukwaji wa taratibu za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, ukiukwaji wa Mwongozo wa Utekelezaji wa Miradi kwa kutumia njia ya *Force Account*. Mwongozo wa matumizi ya *Force Account* umeeleza juu ya majukumu ya kila mdau katika utekelezaji wa miradi husika. Kuna Kamati ya Ujenzi ambayo inahusika na masuala mazima ya kusimamia shughuli za ujenzi. Kuna Kamati ya Ununuzi inayohusika na masuala mazima ya ununuzi. Vilevile, kuna Kamati ya Mapokezi na Kukagua Vifaa ambayo inatakiwa kuhakikisha bidhaa zote zinazowasilishwa ni za kiwango na ubora ulioainishwa katika mkataba.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukutana na baadhi ya halmashauri zilizotekeleza miradi kwa kutumia njia ya *Force Account,* Kamati imebaini kuwa, Kamati tajwa hapo juu hazikuundwa na baadhi ya maeneo Kamati zilizoundwa hazitekelezi majukumu yake kama inavyotakiwa kutokana na kukosekana kwa wataalamu kama inavyoelekezwa katika

Mwongozo pamoja na Maafisa Masuuli kutozishirikisha katika mchakato wowote pale inapotokea Kamati husika zipo. Ukiukwaji wa taratibu na miongozo iliyowekwa kwa kiasi kikubwa umesababisha miradi mingi kutofikia viwango vinavyohitajika.

Mheshimiwa Spika, ukiukwaji wa Miongozo ya TAMISEMI. Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilipeleka kiasi cha shilingi bilioni 100.58 kwa ajili ya ujenzi wa Shule za Sekondari mpya 214 ambazo zilitarajiwa kujengwa kwenye majimbo yote nchini na shilingi bilioni 30 zilipelekwa kwa ajili ya ujenzi wa Shule za Sekondari mpya za Wasichana kwenye mikoa 10, yaani shule moja katika kila mkoa na ilianza kwenye mikoa 10, kupitia Utaratibu wa Uenezaji wa Elimu ya Sekondari Nchini *(SEQUIP)*

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa mradi huo, tarehe 2/12/2021 Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilitoa Mwongozo wa matumizi ya fedha hizo za mradi ambapo, gharama ya ujenzi wa shule za sekondari katika majimbo ilikuwa ni shilingi milioni 600 katika awamu mbili. Awamu ya kwanza ilihusisha shilingi milioni 470 ambayo ilijumuisha ujenzi wa vyumba vya madarasa nane, maabara za sayansi tatu, jengo moja la utawala, maktaba moja, chumba cha *ICT* kimoja, vyoo 20 vya wanafunzi (wavulana 10 na wasichana 10), matanki mawili ya maji (kila moja lita 10,000), nguzo ya kuweka tanki, moja; na ujenzi wa miundombinu ya kunawia mikono na miundombinu ya kuvuna maji. Aidha, awamu ya pili ya mradi ambayo bado haijaenda, inatarajiwa kutumia shilingi milioni 130 ambayo inajumuisha nyumba za walimu na vifaa vya *ICT*.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipanga kutumia jumla ya shilingi milioni 24.038 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya *SEQUIP* katika awamu ya kwanza. Hata hivyo, wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo, gharama halisi zilizotumika ni tofauti na kilichokadiriwa. Vile vile, baadhi ya miradi haijakamilika na inahitaji nyongeza ya fedha kama inavyoonekana katika jedwali Na.3.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mchanganuo wa miradi kimkoa. Mkoa wa Katavi ulitakiwa upewe shilingi bilioni 2.8 na ilipewa shilingi bilioni 2.8. Kiasi ambacho imetumia mpaka sasa ni shilingi

bilioni 3.347 ambayo sasa hivi ni tofauti peke yake ya shilingi milioni 527. Kiasi ambacho Katavi inahitaji ziada ni shilingi milioni 285. Kwa hiyo, kwa Katavi peke yake kuna nyongeza ya shilingi milioni 812 kama Mkoa.

Mheshimiwa Spika, Tabora walipewa bilioni 9.4 mpaka sasa wametumia bilioni 10.1 tofauti ya milioni 643. Nyongeza wanayoiomba ndugu zetu wa Tabora ni bilioni 1.2, ukijumlisha walichokiongeza pamoja na nyongeza ni bilioni 1.1.

Mheshimiwa Spika, Lindi walipewa bilioni 3.29 walichotumia mpaka sasa ni bilioni 3.4 walichokiongeza ambayo tofauti yake na ile waliyopewa ni milioni 187, nyongeza ambayo wanaiomba kukamilisha ni milioni 407. Jumla kwa Mkoa wa Lindi ziada ni 595, ukija Mtwara ziada ni bilioni 1.2, ukija Ruvuma ziada ni bilioni 1.3.

Mheshimiwa Spika, sasa hapa tunajiuliza wenye shida ni TAMISEMI wanaopanga mipango na *BOQ* yao? Hatuna wataalam? Wenye shida ni Mikoa na halmashauri pesa zinapelekwa wanapiga ndio maana hazitoshi? Hili ni jambo ambalo linatakiwa liangaliwe kwa umakini na uzito wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Serikali imetumia jumla ya shilingi bilioni 26.5 mpaka sasa ambayo ni fedha kutoka Serikali Kuu na mapato ya ndani kwa ajili ya kutekeleza miradi katika Mikoa mitano waliyotakiwa watekeleze kwa bilioni 24, lakini makadirio ya jumla yanaonesha kwamba, pamoja na nyongeza ile bilioni 2 katika hiyo Mikoa, wanaomba ziada bilioni 3.3 ambayo inafanya ziada ya jumla ya mikoa hii mitano kuwa bilioni 5.8.

Mheshimiwa Spika, sasa twende kwenye uchambuzi wa halmashauri kadha wa kadha, ili mjisikilize hapa. Tulisema tutawataja mpaka mnyooke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukianza Katavi, *Tanganyika DC,* walipewa 470 wakatumia 557 shule za *SEQUIP*. Tukija Nkenda walipewa 470 wakatumia 575. Tuje kwa ndugu zetu wa Lindi, *Nachingwea DC,* walipewa 470 na pale tumeambiwa huku Kusini kuna Dangote, wakatumia 718, yaani kwa mantiki ya kwamba,

470 ya Serikali, mapato ya ndani 46, kuna nyingine 11 michango ya wananchi, milioni 191 wanaomba waongezewe. Ukija *Kilwa DC,* 470 walipewa wanaomba ziada milioni 146 nguvu za wananchi zilikuwa milioni 32 wametumia ama wanahitaji kutumia mpaka mradi ukamilike milioni 648. *Ulanga DC,* walipewa 470 kukamilisha mradi, wanaomba nyongeza ya 160, mradi mzima utagharimu milioni 630.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika Mvomero walipewa 470, wameomba 241 ziada. Mradi wa 470 unatakiwa ukamilike kwa milioni 711, lakini Morogoro hiyohiyo tuna Mlimba, mradi wa 470 wameomba ziada 139, mradi wa 470 utakamilika kwa milioni 609. Halikadhalika Mtwara ukienda Newala, 470 unakamilika kwa 629. Ukienda kwa *brother* wa Nzega *DC,* hii ndio ilikuwa ni kubwa kuliko zote, mradi wa 470 Ndugu zetu wa Nzega wameugharamia na hawa walikuwa na bahati wamepata hela zote kutoka Serikali Kuu, kulikuwa kuna 470 ya *SEQUIP* halafu kulikuwa kuna 379 ambayo ilikwenda kule bila maelezo wao wakajiongeza wakaomba itumiwe ujenzi wa shule. Kwa hiyo, mradi wa 470 ndugu zetu wa Nzega wamejenga kwa milioni 849. Tunaendelea kujiuliza shida ni TAMISEMI, shida huku chini kuna upigaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ujenzi wa shule za mikoa za wasichana, mwongozo umefafanua kuwa gharama za ujenzi wa shule za sekondari za wasichana ni shilingi bilioni nne, ambapo kiasi cha shilingi bilioni 3 kimetolewa ikiwa ni awamu ya kwanza ya ujenzi kwa kila shule. Halmashauri ya Manispaa ya Lindi haikuzingatia mwongozo kwa kutumia jumla ya shilingi bilioni 3.1 katika kutekeleza mradi kwa awamu ya kwanza ya shule husika. Lakini ndugu zetu wa Lindi hawa wameiambia kamati bilioni 3.1 haijatosha wanahitaji nyongeza nyingine kwa pesa ambazo zipo Serikali Kuu bilioni 1.5 kwa hiyo, kwa mradi ambao wenzao wamejenga kwa kutumia bilioni 3 ndugu zetu wa Lindi wanataka kujenga kwa bilioni 4.6, tunajiuliza tatizo ni Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuna shida? Tatizo Halmashauri kuna upigaji? Tunataka majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halikadhalika kwenye vituo vya afya, Mkoa wa Katavi walipewa bilioni 5.5 wametumia bilioni 6.2 tofauti

ya gharama ni milioni 745 wanaomba nyongeza milioni 665. Maana yake wanataka ziada bilioni 1.4.

Mheshimiwa Spika, Tabora, walipewa bilioni 5.6 wameshindwa kuzitumia, wanataka ziada bilioni 1.62, Lindi, kwa sababu ya muda inabidi niende *faster;* Lindi bilioni 5 hawajamaliza kazi waliyotakiwa kufanya wanaomba nyongeza milioni 1.125. Mtwara bilioni 5.75 wameomba nyongeza ambayo itakadiria milioni 691.

Mheshimiwa Spika, ukija Ruvuma walipewa bilioni 8.6 wametumia bilioni 9.2 ambayo ni tofauti na pesa waliyopewa kwa milioni 593 na wao wanahitaji nyongeza milioni 718. Na kule kwa dada yangu Mheshimiwa Jenista huko Ruvuma wanaomba ziada ya bilioni 1.5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja yetu iko palepale, shida ni TAMISEMI hamjipangi? Hamjui mnachokikadiria? Ama shida tunaibiwa? Tunahitaji majibu.

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti za Mkoa Kutokufuatilia Utekelezaji wa Mradi, Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa ina jukumu la moja kwa moja kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo ya usimamizi. Hata hivyo, kamati imebaini kutokufanyika kwa jukumu hilo kutokana na wataalamu hao kutoka mikoani waliofika mbele ya kamati kutokufahamu shughuli za utekelezaji wa miradi inayoendelea katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi ndugu zetu wa Ofisi ya *RAS,* na hii tunalisema ili muelewe, inawezekana wengi wanaajiriwa kwa kazi ambazo hawajui wanatakiwa wafanye nini, hawana majibu. Kwa hiyo, ni jukumu lenu kwenda kufanya tathmini ya kina watu waweze kupewa kazi wanazoelewa wanatakiwa wakafanye nini.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Mapendekezo, mapendekezo ya kamati yanatokana na changamoto na mapungufu yaliyoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mapendekezo hayo yanalenga kuondoa mapungufu yaliyobainika katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya

maendeleo kwa njia ya *force account*. Mapendekezo ya kamati ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na uwepo wa ukomo wa gharama za miradi inayotekelezwa kwa kutumia *Force Account;* tunaomba Bunge liazimie kwamba:-

(i) Serikali ifanye utafiti wa kina juu ya ukubwa wa miradi pamoja na gharama za miradi zinazopaswa kutumika katika utekelezaji wa miradi kwa kutumia njia ya *Force Account*; na

(ii) Serikali ihakikishe Kanuni ya ununuzi wa umma inayotokana na Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 10 ya Mwaka 2023 inajumuisha ukomo wa gharama ya miradi inayopaswa kutekelezwa kwa kutumia *Force Account*. Hamuwezi kutumia bilioni sita mnataka fundi mchundo atengeneze ghorofa.

Mheshimiwa Spika, gharama za utekelezaji wa miradi zisizoakisi uhalisia, kwa miradi ambayo inatekelezwa kwa fedha kutoka Serikali Kuu; Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Serikali ifanye tathmini ya kina juu ya gharama halisi zilizotumika katika kutekeleza miradi kwa kutumia njia ya *force account* na kubainisha iwapo lengo lililokusudiwa kupunguza gharama limefikiwa;

(b) Serikali ihakikishe gharama za usimamizi wa ufuatiliaji wa miradi zinajumuishwa kama sehemu ya fedha zinazopelekwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya *force account;* na

(c) Serikali ipeleke fedha za utekelezaji wa miradi ya *Force Account* kulingana na gharama halisi za maeneo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upungufu wa wataalam wa kada mbalimbali, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe inaongeza idadi ya wataalam katika Halmashauri zote nchini

zenye upungufu wa wataalam hao, ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa miradi na kuacha kuwatumia walimu, madaktari, kama wasimamizi wa miradi ili waweze kutekeleza majukumu yao ya msingi na kisha mtoe taarifa ya utekelezaji katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, kufanyika tathmini ya mahitaji ya miundombinu muhimu kabla ya utekelezaji wa miradi na ubora wa miradi; Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali ihakikishe kila Mkurugenzi anafuata taratibu za ujenzi kwa kutekeleza mambo yote muhimu kama upimaji udongo, tathmini ya mazingira, ununuzi wa bidhaa zenye ubora, kutumia mafundi wenye taaluma ya mradi husika na kuwachukulia hatua stahiki wote watakaokiuka taratibu hizo;

(ii) Serikali ifanye tathmini ya miradi iliyotekelezwa kwa kutumia *Force Account* na kukokotoa gharama za uchakavu wa miradi hiyo kama ilivyoelezwa kwenye mwongozo wa usimamizi wa mali za Serikali pamoja na kuchukua hatua kwa watendaji wote watakaobainika kutekeleza miradi chini ya kiwango;

(iii) Kuomba Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, yani jicho letu sisi Bunge maana Serikali mnaweza mkazembea msifanye, kufanya ukaguzi wa kina juu ya ubora wa miradi iliyotekelezwa kwa kutumia njia ya *Force Account* kwa kuzingatia hali ya miradi *(Economic Life)* kama ilivyoainishwa katika mwongozo wa usimamizi wa mali za Serikali;

(iv) Kuiomba Ofisi ya Ukaguzi kufanya ukaguzi wa kina kwa miradi yote yenye changamoto iliyotekelezwa kwa kutumia njia ya *Force Account* katika Halmashauri ya Nsimbo, Halmashauri ya Newala na Halmashauri ya namtumbao. Huku tumekutana na madudu ndio maana tunataka mkaguzi aende akatupe jicho la ziada.

Mheshimiwa Spika, kutozingatiwa kwa hatua za kitaalam za ujenzi, Bunge linaazimia kwamba, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na

Serikali za Mitaa, kwa kushirikiana na sekretarieti za Mikoa ihakikishe miradi yote inayotekelezwa katika Halmashauri inazingatia hatua zote za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, ukiukwaji wa Mwongozo wa Utekelezaji wa Miradi kwa Kutumia *Force Account,* Bunge liazimie kwamba, Serikali ichukue hatua stahiki kwa watendaji wote waliokiuka mwongozo wa utekelezaji wa miradi kwa njia ya *Force Account* halikadhalika Kuhusiana na Ukiukwaji wa Miongozo ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Bunge lihakikishe linasimamia na kuchukua hatua dhidi ya watendaji watakaobainika kukiuka miongozo iliyotolewa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, TAMISEMI ilitoa muongozo, tunataka TAMISEMI ikafanye yenyewe uhakiki kwa wale wote ambao wamekiuka mwongozo wote kama ulivyo na Sheria ya Manunuzi tuliyoitaja hapa wachukuliwe hatua.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Sekretarieti za Mikoa, Bunge linaazimia Serikali ifanye tathmini ya utendaji kazi wa Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa katika kusimamia miradi yote ya maendeleo katika mikoa yao na kuchukua hatua stahiki kwa wale ambao watabainika kutotekeleza wajibu wao kikamilifu hasa katika eneo la kusimamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti za Mikoa zifanye ukaguzi wa miradi inayotekelezwa katika halmashauri zao na kuwasilisha taarifa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Miradi Kutokamilika kwa Wakati, TAMISEMI kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa zisimamie kikamilifu kuhakikisha miradi yote iliyotekelezwa kwa kutumia *Force Account* ambayo haijakamilika inakamilika mapema.

Mheshimiwa Spika, mwisho kwa kuhitimisha, tunakushukuru wewe binafsi, tunashukuru Ofisi ya Katibu wa Bunge, tunawshukuru Wajumbe wa Kamati na Makatibu wetu wote kwa

kazi nzuri wanayoifanya. Tunashukuru Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kazi nzuri inayofanya.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kutoa hoja Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mita ana likubali maoni na mapendekezo yote ya kamati yetu kama yalivyo. Ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI KWA MWAKA 2023 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

(Inatolewa chini ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023)

SEHEMU YA KWANZA

1.0 MAELEZO YA JUMLA

1.1 Utangulizi

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai, afya njema na fursa ya kukutana leo ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), kuhusu shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha kuanzia Februari 2023 hadi Februari 2024 ili iweze kujadiliwa.

1.2 Majukumu ya Kamati

Mheshmiwa Spika, Katika kipindi cha mwaka mzima, utekelezaji wa majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa ulizingatia matakwa ya Kifungu cha 14 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023. Kwa mujibu wa Kifungu hicho, majukumu ya Kamati hii ni yafuatayo: -

a) Kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za Serikali za Mitaa yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;
b) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati ili kuondoa matatizo hayo; na
c) Kutoa mapendekezo na ushauri kwa Serikali za Mitaa kuhusu matumizi mazuri ya fedha ili kuhakikisha kwamba, tatizo la matumizi mabaya ya fedha za Umma linapungua.

Mheshimiwa Spika, Msingi wa majukumu hayo unatokana na Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kama ilivyobainishwa katika Kifungu cha 15 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

1.3 Muundo wa Taarifa

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 imeweka sharti la muundo wa Taarifa ya Kamati inayowasilishwa Bungeni. Kwa muktadha wa Kanuni hii, Sehemu ya kwanza ya Taarifa ni maelezo ya jumla kuhusu majukumu ya Kamati, rejea zilizotumika na njia au mbinu zilizotumika wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

Sehemu ya Pili inafafanua kwa kina kuhusu uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022 kuhusu utekelezaji wa miradi kwa kutumia njia ya force account. Mantiki ya sehemu hii ni kubainisha maeneo yenye matatizo makubwa ya matumizi mabaya ya fedha za Umma. Uchambuzi wa eneo hili ndio msingi wa Sehemu ya Tatu yenye maoni na mapendekezo ya Kamati.

1.4 Rejea zilizotumika

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma wakati wa utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ilifanya rejea ya Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali ifuatayo: -

a) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977;
b) Sheria ya Ukaguzi wa Umma (Sura ya 418) na kanuni zake za Mwaka 2009;
c) Sheria ya Fedha za Halmashauri (Sura ya 290) na Mwongozo wa Matumizi ya fedha katika Serikali za Mitaa (*the Local Government Financial Memoranda*);
d) Sheria ya Ununuzi wa Umma (Sura ya 410) na kanuni zake, (kama zilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2016);
e) Sheria ya Bajeti (Sura ya 439) na kanuni zake, 2015;
f) Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge, Sura 296;
g) Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023; na
h) Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma, 2009.

1.5 Njia zilizotumika katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu ya Kamati hufanyika kwa kutumia njia mbalimbali zifuatazo: -

a) Kupokea, kuchambua na kujadili maelezo mafupi "*briefs*" za CAG kuhusu hoja za ukaguzi za Halmashauri husika;
b) Mahojiano na Maafisa Masuuli/ Wakurugenzi wa Halmashauri kuhusu hoja za ukaguzi;
c) Uchambuzi wa kina wa taarifa za ukaguzi za Halmashauri mahususi pamoja na majibu ya Wakurugenzi wa Halmashauri husika;
d) Ziara za ukaguzi wa ufanisi katika miradi ya maendeleo; na
e) Semina kuhusu majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa kina wa hoja zilizofanyiwa kazi na Kamati umefafanuliwa katika sehemu ya pili ya taarifa hii.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI

2.1 Maelezo ya Jumla Kuhusu Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Februari, 2023 hadi Februari, 2024, Kamati ilitekeleza majukumu yake yaliyoainishwa katika Kifungu cha 14 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 kwa kuangalia iwapo kuna matumizi

sahihi ya fedha za Umma katika eneo la Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoainishwa katika Kifungu cha 15 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023, Kamati ilitumia Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kubainisha maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma na kutoa ushauri stahiki.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa kina wa Taarifa hizo uliiwezesha Kamati kushughulikia kwa kina matatizo ya matumizi mabaya ya fedha za umma ili kuimarisha ustawi wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha wa ufuatiliaji wa taarifa hii, maeneo yaliyoshughulikiwa na Kamati katika kipindi kinachotolewa Taarifa ni kama ifuatavyo: -

2.2 Uchambuzi wa Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2022.

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Mwezi Februari, 2023 hadi Februari, 2024, Kamati ilipitia na kuchambua Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2022.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alikagua jumla ya **Halmashauri 184**. Kati ya Hizo, Halmashauri 170 sawa na 92.39% zilipata Hati zinazoridhisha za ukaguzi, Halmashauri 13 sawa na 7.06% zilipata Hati zenye Shaka za ukaguzi, Halmashauri 1 sawa na 0.54% ilipata Hati Mbaya ya ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, katika kushughulikia Taarifa iliyowasilishwa na CAG, Kamati ilifanikiwa kuchambua na kujadili Taarifa za Hesabu zilizokaguliwa na kufanya mahojiano na Wakurugenzi wa jumla ya

Halmashauri **95** ambazo ni sawa na **Asilimia 51.6** ya Halmashauri zote 184 zilizokaguliwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi wa kina wa Taarifa za hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2021/2022, mnamo tarehe 02 Novemba, 2023, Kamati ilipata fursa ya kipekee ya kuwasilisha katika Bunge lako Tukufu Taarifa yenye jumla ya mapendekezo 13. Taarifa hiyo pamoja na mapendekezo yake ilijadiliwa kwa kina na Bunge na hatimaye kupatikana kwa maazimio ya Bunge ambayo, Serikali ilielekezwa na Bunge kuyafanyia kazi. Ni matarajio yetu Serikali imeyabeba kwa uzito wake na imeanza kuyafanyia kazi maazimio husika.

Mheshimiwa Spika, Uwasilishaji wa Taarifa ya Kamati katika Mkutano huu wa Bunge utajikita zaidi kwenye eneo la Force Account. Uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa miradi kwa kutumia njia ya force account ni kama ifuatavyo: -

(a) Chimbuko la Force Account (FA)

Mheshimiwa Spika, *Force Account* (FA) ni mchakato ambapo kazi zinafanywa na idara au wakala wa umma kwa kutumia wafanyakazi wake na vifaa au kwa ushirikiano na taasisi nyingine yoyote ya umma au ya kibinafsi.
Kifungu cha 64(5) cha Sheria ya Ununuzi ya Umma ya Mwaka 2011 na Kanuni ya 167 (1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2013 GN No. 446 kama ilivyorekebishwa inaainisha masharti yanayoweza kuhalalisha matumizi ya *force account* (FA).

Mheshimiwa Spika, tunatambua kuwa, Bunge lako limepitisha Sheria mpya ya Ununuzi ya Umma. Taarifa yetu inafanya Rejea ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011 na marekebisho yake mbalimbali kwa kuwa ndiyo Sheria iliyotumika wakati wa ukaguzi wa Hesabu za Halmashauri kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022.

Mheshimiwa Spika, Utafiti uliofanywa na National Construction Council (NCC) kuhusu matumizi ya *Force Account* katika baadhi ya miradi ya ujenzi katika sekta ya Elimu, Afya na baadhi ya

majengo ya Serikali yaliyojengwa kwa kutumia *Force Account*, ulibaini kuwa FA ni mbinu mwafaka ya utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo kama ikisimamiwa vyema na kufuata taratibu zote za utumiaji wa *force account*.

Mheshimiwa Spika, Utafiti huo uliofanywa na NCC kwa ushirikiano na Bodi ya Usajili ya wabunifu majengo (Architects and Quantity Surveyors Board -AQRB), Bodi ya Usajili wa Makandarasi (Contractors Registration Board –CRB) na Mamlaka ya Usimamizi wa Ununuzi wa Umma (Public Procurement Regulatory Authority - PPRA) umeendelea kubainisha kwamba miradi 24 kati ya miradi 175 ambayo walishughulikia ilikidhi matakwa ya ununuzi na usimamizi wa mikataba. Miradi mingi ya Taasisi nunuzi (Procuring Entities – PEs) iliyotekelezwa bila mipango sahihi ya ujenzi na usimamizi wa mikataba imetokana na ukosefu wa makadirio ya wahandisi (upangaji wa gharama), kujua kiwango cha vifaa vinavyohitajika, programu za kazi, vipimo, ukaguzi/usimamizi na mipango ya kukubalika kwa kazi iliyotekelezwa, kukosa nyaraka sahihi za miradi na baadhi ya malipo ya miradi kutozingatia vipimo na hati za malipo.

(b) Sababu za Kutumia Force Account

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 64 (5) cha Sheria ya Ununuzi wa umma ya mwaka 2011 na kanuni zake za mwaka 2013 kama zilivyorekebishwa imeeleza mazingira yanayozilazimu Taasisi nunuzi kutumia njia ya Force Account katika utekelezaji wa miradi.

Tarehe 22 Mei, 2020, Mamlaka ya usimamizi wa Ununuzi wa Umma (PPRA) ilitoa Mwongozo kwa Taasisi zote nunuzi zinazotekeleza miradi kwa njia ya *Force Account*. Mwongozo wa utekelezaji wa miradi kwa njia ya *Force Account* umewekwa ili kuziwezesha Taasisi nunuzi kufanya ununuzi wa bidhaa, kazi za ujenzi na huduma, kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Ununuzi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, PPRA imetoa mwongozo wa taratibu za ununuzi zinazotakiwa kufuatwa na Taasisi nufaika zote zinazotekeleza miradi ya maendeleo kwa ustawi wa Taifa. Masharti ya matumizi ya Force Account kwa Taasisi nunuzi

yametolewa chini ya Kifungu cha 64(5) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, 2011 na kanuni zake za mwaka 2013 kama zilivyorekebishwa.

Masharti ya jumla (General Principles) kwa matumizi ya Force Account yaliyofafanuliwa katika Mwongozo huo ni kama yafuatayo: -

i. Itumike kwenye kazi ndogo, zilizotawanyika na ziko katika eneo la mbali ambalo kampuni za ujenzi zilizohitimu haziwezi kutoa zabuni kwa bei nzuri;
ii. Kazi zinatakiwa zifanyike bila kutatiza au kukwamisha shughuli zinazoendelea;
iii. Kunapotokea jambo la dharura ambalo linahitaji utekelezaji na uangalizi wa haraka;
iv. Madhara yasiyoweza kuzuilika katika kukwamisha kazi hubebwa na Vyombo vya Ununuzi vya mamlaka ya umma (Procuring Entities – PEs) kuliko kwa mkandarasi;
v. Taasisi nunuzi ina wafanyakazi wenye sifa zinazotambuliwa na vyombo husika vya kitaaluma ili kutekeleza na kusimamia kazi zinazohitajika; na
vi. Matengenezo au ujenzi ni sehemu ya shughuli za kawaida za Taasisi nunuzi.

(c) Masuala ya kuzingatia katika kutumia Force Account

Mheshimiwa Spika, utumiaji wa Force Account umewekewa taratibu mbalimbali zinazotakiwa kuzingatiwa. Mwongozo uliotolewa na OR – TAMISEMI umefafanua maeneo muhimu ambayo ni pamoja na uteuzi wa Meneja wa mradi, uteuzi wa timu ya utekelezaji wa mradi, namna ya kubaini mawanda ya kazi, uandaaji wa bajeti na mpango wa mwaka wa ununuzi, ununuzi wa vifaa vya ujenzi, ununuzi wa vibarua wenye utaalamu wa kati (*semi-skilled*) na vibarua wasio na utaalamu (*un-skilled*), utunzaji wa kumbukumbu, namna ya kufanya tathmini na ufuatiliaji wa mradi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, masuala ya kuzingatia katika kutumia Force Account kama njia ya utekelezaji wa miradi ni kama ifuatavyo: -

i. Kuwepo na mpango kwenye ununuzi wa vifaa vitakavyotumika, kuwepo na kikosi kazi na kiongozi wa hicho kikosi kazi cha kutekeleza mradi husika pamoja na kuzingatia gharama na ubora kwenye utekelezaji na ufuatiliaji;
ii. Kushirikiana na taasisi nyingine ambazo zina wafanyakazi na vifaa vinavyohitajika, Taasisi hiyo iwe ya Serikali au binafsi ila iwe inajulikana na bodi ya wataalamu au Mamlaka husika, pamoja na kuainisha sifa zinazotakiwa ziainishwe kabla mradi kuanza;
iii. Kanuni ya 164 (2) (b) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2013 inataka barua ya mwaliko wa nukuu na viambatisho vyovyote iwe na maelezo kamili ya bidhaa, kazi au huduma zitakazonunuliwa, ikijumuisha sifa za kiufundi au ubora unaohitajika, vipimo, miundo, mipango na michoro inavyofaa; na
iv. Kifungu cha 24.2 cha Mwongozo wa kufanya kazi chini ya *force account* cha 2020, kinatoa ufafanuzi kwamba, vifaa vya ujenzi vitakavyonunuliwa vitaendana na ratiba ya mahitaji pamoja na maelezo yaliyotajwa na yaliyoidhinishwa na Meneja wa Mradi.

Mheshimiwa Spika, Ili kulisaidia Bunge kupata uelewa mpana wa utekelezaji wa miradi kwa kutumia utaratibu wa force account na hatimaye kuweza kuishauri Serikali kufanya maboresho pale yanapohitajika na kusahihisa penye mapungufu, katika kipindi cha tarehe 15 hadi 24 Januari, 2024, Kamati ilikutana na kufanya mahojiano na Halmashauri 21. Halmashauri hizo ni: -

a) Halmashauri ya Mji Nzega;
b) Halmashauri ya Wilaya ya Uyui;
c) Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua;
d) Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika (Mpanda);
e) Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe;
f) Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda;
g) Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo;
h) Halmashauri ya Wilaya ya Mlele;
i) Halmashauri ya Manispaa ya Lindi;
j) Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea;
k) Halmashauri ya Wilaya ya Mtama;
l) Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa;

m) Halmashauri ya Wilaya ya Newala;
n) Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu;
o) Halmashauri ya Mji Masasi;
p) Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba (Kilombero);
q) Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga;
r) Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi;
s) Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero;
t) Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro; na
u) Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifikia uamuzi wa kutupia jicho katika eneo hili ikizingatiwa kwamba, utaratibu huu ulianza kutumika tangu mwaka wa fedha 2016/17.

2.3 Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa miradi kwa kutumia *force Account.*

Mheshimiwa Spika, kabla ya utaratibu wa force account, Halmashauri zilikuwa zikiwatumia wakandarasi katika utekelezaji wa miradi. Ili kupunguza gharama za ujenzi, Serikali ilifikia uamuzi wa kutumia njia ya force account. Njia hii imetumika kwa kiwango kikubwa katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa shule, hospitali, vituo vya Afya, Zahanati na majengo mengine ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Taarifa hii ambayo uchambuzi wa Kamati umefanyika kwa Halmashauri tajwa hapo juu ambazo CAG alifanya uhakiki na hatimaye kuziwasilisha mbele ya Kamati yako ya Bunge na kufanya mahojiano, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alifanya ukaguzi wa ufanisi kuhusu ufuatiliaji na usimamizi wa miradi iliyotekelezwa kwa kutumia njia ya force account katika sekta ya elimu kwa kipindi cha miaka minne 2016/2017 hadi 2019/2020 (Performance Audit Report on Monitoring and Supervision of Projects implemented through Force Account Method in Education Sector). Ripoti hii ilitoka mwezi Machi, 2021.
Katika Ripoti hiyo, mapungufu kadhaa yalibainika ikiwa ni pamoja na usimamizi hafifu wa miradi wa Mamlaka zinazohusika, rasilimali finyu ya kuweza kusimamia miradi husika, gharama kubwa za mafundi ujenzi, kutozingatiwa kwa muda wa utekelezaji wa miradi na uimara wa miradi.

Mheshimiwa Spika, Kamati imechambua Taarifa ya baadhi ya miradi iliyotekelezwa kwa kutumia utaratibu huo katika baadhi ya Halmashauri. Uchambuzi huo ni kama ifuatavyo:-

a) Matokeo ya Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, Wakati wa majadiliano na Maafisa Masuuli (Wakurugenzi wa Halmashauri) waliofika mbele ya Kamati, Kamati ilibaini yafuatayo;

i. Gharama za utekelezaji wa Miradi Zisizoakisi uhalisia

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali kutumia njia ya Force account, ni kupunguza gharama za utekelezaji wa miradi. Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati umebaini kukosekana kwa thamani halisi ya gharama za utekelezaji wa miradi kwakuwa, taarifa nyingi zilizowasilishwa mbele ya Kamati zimeonesha kuongezeka kwa gharama za miradi katika miradi mingi tofauti na gharama zilizoainishwa katika orodha ya gharama ya vifaa vya ujenzi (B.O.Q). Hali hii inaondoa dhana ya kupunguza gharama za miradi kama ilivyotarajiwa.

Mapungufu mengine yaliyobainika katika eneo la gharama ni kutojumuishwa kwa gharama za usimamizi na ufuatiliaji zinazotumika na Halmashauri wakati wa utekelezaji wa miradi kwa njia ya force account. Kimsingi fedha zinazotumiwa na Halmashauri kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji ni sehemu ya gharama za mradi hivyo zinatakiwa kujumuishwa katika gharama za utekelezaji wa mradi ili kupata thamani halisi ya gharama za mradi husika.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi uliofanywa na Kamati katika eneo la gharama umebaini kuwa, gharama za kutekeleza miradi kwa njia ya force account haitolewi kulingana na uhalisia wa mazingira ya Halmashauri inayotekeleza mradi na bei halisi zinazopatikana katika maeneo hayo kwa kuwa, Halmashauri zote nchini zinapata kiasi sawa cha fedha hali ambayo haiakisi uhalisia.

Kamati inafahamu kuwa, katika kipindi cha hivi karibuni, OR – TAMISEMI imefanya mapitio (review) ya gharama za miradi kulingana na Kanda za Halmashauri ili kuondoa changamoto

zilizojitokeza katika maeneo mbalimbali ambapo, Halmashauri nyingi zimekuwa na ongezeko kubwa la gharama za miradi. Hata hivyo, bado Kamati ina mashaka iwapo mapitio yaliyofanyika yamezingatia tafiti za kina ili kubaini iwapo changamoto zilizopo zitaondolewa.

Mheshimiwa Spika, kazi ya Kamati katika eneo hili ilikuwa ni kuchambua gharama zilizotumika kutekeleza mradi husika ili kujiridhisha iwapo kulikuwa na udhibiti wa gharama, usimamizi wa mradi na kama mradi umeleta manufaa na kuna thamani ya fedha kwa kuzingatia bajeti iliyotengwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri OR – TAMISEMI kuhakikisha kunakuwa na usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha za miradi kutoka Serikali Kuu ili kuimarisha uwajibikaji wa viongozi waliopewa dhamana ya kutumia fedha hizo kwa ajili ya maendeleo ya Taifa.

ii. Upungufu wa Wataalamu wa Kada ya Uhandisi, Ukadiriaji Majenzi na Usanifu Majengo katika Halmashauri

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha utekelezaji wa miradi hasa katika ngazi za kata na vijiji kunahitajika wataalamu wa ndani wa kutosha kwa ajili ya kusimamia miradi kama ilivyofafanuliwa katika Sheria na Kanuni zake. Katika kuweka msisitizo, Mwongozo wa utekelezaji wa miradi ya force account (guideline for carring out works under force account) inahitaji uwepo wa wataalamu ili kuhakikisha miradi inasimamiwa kwa weledi na kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa.

Kamati imebaini kuwepo kwa upungufu mkubwa wa wataalamu wanaohitajika katika usimamizi wa miradi kama wahandisi, wakadiriaji majenzi na wasanifu majengo. Kwa ujumla, idadi ya wataalamu waliopo katika Halmashauri zetu ni pungufu ikilinganishwa na idadi ya miradi inayotekelezwa. Kukosekana kwa wataalamu hao kwa kiasi kikubwa kumechangia kushuka kwa kiwango cha utendaji, kuwa na miradi isiyo na tija na isiyo na ubora, kuchelewa kukamilika kwa miradi kwa muda uliopangwa na matumizi yasiyo sahihi ya rasilimali za umma.

Mheshimiwa Spika, Ripoti ya CAG ya Ukaguzi wa ufanisi wa Force Account iliyorejewa hapo juu ilionesha kwamba, hadi kufikia

mwezi Mei 2019 kulikuwa na wataalamu wenye sifa **213** tu kati ya **859** wanaohitajika sawa na 24.8% tu. Upungufu huu ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na uanzishwaji wa TARURA ambapo wahandisi 419 (sawa na 66.2%) kati ya 632 waliokuwepo kwenye Halmashauri na Ofisi ya Rais TAMISEMI walihamishiwa TARURA. Ombwe ambalo Bado halijazibwa mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati katika eneo hili umebaini upungufu mkubwa wa wataalamu katika Hamashauri nyingi nchini kwakuwa, idadi ya wataalamu wa kada ya uhandisi haiendani na wingi wa miradi inayotekelezwa. Kwa Halmashauri zilizofika mbele ya Kamati, kuna Halmashauri zinatekeleza miradi mingi ya force account hadi kufikia miradi Mia Moja lakini Mhandisi ni mmoja au wawili tu.

Kukosekana kwa wataalamu wanaohitajika, imelazimika kutumia watumishi wa kada ya elimu na afya kusimamia miradi hiyo. Watumishi hao wamekuwa wakitumia muda mwingi katika kusimamia miradi badala ya kutekeleza majukumu yao ya msingi hali inayozorotesha utoaji wa huduma kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa idadi ya wahandisi, wakadiriaji majenzi na wasanifu majengo waliopo katika Mikoa Mitano ni kama inavyoonekana katika Jedwali Namba 1.

Jedwali Na. 1: Idadi ya Wataalamu katika Halmashauri

MKOA	HALMASHAURI	WAHANDISI (ENGINEERS)	WAKADIRIAJI MAJENZI (QS)	WASANIFU MAJENGO (ARCHTECT)	IDADI YA MIRADI
RUVUMA	SONGEA MC	2	1	1	32
	SONGEA DC	2	0	0	34
	MADABA DC	2	1	0	62
	NYASA DC	1	1	0	28
	NAMTUMBO DC	2	1	1	143
	TUNDURU DC	2	0	0	52
	MBINGA TC	2	1	0	10
	MBINGA DC	1	1	1	11
	JUMLA NDOGO	14	6	3	372
LINDI	MTAMA DC	2	0	1	44

MKOA	HALMASHAURI	WAHANDISI (ENGINEERS)	WAKADIRIAJI MAJENZI (QS)	WASANIFU MAJENGO (ARCHTECT)	IDADI YA MIRADI
	RUANGWA DC	3	1	0	140
	LIWALE DC	1	1	0	91
	NACHINGWEA DC	4	1	0	82
	KILWA DC	4	1	0	157
	LINDI MC	2	0	0	81
	JUMLA NDOGO	16	4	1	595
TABORA	TABORA MC	3	0	0	99
	IGUNGA DC	4	0	0	102
	URAMBO DC	3	0	0	82
	SIKONGE DC	2	2	1	111
	NZEGA TC	2	0	0	40
	KALIUA DC	2	1	2	141
	NZEGA DC	1	1	0	115
	UYUI DC	2	1	0	119
	JUMLA NDOGO	19	5	3	812
KATAVI	MLELE DC	2	1	0	88
	NSIMBO DC	2	1	0	76
	MPIMBWE DC	2	1	0	59
	TANGANYIKA DC	4	1	0	169
	MPANDA MC	4	1	0	169
	JUMLA NDOGO	14	5	0	561
MTWARA	MASASI TC	2	0	0	81
	MTWARA MC	2	1	0	68
	NANYAMBA TC	2	0	0	74
	TANDAHIMBA DC	1	0	0	108
	NEWALA DC	2	1	0	98
	MASASI DC	2	0	0	108
	NANYUMBU DC	1	1	0	89
	MTWARA DC	2	1	0	103
	NEWALA TC	2	0	0	98

MKOA	HALMASHAURI	WAHANDISI (ENGINEERS)	WAKADIRIAJI MAJENZI (QS)	WASANIFU MAJENGO (ARCHTECT)	IDADI YA MIRADI
	JUMLA NDOGO	16	4	0	827
	JUMLA KUU	**79**	**24**	**7**	**3167**

Chanzo: Taarifa ya OR - TAMISEMI

iii. Kutofanyika kwa Tathimini ya Mahitaji ya Miundombinu Muhimu kabla ya Utekelezaji wa Mradi

Mheshimiwa Spika, kabla ya utekelezaji wa mradi wowote inatakiwa kufanyika tathimini ya kina juu ya mahitaji ya miundombinu muhimu katika eneo la mradi kama miundombinu ya barabara, maji na umeme ili huduma iweze kutolewa pindi mradi unapokamilika. Kamati imebaini kuwa, Halmashauri nyingi hazifanyi tathmini katika eneo hilo hivyo kusababisha kuongezeka kwa gharama mara kwa mara (variations) na miradi kutoanza kutumika pindi inapokamilika.

Miradi iliyoangaliwa na Kamati katika kipindi cha Januari, 2024 imebainika kuwepo kwa ongezeko la gharama kwa ajili ya ukamilishaji wa miundombinu mbalimbali na kusababisha kuchelewa kukamilika kwa miradi na wananchi kutopata huduma iliyokusudiwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefahamishwa kuwa, ipo baadhi ya miradi ambayo gharama za utekelezaji wake imeongezeka kutokana na kutokuwepo kwa barabara kuelekea eneo la mradi hali iliyosababisha Halmashauri kutumia kiasi kikubwa cha fedha katika kusafirisha vifaa vya ujenzi hadi eneo la mradi.

Vile vile, maeneo mengi ya miradi yamekumbwa na changamoto ya kutokuwa na maji hivyo kusababisha Halmashauri kutumia fedha nyingi katika ununuzi wa maji tangu kuanza kwa mradi mpaka kukamilika kwake. Vile vile, miradi hiyo inapokamilika, haianzi kutumika kwa wakati kutokana na kukosekana kwa maji. Iwapo miundombinu ya maji ingekuwa imeshawekwa na Mamlaka zinazohusika, changamoto hiyo ingeondolewa na kuwezesha miradi hiyo kutoa huduma iliyokusudiwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia imebaini uwepo wa miradi mingi ya force account kukamilika lakini kutoanza kutumika kutokana na kukosekana kwa nishati ya umeme. Na kwa maeneo ambayo nishati ya umeme inapatikana, changamoto kubwa ni nishati hiyo kuwa na uwezo hafifu ikilinganishwa na uwezo unaohitajika kuendesha mitambo iliyopo katika Hospitali, zahanati, vituo vya afya na maeneo mengineyo.

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi Kamati imebaini kuwa, Taasisi na Idara za Serikali kutowasiliana/ kutoshirikishana na kutokuwa na mpango wa pamoja wa utekelezaji wa miradi. Hali hii inatokana na Taasisi moja kupanga kutekeleza mradi bila ya kushirikisha Taasisi nyingine zinazohusika katika uwekaji wa miundombinu muhimu. kutowasiliana/kutoshirikishana huko, kumesababisha baadhi ya Halmashauri kuhamisha miradi kutoka katika maeneo ambayo yana uhitaji kwa hofu ya kuongezeka kwa gharama kutokana na kutokuwepo kwa miundombinu muhimu katika eneo ambalo mradi ulipangwa kutekelezwa.

iv. Ubora usiokidhi vigezo wa Miradi inayotekelezwa kwa force Account

Mheshimiwa Spika, inafahamika kuwa miradi ya Serikali hasa majengo ina muda wa matumizi (economic life) ambao umekadiriwa kwa mradi huo kutoa huduma kwa wananchi. Katika utekelezaji wa miradi kwa njia ya force account, Halmashauri inapaswa kufanya uchambuzi wa kina juu ya ubora wa miradi inayotekelezwa katika maeneo yao ya usimamizi.

Mheshimiwa Spika, Mwongozo kuhusu usimamizi wa mali za Serikali na marekebisho yake ya mwaka 2019 uliotolewa na Wizara ya Fedha, umefafanua kuhusu muda wa matumizi wa mali za Serikali ikiwemo majengo, mashine na vifaa. Mchanganuo huo kwa mujibu wa kiambatisho namba 3 cha mwongozo huo ni kama inavyoonekana katika Jedwali Namba 2.

Jedwali Na. 2: Muda wa Matumizi wa Mali za Serikali

S/N	Aina ya Mali (Asset Category)	Muda wa matumizi (Economic Life - yrs)
1.	Nyumba ya makazi	50
2.	Shule	75

3.	Hospitali	60
4.	Ofisi	50
5.	Mashine	15
6.	Samani	5
7.	Vifaa vya ofisi	5

Chanzo: uk viii wa mwongozo wa usimamizi wa mali za Serikali, 2019

Mheshimiwa Spika, Ukaguzi uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika miradi iliyotekelezwa kwa njia ya force account umebaini ubora hafifu wa miradi hiyo hali inayoleta kiashiria ambacho si kizuri kwakuwa miradi mingi haitaishi kwa kipindi cha muda mrefu kama ilivyoainishwa katika Mwongozo wa Serikali.

Kwa muktadha huo, katika kipindi cha muda mchache cha uhai wa majengo hayo ambayo hayajakidhi vigezo, Serikali itaingia tena gharama kubwa kwa ajili ya kufanya marekebisho ya mara kwa mara ya miradi hiyo iliyojengwa chini ya kiwango na kushindwa kutumika kwa muda mrefu uliotarajiwa. Hali hii inatokana na kutofanyika kwa hatua muhimu kama vile upimaji wa udongo wa eneo husika la mradi, kutumia vifaa visivyo na ubora kutokana na kutofanyika kwa ukaguzi wa kina wa vifaa vya ujenzi na kutumia mafundi wasio na taaluma kuhusu mradi husika.

v. Ukiukwaji wa Hatua za Kitaalamu za Ujenzi

Mheshimiwa Spika, miradi mingi iliyotekelezwa kwa njia ya force account imejengwa bila ya kuzingatia hatua za kitaalamu za ujenzi kutokana na uharaka wa kukamilisha miradi husika ili kuwahi muda wa mwisho wa utekelezaji uliowekwa, hali inayopelekea kukiuka hatua muhimu za ujenzi na kupelekea miradi kukosa ubora.

Miradi mingi ya ujenzi wa shule na vituo vya afya imetekelezwa katika kipindi cha muda mfupi sana hali inayoashiria kukosekana kwa ubora wa majengo hayo kutokana na kutofuatwa kwa hatua za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi uliofanywa na CAG katika baadhi ya miradi umebaini baadhi ya majengo kuweka nyufa kabla ya kukamilika, milango na madirisha kudondoka, marumaru

kupasuka na kuweka vishimo na baadhi ya kuta za madarasa kusagika. Mapungufu haya yanatokana na ukiukwaji wa taratibu za ujenzi.

vi. Ukiukwaji wa Mwongozo wa utekelezaji wa miradi kwa kutumia njia ya force account

Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa matumizi ya Force account umeeleza juu ya majukumu ya kila mdau katika utekelezaji wa miradi. Wadau walioelezewa ni wanaohusika moja kwa moja na utekelezaji wa mradi (internal actors) na wadau wasiohusika moja kwa moja na utekelezaji wa mradi (external actors).

Mheshimiwa Spika, katika kujiridhisha iwapo mwongozo umefuatwa kikamilifu, Kamati imechambua kwa kina juu ya uwepo wa Kamati za force account (force account committee) ambazo Afisa Masuuli anatakiwa kuziunda kwa ajili ya utekelezaji bora wa mradi. Kamati hizo ni zifuatazo:

- ✓ **Kamati ya ujenzi (Construction Committee)**

Mheshimiwa Spika, Kamati hii ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa shughuli zote za ujenzi kuanzia hatua za awali za ufungaji wa mkataba. Kwa mujibu wa mwongozo, Kamati inatakiwa kuwa na watu wenye taaluma ya uhandisi au usanifu majengo au mkadiriaji majenzi.

- ✓ **Kamati ya Ununuzi (Procurement Committee)**

Mheshimiwa Spika, Kamati hii inajumuisha Afisa Manunuzi ambapo, jukumu kubwa la Kamati ni kutekeleza shughuli zote za ununuzi ikiwa ni pamoja ununuzi wa vibarua, ununuzi wa vifaa na huduma nyingine zitakazohitajika katika mradi kama vile usafiri.

- ✓ **Kamati ya Mapokezi na Ukaguzi (Inspection and Receiving Committee)**

Mheshimiwa Spika, Kamati hii inatakiwa kuhakikisha bidhaa zote zinazowasilishwa ni za kiwango na ubora ulioainishwa katika mkataba.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukutana na baadhi ya Halmashauri zilizotekeleza miradi kwa kutumia njia ya force account, Kamati imebaini kuwa, Kamati tajwa hapo juu hazijaundwa na kwa baadhi ya maeneo, Kamati zilizoundwa hazitekelezi majukumu yake kama inavyotakiwa kutokana na kukosekana kwa wataalamu kama inavyoelekezwa katika mwongozo pamoja na Maafisa Masuuli kutozishirikisha katika mchakato wowote. Ukiukwaji wa taratibu na miongozo iliyowekwa kwa kiasi kikubwa kumesababisha miradi mingi kutofikia viwango vinavyotakiwa.

vii. Ukiukwaji wa Miongozo inayotolewa na Ofisi ya Raisi TAMISEMI

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilipeleka kiasi cha **Shilingi Bilioni 100.58** kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari mpya 214 ambazo zilitarajiwa kujengwa kwenye majimbo yote nchini, na **Shilingi Bilioni 30** zilipelekwa kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari mpya za wasichana kwenye Mikoa 10 (shule 1 katika kila mkoa) Tanzania Bara kupitia mradi wa kuboresha elimu ya sekondari nchini (SEQUIP)

Katika utekelezaji wa mradi huo wa SEQUIP, tarehe 2.12.2021 OR – TAMISEMI ilitoa Mwongozo wa matumizi ya fedha hizo za mradi ambapo, gharama ya ujenzi wa shule za sekondari za kata ni **Shilingi Milioni 600** kwa kila shule ambayo ilitarajiwa kupelekwa kwa awamu mbili ambapo, kiasi kilichopelekwa katika awamu ya kwanza ni **Shilingi Milioni 470**.

Mheshimiwa Spika, katika awamu ya kwanza inayohusisha **Shilingi Milioni 470** ilijumuisha ujenzi wa Vyumba vya madarasa 8, Maabara za Sayansi 3, Jengo moja la Utawala, Maktaba 1, Chumba cha ICT 1, Vyoo 20 vya wanafunzi (Wav 10 &, Was 10), Matanki mawili ya Maji (kila moja lita 10,000), Nguzo ya kuweka Tanki 1, Ujenzi wa Miundombinu ya kunawa mikono na Miundombinu ya Kuvuna/ Kuunganisha Maji. Aidha, Awamu ya pili ya mradi inayotarajiwa kutumia **Shilingi Milioni 130** itajumuisha Nyumba za Walimu na Vifaa vya ICT.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa miradi ya SEQUIP, Kamati imefanya uchambuzi katika mikoa Mitano ambayo baadhi ya

Halmashauri zake zimefika kwa mahojiano ili kujiridhisha iwapo kiasi cha fedha kilichotolewa na OR – TAMISEMI ndicho kilichotumika.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipanga kutumia jumla ya **Shilingi 24,038,696,257.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa Shule za Sekondari za kata ambapo kila shule moja ilitakiwa kutumia **Shilingi Milioni 470**. Hata hivyo, wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo, gharama halisi zilizotumika ni tofauti na kilichokadiriwa. Vile vile, baadhi ya miradi haijakamilika na inahitaji nyongeza ya fedha kama inavyoonekana katika **Jedwali namba 3.**

Jedwali Na. 3: Mchanganuo wa matumizi ya miradi ya SEQUIP

Mkoa	Gharama ya Mradi (OR-TAMISEMI)	Kiasi Halisi kilichotumia	Tofauti (Ghara za TAMISEMI – Kiasi kilichotumika)	Nyongeza inayohitajika kukamilisha mradi	Jumla (Tofauti +nyongeza inayohitajika)
Katavi	2,820,000,000.00	3,347,079,364.00	527,079,364.00	285,006,100.00	812,085,464.00
Tabora	9,468,696,257.00	10,112,065,296	643,369,039	1,250,000,000.00	1,893,369,039.00
Lindi	3,290,000,000.00	3,477,600,000	187,600,000	407,867,197.00	595,467,197.00
Mtwara	3,760,000,000.00	4,145,804,939	385,804,939	828,247,300.00	1,214,052,239.00
Ruvuma	4,700,000,000.00	5,507,576,010	807,576,010	568,122,374.00	1,375,698,384

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, Serikali imetumia jumla ya **Shilingi 26,590,125,608.73** (fedha kutoka Serikali Kuu na mapato ya ndani) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi katika mikoa mitano kati ya **Shilingi 24,038,696,257.00** zilizopangwa kutumika na Serikali (OR – TAMISEMI). Aidha, makadirio ya jumla ya kiasi cha **Shilingi 3,339,242,971.00** kinahitajika ili kukamilisha miradi iliyosimama.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati juu ya matumizi ya fedha za SEQUIP zilizotumika katika utekelezaji wa miradi kwa njia ya force account ulijikita pia katika kuangalia tofauti ya fedha zilizotumika baina ya Halmashauri zilizopo katika Mkoa mmoja.

Lengo la tathimini hiyo lilikuwa ni kufanya ulinganifu wa gharama za miradi zilizotumika pamoja na nyongeza ya fedha kati ya Halmashauri moja na nyingine kwa miradi inayofanana.

Mheshimiwa Spika, uchanganuzi wa matumizi ya fedha za miradi ya Force account kwa Halmashauri zilizofika mbele ya Kamati ni kama inavyoonekana katika jedwali namba 4.

Jedwali Na. 4: Matumizi ya fedha za miradi ya SEQUIP

Mkoa	Halmashauri	Fedha zilizopelekwa na Serikali Kuu (Sh.)	Nyongeza ya Fedha (Mapato ya Ndani)	Nyongeza ya Fedha (Michango ya Jamii)	Kinachohitajika kukamilisha mradi (Sh.)	Jumla ya gharama ya Mradi (Sh.)
Katavi	Nsimbo DC	470,000,000	-	-	70,300,600	540,300,600
	Tanganyika DC	470,000,000	-	-	87,776,500	557,776,500
	Mpanda MC	a) 470,000,000 b) 470,000,000	a) 80,000,000 b) 80,000,000	- -	a) 25,845,300 b) 31,695,300	a) 575,845,300 b)581,695,300
	JUMLA	**1,880,000,000**	**160,000,000**	**-**	**215,617,700**	**2,255,617,700**
LINDI	Mtama DC	470,000,000	56,000,000	255,000	129,017,304	655,272,304
	Nachingwea DC	470,000,000	46,000,000	11,100,000	191,132,591	718,232,591
	Lindi MC	470,000,000	30,000,000	1,800,000	71,990,000	573,790,000
	Kilwa DC	470,000,000	32,500,000	-	146,196,194	648,696,194
	JUMLA	**1,880,000,000**	**164,500,000**	**13,155,000**	**538,336,089**	**2,595,991,089**
MOROGORO	Mvomero DC	470,000,000	-	-	241,256,231	711,256,231
	Morogoro DC	470,000,000	-	-	73,363,739.2	543,363,739.2
	Ulanga DC	470,000,000	-	-	160,000,000	630,000,000
	Malinyi DC	470,000,000	-	-	122,587,395	592,587,395
	Mlimba DC	470,000,000	-	-	139,047,425	609,047,425
	JUMLA	**2,350,000,000**	**-**	**-**	**736,254,790.2**	**3,086,254,790.2**
MTWARA	Nanyumbu DC	470,000,000	30,000,000	-	84,730,000	584,730,000
	Newala DC	470,000,000	-	-	159,727,000	629,727,000
	Masasi TC	470,000,000	65,000,000	-	37,000,000	572,000,000

	JUMLA	**1,410,000,000**	**95,000,000**	**-**	**281,457,000**	**1,786,457,000**
TABORA	Kaliua DC	470,000,000	51,800,000	-	47,380,000	569,180,000
	Nzega TC	470,000,000 + 379,575,825		-	-	849,575,828
	JUMLA	**1,319,575,825**	**51,800,000**	**-**	**47,380,000**	**1,410,755,825**
RUVUMA	Namtumbo DC	470,000,000	-	-	100,034,223	570,034,223

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo imefafanuliwa katika jedwali namba 4 hapo juu, OR – TAMISEMI kupitia wataalamu wa Sekretarieti za Mikoa, wanatakiwa kufanya ufuatiliaji wa kina kuhusu matumizi ya fedha hizo na kujiridhisha juu ya tofauti kubwa ya nyongeza ya gharama za miradi ikizingatiwa kwamba, Halmashauri hizo zinapatikana katika maeneo ya kijiografia yanayofanana.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ujenzi wa shule za mkoa za wasichana, mwongozo umefafanua kuwa, gharama ya ujenzi wa shule za sekondari za wasichana za mikoa ni **Shilingi Bilioni 4** ambapo Kiasi cha **Shilingi Bilioni 3** kimetolewa ikiwa ni malipo ya awamu ya kwanza ya ujenzi kwa kila shule.

Majengo ambayo yamejumuishwa katika mradi huo ni kama inavyoonekana katika jedwali namba 5 la Taarifa hii.

Jedwali Na. 5: Mchanganuo wa Miundombinu itakayojengwa katika shule za Sekondari za Wasichana kila Mkoa

S/N	Aina ya jengo	Idadi ya majengo	Idadi ya vyumba kwa majengo yote
AWAMU YA KWANZA			
1.	Jengo lenye vyumba vya madarasa 2	2	4
2.	Jengo lenye vyumba vya madarasa 2 na ofisi 01	3	6
3.	Jengo lenye vyumba vya madarasa 2 na vyoo	1	2
4.	Jengo lenye Maabara ya Fizikia na chumba cha Jiografia	1	2
5.	Jengo lenye maabara za Kemia na Biolojia	1	2

S/N	Aina ya jengo	Idadi ya majengo	Idadi ya vyumba kwa majengo yote
6.	Jengo la Utawala	1	1
7.	Jengo la vyoo yya wanafunzi (Wasichana)	1	16
8.	Chumba cha Jenereta	1	1
9.	Bwalo/ Ukumbi	1	1
10	Nyumba za Mwalimu (Vyumba 3)	1	
11.	Nyumba za Mwalimu (2 in 1)	1	
12.	Mabweni @ 120 Wanafunzi	5	
KAZI ZA NJE			
1.	Mitaro ya Maji (1050M)		
2.	Vichomea Taka	1	1
3.	Uzio (CHAIN LINK) – 350m	1	1
4.	Matanki ya Ardhini ya Kutunzia Maji (32,000 LITRES)	2	2
5.	Tanki za Maji (KIBOKO) na nguzo zake	2	2
6.	MANHOLE NA GULLY TRAP	2	2
7.	Njia za Miguu (WALK WAY & PAVING)		
AWAMU YA PILI			
1.	Jengo lenye vyumba vya madarasa 2	2	4
2.	Jengo lenye vyumba vya madarasa 2 na ofisi 1	3	6
3.	Chumba cha ICT	1	1
4.	Maktaba	1	1
5.	Nyumba za Mwalimu (Vyumba 3)	4	
6.	Mabweni @ 120 Wanafunzi	4	

***Chanzo**: kiambatisho II cha utekelezaji wa mradi wa SEQUIP*

Mheshimiwa Spika, kinyume na Mwongozo uliotolewa na OR – TAMISEMI, Kamati imebaini ukiukwaji wa Mwongozo huo ambapo, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi haikuzingatia Mwongozo kwa kutumia Jumla ya **Shilingi Bilioni 3.1** kutekeleza awamu ya kwanza ya mradi wa ujenzi wa shule ya Sekondari ya Wasichana Lindi na kuhitaji fedha ya nyongeza ya **Shilingi Bilioni 1.5** ili kukamilisha mradi huo badala ya kukamilisha kwa **Shilingi Bilioni 3** zilizopangwa na OR – TAMISEMI. Vile vile, Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo ilikiuka Mwongozo uliotolewa na OR – TAMISEMI ambapo, Halmashauri imekwishatumia **Shilingi 2,915,857,748** kwa

ajili ya ujenzi wa shule ya sekondari ya Daktari Samia Suluhu Hassan na kuhitaji ziada ya **Shilingi 784,861,150** ili kukamilisha kazi zilizotakiwa kukamilika kwa **Shilingi Bilioni 3**.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Miradi ya ujenzi wa vituo vya afya pamoja na ukamilishaji wa Zahanati, Serikali kuu ilipeleka jumla ya **Shilingi 30,557,776,656.00** katika miradi Iliyotekelezwa na Halmashauri zilizopo katika mikoa mitano kama ifuatavyo.

Jedwali Na. 6: Mchanganuo wa matumizi ya ujenzi wa Vituo vya Afya

Mkoa	Gharama ya Mradi (OR-TAMISEMI)	Kiasi halisi kilichotumika	Tofauti (Gharama za TAMISEMI – Kiasi kilichotumika)	Nyongeza inayohitajika kukamilisha mradi	Jumla (Tofauti + nyongeza inayohitajika)
Katavi	5,550,000,000.00	6,295,834,000	745,834,000.00	665,221,280.00	1,411,055,280.00
Tabora	5,603,081,656.00	6,270,980,770.79	667,899,114.79	960,842,600.00	1,628,741,714.79
Lindi	5,000,000,000.00	5,455,785,747.00	455,785,747.00	670,192,182.50	1,125,977,929.50
Mtwara	5,750,000,000.00	5,507,000,308.00	-242,999,692.00	934,000,000.00	691,000,308.00
Ruvuma	8,654,695,000.00	9,248,391,900.00	593,696,900.00	718,364,716.34	1,312,061,616.34

Mheshimiwa Spika, kama inavyoonekana katika jedwali namba 6 hapo juu, kwa ujumla, Serikali imetumia jumla ya **Shilingi 32,777,992,726** (Fedha za Serikali Kuu, mapato ya ndani na nguvu za wananchi) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Vituo vya Afya na Zahanati katika mikoa Mitano kati ya **Shilingi 30,557,776,656.00** zilizopangwa kutumika na Serikali (OR – TAMISEMI). Aidha, kwa baadhi ya miradi ambayo haijakamilika, kiasi cha **Shilingi 3,948,620,778.84** kimekadiriwa ili kukamilisha miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imepitia na kufanya uchambuzi wa kina wa taarifa za miradi iliyohakikiwa na CAG na kubaini Halmashauri nyingi kutozingatia mwongozo uliotolewa na OR – TAMISEMI katika utekelezaji wa miradi ya SEQUIP pamoja na miradi ya vituo vya afya ambapo, baadhi ya Halmashauri zimekuwa zikiongeza kiasi kikubwa cha fedha na kufanya gharama ya miradi kuongezeka kwa kiasi kikubwa.

viii. Sekretarieti za Mikoa Kutofuatilia Utekelezaji wa Miradi

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa ina jukumu la moja kwa moja la kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo yao ya usimamizi. Ili kuimarisha utendaji wa Ofisi hiyo, Serikali inapeleka bajeti na imepeleka wasaidizi wawili wa Katibu Tawala Mkoa. Mmoja wa wasaidizi hao ni Katibu Tawala Msaidizi Mkoa upande wa Tathmini na ufuatiliaji ambaye jukumu lake kubwa ni kufanya ufuatiliaji wa miradi yote inayotekelezwa katika Halmshauri za Mkoa wake.

Hata hivyo, Kamati imebaini kutofanyika kwa jukumu hilo kutokana na wataalamu hao kutoka mkoani waliofika mbele ya Kamati kutofahamu shughuli za utekelezaji wa miradi inayoendelea katika mikoa yao pamoja na kutofahamu changamoto zilizopo. Kukosekana kwa usimamizi wa mkoa katika Halmshauri kunachangia kwa kiasi kikubwa kwa Maafisa Masuuli kutekeleza majukumu yao kinyume na Sheria, Kanuni na Miongozo ya Nchi.

ix. Miradi kutokamilika kwa Wakati

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni miradi mingi kushindwa kukamilika kwa wakati uliopangwa kutokana na kutofanyika kwa tathimini ya kina kuhusu muda halisi unaotakiwa kutumika katika kutekeleza miradi mbalimbali hivyo kusababisha Halmashauri kushindwa kufikia malengo ya muda uliowekwa.
Sababu nyingine inayochangia miradi mingi iliyotekelezwa na Hamashauri kwa njia ya force account kushindwa kukamilika kwa wakati ni pamoja na kukosekana kwa wataalamu wa utekelezaji na usimamizi wa miradi, ongezeko la gharama za mradi mara kwa mara, ukiukwaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini uwepo wa nyongeza ya muda wa utekelezaji wa miradi katika maeneo mengi. Miradi ya maendeleo kushindwa kukamilika kwa wakati kunaondoa thamani ya fedha ya miradi hiyo kutokana na kushindwa kutoa huduma iliyokusudiwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, tathimini ya jumla ya Kamati kuhusu utumiaji wa njia ya force account kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni kuwa, endapo taratibu zote zilizowekwa katika Sheria, Kanuni na miongozo zikifuatwa kikamilifu zitaondoa changamoto zote zilizobainika na kama zisipofuatwa, hakutakuwa na thamani ya fedha (value for money) ya miradi hiyo. Hata hivyo, uhalisia uliopo katika utekelezaji wa miradi kwa kutumia njia ya force account ni kwamba, baadhi ya Halmashauri hazifuati Sheria, Kanuni na miongozo mbalimbali ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyofafanuliwa hapo juu, katika kipindi cha Januari, 2024, Kamati ilijikita katika kuangalia utekelezaji wa miradi kwa njia ya force account. Matokeo ya uchambuzi wa taarifa hizo kwa kila Halmashauri ni kama ifuatavyo: -

2.3.1 Uchambuzi wa Taarifa ya miradi iliyotekelezwa kwa njia ya force account na Halmashauri ya Mji Nzega

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Mwezi Juni, 2022, Halmashauri ya Mji Nzega ilitumia njia ya force account kutekeleza jumla ya **miradi 40** yenye thamani ya **Shilingi 2,218,934,495**. Wakati wa utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ilipokea na kufanya uchambuzi wa taarifa ya miradi Sita yenye thamani ya jumla ya **Shilingi 1,822,075,828**.

Uchambuzi wa Taarifa iliyowasilishwa na CAG ilibainisha mapungufu kadhaa ambayo yanaondoa thamani ya fedha na tija ya miradi hiyo. Miradi ambayo ilibainika kuwa na mapungufu mengi ni kama ifuatavyo: -

a) Mradi wa ujenzi wa shule mpya ya sekondari katika eneo la uwanja wa ndege kata ya Nzega Mashariki

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Mji Nzega ilipokea kiasi cha **Shilingi Milioni 470** kutoka Serikali Kuu za mradi wa SEQUIP. Hadi taarifa ya mradi huu inaletwa mbele ya Kamati, mradi huu umetumia jumla ya **Shilingi 849,575,828** ambapo, **Shilingi Milioni 379** ni fedha ambazo ziliingia Halmashauri katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya elimu bure. Mwaka 2021/2022, Halmashauri ya Mji Nzega iliomba kibali cha kutumia **Shilingi**

Milioni 379 za elimu bure kwa ajili ya ujenzi wa shule ya sekondari kata ya Nzega Mashariki ambayo ilikwishapelekewa fedha za mradi wa SEQUIP na kufanya mradi kutumia **Shilingi Milioni 849**.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Halmashauri ya Mji Nzega kutumia fedha zote katika mradi huo, na pamoja na gharama za utekelezaji wa mradi kuwa kubwa kuliko uhalisia, bado mradi huo hautumiki kwa ukamilifu wake kutokana na baadhi ya majengo kutokamilika.

b) Mradi wa ujenzi wa Kitua cha Afya Kitengwe

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengine, Kamati imekua ikiangalia thamani ya fedha ya mradi na iwapo lengo lililokusudiwa la utekelezaji wa mradi linafikiwa. Baada ya uchambuzi wa taarifa ya miradi, Kamati ilibaini kukosekana kwa tija katika mradi wa ujenzi wa kituo cha afya kitengwe kutokana na baadhi ya majengo ya mradi huo kutoanza kutumika tangu kukamilika kwa mradi huo tarehe 30 Septemba, 2022 ambapo Halmashauri ilipokea kiasi cha **Shilingi Milioni 500** kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia taarifa ya miradi, Kamati imebaini ukiukwaji wa mwongozo uliotolewa na TAMISEMI katika ukamilishaji wa maboma ya Zahanati hali iliyochangia majengo hayo kutokamilika kwa kiasi cha fedha cha **Shilingi Milioni 50** kilichopelekwa na Serikali. Vile vile, Halmashauri ina upungufu wa wataalamu ambapo ni Wahandisi Wawili pekee ndio waliopo kusimamia miradi yote.

2.3.2 Uchambuzi wa Taarifa ya miradi iliyotekelezwa kwa njia ya force account na Halmashauri ya Wilaya ya Uyui

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya wilaya ya Uyui imetekeleza jumla ya miradi **119** kwa kutumia njia ya force account. Hadi kufikia Juni, 2022 jumla ya **Shilingi 10,289,555,032** zilitumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo 119 ambapo kati ya miradi hiyo kuna iliyokamilika na inayoendelea kutekelezwa.

Kwa upande wa uchambuzi, Kamati imepitia na kuchambua taarifa ya **miradi 7** yenye thamani ya **Shilingi 1,700,000,000**. Katika

utekelezaji wa majukumu yake, miradi iliyobainika kuwa na mapungufu ni kama ifuatavyo: -

a) Mradi wa ujenzi katika Kituo cha Afya cha Ilolangulu

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ilipokea **Shilingi Milioni 500** kwa ajili ya ujenzi wa mradi huo. Mradi ulianza tarehe 15/09/2021 na kutarajiwa kukamilika tarehe 30/06/2022. Hata hivyo tarehe halisi ya kukamilika ilikuwa ni tarehe 30/05/2023. Hadi kuwasilishwa kwa taarifa hii, mfumo wa umeme na maji ulikuwa haujawekwa katika jengo la upasuaji licha ya fedha zote kutumika. Aidha, wodi ya wazazi ilikamilika lakini haijaanza kutumika hali inayoweza kuchangia uchakavu wa majengo kabla hayajatumika.

b) Mradi wa ujenzi wa Kituo cha Afya cha Loya

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa mradi huu, Halmashauri ilipokea **Shilingi Milioni 500**. Mapungufu yaliyobainika katika mradi huu ni pamoja na kazi kutokamilika katika eneo la upasuaji na kichomea taka. Ili kukamilisha miradi hiyo, Afisa Masuuli ameeleza kuwa inahitaji **Shilingi Milioni 30** kukamilisha jengo la mama na mtoto, **Shilingi Milioni 44** kukamilisha jengo la upasuaji na **Shilingi Miioni 6** kukamilisha jengo la kufulia hivyo kufanya jumla ya gharama ya mradi kuwa **Shilingi Milioni 580** badala ya **Shilingi Milioni 500**.

c) Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Afya cha Tura

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa **Shilingi Milioni 300** kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya cha Tura. Mradi huo ulioanza tarehe 15/09/2021 ulitarajiwa kukamilika tarehe 30/06/2022. Hata hivyo, hadi Kamati ilipokutana na Afisa Masuuli wa Halmashauri ya Wilaya ya Uyui mradi ulikuwa haujakamilika kutokana na baadhi ya kazi kutokamilika katika jengo la upasuaji, jengo la wagonjwa wa nje na kichomea taka.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla hali ya utekelezaji wa miradi katika Halmashauri ya Wilaya ya Uyui si ya kuridhisha kutokana na miradi

mingi kutokamilika kwa wakati kwa kutoa sababu kuwa, jiografia ya mahali ambapo miradi inatekelezwa kutofikika kwa urahisi.

2.3.3 Uchambuzi wa Taarifa ya miradi iliyotekelezwa kwa njia ya force account na Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana na Afisa Masuuli wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua kwa ajili ya uchambuzi wa taarifa ya miradi iliyotekelzwa kwa kutumia njia ya force account. Hadi kufikia mwezi Juni, 2022, Halmashauri ilitekeleza jumla ya **miradi 141** yenye thamani ya **Shilingi 9,176,287,582.81**.

Katika utekelezaji wa miradi hiyo, mapungufuu kadhaa yamebainika. Katika uhakiki uliofanywa na CAG, Baadhi ya miradi iliyokutwa na mapungufu ni: -

a) Mradi wa ujenzi wa Kituo cha Afya cha Usinge

Mheshimiwa Spika, Halmashauri iletekeleza mradi huo wenye thamani ya **Shilingi 631,785,137** ambao ulikamilika. Hata hivyo, jengo la kuhifadhia maiti halitumiki kutokana na kutokuwepo kwa jokofu la kutunzia maiti lenye thamani ya **Shilingi 32,276,653**. Kwa upande wa jengo la wazazi, upande wa upasuaji haujaanza kutumika kwasababu vifaa vyenye thamani ya **Shilingi 214,253,955** vimenunuliwa tangu mwezi Oktoba, 2023 havijafungwa kutokana na Bohari Kuu ya Dawa (MSD) kutokwenda kufunga vifaa hivyo.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya MSD kupeleka vifaa katika Hospitali na vituo vya afya na kuviacha kwa muda mrefu bila ya kuvifunga limetokea katika Halmashauri mbalimbali Nchini.

Tathimini ya Kamati ni kuwa, vifaa hivyo kuendelea kukaa kwa muda mrefu bila ya kufungwa, kunawanyima wananchi fursa ya kupata huduma kama ilivyokusudiwa. Vile vile, vifaa hivyo vitachakaa kabla ya kuanza kutumika hivyo kukosa thamani ya fedha.

b) Mradi wa Umaliziaji wa Kituo cha Afya cha Uyowa

Mheshimiwa Spika, mradi wa umaliziaji wa Kituo cha Afya ulikuwa na gharama ya jumla ya **Shilingi 698,014,700** ambapo katika fedha hizo, kiasi cha **Shilingi 23,014,700** michango ya wananchi, **Shilingi 600,000,000** kutoka Serikali Kuu na **Shilingi 75,000,000** kutoka katika mapato ya ndani. Ili kukamilisha mradi huo, bado Halmashauri imeeleza kuhitaji **Shilingi Milioni 50** na kufanya gharama za mradi kufikia **Shilingi 748,014,700**.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua imetekeleza jumla ya **miradi 141** kwa kutumia force account lakini wataalamu waliotakiwa kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa katika ufanisi wa hali ya juu ni Watano tu ambapo, Wahandisi ni Wawili, Mafundi (technicians) Wawili na Mkadiriaji majenzi (QS) Mmoja.

2.3.4 Uchambuzi wa Taarifa ya miradi iliyotekelezwa kwa njia ya force account na Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kutumia force account umefanyika pia katika Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika ambapo jumla ya **miradi 169** yenye thamani ya **Shilingi 9,867,839,193** ilitekelezwa. Kamati imepata fursa ya kufanya uchambuzi wa miradi 6 yenye thamani ya **Shilingi 1,253,533,659.14** kati ya miradi 169. Katika uchambuzi wa taarifa zilizowasilishwa, changamoto kadhaa zilizobainika katika baadhi ya miradi ni kama ifuatavyo: -

a) Ujenzi wa Kituo cha afya Mnyagala

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa kituo cha afya cha Mnyagala kilitarajiwa kuanza tarehe 11/08/2021 na kukamilika tarehe 14/05/2022 kwa gharama ya **Shilingi Milioni 200**. Hata hivyo, mradi huo bado haujakamilika na kiasi cha **Shilingi Milioni 220** kimekwishatumika.

Mheshimiwa Spika, ili kukamilisha mradi huo, Kamati imearifiwa kuwa bado zinahitajika **Shilingi 28,118,000** kutoka katika mapato ya ndani. Kuchelewa kukamilika kwa mradi huo kinyume na mipango iliyowekwa kunakwamisha juhudi za Serikali za kutoa huduma bora kwa wananchi wake.

b) Mradi wa Umaliziaji wa Maabara ya Kemia na Biolojia katika Shule ya Kapalamsenga

Mheshimiwa Spika, Serikali imepeleka jumla ya **Shilingi Milioni 75** katika Halmashuri ya Wilaya ya Tanganyika kwa ajili ya mradi wa maabara ya Kemia na Biolojia. Mradi huo ulianza tarehe 1 Disemba, 2021 na kutarajiwa kukamilika tarehe 12 Julai, 2022. Hata hivyo, hadi Kamati inakutana na Afisa Masuuli wa Halmashauri hii, mradi huo ulikuwa bado haujakamilika licha ya fedha yote kumalizika na muda wa utekelezaji wa mradi kumalizika tangu mwezi Julai, 2022. Makadirio ya umaliziaji wa ujenzi wa vyumba vya maabara iliyowasiishwa na Afisa Masuuli ni **Shilingi 26,276,000**.

c) Mradi wa Ujenzi wa Shule ya Sekondari Majalila

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuboresha elimu nchini, Serikali ilipeleka **Shilingi Milioni 470** za mradi wa SEQUIP kwa ajili ya ujenzi wa shule ya sekondari Majalila. Mradi huo ulianza kutekelezwa tarehe 15/03/2022 na kutarajiwa kukamilika tarehe 09/01/2023. Hadi kuwasilishwa kwa taarifa hii, mradi huu haujakamilika na kwa mujibu wa taarifa iliyowasilishwa na Afisa Masuuli, kiasi cha **Shilingi 87,776,500** kinahitajika ili kukamilisha mradi huo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa ukaguzi uliofanywa na CAG na uchambuzi uliofanywa na Kamati, changamoto kubwa iliyobainika katika miradi iliyotekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika kwa njia ya force account ni pamoja na gharama kutohusisha gharama za kufanya vipimo vya vifaa (test of material), gharama za ujenzi wa stoo, gharama za mlinzi na gharama za maji ya ujenzi. Kimsingi gharama zote zilitakiwa kukadiriwa kabla ya kuanza kwa utekelezaji ili miradi iweze kukamilika kwa wakati.

2.3.5 Uchambuzi wa Taarifa ya miradi iliyotekelezwa kwa njia ya force account na Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu lake la kikanuni, Kamati ilifanya uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa miradi iliyotumia njia ya force account. Kwa mujibu wa taarifa

iliyowasilishwa, hadi kufikia mwezi Juni, 2022, Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe ilitekeleza **miradi 59** yenye jumla ya **Shilingi 4,037,437,441**.

Kwa ngazi ya Kamati, taarifa ya kina kuhusu **miradi 7** yenye thamani ya **Shilingi 3,365,857,149** iliwasilishwa na kujadiliwa kwa kina. Katika uchambuzi wake, miradi kadhaa iliyobainika kuwa na mapungufu ni kama ifuatavyo: -

a) Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Afya cha majimoto katika Kijiji cha Ikulwe

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ilitumia mapato yake ya ndani ya jumla ya **Shilingi 548,994,708** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo ambapo, fedha hizo zilipelekwa kwa awamu sita. Tija ya utekelezaji wa mradi huo bado haijapatikana kwakuwa, majengo ya maabara, jengo la mama na mtoto na jengo la kufulia hayatumiki kutokana na kukosekana kwa vifaa. Vile vile, umeme katika majengo yote haujaunganishwa licha ya miundombinu yote ya umeme kukamilika.

b) Mradi wa Ujenzi wa Wodi za Wanawake, Watoto na Wanaume katika Hospitali ya Halmashauri

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha afya ya wananchi wake, Halmashauri ilipokea **Shilingi Milioni 500** kutoka Serikali kuu kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo. Katika mradi huo, fedha yote iliyopokelewa ilitumika ambapo, jengo la wodi ya wanawake limekamilika lakini jengo la wodi ya watoto na wodi ya wanaume hayajakamilika. Ili mradi huo uweze kukamilika, Kamati imeelezwa kuwa inahitajika **Shilingi 41,228,300**.

Kwa upande wa jengo la wodi ya wanaume, kazi ambazo hazijakamilika ni pamoja na madirisha, milango, mifumo ya umeme, mifumo ya maji safi na majitaka ambapo, gharama za kumalizia mradi huu ni **Shilingi 44,172,198**.

Mheshimiwa Spika, changamoto za jumla za utekelezaji wa miradi kwa njia ya force account katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe ni upungufu wa wataalamu wa kada ya uhandisi,

miradi mingi kutoanza kutumika kutokana na kukosekana kwa vifaa au wataalamu. Hali hii inaondoa thamani ya miradi hiyo kinyume na ilivyokusudiwa.

2.3.6 Uchambuzi wa Taarifa ya miradi iliyotekelezwa kwa njia ya force account na Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa miradi Saba yenye thamani ya **Shilingi 2,040,000,000** kati ya miradi yote **53** yenye jumla ya **Shilingi 4,730,530,000** inayotekelezwa na Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda.

Mapungufu yaliyobainika na Kamati katika baadhi ya miradi ambayo imehakikiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni kama ifuatavyo: -

a) Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Afya Mwamkulu

Mheshimiwa Spika, mradi huu ulipokea na kutumia jumla ya **Shilingi Milioni 500** na mradi ulitakiwa kukamilika tarehe 15 Novemba, 2022. Hata hivyo, bado mradi wote haujakamilika katika ukamilifu wake. Uchambuzi wa taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati umebaini kuwa, makadirio ya gharama ya kukamilisha mradi huo ni **Shilingi 22,243,300**.

b) Mradi wa Ujenzi wa Shule ya Sekondari Kawalyowa

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Halmashauri ilipokea **Shilingi Milioni 470** kutoka Serikalini fedha ambazo ni za mradi wa SEQUIP. Katika utekelezaji wa mradi huo, Halmashauri iliongeza **Shilingi Milioni 80** na kufanya mradi huo kutumia jumla ya **Shilingi Milioni 550**. Pamoja na kiasi chote cha fedha kutumika, Kamati imeelezwa kuwa, bado zinahitajika **Shilingi 31,695,300** kukamilisha maeneo mbalimbali.

c) Mradi wa Ujenzi wa Shule za Sekondari za Nsemulwa, Misunkumilo, Mpanda day na Shanwe

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda ilitekeleza miradi ya ujenzi wa Shule za Sekondari katika kata za

uwanja wa ndege, Misunkumilo, Makanyagio na shanwe. Jumla ya **Shilingi Milioni 310** zilitumika katika kutekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, miradi hiyo imekamilika na inatumika. Hata hivyo, ukaguzi uliofanywa na CAG umebaini kuwepo kwa nyufa katika kuta za madarasa ya shule hizo. Hali hiyo inaleta tafsiri ya kukosekana kwa ubora wa miradi ikiwa ni pamoja na kuhatarisha usalama wa wanafunzi wa shule hizo.

2.3.7 Uchambuzi wa Taarifa ya Miradi iliyotekelezwa kwa njia ya force account na Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa iliyowasilishwa na CAG, Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo ilitekeleza kwa njia ya force account jumla ya **miradi 76** yenye thamani ya **Shilingi 3,236,899,361.82**. Kwa muktadha wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati, taarifa za **miradi 7** iliyotumia jumla ya **Shilingi 1,916,000,000** ilichambuliwa.

Tathimini ya Kamati katika Halmashauri hii imebaini utendaji usioridhisha katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo hali iliyosababisha miradi mingi kutokamilika kwa wakati licha ya kutumia kiasi kikubwa cha fedha, ongezeko la gharama za utekelezaji wa miradi na usimamizi usioridhisha wa miradi.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya miradi iliyobainika kuwa na mapungufu ni kama ifuatavyo: -

a) Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Afya Itenka

Mheshimiwa Spika, mradi huu wenye thamani ya **Shilingi 500,000,000** ulianza kutekelezwa tarehe 20/11/2021 na kutarajiwa kukamilika tarehe 20/11/2022. Pamoja na kiasi chote cha fedha kutumika, mradi huo bado haujakamilika. Miongoni mwa majengo ambayo hayajakamilika ni pamoja na Jengo la upasuaji ambalo kwa mujibu wa taarifa iliyowasilishwa na CAG inahitajika **Shilingi 71,369,000** ili jengo hilo liweze kukamilika, Jengo la wodi ya wazazi linahitaji **Shilingi 16,978,800** ili kukamilika na jengo la kufulia linahitaji **Shilingi 5,118,000** ili kukamilika na kufanya jumla ya gharama za mradi kuwa **Shilingi 593,465,800**.

b) Mradi wa Ujenzi wa Shule mpya ya kata katika Kata ya Kapalala

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ilipokea **Shilingi Milioni 470** za mradi wa SEQUIP ambapo mradi huo haujakamilika kwa ukamilifu wake. Makisio ya gharama ya ukamiliishaji wa jengo hilo kwa mujibu wa Taarifa ya CAG ni **Shilingi 9,265,000**.

Katika mradi huo, ujenzi wa maabara za fizikia, kemia na baiolojia zipo katika hatua za umaliziaji na zinahitaji **Shilingi 58,634,760** ili kukamilika. Licha ya kuwa muda wa ukamiishaji wa mradi huo kuisha tarehe 07/04/2022 bado kuna kazi ambazo hazijakamilika.

c) Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Afya Ugalla

Mheshimiwa Spika, Serikali Kuu ilipeleka **Shilingi Milioni 500** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Ukaguzi huo ulianza kutekelezwa tarehe 10/02/2022 na kutarajiwa kukamilika tarehe 10/05/2022. Hadi kuwasilishwa kwa taarifa ya mradi mbele ya Kamati, kiasi chote cha fedha kimekwishatumika na mradi haujakamilika.

Jengo la wagonjwa wa nje (OPD) limeanza kutumika lakini kuna baadhi ya kazi zenye makadirio ya **Shilingi 12,602,000** hazijafanyika. Majengo mengine ambayo hayajakamilika ni pamoja na jengo la maabara ambalo lipo katika hatua za umaliziaji na linahitaji **Shilingi 19,418,800** ili kulikamilisha.

Mheshimiwa Spika, jengo la upasuaji ni miongoni mwa majengo ambayo utekelezaji wake haujakamilika ambapo, Ili kukamilisha kazi zilizobaki, makisio ya gharama ni **Shilingi 40,354,800**. Jumla ya nyongeza yote ni **Shilingi 72,375,600**.

d) Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya

Mheshimwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Halmashauri ilipokea na kutumia **Shilingi 616,000,000** kutoka Serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa majengo 13 ambapo miradi iliyokamilika na kutumika ni majengo 7, majengo 6 hayajakamilika na jengo moja na kuhifadhia maiti limekamilika lakini halitumiki kutokana na kutokuwepo kwa jokofu.

Mheshimiwa Spika, tangu kuanza utekelezaji wake, mradi umekwishatumia jumla ya **Shilingi 2,100,000,000**. Hata hivyo, bado sehemu kubwa ya mradi haijakamilika. Majengo ambayo hayajakamilika ni jengo la utawala ambalo ili likamilike kikamilifu makadirio ya Halmashauri ni **Shilingi 92,850,460**. Vile vile, ujenzi wa wodi ya wazazi haujakamilika ambapo, gharama ya makadirio ya kukamilisha mradi huo iliyowasilishwa na CAG ni **Shilingi 328,668,600**.

Mheshimiwa Spika, majengo mengine ambayo hayajakamilika ni jengo la dawa ambalo linahitaji **Shilingi 84,660,280** ili kukamilika, jengo la kufulia linahitaji **Shilingi 43,145,040** ili kukamilika na kichomea taka ambacho makadirio ya kukamilisha ujenzi ni **Shilingi 75,046,500**.

Mheshimiwa Spika, katika mradi huu, tathmini ya Kamati imebaini kuwa, gharama za mradi zimeongezeka kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na gharama zilizotolewa katika mwongozo wa ofisi ya Raisi – Tamisemi. Jumla ya gharama zinazotakiwa na Halmashauri ili kukamilisha mradi huu wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ni **Shilingi 660,189,110.00**.

2.3.8 Uchambuzi wa Taarifa ya miradi iliyotekelezwa kwa njia ya force account na Halmashauri ya Wilaya ya Mlele

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijadili na kuchambua taarifa ya miradi 7 kati ya miradi 88 yenye thamani ya **Shilingi 4,800,508,852** iliyotekelezwa na Halmashauri kwa kutumia njia ya force account. Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini mapungufu kadhaa katika baadhi ya miradi ifuatayo: -

a) Mradi wa Ujenzi wa majengo manne ya Hospitali ya Wilaya

Mheshimiwa Spika, katika mradi huu, Halmashauri ilikamilisha majengo ya upasuaji, wodi ya upasuaji wanaume na wanawake na yanatumika. Hata hivyo, jengo la kuhifadhia maiti halijaanza kutumika tangu kukamilika kwake miezi 12 iliyopita. Kutotumika kwa jengo hilo kunatokana na kukosekana kwa jokofu la kuhifadhia maiti lenye uwezo wa kuhifadhi miili 12 ambapo vifaa

vyote kwa ajili ya ukamilishaji vinavyotakiwa kupelekwa na Bohari Kuu ya Dawa (MSD) vinagharama ya **Shilingi 33,250,000**.

b) Mradi wa Ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje Zahanati ya Ilela

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huu ulifanyika kwa awamu na ulianza kutekelezwa tarehe 01 Machi, 2022 na kutakiwa kukamilika tarehe 30 Juni, 2022 ambapo, Halmashauri ilitumia mapato yake ya ndani ya **Shilingi Milioni 50**. Hata hivyo, umebainika kuwa na changamoto nyingi ikiwemo mradi kuanza kutekelezwa bila ya kuwepo mpango wa awali wa utekelezaji hali iliyochangia mradi kutokamilika kwa wakati na kusimama kwa muda wa miezi 18 kutokana na kukosekana kwa fedha.

Mradi huu ulianzishwa kwa fedha iliyozidi katika makusanyo ya ndani na kwa mujibu wa makisio ya gharama za kukamilisha mradi huo, Halmashauri imeeleza kuwa, **Shilingi 83,521,035** zinahitajika.

2.3.9 Uchambuzi wa Taarifa ya miradi iliyotekelezwa kwa njia ya force account na Halmashauri ya Manispaa ya Lindi

Mheshimiwa Spika, Halmashauri hii ina jumla ya **miradi 81** yenye thamani ya **Shilingi 8,136,719,000** inayotekelezwa kwa njia ya force account na Kamati iliweza kupokea taarifa ya **miradi 10** iliyofanyiwa uhakiki na CAG yenye thamani ya **Shilingi 5,270,000,000**.
Wakati wa uchambuzi wake, Kamati ilibaini mapungufu kadhaa na kuongezeka kwa gharama za ujenzi kwa kiasi kikubwa ambapo katika baadhi ya maeneo, Halmashauri ilishindwa kutoa maelezo kuhusu uthibitisho wa kuongezeka kwa gharama za mradi.

Mheshimiwa Spika, Mradi uliokutwa na changamoto kubwa ni mradi wa ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Lindi (Lindi Girls Grand High school). Shule hii ya Wasichana iliyopo kilangala inatarajiwa kuchukua wanafunzi kuanzia 1,000 hadi 1,080 na inatakiwa kutekelezwa katika awamu Mbili.
Kwa mujibu wa taarifa iliyowasilishwa na OR – TAMISEMI, awamu ya kwanza ya mradi ilitakiwa kutekelezwa na kukamilika kwa

gharama ya **Shilingi 3,000,000,000** kiasi ambacho, kilipokelewa na Halmashauri kutoka Serikali Kuu na Awamu ya Pili inatakiwa kutekelezwa kwa **Shilingi 1,100,000,000**.

Mheshimiwa Spika, katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi imekwishatumia **Shilingi 3,100,000,000** ambapo **Bilioni 3** ni kutoka Serikali Kuu na **Milioni 100** ni mapato ya ndani ya Halmashauri. Licha ya kufanyika kwa Matumizi ya **Shilingi Bilioni 3.1**, bado kuna majengo ambayo hayajakamilika.
Kulingana na taarifa iliyowasilishwa na CAG, Halmashauri imefanya makadirio ya gharama ya kukamilisha mradi huu kwa awamu ya kwanza inayofikia **Shilingi Bilioni 1.5** na kufanya jumla ya gharama zote kwa awamu ya kwanza kuwa **Shilingi Bilioni 4.6** badala ya **Shilingi Bilioni 3** zilizopangwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, tathimini ya jumla ya Kamati imebaini kuwa, gharama za mradi za nyongeza zilizoainishwa na Halmashauri ni **Asilimia 50** ya gharama za awali hali inayotia shaka ya uwepo wa thamani ya fedha ya mradi huu.

2.3.10 Uchambuzi wa Taarifa ya miradi iliyotekelezwa kwa njia ya force account na Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi kwa njia ya force account pia umefanyika kwa Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea kwa miradi ya jumla ya **Shilingi 5,607,318,452**. Katika fedha hizo, ipo miradi iliyokamilika na inayoendelea kutekelezwa.
Katika Ngazi ya Kamati, taarifa ya **miradi 7** yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 2.72** ilichambuliwa. Baada ya majadiliano ya kina, changamoto kadhaa zilizobainika katika baadhi ya miradi ni kama ifuatavyo: -

a) Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Afya cha Namatula

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huu umegharimu kiasi cha **Shilingi 580,045,747.29** ambapo, **Shilingi 2,500,000** ni michango ya wananchi, **Shilingi 77,545,747.29** na **Shilingi 500,000,000** kutoka Serikali Kuu.

Pamoja na kiasi tajwa hapo juu kutumika chote bado njia ya watembea kwa miguu na jengo la kufulia hayajakamilika na hivyo kuhitaji **Shilingi 11,002,500.00** kukamilisha mradi huo ambapo, itafanya gharama za jumla kuwa ni **Shilingi 591,048,247.29**.

b) Mradi wa Ujenzi wa Shule ya Sekondari Ngunichile

Mheshimiwa Spika, taarifa ilibainisha kuwa, Halmashauri ilikiuka taratibu za manunuzi kwa kufungua tenda na kumzawadia fundi siku hiyo hiyo bila ya kupitia mchakato wa tenda. Kwa mujibu wa Taarifa ya CAG, makadirio ya mradi yalikuwa ni **Shilingi 732,435,205** na kiasi cha **Shilingi 516,000,000** kimekwishatumika kati ya **Shilingi 527,100,000** kinachojumuisha fedha kutoka Serikali kuu **Shilingi 470,000,000**, mapato ya ndani **Shilingi 46,000,000** na mchango wa wananchi **Shilingi 11,100,000**.

Pamoja na kiasi cha **Shilingi Milioni 516** kutumika, bado kuna majengo ambayo hayajakamilika. Makadirio ya umaliziaji wa mradi huu yaliyoainishwa na mkaguzi ni **Shilingi 191,132,591**.

c) Mradi wa Ujenzi wa miundombinu katika Shule ya Sekondari ya Wavulana ya Rugwa

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ilitumia mapato yake ya ndani ya jumla ya **Shilingi 462,451,000** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo. Vile vile, mchango wa wananchi katika mradi huo ni **Shilingi 4,100,000** na kufanya jumla ya gharama za mradi kuwa **Shilingi 466,551,000**.

Mpaka kuwasilishwa kwa taarifa hii, kiasi cha **Shilingi 202,403,000** kilikwishatumika na kuwekewa makadirio ya **Shilingi 50,449,500** kwa ajili ya ukamilishaji wa majengo hayo na kufanya gharama kuongezeka hadi kufikia **Shilingi 252,852,500**.

Mheshimiwa Spika, katika miradi 7 ambayo taarifa zake ziliwasilishwa na kujadiliwa na Kamati, Halmashauri iliieleza Kamati kuwa, inahitaji **Shilingi 342,584,591** kukamilisha miradi ambayo haijakamilika. Ongezeko hilo la gharama ni sawa na **Asilimia 12.5** ya gharama za miradi yote 7 ya **Shilingi Bilioni 2.72**.

2.3.11 Uchambuzi wa Taarifa ya miradi iliyotekelezwa kwa njia ya force account na Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa

Mheshimiwa Spika, jumla ya miradi **157** yenye thamani ya **Shilingi 8,339,665,407.09** imetekelezwa na Halmashauri hadi kufikia juni, 2022 ambapo kati ya hiyo, miradi 8 yenye thamani ya **Shilingi 4,201,241,569** imehakikiwa na CAG na kuchambuliwa na Kamati.
Katika miradi hiyo 8, Kamati ilibaini mapungufu kadhaa wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo katika baadhi ya miradi ikiwa ni pamoja na: -

a) Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Afya Hotelitatu
Mheshimiwa Spika, Serikali Kuu ilipeleka jumla ya **Shilingi Milioni 500** kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la wagonjwa wa nje, maabara na kichomea taka **Shilingi Milioni 250** kwa awamu ya kwanza na ujenzi wa jengo la kufulia, jengo pacha la mama na mtoto na upasuaji kwa gharama ya **Shilingi Milioni 250** kwa awamu ya pili. Mradi huu ulioanza tarehe 30 Oktoba, 2021, ulitarajiwa kukamilika tarehe 10 Novemba, 2022.
Ujenzi wa awamu ya kwanza umekamilika kwa Asilimia 99 na Halmashauri iliongeza **Shilingi Milioni 32** kutoka katika mapato yake ya ndani ambapo gharama zilizotumika kumlipa fundi ujenzi ni **Shilingi Milioni 43**.

Mheshimiwa Spika, Awamu ya pili ya mradi haijakamilika ambapo, jengo pacha la mama na mtoto na jengo la upasuaji limefikia **Asilimia 73** ya ujenzi na ujenzi wa jengo la kufulia haujaanza. Katika ukaguzi uliofanywa na CAG katika mradi huo, ilibainika uwepo wa nyufa kwenye baadhi ya majengo ya kituo wakati ujenzi haujakamilika. Ili kukamilisha mradi huu, Halmashauri imekadiria kutumia fedha za ziada kwa kiasi cha **Shilingi 150,745,315**.

b) Mradi wa Ujenzi wa Shule mpya ya Sekondari katika Kitongoji cha Ngome
Mheshimiwa Spika, mradi mwingine ambao umebainika kuwa na mapungufu ni katika ujenzi wa Shule iliyopo Ngome kwa kutumia fedha za mradi wa SEQUIP **Shilingi Milioni 470**. Jumla ya **Shilingi 502,500,000** zilitumika ambapo kuna nyongeza ya **Shilingi 32,500,000** kutoka katika mapato ya ndani. Kamati ilielezwa kuwa,

bado kuna kiasi cha **Shilingi 146,196,193.5** ili kukamilisha mradi huu.

c) Mradi wa Ujenzi wa Stendi ya Mabasi Nangurukulu

Mheshimiwa Spika, Halmashauri imetumia **Shilingi 701,628,998** kwa ajili ya ujenzi wa stendi ya mabasi awamu ya kwanza. Fedha hizo zimetumika kulipa fidia kwa wananchi **Shilingi 139,555,029.12** na kiasi cha **Shilingi 562,073,969.98** kimetumika kuchimba eneo la ujenzi, kuweka kifusi kwa awamu ya kwanza, kujenga kibanda cha mlinzi, kujenga matundu 10 ya choo, kujenga jengo la abiria na kuchonga barabara inayoruhusu magari ya liwale kuingia.
Utekelezaji wa mradi huo ulianza mwaka wa fedha 2019/2020 lakini hadi kuwasilishwa kwa taarifa hii haujakamilika. Aidha Halmashauri imefanya makisio ya **Shilingi Milioni 100** kukamilisha awamu hiyo ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, Licha ya kiasi kikubwa cha fedha kutumika katika mradi huo, njia ya kwenda kwenye vyoo vya stendi haijatengenezwa na haiwezi kupitika katika kipindi cha mvua.
Aidha, wakati CAG akiwa anafanya uhakiki wa utekelezaji wa mradi huu, nyaraka zinazohusiana na mradi wa stendi hazikuwasilishwa kwa mkaguzi ikijumuisha faili la ujenzi wa mradi na hivyo CAG kushindwa kufanya tathmini ya mwenendo mzima wa mradi ikiwemo taratibu za manunuzi.

2.3.12 Uchambuzi wa Taarifa ya miradi iliyotekelezwa kwa njia ya force account na Halmashauri ya Wilaya ya Newala

Mheshimiwa Spika, jumla ya **Shilingi 5,164,478,837.22** imetumika kutekeleza miradi **98** kwa njia ya force account. Katika miradi hiyo, ipo iliyokamilika na inayoendelea kutekelezwa. CAG amefanya uhakiki wa miradi 7 yenye thamani ya **Shilingi 2,526,650,437** na taarifa yake imefanyiwa uchambuzi na Kamati.
Katika uchambuzi wa taarifa hizo, Kamati ilibaini changamoto na mapungufu kadhaa katika baadhi ya miradi ifuatayo: -

a) Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Utawala

Mheshimiwa Spika, Fedha za utekelezaji wa mradi huu ziliingia kwa awamu tatu ambapo, kwa mwaka 2020/2021 Halmashauri

ilipokea **Shilingi Bilioni 1**, mwaka 2021/2022 **Shilingi Bilioni 1** na mwaka 2022/2023 **Shilingi Milioni 750**.
Uchambuzi wa kina wa taarifa ya mradi huu umebaini kuwa, kiasi cha **Shilingi 2,630,222,146** kimekwishatumika na mradi upo katika hatua za umaliziaji. Aidha, kiasi cha **Shilingi 615,500,000** kimelipwa kwa Mhandisi mjenzi na kiasi cha **Shilingi 71,272,000** kimelipwa kwa Mhandisi Mshauri na kufanya gharama za ufundi kuwa **Shilingi 686,772,000** kati ya kiasi chote cha gharama ya mradi ambayo ni sawa na **Asilimia 24.97** ya **Shilingi Bilioni 2.75**.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huu umetumia utaratibu wa force account na mkandarasi kinyume na mwongozo uliotolewa na OR – TAMISEMI. Aidha, kiasi kilicholipwa kwa Mhandisi Mshauri ni kikubwa kinyume na mwongozo unaotaka Mhandisi Mshauri kulipwa **Shilingi Milioni 20** lakini Halmashauri ya Wilaya ya Newala ililipa **Shilingi Milioni 71**.
Pamoja na hayo Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Newala aliitaarifu Kamati kuwa, ujenzi wa uzio, mandhari (land scaping), kituo cha umeme na kibanda cha mlinzi havikuwepo katika mwongozo wa Serikali kinyume na maelekezo ya Serikali ambayo miradi yote ilitakiwa kukamilika kwa **Shilingi 2,750,000,000**.

b) Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Mchemo

Mheshimiwa Spika, mradi huu ulioanza kutekelezwa tarehe 22 Julai, 2021 ulitarajiwa kukamilika tarehe 21 Julai, 2022 kwa makisio ya gharama ya **Shilingi 2,975,363,542**. Hadi kufikia mwezi Juni, 2022, kiasi cha **Shilingi 2,473,728,289** kimekwishatumika kati ya kiasi cha **Shilingi 2,550,000,000** kilichopokelewa kutoka Serikali Kuu lakini bado kuna majengo ambayo ujenzi wake haujakamilika.

c) Mradi wa Ujenzi wa Shule ya Sekondari Nakahako

Mheshimiwa Spika, mradi huu ulipokea **Shilingi Milioni 470** za SEQUIP, na ulianza tarehe 20 Februari, 2022 na kutakiwa kukamilika tarehe 20 Juni, 2022 ambapo, hadi taarifa inawasilishwa mbele ya Kamati, mradi huu ulikuwa haujakamilika na zinahitajika fedha za ziada za **Shilingi 159,727,000** kwa ajili ya ukamilishaji.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wa miradi katika Halmashauri ya Wilaya ya Newala kutokana na utendaji usioridhisha wa wataalamu waliopewa dhamana ya kusimamia miradi hiyo hali iliyosababisha miradi kutokamilika na ongezeko kubwa la gharama za utekelezaji wa miradi hiyo.

2.3.13 Uchambuzi wa Taarifa ya miradi iliyotekelezwa kwa njia ya force account na Halmashauri ya Mji Masasi

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Mji Masasi imetekeleza miradi **49** yenye thamani ya **Shilingi 3,463,654,057.** Aidha ukaguzi umehakiki miradi 7 yenye thamani ya **Shilingi 2,609,411,100**. kati ya miradi 49 iliyotekelezwa kwa njia ya force account.

Mheshimiwa Spika, mradi ambao ulibainika kuwa na mapungufu mengi ni mradi wa ujenzi wa shule mpya ya sekondari Temeke Masasi ambapo, Halmashauri ilitumia jumla ya **Shilingi 535,000,000** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu ambapo **Shilingi Milioni 470** ni kutoka Serikali Kuu na **Shilingi Milioni 65** ni mapato ya ndani. Pamoja na kiasi hicho chote kutumika, mradi bado haujakamilika na zinahitajika fedha ya ziada kiasi cha **Shilingi 37,000,000** ili kuweza kukamilisha kazi zilizobakia.

2.3.14 Uchambuzi wa Taarifa ya miradi iliyotekelezwa kwa njia ya force account na Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba (Kilombero)

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba imetekeleza jumla ya miradi **81** yenye thamani ya **Sh.6,265,930,749.26.** Kwa upande wa uchambuzi, Kamati imepitia na kuchambua taarifa ya miradi 7 yenye thamani ya **Shilingi 5,255,702,332** ambapo hadi kipindi Kamati inapokea taarifa ya miradi hii, kiasi cha **Sh.4,732,478,691** kilishatumika. Aidha, katika uchambuzi wa miradi, Kamati imebaini mapungufu kama ifuatavyo: -

a) Mradi wa Ujenzi wa Shule ya Sekondari Ihenga

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza mradi huu, Halmashauri ilipokea kiasi cha **Shilingi Milioni 470** kutoka Serikali Kuu za mradi wa SEQUIP. Utekelezaji ulianza tarehe 03/09/2022 na ulitarajiwa

kukamilika tarehe 02/12/2022. Hadi kuwasilishwa kwa taarifa hii, kiasi chote cha fedha kilichotolewa kimeshatumika lakini mradi haujakamilika. Makisio ya gharama za umaliziaji wa mradi huo ni **Shilingi 139,047425**.

b) Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Afya Chita

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa mradi huu, Halmashauri ilitenga na kutumia **Shilingi 305,702,332** kutoka kwenye mapato yake ya ndani kwa ajili ya ujenzi wa kituo hiko ambapo, utekelezaji ulianza tarehe 15/08/2021 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 27/06/2022. Aidha, mradi huu haujakamilika na makisio ya gharama za umaliziaji ni **Shilingi 72,282,675**.

2.3.15 Uchambuzi wa Taarifa ya miradi iliyotekelezwa kwa njia ya force account na Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga

Mheshimiwa Spika, jumla ya **miradi 86** yenye thamani ya **Shilingi 11,255,893,170** ilitekelezwa na Halmashauri hii kwa kutumia njia ya force account. Changamoto kubwa ni miradi mingi kutekelezwa bila ya usimamizi wa kitaalamu ambapo kati ya miradi 7 yenye thamani ya **Shilingi 4,110,000,000** iliyojadiliwa na Kamati, changamoto iliyobainika ni katika mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Shule ya Sekondari Msogezi.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya wilaya ya Ulanga ilipokea kiasi cha **Shilingi Milioni 470** kutoka Serikali Kuu za mradi wa SEQUIP kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya Shule ya Sekondari Msogezi. Hadi kuwasilishwa kwa taarifa hii, fedha yote imekwishatumika na mradi huo haujakamilika. Aidha, kiasi cha **Shilingi 160,000,000** kinahitajika ili kukamilisha mradi huo.

2.3.16 Uchambuzi wa Taarifa ya miradi iliyotekelezwa kwa njia ya force account na Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi

Mheshimiwa Spika, Halmashauri imetekeleza jumla ya **miradi 44** yenye thamani ya **Shilingi 3,498,845,397**. Aidha, Kamati imepitia na kuchambua taarifa ya miradi 7 yenye thamani ya **Shilingi 1,681,468,866**. Mapungufu yaliyobainika na Kamati kwa baadhi ya miradi ni kama ifuatavyo: -

a) Mradi wa ukamilishaji wa majengo matano katika hospitali ya Wilaya ya Malinyi

Mheshimiwa Spika, mradi huu ulianza tangu mwaka wa fedha 2019/2020 ambapo, Halmashauri ilipokea fedha kutoka Serikali Kuu na kutumia jumla ya **Shilingi Bilioni 1.8** kwa ajili ya ujenzi wa majengo 7 ya hospitali. Hata hivyo, Halmashauri ilitumia fedha hizo kukamilisha majengo Mawili pekee na kuacha majengo mengine Matano yakiwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Halmashauri imetumia **Shilingi Milioni 561** kutoka katika mapato ya ndani kwa ajili ya ukamilishaji wa majengo hayo matano. Aidha, mradi huo umejengwa katika eneo oevu ambalo kiutaratibu mradi haukupaswa kutekelezwa katika eneo hilo.

b) Mradi wa Ujenzi wa Shule ya Sekondari Ndewele

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ilianza kutekeleza mradi huu tarehe 21 Machi, 2022 ambao ulitarajiwa kukamilika tarehe 15 Agosti, 2023. Utekelezaji wa mradi ulitokana na fedha za mradi wa SEQUIP za jumla ya **Shilingi Milioni 470**. Taarifa iliyowasilishwa ni kuwa, mradi huu unahitaji ziada ya **Shilingi 122,587,395** ili kuukamilisha.

2.3.17 Uchambuzi wa Taarifa ya miradi iliyotekelezwa kwa njia ya force account na Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero

Mheshimiwa Spika, jumla ya miradi **76** yenye thamani ya **Shilingi 4,953,613,162** imetekelezwa hadi kufikia Juni, 2022. Kamati imefanya uchambuzi wa miradi **7** kati ya hiyo yenye thamani ya jumla ya **Shilingi 2,839,160,995**. Changamoto zilizobainika katika baadhi ya miradi ni kama ifuatavyo: -

a) Mradi wa ujenzi wa shule ya Sekondari ya Homboza

Mheshimiwa Spika, kiasi cha **Shilingi Milioni 470** cha mradi wa SEQUIP kilipokelewa na kutumiwa kwa ajili ya mradi huu. Aidha, mradi huu haujakamiilika na unahitaji fedha ya ziada ya jumla ya **Shilingi Milioni 241** ili kuweza kukamilisha kazi zilizobaki.

b) Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Afya Mziha

Mheshimiwa Spika, mradi huu ulioanza kujengwa tarehe 21/5/2022 na kukamilika tarehe 22/9/2023 bado haujaanza kutumika hadi sasa. Mradi huu uliotumia jumla ya **Shilingi Milioni 500** unakosa thamani ya fedha iliyowekezwa katika ujenzi wa kituo hicho kutokana na kutokuwepo kwa vifaa tiba, kutounganishwa kwa maji na kutokuwa na mradi wowote wa umeme katika Kijiji cha Msiha.

2.3.18 Uchambuzi wa Taarifa ya miradi iliyotekelezwa kwa njia ya force account na Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Mwezi Juni, 2022, Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo ilitumia njia ya force account kutekeleza jumla ya **miradi 143** yenye thamani ya **Shilingi 7,789,472,420.91**. Aidha, Kamati ilichambua taarifa ya miradi 7 kati ya hiyo yenye thamani ya jumla ya **Shilingi 5,090,000,000**. Kamati ilibaini changamoto zifuatazo: -

a) Mradi wa ujenzi wa shule ya sekondari ya Daktari Samia Suluhu Hassani

Mheshimiwa Spika, jumla ya **Shilingi 2,915,857,748** zilitumika kwa ajili ya utekelezaji huu ambapo, **Shilingi Bilioni 3** kutoka Serikali Kuu zilipokelewa. Hata hivyo, bado mradi huo haujakamilika na unahitaji fedha zaidi ya **Shilingi 784,861,150** kuweza kukamilisha kazi zilizotakiwa kukamilika kwa **Shilingi Bilioni 3**.

b) Mradi wa ujenzi wa shule Mpya ya Sekondari ya Msisima

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ilipokea **Shilingi Milioni 470** za mradi wa SEQUIP kwa ajili ya ujenzi wa shule ya sekondari ya Msisima. Kiasi hicho cha fedha kimetumika na mradi haujakamilika na kuhitajika kiasi cha **Shilingi 100,034,223** ili kuweza kukamilisha kazi zilizobakia.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo imekuwa na utekelezaji usiofaa wa miradi ya force account kutokana na miradi mingi kufanyika bila ya usimamizi, miradi kutokuwa na ubora na miradi kutokamilika kwa wakati uliopangwa. Vile vile, Kamati haikupatiwa mchanganuo wa gharama za miradi na sababu ya ongezeko la gharama za miradi

hiyo. Aidha, wakati wa ukaguzi, Mkaguzi hakupatiwa BOQ kwa ajili ya ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto na mapungufu yaliyobainishwa na Kamati katika utekelezaji wa miradi kwa kutumia njia ya force account, Kamati imebaini kuwa, kutozingatiwa kwa Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali ya Serikali, kwa kiasi kikubwa kumechangia utekelezaji wa miradi mbalimbali kuwa ni chini ya kiwango. Hali hiyo imetokana na ukweli kwamba, zipo baadhi ya Halmashauri ambazo zimefanya vizuri katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kutumia njia ya force account ambapo, miradi hiyo imekamilika na inatumika kama ilivyotarajiwa. Tafsiri ya haraka ya Kamati ni kwamba, iwapo Halmashauri zote zitazingatia Sheria na miongozo iliyowekwa miradi mingi itatekelezwa kwa ufanisi na italeta tija.

2.3 Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, ili kutathimini thamani ya fedha iliyotumika katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Mwezi Machi, 2023 Kamati ilipata fursa ya kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na Halmashauri zilizopo katika mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Mtwara, Ruvuma, Rukwa, Katavi, Tabora na Songwe.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi uliofanyika kwa baadhi ya Halmashauri zilizopo katika mikoa tajwa hapo juu ulijumuisha miradi ya Afya, Elimu, vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, ghala la kuhifadhia nafaka, na miradi ya majengo ya ofisi za Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha miradi inayotekelezwa katika Halmashauri inaleta tija iliyokusudiwa, Taarifa ya miradi hiyo na dosari zilizobainika ni kama ifuatavyo: -

a) Miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa huu, Kamati ilifanikiwa kukagua miradi inayotekelezwa katika Manispaa za Ubungo na Kigamboni.

Katika Manispaa ya Ubungo, Kamati ilibaini changamoto za uendeshaji wa Soko la Mabibo ambapo Ofisi ya Raisi TAMISEMI ilielekezwa kuhakikisha michakato ya umiliki wa eneo na uendeshaji wa Soko hilo inakamilika haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni, Kamati ilifanya ukaguzi katika miradi mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujenzi wa vyumba 12 vya madarasa katika shule mbalimbali za msingi kwa gharama ya **Shilingi Milioni 20**, Ukarabati wa madarasa 12 katika shule mbalimbali za msingi kwa gharama ya **Shilingi Milioni 4.6** kwa kila chumba, ujenzi wa shule mpya ya Msingi ya Gezaulole kwa gharama ya **Shilingi Milioni 334.4**.

Miradi mingine iliyokaguliwa ni pamoja na ujenzi wa Jengo la Ghorofa Tatu lenye vyumba 16 vya madarasa kwa ajili ya shule mpya ya Sekondari ya Paulo Makonda ambapo mradi huu unategemea kukamilishwa kwa gharama ya **Shilingi Milioni 950**. Hadi Kamati ilivyofanya ukaguzi, kiasi cha **Shilingi Milioni 454** kilikwishatumika na ujenzi ulifikia **Asilimia 45**. Vile vile, Kamati ilikagua mradi wa ukarabati wa vyumba 13 vya madarasa katika shule mbalimbali za Sekondari kwa gharama ya jumla ya **Shilingi Milioni 95**, na mradi wa ujenzi wa uzio wa Shule ya Sekondari ya Nguva kwa gharama ya **Shilingi Milioni 25**.

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya Afya, Kamati ilikagua maendeleo ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kibada kinachotegemewa kuwa na jumla ya majengo Tisa yanayoendelea kujengwa kwa awamu. Awamu ya kwanza ilikamilisha ujenzi wa Jengo la wagonjwa wa nje (OPD), jengo la upasuaji, wodi ya wazazi, jengo la kufulia na choo cha nje kwa gharama ya **Shilingi Milioni 598.2**. Mradi huu umetekelezwa na Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, Changamoto kubwa iliyobainika na Kamati katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni ni Manispaa kushindwa kutoa maelezo ya kina kuhusu uzingatiaji wa utoaji wa fedha za mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, mwenendo wa marejesho kutoka kwa wakopaji na kushindwa kubainisha vikundi vya wanufaika tangu mwaka 2018/2019-2020/21.

b) Miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri za Mkoa wa Lindi

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi iliyotekeleza na Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea. Miradi iliyokaguliwa ni pamoja na upanuzi wa miundombinu ya kituo cha afya cha Naipanga chenye wodi ya mama na mtoto, nyumba Tatu za watumishi, maabara, jengo la kufulia, jengo la kuhifadhia maiti, njia unganishi za watembea kwa miguu kati ya jengo moja na jingine kwa gharama ya jumla ya **Shilingi Milioni 429.02**. Aidha, changamoto iliyobainika katika mradi huu ni ya upungufu wa watumishi ambapo hadi ukaguzi unafanyika, kituo kilikuwa na watumishi 17 tu kati ya watumishi 38 wanaohitajika.

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtama, Kamati ilifanya ukaguzi katika miradi mitatu ambayo ni Hospitali ya Wilaya ya Mtama, Zahati ya Chiodya na Ujenzi wa Jengo la Utawala la Halmashauri.

Katika utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Mtama, mradi huu ulianza mwaka 2019 ambapo, Kati ya mwaka wa fedha 2019/20 hadi mwaka 2021/22, mradi ulipokea ruzuku ya Serikali Kuu kiasi cha **Shilingi Bilioni 3.7**. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Mradi ulipokea ruzuku ya Serikali Kuu kiasi cha **Shilingi Milioni 500**. Kamati haikuridhishwa na ubora wa mradi huo kutokana na kuwepo kwa viashiria vya kukosekana kwa thamani ya fedha.

Kuhusu mradi wa ujenzi wa jengo la ofisi za utawala katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtama, Kamati haikuridhishwa na mwenendo wa utekelezaji wa mradi huo kwa kuwa, Mkataba wa ujenzi ulisainiwa mwezi Oktoba, 2021 kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Mtama na Mkandarasi *Suma JKT Construction*

Company Ltd ambapo, kwa mujibu wa Mkataba, Mradi ulitegemewa kukamilika mwezi Novemba, 2022. Hata hivyo hadi kufanyika kwa ziara ya Kamati mwezi Machi, 2023, Jengo hilo lilikuwa halijakamilika licha ya mradi huo kupokea ruzuku ya Serikali Kuu ya jumla ya **Shilingi Bilioni 3.7**.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 23 Machi, 2023, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri ya Manispaa ya Lindi. Miradi iliyokaguliwa ni pamoja na miradi ya sekta ya afya na elimu. Changamoto kubwa iliyobainika na Kamati ni miradi kutokamilika kwa wakati na kutelekezwa kwa muda mrefu ambapo, katika shule ya msingi Mitwero, Kamati ilibaini uwepo wa nyumba ya mwalimu yenye vyumba vitatu vya kulala iliyoishia ngazi ya kupaua tangu mwaka 2004.

Vile vile, Katika shule ya Sekondari ya Mingoyo kuna nyumba tatu za walimu zilizotelekezwa kwa muda mrefu na hazifai tena kutumika kama makazi. Aidha, ukaguzi wa Kamati ulibaini uwepo wa madarasa mawili yaliyotelekezwa kwa muda mrefu na kuchakaa katika shule ya msingi Msinjahili ambapo, ukarabati wa madarasa hayo utaigharimu Serikali fedha nyingi.

c) Miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri za Mkoa wa Mtwara

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha tarehe 27 hadi 30 Machi, 2023, Kamati ilifanya ziara katika Halmashauri za Wilaya ya Masasi, Mji wa Nanyamba na Manispaa ya Mtwara. Miradi iliyokaguliwa katika Halmashauri hizo ni ya sekta ya elimu, afya pamoja na miradi ya majengo ya utawala.

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, Kamati ilifanikiwa kufanya ukaguzi katika miradi mitano ambayo ni mradi wa ujenzi wa shule ya sekondari Mpeta iliyogharimu kiasi cha **Shilingi Bilioni 1**, mradi wa ujenzi wa Ghala la kuhifadhia nafaka lililojengwa katika Kata ya Chiungutwa ambalo lilikadiriwa kugharimu kiasi cha **Shilingi Bilioni 1.8**, mradi wa ujenzi wa nyumba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri iliyotarajiwa kugharimu kiasi cha **Shilingi Milioni 150**, mradi wa ujenzi wa jengo la Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Masasi lililokadiriwa kugharimu kiasi cha **Shilingi Bilioni 2.8** na Mradi wa Hospitali ya Wilaya ambao, pamoja na gharama

zingine, katika mwaka wa fedha 2020/21 ulitumia kiasi cha **Shilingi Milioni 440** cha mapato ya ndani.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa iliyobainika katika utekelezaji wa miradi hiyo ni miradi kuchelewa kukamilika kwa wakati hali iliyosababishwa na usimamizi usiofaa wa miradi hiyo, uhaba wa watumishi wa kada ya Uhandisi, kutowalipa wakandarasi madai yao kwa wakati pamoja na kutozingatiwa kwa Miongozo ya ujenzi iliyotolewa na Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Mtwara, Kamati pia ilifanya ziara ya ukaguzi wa miradi katika Halmashauri ya Mji wa Nanyamba ambapo, Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Nanyamba tangu kuanza kwa mradi mwaka 2018 hadi hatua iliyofikiwa kipindi cha ukaguzi. Ujenzi wa mradi huo ambao hadi kipindi cha ziara ya Kamati uligharimu jumla ya **Shilingi Bilioni 3.1** ulikuwa ukisimamiwa na mwalimu ambaye si mhandisi.

Katika Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara, Kamati ilifanya ukaguzi wa ufanisi katika matumizi ya **Shilingi Milioni 776.6** zilizotolewa na Serikali Kuu kwa ajili ya kukarabati shule kongwe ya Wasichana ya Mtwara (Mtwara Girls Secondary School).

Katika mradi huu, Fedha zilizotolewa zilitumika kugharamia shughuli mbalimbali kama vile kubadilisha sakafu za majengo 38, kubadilisha milango ya baadhi ya majengo, kuweka paa jipya kwa baadhi ya majengo, kutandaza upya mfumo wa umeme darini na ardhini, kukarabati vyoo, maliwato na mifumo ya maji taka, kuweka mifumo mipya ya majiko ya gesi kwa ajili ya kupikia chakula cha wanafunzi na kuanza ujenzi wa mabweni mapya mawili ambayo ujenzi wake umefikia zaidi ya Asilimia 60.

d) Miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri za Mkoa wa Rukwa

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Rukwa, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri za Wilaya za Sumbawanga, Kalambo na Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga. Miradi iliyokaguliwa na Kamati katika Halmashauri hizo ni miradi ya Sekta ya Afya, Elimu na Maji.

Baada ya ziara ya ukaguzi wa miradi katika Halmashauri hizo, changamoto zilizobainika na Kamati ni miradi mingi kutokamilika kwa wakati, Halmashauri kushindwa kutenga fedha zinazotokana na mapato ya ndani kwa ajili ya utekelzaji wa miradi, kutozingatiwa kwa Miongozo ya ujenzi inayotolewa na Serikali Kuu, kutokamilika kwa mifumo ya maji taka na maji safi katika majengo ya hospitali pamoja na kukosekana kwa mifumo ya umeme katika baadhi ya shule za msingi na sekondari.

e) Miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri za Mkoa wa Katavi

Mheshimiwa Spika, ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo katika Mkoa wa Katavi ilifanyika katika Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda, Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda/Tanganyika na Halmashauri ya Wilaya ya Mlele. Wakati wa ukaguzi wa miradi ya sekta ya afya na elimu iliyotekelezwa na Halmashauri hizo, Changamoto kadhaa zilibainika ikiwa ni pamoja na kutounganishwa kwa mifumo ya umeme na maji katika vituo vya afya na shule za sekondari, Halmashauri kutotenga fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi, kutokamilika kwa wakati kwa miradi ya ujenzi wa wodi za wanawake, wanaume na watoto, ujenzi wa tofali zilizo na kiwango chini ya ubora zilizotengenezwa kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Mlele na kukosekana kwa vifaa tiba katika vituo vya afya na hospitali za wilaya.

f) Miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri za Mkoa wa Tabora

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo katika maeneo mengine, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri ya Manispaa ya Tabora na Halmashauri ya Wilaya ya Uyui zilizopo katika Mkoa wa Tabora. Ukaguzi wa Kamati ulifanyika katika miradi ya sekta ya elimu na sekta ya afya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya ukaguzi katika miradi ya Halmashauri hizo mbili, Kamati ilibaini changamoto kadhaa katika utekelezaji wa miradi hiyo. Changamoto zilizobainika ni pamoja na kutokamilika kwa mifumo ya umeme, mifumo ya majitaka na maji safi na matundu ya vyoo katika vituo vya Afya pamoja na

shule za msingi na sekondari pamoja na miradi ya ujenzi wa shule za sekondari, bwalo la shule na vituo vya afya kutokamilika kwa wakati uliopangwa.

g) Miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri za Mkoa wa Songwe

Mheshimiwa Spika, ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo ilifanyika katika Halmashauri ya Mji Tunduma ambapo Kamati ilikagua miradi ya sekta ya afya na elimu. Wakati wa ziara hiyo, Kamati ilibaini uwepo wa miradi ambayo haijakamilika kwa muda mrefu kama ilivyo kwa mradi wa ujenzi wa Kituo cha Afya cha Mpemba kilichoanza kujengwa toka mwaka 2016/2017 lakini hadi wakati wa ukaguzi mradi huo haujakamilika.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine iliyobainika na Kamati wakati wa ukaguzi ni usimamizi hafifu na usioridhisha wa miradi katika ujenzi wa shule ya Sekondari Tunduma hali iliyosababisha baadhi ya kazi kama kichomea taka na jiko kushindwa kukamilika kwa wakati, ujenzi wa shule ya Mchepuo wa Kiingereza kushindwa kukamilika kwa wakati na ukiukwaji wa miongozo ya ujenzi inayotolewa na Serikali.

2.4 Mafunzo na Semina kwa Kamati

Naomba nitoe shukurani zangu za dhati kwako kwa kuridhia Kamati ya LAAC kupatiwa mafunzo na semina mbalimbali kwa ajili ya kuongeza uelewa, stadi za uchambuzi wa Taarifa, ufanisi na uwezo wa wajumbe katika kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, napenda kuishukuru Ofisi ya Katibu wa Bunge kwa kufanya uratibu na kuwezesha kufanyika kwa shughuli hizo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia mwezi Februari, 2023 hadi mwezi Februari, 2024, Kamati ilipata jumla ya mafunzo na semina Kumi na Moja (11). Mafunzo na Semina hizo yalitolewa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, OR – TAMISEMI, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma pamoja na Asasi za Kiraia zinazoangalia matumizi ya fedha za umma. Maeneo yaliyowekewa msisitizo katika mafunzo na Semina hizo ni yafuatayo; -

i. Uchambuzi wa Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;
ii. Uelewa kuhusu kaguzi mbalimbali zinazofanywa na CAG katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
iii. Uelewa kuhusu hati mbalimbali za ukaguzi zinazotolewa na CAG;
iv. Uelewa kuhusu Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura 290;
v. Uelewa kuhusu Sheria ya Ukaguzi wa Umma Sura 418;
vi. Uelewa kuhusu Mwongozo wa usimamizi wa mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019;
vii. Uelewa kuhusu Kanuni za utoaji na usimamizi wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu, 2019;
viii. Uelewa kuhusu Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410;
ix. Uelewa kuhusu Mfumo wa Kisheria wa matumizi ya *Force Account*;
x. Nafasi ya Mkaguzi wa ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; na
xi. Uelewa kuhusu uwazi na uwajibikaji katika kusimamia matumizi ya fedha za umma.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

3.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi wa kina wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022, Kamati ina maoni na mapendekezo kama ifuatavyo: -

3.2 Maoni ya Jumla

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati yanatokana na ukweli kwamba, Bunge ndio chombo mahususi cha kuhakikisha kunakuwa na matumizi sahihi ya fedha za Umma kwa niaba ya wananchi. Kwa muktadha huo, maoni ya Kamati ni pamoja na kuhakikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa njia ya force

account unazingatia Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu mbalimbali zilizowekwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zote nchini zimepatiwa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo hasa katika sekta ya afya na elimu ili kuboresha ustawi wa wananchi. Ili kuhakikisha dhamira hiyo ya Serikali inatekelezwa kikamilifu, Kamati ina maoni kuwa, Wakurugenzi wote wa Halmashauri kuhakikisha kiasi cha fedha kinachopelekwa kinatekeleza miradi kusudiwa kwa ubora, weledi na ufanisi wa hali ya juu na kuhakikisha kunafanyika ufuatiliaji wa mara kwa mara na tathimini ya miradi husika ili kuhakikisha kunakuwa na thamani ya fedha na tija kuweza kupatikana.

3.3 Mapendekezo

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Kamati yanatokana na changamoto na mapungufu yaliyoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mapendekezo hayo yanalenga kuondoa mapungufu yaliyobainika katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwa njia ya force account. Mapendekezo ya Kamati ni kama yafuatayo: -

3.3.1 Uwepo wa Ukomo wa gharama za miradi inayotekelezwa kwa kutumia Force account

KWA KUWA, uchambuzi wa jumla wa Kamati umebaini changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa miradi kwa njia ya force account ikiwa ni pamoja na kutokuwa na wataalamu na kukosekana kwa mafundi wenye utaalamu katika ujenzi wa majengo makubwa yanayohitaji utaalamu wa hali ya juu;

NA KWA KUWA, uwepo wa changamoto hizo umesababisha miradi mingi kutokuwa na ubora, kuongezeka kwa gharama na miradi kutokamilika kwa wakati;

KWA HIYO BASI; Bunge linaazimia kwamba, Serikali ifanye utafiti wa kina juu ya ukubwa wa miradi pamoja na gharama za miradi zinazopaswa kutumika katika utekelezaji wa miradi kwa kutumia njia ya force account. Aidha, Serikali (Wizara ya Fedha) ihakikishe

Kanuni ya Ununuzi wa umma itakayotokana na Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 10 ya Mwaka 2023 inajumuisha ukomo wa gharama ya mradi unayopaswa kutekelezwa kwa kutumia njia ya force account.

3.3.2 Gharama za Utekelezaji wa Miradi zisizoakisi uhalisia

KWA KUWA, Kamati imebaini kutojumuishwa kwa gharama za usimamizi na ufuatiliaji zinazotumika na Halmashauri wakati wa utekelezaji wa miradi kwa njia ya force account pamoja na fedha kutolewa kwa usawa kwa Mikoa yote bila ya kuzingatia uhalisia wa maeneo husika;

NA KWA KUWA, changamoto hiyo imepelekea kuongezeka kwa gharama za utekelezaji wa miradi hiyo ikilinganishwa na makisio ya gharama zilizoainishwa na Serikali katika orodha ya gharama ya vifaa vya ujenzi (BOQ) pamoja na kuzifanya Halmashauri kutumia mapato yake ya ndani kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji wa miradi husika;

KWA HIYO BASI, kwa miradi ambayo inatekelezwa kwa fedha kutoka Serikali kuu, Bunge linaazimia kwamba: -

a) Serikali ifanye tathimini ya kina juu ya gharama halisi zilizotumika katika kutekeleza miradi kwa kutumia njia ya force account na kubainisha iwapo lengo lililokusudiwa la kupunguza gharama limefikiwa;
b) Serikali ihakikishe gharama za usimamizi na ufuatiliaji wa miradi zinajumuishwa katika fedha zinazopelekwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya force account katika kila Halmashauri; na
c) Serikali ipeleke fedha za utekelezaji wa miradi ya force account kulingana na gharama halisi za maeneo husika.

3.3.3 Upungufu wa Wataalamu wa Kada ya Uhandisi, wakadiriaji majenzi na wasanifu majengo katika Halmashauri

KWA KUWA, kumebainika upungufu wa wataalamu wa ujenzi (wahandisi, wakadiriaji majenzi na wasanifu majengo) kinyume na Mwongozo wa utekelezaji wa miradi kwa njia ya force account

unaohitaji uwepo wa wataalamu ili kuhakikisha miradi inasimamiwa kwa weledi na kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa;

NA KWA KUWA, kukosekana kwa wataalamu hao kwa kiasi kikubwa kumechangia kuwa na miradi isiyo na ubora na tija pamoja na kuchelewa kukamilika kwa miradi kwa muda uliopangwa;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe inaongeza idadi ya wataalamu (wahandisi, wakadiriaji majenzi na wasanifu majengo) katika Halmashauri zote nchini zenye upungufu wa wataalamu hao ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa miradi na kuacha kuwatumia Walimu na Madaktari kama wasimamizi wa miradi ili waweze kutekeleza majukumu yao ya msingi na kutoa taarifa Bungeni juu ya utekelezaji wake.

3.3.4 Kutofanyika kwa Tathimini ya Mahitaji ya Miundombinu Muhimu kabla ya Utekelezaji wa Mradi

KWA KUWA, Halmashauri nyingi zimebainika kutekeleza miradi bila ya kufanya tathimini ya kina juu ya mahitaji ya miundombinu muhimu katika eneo la mradi kama miundombinu ya barabara, maji na umeme;

NA KWA KUWA, kutofanyika kwa tathimini hiyo kumesababisha kuongezeka kwa gharama mara kwa mara (variations) pamoja na huduma kushindwa kutolewa pindi mradi unapokamilika;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ifanye tathimini ya kina juu ya mahitaji ya miundombinu muhimu na kuhakikisha Mamlaka zinazohusika na uwekaji wa miundombinu ya barabara, maji na umeme zinashirikishwa kabla ya utekelezaji wa mradi katika maeneo yao.

3.3.5 Ubora usiokidhi vigezo wa Miradi inayotekelezwa kwa force account

KWA KUWA, ukaguzi umebaini kuwepo kwa viashiria vya miradi iliyotekelezwa kwa njia ya force account kutoishi kwa kipindi cha muda mrefu kama ilivyoainishwa katika Mwongozo wa usimamizi

wa mali za Serikali na marekebisho yake ya mwaka 2019 hali iliyosababishwa na kutopimwa kwa udongo wa eneo husika la mradi, kutumia vifaa visivyo na ubora na kutumia mafundi wasio na taaluma ya mradi husika;

NA KWA KUWA, changamoto hizo zitasababisha Serikali kutumia gharama kubwa kwa ajili ya matengenezo ya mara kwa mara ya miradi hiyo badala ya fedha hizo kuelekezwa katika maeneo mengine ya maendeleo;

NA KWA KUWA, Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo, Halmashauri ya Wilaya ya Newala na Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo zilibainika kuwa na mapungufu mengi zaidi na miradi mingi kukosa ubora ambapo watendaji wake walishindwa kutoa maelezo yaliyojitosheleza kuhusu mapungufu yaliyobainika hali iliyoipelekea Kamati kushindwa kuendelea na mahojiano;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba: -

a) Serikali ihakikishe kila Mkurugenzi anafuata taratibu za ujenzi kwa kutekeleza mambo yote muhimu kama upimaji wa udongo, tathimini ya mazingira, ununuzi wa vifaa vyenye ubora, kutumia mafundi wenye taaluma ya mradi husika na kuwachukulia hatua stahiki wote watakaokiuka taratibu hizo;
b) Serikali ifanye tathimini ya miradi iliyotekelezwa kwa kutumia force account na kukokotoa gharama za uchakavu wa miradi hiyo, kama ilivyoelezwa kwenye mwongozo wa usimamizi wa mali za Serikali pamoja na kuchukua hatua kwa watendaji wote watakaobainika kutekeleza miradi chini ya viwango;
c) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afanye ukaguzi wa kina juu ya ubora wa miradi iliyotekelezwa kwa kutumia njia ya force account kwa kuzingatia uhai wa mradi (economic life) kama ilivyoainishwa katika mwongozo wa usimamizi wa mali za Serikali; na
d) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afanye Ukaguzi wa kina kwa miradi yote yenye changamoto iliyotekelezwa kwa kutumia njia ya force account kwa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo, Halmashauri ya Wilaya

ya Newala na Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo kuanzia mwaka wa fedha 2019/2020 hadi 2021/22.

3.3.6 Kutozingatiwa kwa Hatua za Kitaalamu za Ujenzi

KWA KUWA, Ukaguzi uliofanywa na CAG katika miradi iliyotekelezwa kwa force account umebaini kuwa, miradi mingi imejengwa bila ya kuzingatia hatua za kitaalamu za ujenzi kama muda unaopaswa kutumika katika kila hatua ya ujenzi hali iliyotokana na uharaka wa kukamilisha miradi husika na kukimbiza kuwahi muda wa mwisho wa utekelezaji uliowekwa;

NA KWA KUWA, kukiukwa kwa hatua muhimu za ujenzi kumesababisha baadhi ya miradi kujengwa chini ya viwango na miradi mingine kutengeneza nyufa kabla ya kukamilika;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, OR – TAMISEMI kwa Kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa ihakikishe miradi yote inayotekelezwa katika Halmashauri inazingatia hatua zote za kitaalamu za ujenzi na kuchukua hatua kwa wataalamu watakaobainika kukiuka taratibu za ujenzi.

3.3.7 Ukiukwaji wa Mwongozo wa utekelezaji wa Miradi kwa Kutumia Njia ya Force account

KWA KUWA, imebainika kuwepo kwa ukiukwaji wa Mwongozo wa matumizi ya force account ikiwa ni pamoja na kutoundwa kwa Kamati (force account committees) au Kamati zilizoundwa kutofanya kazi iliyokusudiwa kutokana na Wakurugenzi wa Halmashauri kutozishirikisha katika mchakato mzima;

NA KWA KUWA, kukiukwa kwa Mwongozo huo kwa ujumla wake na kutofanya kazi kikamilifu kwa Kamati hizo kumesababisha miradi mingi kutofikia viwango vinavyotakiwa;

NA KWA KUWA, Halmashauri zote zilizofika mbele ya Kamati katika kipindi cha Januari, 2024 kwa namna moja au nyingine zimebainika kukiuka Mwongozo huo wa utekelezaji wa miradi kwa kutumia njia ya force account na kusababisha kukosekana kwa tija ya miradi hiyo;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali (OR –TAMISEMI na PPRA) ichukue hatua stahiki kwa watendaji wote waliokiuka Mwongozo wa utekelezaji wa miradi kwa njia ya force account (Guidline for Carrying out Works under Force Account 2020).

3.3.8 Ukiukwaji wa Miongozo inayotolewa na Ofisi ya Raisi TAMISEMI

KWA KUWA, imebainika uwepo wa baadhi ya Wakurugenzi wa Halmashauri kutofuata miongozo inayotolewa na OR – TAMISEMI katika utekelezaji wa miradi mbalimbali;

NA KWA KUWA, kutofuatwa kwa miongozo hiyo kumepelekea kuongezeka kwa gharama za utekelezaji wa miradi hiyo, miradi kutotekelezwa na kutokamilika kwa wakati na kusababisha Serikali kuingia gharama zaidi ya kiasi cha fedha kilichokusudiwa;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, OR - TAMISEMI ihakikishe inasimamia na kuchukua hatua dhidi ya watendaji watakaobainika kukiuka miongozo iliyotolewa.

3.3.9 Sekretarieti za Mikoa kutofuatilia Utekelezaji wa Miradi

KWA KUWA, imebainika kwamba, baadhi ya Sekretarieti za mikoa zimeshindwa kutekeleza jukumu lake la usimamizi na ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa katika Halmashauri zilizopo katika maeneo yao ya usimamizi;

NA KWA KUWA, kukosekana kwa usimamizi wa mkoa katika Halmshauri kumechangia kwa kiasi kikubwa kwa Wakurugenzi wa Halmashauri kutotekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo ya Nchi na kuzorotesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

a) Serikali ifanye tathimini ya utendaji kazi wa Ofisi ya Makatibu Tawala Mikoa katika kusimamia miradi yote ya maendeleo katika mikoa yao na kuchukua hatua stahiki kwa wale ambao watabainika kutotekeleza wajibu wao kikamilifu hasa katika eneo la kusimamia miradi yote ya maendeleo; na;

b) Sekretarieti za Mikoa zifanye ukaguzi wa miradi inayotekelezwa katika Halmashauri zao na kuwasilisha Taarifa hiyo OR – TAMISEMI katika kila robo mwaka.

3.3.10 Miradi kutokamilika kwa Wakati

KWA KUWA, miradi mingi iliyotekelezwa kwa njia ya force account imebainika kushindwa kukamilika kwa wakati uliopangwa;

NA KWA KUWA, kutokamilika kwa miradi hiyo kunakwamisha juhudi za Serikali za kutoa huduma bora kwa jamii pamoja na kukosekana kwa thamani ya fedha ya miradi hiyo;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, OR – TAMISEMI kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa kusimamia kikamilifu na kuhakikisha miradi yote iliyotekelezwa kwa kutumia njia ya force account ambayo haijakamilika inakamilika kabla ya kuanza kwa mwaka mpya wa fedha ili iweze kutoa huduma iliyokusudiwa.

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako thabiti ambao umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake kikamilifu katika kipindi cha mwaka mzima na kutoa miongozo mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli za Kamati. Aidha, napenda kumshukuru Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa ushirikiano wao kwa Kamati.

4.1 Shukurani

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kwa kutekeleza majukumu yao kwa weledi, ufanisi na uvumilivu wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo: -

1) Mhe. Halima James Mdee, Mb – Mwenyekiti

2) Mhe. Stanslaus Shing'oma Mabula, Mb -M/Mwenyekiti
3) Mhe. Ally Mpembenwe Twaha, Mb – Mjumbe
4) Mhe. Conchesta Leonce Rwamlaza, Mb – Mjumbe
5) Mhe. Ester Amos Bulaya, Mb – Mjumbe
6) Mhe. Issa Ally Mchungahela, Mb – Mjumbe
7) Mhe. Jeremiah Mrimi Amsabi, Mb – Mjumbe
8) Mhe. Jesca J. Msambatavangu, Mb – Mjumbe
9) Mhe. Munde Tambwe Abdallah, Mb – Mjumbe
10) Mhe. Lemburis Saputu Mollel, Mb – Mjumbe
11) Mhe. Suma Ikenda Fyandomo, Mb – Mjumbe
12) Mhe. Daimu Iddi Mpakate, Mb – Mjumbe
13) Mhe. Ally Juma Makoa, Mb – Mjumbe
14) Mhe. Hawa Mchafu Chakoma, Mb – Mjumbe
15) Mhe. Michael C. Mwakamo, Mb – Mjumbe
16) Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb – Mjumbe
17) Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mb – Mjumbe
18) Mhe. Idrissa Juma Abdul-Hafar, Mb – Mjumbe
19) Mhe. Abdul Yusuf Maalim, Mb – Mjumbe
20) Mhe. Mussa Omar Salim, Mb - Mjumbe

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Bi. Nenelwa Mwihambi, ndc. kwa ushauri wake kwa Kamati pamoja na wasaidizi wake wote kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kusomwa kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua na kuthamini ushirikiano mkubwa ilioupata kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) na kwa namna ya kipekee kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Ndugu Charles Kichere. Vile vile, napenda kuishukuru OR – TAMISEMI kwa ushirikiano walioutoa katika Kamati kwa kutoa ufafanuzi kila ilipohitajika kufanya hivyo. Mwisho japo sio kwa umuhimu napenda kuishukuru Wizara ya Fedha kwa kushiriki nasi katika vikao vya Kamati.

4.2 Hoja

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako sasa lipokee Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa na likubali Maoni na Mapendekezo yote ya Kamati kama yalivyo.

Mheshimiwa Spika, Naomba kutoa Hoja.

Halima James Mdee, Mb.
MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC)

15 Februari, 2024

MHE. SUMA I. FYANDOMO: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mwenyekiti. Sasa kabla hujatoka hapo mbele ngoja kwanza, ahsante sana. *(Makofi)*

Kwenye hayo makaratasi yako 3.3.5 karibu na mwisho huku kwenye Maazimio 3.3.5 Ubora Usiokidhi Vigezo vya Miradi Inayotekelezwa kwa *Force Account*. Kwenye Mapendekezo, umeshafika hapo? 3.3.5 Ubora Usiokidhi Vigezo vya Miradi Inayotekelezwa kwa *Force Account*.

MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, hii ni *summary,* sasa …

SPIKA: Aah, hukuweka hivyo?

MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, *yes.*

SPIKA: Sawa, sasa kwenye haya Maazimio, kama ndivyo, basi twende kwenye ile Taarifa yako inayoingia kwenye Taarifa Rasmi za Bunge, inahusu mapendekezo. Na hapa kwenye 3.3.5 inayohusu Ubora Usiokidhi Vigezo vya Miradi Inayotekelezwa kwa *Force Account* kwenye Bunge linaazimia kwamba, kuna (a), (b), (c) na (d).

MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, ndio.

SPIKA: Kwenye (c) inasema kuiomba Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, uko hapo?

MHE. HALIMA J. MDEE: Ndio.

SPIKA: Kufanya ukaguzi.

MHE. HALIMA J. MDEE: Yaa.

SPIKA: Sasa sisi, Bunge haliwezi kuazimia kuiomba ofisi, Bunge linaazimia kwamba, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ifanye ukaguzi. Halafu, hiyo ni (c), (d) Bunge linaazimia kwamba, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ifanye ukaguzi wa kina. *(Makofi)*

MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, sawa na ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Kwa hiyo, kutakuwa na hayo marekebisho waheshimwia Wabunge kwenye hii hoja ya Kamati. Ahsante sana Mwenyekiti. *(Makofi)*

Ahsanteni sana. Waheshimiwa Wabunge, naona hapa mbele nimeshaanza kupata vikaratasi, kuna watu wanajua tunaunganisha na leo. Leo hatuunganishi Waheshimiwa Wabunge, leo tutapata mapumziko ili watu wakatafakari mambo mazito yaliyotajwa kwenye hizi taarifa mbili, halafu tujue Bunge litakuwa linaielekeza nini Serikali kwenye Maazimio yale ambayo Kamati zimeyaleta kwenu na ninyi kama mnavyojua kanuni zinawaruhusu kuchangia. Kwa hivyo, mchana tutaendelea na uchangiaji pia na kuhitimisha hoja hizi za kamati mbili, na tutakapoanza uchangiaji tukirejea tutaanza…

Waheshimiwa Wabunge nimesimama, nawakumbusha kila siku na sitachoka kwa sababu, nilikuwa mwalimu, nikiwa

nimesimama utulivu ni muhimu ili unisikilize, enhee. Usiwe unachukua chukua pochi, unajiandaa, utakuwa hunisikii ninachosema kwa hiyo, unakuwa umetulia kidogo, ili umsikilize Spika maana amesimama ili azungumze nawe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji mchana, tutakuwa na Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, Mheshimiwa Venant Daud Protas, Mheshimiwa Daudi Iddi Mpakate, Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo. Hao ndio tutakaoanza nao mchana, halafu tutaendelea na kutaja wengine kadiri muda utakavyokuwa unakwenda.

Baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka Saa 11:00 Kamili, Jioni leo.

(Saa 7.20 mchana, Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)

SPIKA: Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIB MEZANI:

HOJA ZA KAMATI

Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023
na
Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023

(Majadiliano Yanaendelea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, atafuatiwa na

Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah ajiandae.

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuwa mchangiaji wa kwanza katika taarifa zetu mbili ambazo ziko mezani. Awali ya yote niseme tu kwamba naunga mkono hoja. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *LAAC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza mchango wangu sina bundi kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaendelea kuifanya. Dunia inajua, Afrika inajua na sisi Watanzania tunamwelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni historia ambayo imewekwa Tanzania, kwa mara ya kwanza hakuna wilaya hata moja ambayo haijawahi kuguswa na mkono wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika sekta zote zile za kimaendeleo; iwe sehemu ya afya, iwe katika Sekta ya Elimu au iwe katika Sekta ya Barabara zile ambazo ziko chini ya *TARURA*. Katika hili sina budi kumpongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo naipongeza vilevile Ofisi ya TAMISEMI kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaendelea kuifanya katika kuweza kuhakikisha kwamba ni kweli ile tafsiri ya kusema kwamba Wizara hii ni Wizara ya wananchi sasa tunaanza kuiona. Kwa namna ya kipekee kabisa naomba vilevile nichukue fursa hii kumpongeze mchumi mbobezi, ndugu yangu Mheshimiwa Lameck Mwigulu Nchemba kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuweza kusukuma fedha katika halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, historia imeweza kutengenezwa hapa Tanzania, mathalani katika Jimbo la Kibiti, tuna kata 16; hakuna hata kata moja ambayo fedha haijaenda katika miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, niko hapa kuweza kujadili na kuchangia hii Taarifa ya Kamati ya *LAAC* na mimi nitagusa kipengele kimoja tu cha *force account*. Baada ya hapo nitakwenda kidogo pale jimboni, kuna mambo mawili matatu ya kuyaweka sawa.

Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Serikali, hapa tulipofika tumefika kwa sababu ya *force account*. Wote mliopo humu ndani ni mashahidi mnajua, shughuli zote za ukandarasi zilikuwa zinafanywa na wakandarasi. Ujenzi wa namna yoyote ulikuwa unafanywa na wakandarasi, lakini tunajua athari kubwa sana iliyokuwa imepatikana na ndiyo maana *force account* ikawa *introduced*.

Kwa hiyo, kwanza kabisa nawapongeza Wakurugenzi na watendaji kwa jitihada kubwa ambazo wanajitahidi kuzifanya pamoja na mapungufu mengi ambayo tumeyaona na ni kazi yetu sasa kama Wabunge kuweza kuishauri Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye hii *force account* kuna masharti ambayo yamewekwa ya kutumia *force account*. Mimi katika mjadala wangu nitaongelea sharti moja tu. Sharti hili lililokuwa limewekwa linasema kwamba *force account* itumike kwenye kazi ndogo ndogo zitakazoweza kufanyika katika maeneo ambayo yako mbali kidogo na eneo la mjini kule ambako wakandarasi kwa namna moja ama nyingine wakiwa wanatupa *quotation* zitakuwa ni ari ya juu sana, mapungufu ndiyo yanaanzia hapa.

Mheshimiwa Spika, Serikali haijaweka wazi, tunapozungumza miradi midogo midogo, ni miradi gani hiyo? Je, ni ujenzi wa matundu ya vyoo, ujenzi wa madarasa au ujenzi wa ofisi za halmashauri? Hiyo miradi ni miradi gani? Kwa hiyo, pamoja na mapungufu yaliyopo ndani ya *force account.* Naomba niseme tu, ni msingi sasa Serikali iweze kuhakikisha inakwenda kuchanganua kwa mapana yake ili kuanza kuweka tafsiri sahihi kama vile Kamati ilivyokuwa imeshauri. *Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye Kamati tulikuwa tumeshauri kuhusiana na suala zima la fedha ambazo zinaweza kutumika katika miradi ya *force account,* lakini kwa bahati mbaya zaidi

Serikali walichoweza kukisema katika masharti ambayo yalikuwa yameoneshwa hapa, tumeambiwa kwamba miradi midogo midogo ndiko *force account* inakoweza ikatumika.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha, tunashindwa kupata tafsiri halisia, wanapozungumza miradi midogo midogo ni nini? Tukiwa tunakwenda kwenye Kamati kukagua miradi, unakuta kwamba mradi unatengenezwa kwa kupitia *force account* una thamani ya shilingi bilioni tano au shilingi bilioni sita; je, hii ndiyo miradi midogo midogo? Sasa hapa ndiyo shida inapoanza. Kwa hiyo, kuna shida ya msingi ambayo lazima sasa Serikali waweze kukaa kitako na kuweza ku-*address* hizi *issues* ili sasa tuweze kuona *force account* kwa madhumuni yake iliyokuwa imeanzishwa kweli inakwenda kuleta tija ili sasa wananchi waweze kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mapungufu haya yaliyokuwa yameelezwa ya shughuli ya miradi midogo midogo, lakini kuna mapungufu kadha wa kadha ambayo vilevile kwenye Kamati tumeweza kuyaainisha. Miongoni mwa mapungufu ambayo tumeweza kuyaanisha kwenye Kamati, kuna shida kubwa sana ya wataalamu na inashangaza, katika halmashauri unaweza kukuta kwamba *Head of the Department* yeye ni *QS*. Sasa unaambiwa sijui mimi siyo *engineer,* mimi niambie mambo ya namba, *debits and credits,* lakini unashangaa *QS* huyo yeye ndiyo anakuwa mtaalamu wa kwenda kukagua majengo. Sasa unapata shida, *QS* na *engineering* hivi vitu vinafanana? Ninyi mliokuwa wataalamu katika fani hii mnaweza mkatuambia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali ifike wakati sasa muweze kuangalia ili miradi ya *force account* iweze kuwa na tija, lazima muweze kuajiri watumishi wenye sifa ambao kwa namna moja ama nyingine wanaweza wakaisimamia miradi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa kuna shida ya msingi sana, ile *accountability* inashindwa kupatikana. Leo unakwenda kumlaumu *QS* kwamba jengo limejengwa chini ya kiwango, lakini yule si *engineer*, *he is just a normal QS*. Sasa unashindwa kum-*hold accountable, at the end of the day* kinachotokea tunarudi kwa Afisa Masuuli. Tunaanza kumbana Afisa Masuuli tunamwambia

jengo ni bovu, jengo lina nyufa, kwa nini iko hivi? Lakini kiuhalisia ni kwamba, hatuna wataalamu wa kutosha ambao wanaweza wakasimamia kazi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo yote, jambo lingine ambalo ni changamoto kubwa sana, zile taratibu za sheria za manunuzi katika mfumo wa *force account* zinakuwa hazifuatwi. Hii tumeiona katika Kamati na maeneo mengine wakati tunaenda kukagua miradi. Katika mfumo wa *force account* kuna ile Kamati ya Manunuzi na kuna Kamati ambayo kazi yake ni kupokea vile vifaa, lakini kuna shida kubwa sana nah ii shida hii inatokana na changamoto ya mambo ya kimaslahi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika ofisi za Afisa Masuuli, utakuta wao ndio wananunua vitu *in bulk* wanavipeleka kule chini. Wale kule wanaenda kuvipokea tu vile vitu. Wanashindwa kuweza ku-*verify quality* ya vitu vile, lakini wakati mwingine wanashindwa kufahamu mpaka thamani halisi ya vitu hivyo na ndiyo maana unakuta kuna *variation* kubwa wakati mwingine zinaweza kupatikana katika mradi unaofanyika katika halmashauri X na mradi unakuwa unafanyika katika halmashauri Y, hili ni tatizo la msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo kuna tatizo lingine ambalo tumeweza ku-*identify* katika taarifa yetu sisi watu wa Kamati ya *LAAC*. Kuna shida kubwa sana ya msingi hasa katika suala zima la *BOQ* ambazo zinakuwa zinatolewa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Leo Ofisi ya Rais, TAMISEMI inapokuwa inatoa *BOQ* ya kusema kwamba darasa moja linakwenda kutengenezwa kwa shilingi milioni 20, hii kitu haiko sawa sana kwa sababu darasa la shilingi milioni 20 linalokwenda kujengwa kwenye Jimbo la Kibiti kule chini Delta, Mbuchi, Kiongoloni au maeneo mengine au ukienda kule Busekera, ni tofauti kabisa na darasa la shilingi milioni 20 linalokwenda kujengwa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niishauri Serikali, ni lazima wakati wanafanya *BOQ* hizi waweze kuangalia tofauti zilizopo za kijiografia kati ya halmashauri moja na halmashauri nyingine na ndiyo maana katika taarifa yetu kuna tofauti kubwa

sana za fedha, tatizo ni kwamba unamuuliza Afisa Masuuli unamuuliza kwa nini jengo hili wenzio katika halmashauri fulani wamepewa shilingi milioni 470 wameweza kukamilisha, wewe unatumia shilingi milioni 560, tofauti ni nini?

Mheshimiwa Spika, Afisa Masuuli anaanza kukwambia tofauti ya jiografia, vifaa vinapatikana mbali. Kwa hiyo, vitu hivi wakati mwingine hao Maafisa Masuuli tunawabebesha mizigo. Ofisi ya Rais, TAMISEMI ni lazima sasa muweze kuangalia, wakati mnaandaa *BOQ* na wakati mnakwenda kupeleka fedha katika halmashauri husika lazima muweze kuzingatia suala zima la kijiografia… *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Haya ahsante sana Mheshimiwa, kengele ya pili imeshagonga.

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Spika, *oh really?*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Kicheko/Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, atafuatiwa na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, Mheshimiwa Venant Daud Protas ajiandae.

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangine taarifa za Kamati zetu mbili. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anazofanya kwa kuhakikisha kwamba Serikali yetu inapata fedha na zinaenda kwenye majimbo yetu. Pia kipekee nawapongeza Sana Wenyeviti wetu wa Kamati, Kamati yetu ya *LAAC* pamoja na Kamati ya *PAC* na Makamu Wenyeviti kwa kazi kubwa wanazofanya na kutuongoza katika Kamati na kuhakikisha kwamba tunaleta taarifa ambayo ni nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nataka nichangie eneo moja tu leo na nataka nichangie usimamizi wa uondoshwaji wa magari Serikalini.

Mheshimiwa Spika, katika eneo ambalo ni pasua kichwa, hili eneo ni mojawapo ya eneo ambalo ni pasua kichwa. Kwa nini nasema hivyo; *CAG* alifanya ukaguzi wa taasisi nane na kubaini magari zaidi ya 547 yameegeshwa kwa muda wa zaidi ya miaka mitatu. Maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba magari haya tunayaegesha bila mpango wowote.

Mheshimiwa Spika, alivyokwenda *TEMESA* akakuta magari yote yaliyoegeshwa pale, yaliyopelekwa kwa ajili ya kuegeshwa lakini pia yaliyopelekwa kwa ajili ya matengenezo na mengine yakiwa yanasubiri vibali, asilimia 43 ya magari yote yaliyokuwa *TEMESA* yamekaa zaidi ya miaka mitatu; sasa yalipelekwa kufanyaje pale? Kwa sababu kama limepelekwa kutengenezwa, linakaa miaka mitatu halijatengenezwa nini maana yake? Kama lilipelekwa kwa ajili ya kusubiri kibali kutoka Wizara ya Fedha, kibali hakijatoka miaka mitatu, nini maana yake? Hapa kuna tatizo kubwa. Ni lazima sasa Serikali ije na mpango, ije na mwongozo wa muda gani utakuwa kwa ajili ya kuegesha magari. Kama ni muda wa wiki mbili, kama ni muda wa miezi miwili gari limeegeshwa, iwe na sababu za msingi kwa nini bado liko pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna *story* moja *is very interesting;* Mkaguzi alienda kukagua Morogoro nafikiri halmashauri mbili, Halmashauri ya *Morogoro DC* pamoja na Kilosa. Alivyowaambia pale *Morogoro DC* magari yenu yako wapi, wakasema yako gereji binafsi. *CAG* akasema nipelekeni, wakampeleka, wakaanza kusema hili la kwetu, hili la kwetu, hili la kwetu. Baadaye kwenye ile gereji binafsi *CAG* akaona bado kuna gari limeandikwa STK liko pale halina mwenyewe, akashtuka.

Mheshimiwa Spika, alivyoenda Kilosa, Kilosa nao wakasema hatulijui, wakiwa gereji anauliza, hili gari nani alilileta hapa? Yeye anasema hajui. Sasa hii maana yake nini?

Mheshimiwa Spika, *CAG* alivyoenda Wizara ya Fedha, wakaliangalia kwenye Mfumo wa *GAMIS* wakagundua lile gari ni la Kilosa, wakati huyo wa Kilosa alikataa gari si la kwake na liko gereji ya mtu binafsi zaidi ya miaka mitano. *Implication* yake ni

nini? *Implication* yake ni kwamba magari haya tunaya-*dump* ili baadaye waje wauziane watu kwa bei ambayo ni bei chee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima sasa Wizara ya Fedha ije na mpango, i-*set* muda, ni muda gani, ni wakati gani magari yanatakiwa yaegeshwe na baada ya huo muda yatolewe maelezo kwa nini bado yameegeshwa. Eneo hili la magari kuna baadhi ya taasisi zinauziana magari kwa watumishi, kitu ambacho ni sawa, sina tatizo na hilo; lakini hakuna uwazi, hakuna tangazo linalotolewa kwa watumishi ili waweze kununua gari, unashtukia tu tayari watu wameshauziana na mtu anamiliki gari. Hamna tangazo, hamna chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima sasa Wizara ya Fedha ije na mpango, izielekeze taasisi zetu, izielekeze Wizara, izielekeze halmashuri kuwa na uwazi wakati wanataka kuwauzia watumishi magari. *(Makofi)*

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Lusengekile, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Musukuma.

TAARIFA

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nimpe taarifa mzungumzaji, anachangia vizuri. Ni siku tano tu Halmashauri ya *Geita DC* walinyang'anywa gari barabarani na mnunuzi aliyeuziwa gari ya Udhibiti Ubora wa Elimu, ikachukuliwa barabarani, watumishi wakashushwa. Ile gari ameuziwa Mkurugenzi wa Udhibiti Ubora kwa shilingi 1,900,000. Baada ya mimi kuamsha moto kwa Mheshimiwa Mkenda hapa, wameletewa gari bovu la kutengeneza shilingi milioni tano ndiyo liende Geita, nakushukuru mzungumzaji. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Lusengekile, unaipokea taarifa hiyo?

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa anasema na ana uhakika nayo, mimi niipokee, kwa sababu ni sehemu ya maeneo ambayo nilikuwa nataka kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo hilo ambalo tumeliona kutokuwa na uwazi katika kuuziana magari, *CAG* amekagua taasisi nane na katika taasisi nane; sita zote hazikuwa na uwazi katika kuuziana magari. Hili ni tatizo kubwa, lazima Wizara ya Fedha ije na mkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni eneo la uthamini wa zile gari wanapokuwa wanaenda kuziuza kwa watumishi. Unakuwa ni wa bei ya chini kama alivyosema sasa hivi Mheshimiwa Musukuma. Unakuta gari ya shilingi milioni 50, ya shilingi milioni 100 inauzwa kwa shilingi 1,500,000, haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati sijawa Mbunge nikiwa nafanya kazi huko Shirati, kuna gari moja nilikuwa naiona pale Halmashauri ya Rorya, gari imekuja mpya, imenunuliwa zaidi ya shilingi milioni 128, imefanya kazi miaka mitatu ikaharibika kidogo tu Wakai-*park*. Sasa kila siku nikienda pale naikuta, nikaanza kuwaza, *what is the problem?* Baadaye miaka 10, ile gari imeenda kuchukuliwa, imeenda kuuzwa shilingi milioni nane. *V8*! Shilingi milioni nane na huyo aliyeenda kutengeneza ametengeneza sijui kwa shilingi milioni tatu au nne. Unajikuta mtu anamiliki *V8* ya zaidi ya shilingi milioni 120 kwa shilingi milioni 10. Haiwezekani, ni lazima sasa Wizara ya Fedha waje na mpango, ni kwa namna gani uthaminishwaji wa magari unafuata *market value* iliyopo kwenye soko, la sivyo tutakuwa tunayarundika magari, yanaharibika kidogo tunayaweka, watu hawayajali, halafu mwisho wa siku Wizara ya Ujenzi inayachukua halafu inaenda kuyauza kwa watumishi kwa bei ambayo si sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkaguzi alikagua magari 500 na akabaini, katika magari 500 magari nane ndiyo yaliyouzwa kwa bei ambayo iko sawa na soko. Magari 492 yaliuzwa kwa bei chini ya soko na kusababisha hasara kwa Serikali. Ni lazima sasa Wizara ya Fedha ije na mwongozo wa namna gani uthaminishwaji wa

magari unafanyika ili kuendana na soko lililopo kwenye soko letu la magari husika, la sivyo haitakuwa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho eneo hili ni ucheleweshwaji wa vibali kutoka Wizara ya Fedha; Taasisi zimeomba vibali vya kuondoshwa magari, lakini wanaomba kuanzia siku 57 – 2,226 bila kibali kutolewa. Sasa unaona kama wao walichelewa kuomba kibali mwaka mmoja au miwili, wanapeleka Wizara ya Fedha nao wanakaa miaka mitano hawajatoa kibali, maana yake lile gari litakaa zaidi ya miaka saba linasubiri kibali. Tunasababisha *value for money* ya haya magari kukosekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama gari lilinunuliwa lifanye kazi kwa miaka mitano, linafanya kazi kwa miaka mitatu, linaharibika kitu kidogo, wanali-*dump* miaka 10, halifanyiwi *services* na hatimaye linakuja kuuzwa kwa bei ndogo halafu muhusika anaenda kutengeneza kwa bei ndogo na inakuwa gari lake. Shilingi milioni 10 anamiliki *V8*. Hii haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, hivyo niishauri sana Wizara ya Fedha, katika Sheria ya Uthaminishaji nafikiri ni sheria Na. 61 kama sikosei, ni lazima sasa waiboreshe, wamhusishe hata Mthamini Mkuu wa Serikali, kwa sababu kinachofanyika saa hizi ni Wizara ya Ujenzi pekee yake, ikishasema hili gari tuliuze kwa shilingi milioni tano sawa, Mthaminishaji Mkuu wa Serikali hausishwi. Kwa hiyo kwenye kuthaminisha magari tunaomba pia Mthaminishaji Mkuu wa Serikali ahusishwe ili tupate *value for money* ya gari husika ili iweze kuleta tija kwa Watanzania na kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, atafuatiwa na Mheshimiwa Venant Daud Protas, Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate ajiandae.

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia ripoti ya *LAAC* na *PAC*. Awali ya yote niwapongeze wajumbe wa kamati zote mbili

akiwepo Mwenyekiti wangu wa Kamati ya *LAAC*, Mheshimiwa Halima Mdee pamoja na Wajumbe wake wote kwa taarifa nzuri aliyoisoma hapa leo Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nitajikita kabisa kwenye taarifa ya *LAAC*, kwenye upande wa *force account* lakini kabla ya hapo nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ya kihistoria anayoifanya. Hakuna wakati wowote uliyokuwa na pesa nyingi kwenye Serikali hii ya kwetu ya nchi hii hasa kwenye Halmashauri zetu kama kipindi hiki cha Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya yote tunayoyaongelea *force account*, ma-*engineer* wachache wa miradi haisimamiwi ni kwa sababu pesa ni nyingi mno Halmashauri na yote hiyo ni juhudi kubwa zinazofanywa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuwapongeza Mawaziri wanaohusika TAMISEMI ambao wanahusika sana na wanapambana na mambo ya *TARURA* kwa kuangalia hali ya hewa iliyopo sasa hivi, wanahangaika kadri ya uwezo wao kuhakikisha mambo yanakwenda, nimpongeze Kaka yangu Mheshimiwa Bashungwa, tunamuona huku na huku kwa kazi za dharura kwa ajili ya mvua anapambana sana sana.

Mheshimiwa Spika, pia ni kwa ukweli lazima tumpongeze Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, kazi aliyonayo si kazi ndogo ni kazi kubwa sana. Sisi kama Wabunge kuongea kukosoa tunaona ni rahisi lakini ukiwekwa pale Wizara ya Fedha ni changamoto kubwa, bajeti ipo kamili unakuta kuna mambo yamejitokeza ya dharura, mvua imenyesha daraja limekatika unaambiwa toa pesa, ukiangalia bajeti haipo sawa, kwa kweli tuendelee kuwaombea viongozi wetu, tumuombee Mheshimiwa Rais lakini na Mawaziri wake wote waendelee kufanyakazi vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kutoa pongezi kwa Wakurugenzi wote wa Halmashauri zetu zote. Mabilioni yote ya

fedha yanapelekwa kwenye Halmashauri kama kuna ubadhilifu ni watu wachache sana *otherwise* miradi isingekuwepo, tuwatie moyo Wakurugenzi wetu wa Halmashauri kama kuna mapungufu ni machache na tuendelee kuyarekebisha, lakini tusiwe tunatamka Wakurugenzi wote ni wezi ni jambo baya sana, tunawavunja moyo na wakati kila siku wanasimamia miradi wao. Miradi yote tunayoiona nchini kwetu Wakurugenzi wanahusika kuisimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nirudi kuongea kwenye suala la *force account*, mimi binafsi sipingi *force account* ni jambo zuri sana lakini uboreshaji wa *force account* unatakiwa. Mapungufu yake ni mengi na mapungufu yake ni makubwa sana yanasababisha hasara kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nimepata bahati ya kufanya ziara kwenye Mikoa tofauti tofauti lakini tumesikia taarifa ya Kamati kwamba wametoa mfano, nitolee mfano kwenye Mkoa wangu wa Tabora, kuna miradi 812 lakini kuna ma-*engineer* 19 tu. Unaweza ukaona pesa ya Serikali inasimiwaje. Kwa hiyo, ubora wa usimamizi kutafuta *value for money* unakuwa ni mdogo sana kwa sababu hakuna wasimamizi wa karibu. Watu 19 kwa miradi 800 yaani haiingii akilini wataisimamia vipi na yote hiyo ni juhudi za Serikali kutafuta pesa lakini bado tuangalie jinsi *force account* itakavyofanya kazi ili iwe na manufaa badala ya kuleta hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tunawaweka walimu wanasimamia, Madaktari wanasimamia, mpaka Manesi unakuta wanasimamia jengo la Serikali lakini kitakapoharibika kitu Mwalimu huyu ambaye hana *qualification* yoyote ya usimamizi wa hizi kazi anapelekwa Polisi, anasumbuliwa, anaadhibiwa lakini tunasahau hata kuwapa semina kidogo tu za *procurement* kuwaonesha kwamba hata kamwanga kidogo hatuwapi, tunawakabidhi kazi ambazo hawajazisomea, tunawakabidhi kazi ambazo akipata tatizo kidogo unampeleka Polisi wakati hana hiyo *qualification,* tuendelee kuboresha *force account* ikae vizuri, hatuikatai kwamba ni mbaya lakini iendelee kuboreshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utakuta hata kwenye ziara zetu sisi Wabunge unakuta ni Daktari anasimamia hospitali ya Wilaya pale kuna *technician* mmoja Wilaya nzima, Daktari ndiyo anasimamia, unakuta kuna kosa kidogo Mbunge anamfokea Daktari, anatetemeka wakiona Wabunge, anafoka sana badala ya kumuelewesha, siyo *qualification* yake, siyo *qualification* yake kwa hiyo nenda naye taratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unamfokea kitu ambacho anasema mimi nimeletewa kila kitu na *engineer*, mimi nilisimamia tu sijui chochote, yaani mpaka unajisikia saa nyingine kwamba tunakuwa tunawaonea hawa viongozi wengine ambao wapo kule kwenye usimamizi. Kwa kweli, unakuta kazi haijaenda vizuri *value for money* haieleweki yaani unakuwa unasema jamani hivi hela za Serikali zinapotea kiasi hiki! Lakini cha kushangaza kila Mkoa una Ofisi ya TAMISEMI Mkoa, hawa Ofisi ya TAMISEMI Mkoa wanaenda kule chini kuangalia hizi hali? Hapo ndipo tunabaki tunakuwa tunajiuliza lakini kwa kweli *force account* inabidi iboreshwe iboreshwe zaidi.

Mheshimiwa Spika, unakuta wilaya moja tulienda wodi ya wazazi, kuna hospitali mbili zina wodi ya wazazi. Wodi moja ya wazazi kwenye Wilaya moja fundi amechukua shilingi milioni 41 kujenga tu, lakini kuna wodi nyingine ya wazazi fundi amechukua shilingi milioni 15 kuijenga tu ile wodi, na ni Wilaya moja. Huyu milioni 41 na huyu milioni 15 hiyo ndiyo *force account* ambayo bado haijafanyiwa marekebisho na inahitaji marekebisho makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpaka unajiuliza hivi *force account* zingine ni za watumishi tu wanaweka mafundi wao? Maana itakuwaje wodi moja imejengwa kwa shilingi milioni 15, wodi nyingine inajengwa kwa shilingi milioni 41. Ukiangalia Kanuni ya *PPRA* ya 2020 kama alivyosema mwezangu kuna Kamati ya Manunuzi na Kamati ya Mapokezi vitu vingi havifanyi kazi kama inavyotakiwa, kwa hiyo niwaombe Wakurugenzi, Waziri aliopo madarakani na Naibu wake wahakikishe taratibu zinafuatwa. Maana yake unaweza ukajiuliza sasa shida ni nini, kwa nini watu hawa hawafanyi kazi kama kanuni zilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulienda kwenye Halmashauri moja tulipofika Mkurugenzi akatuita pembeni akasema miradi yote ya hapa inafanywa na Mwenyekiti wa Halmashauri na Naibu Mwenyekiti sitataja lakini Wajumbe wenzangu wanajua, naombeni mnisaidie hali ni mbaya mtu mwingine akipewa wanagoma kila kitu inabidi uwape wao wafanye kazi. *Value for money* ni mbaya yaani miradi haieleweki, wameweka mafundi watoto wao wa nyumbani kwao, kwa hiyo hivi vitu kwa kweli inabidi visimamiwe sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkurugenzi huyo ni msichana mdada tu alikuwa umoja wa vijana, alipambana ikatangazwa kazi ya kujenga hospitali ya Wilaya kwa bajeti ya shilingi milioni 500, akatangaza kwa wakandarasi wakaomba. *Lowest* aliomba kwa milioni 900, Mwenyekiti wa Halmashauri na Makamu wanaitaka ile kazi, yule Dada akamuita mkandarasi akamwambia umeomba kwa 900 mimi nataka nikupe hii kazi kwa 500 unakubali? Wakafanya *negotiations* pale, yule Mkandarasi akukubali kujenga ile hospitali ya Wilaya kwa shilingi milioni 500, akaona badala nipeleke *force account* itaenda zikaharibike *value for money* haitapatikana na mimi nimeanza kazi juzi tu ni bora nipate lawama za Mwenyekiti wangu wa Halmashauri lakini jambo liwe salama, akampa Mkandarasi kwa shilingi milioni 500.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema kwamba ifike sehemu hawa Wakandarasi *sometimes* aitwe mkae naye mfanye *negotiations,* akikubali kupunguza bei kwa bajeti yenu mliyonayo basi ni vema achukue hii kazi Mkandarasi kwa sababu, moja atalipa kodi ya Serikali lakini mbili asipofanya *value for money* mnahaki ya kumshtaki na ana haki ya kurudia ile kazi mara mbili mpaka pale ninyi mtakaporidhika. Kwa hiyo miradi ile mikubwa ni vema waichukue Wakandarasi.

MHE. CHARLES M. KAJEGE: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, ile miradi mikubwa nilisema waichukue wakandarasi wakubwa na miradi ya kawaida hatukatai…

SPIKA: Mheshimiwa Munde kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Charles Kajege.

TAARIFA

MHE. CHARLES M. KAJEGE: Mheshimiwa Spika, nashindwa kumuelewa mzungumzaji mara anasema hiki mara kile, sasa atupe msimamo wake je, anaikubali *force account* au hapana? *(Kicheko)*

SPIKA: Mheshimiwa Munde kuna taarifa hiyo iliyokuja kwa sura ya swali unaikubali? *(Kicheko)*

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, kwanza siipokei taarifa yake kwa sababu hasikilizi Bunge, *nadhani ana-chat huko nimesema force account siikatai lakini iboreshwe, ndivyo nilivyoongea aangalie Hansard itamuelewesha. Mnakuja hapa mna-chat halafu mnakuwa mnatupotezea dakika zetu.* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

SPIKA: Mheshimiwa Munde, hayo ya ku-*chat* yaondoe, hayo maneno ya ku-*chat*, Mbunge alikuwa anasisitiza tu.

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, nimefuta maneno ya ku-*chat*, Mbunge hakuwa ana-*chat* humu ndani. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshima Spika, napenda niishauri Serikali Wakandarasi wengi wanatabia ya kupandisha bei mara mbili zaidi lakini atakapopandisha bei ukamuita ukakaa naye ukafanya *negotiations* kwamba kazi hii bajeti yake shilingi milioni 500 kama atakubali kufanya basi ni vema afanye Mkandarasi kwa pesa iliyopo pale.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda niliongelee ni ramani au *BOQ* za TAMISEMI. Mimi kwetu nilipozaliwa Baba yangu alijenga nyumba kabla sijazaliwa miaka mitano au sita toka umri wangu huu niliyofikia, nyumba hiyo bado ipo. Nyumba yenyewe inazege pale kwenye madirisha, pale

kwenye milango ndiyo imewekewa mkanda siyo mkanda wa kuzunguka nyumba nzima, ile nyumba mpaka leo ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ulibahatika kuona *BOQ* ya zahanati msingi wake unaweza ukajenga ghorofa tatu, yaani nondo ni nyingi unashangaa zahanati ni kijumba cha kawaida tu *why* pesa zote hizo mnazilundika chini karibia shilingi milioni 10, milioni 20, milioni 30 zinaenda chini kwa nini? Kwa nini zahanati moja unaweza ukatoa zahanati moja na nusu, msingi wake unakuwa *strong* ambao unaweza kujenga gorofa tatu, mimi sioni faida yoyote kama nyumba ya kawaida tu inaweza ikaishi miaka 70 hiyo nyumba ambayo ni ya kitaalam ikiishi miaka 150 si inatosha? Kwa hiyo naomba TAMISEMI waziangalie upya *BOQ* zao. *BOQ* ukiiangalia ya zahanati unaweza ukacheka sana, unaweza ukashangaa kwa nini wanafanya namna hiyo. Nondo ni nyingi mno ambazo zinasababisha unaweza ukajenga gorofa tatu kwenda juu.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa kengele ya pili tayari.

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Haya ahsante sana. Mheshimiwa Venant Daud Protas, atafuatiwa na Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo ajiandae.

MHE. VENANT D. PROTAS: Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza na mimi nianze kwa kuunga mkono hoja za Kamati zote mbili, naunga mkono hoja ya Mwenyekiti wangu wa Kamati ya *PAC*, Mama yangu amewasilisha hoja vizuri na sisi kama Wajumbe tulikubaliana hiyo hoja kwa niaba ya Bunge zima, kwa hiyo naamini yale tuliyoyashauri kwenye upande wa Serikali yatafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme jambo moja, Serikali ya Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kipindi hiki hakuna Serikali ambayo iliwahi kushusha fedha kama Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan,

hakuna anayebisha mpaka mtoto mdogo ameguswa na fedha ya Serikali yetu ya Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha hii pamoja na kushushwa kwa wingi Mama kazi yake ameimaliza, imebaki sasa sisi ambao tumepewa dhamana ya kwenda kusimamia ibadilishwe kuleta matokeo ili mwananchi wa kawaida aweze kuona matunda na yale tunayosema fedha zimeletwa za Mama Samia, aweze kuona matokeo mazuri. Ninayasema haya kwa sababu gani?

Mheshimiwa Spika, leo tuna miradi ya *REA* kwenye maeneo yetu, Mheshimiwa Rais ameelekeza vijiji vyote vifikiwe na nishati ya umeme, hilo nampongeza na mimi nilikuwa katika Jimbo langu la Igalula katika vijiji 58 nilipokuwa naingia 2020 vilikuwa havina nishati ya umeme vijiji 46 na leo niwaambie vijiji vyote vimepelekewa miundombinu ya nishati ya umeme, hiyo ni kazi kubwa ambayo imefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupelekewa nishati ya umeme bado kuna changamoto. changamoto mojawapo iliyopo lengo na madhumuni ya Mheshimiwa Rais ni kuona matokeo yanatokea lakini ukiangalia tunapeleka mabilioni ya fedha kwenye miradi hii haiwezi kwenda kuonekana kwa uhalisia kwa sababu aidha wataalam wetu walisinzia wakatoa ushauri mbaya na leo tunakwenda kufanya mradi uleule tunakwenda kuingiza Taifa hasara kwa kupeleka kazi kufanyika mara mbilimbili, kwa sababu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunapeleka umeme kwenye vijiji, kijiji ambacho kilitakiwa kifungwe *transformer* ya *KV* kuanzia 200 tunakwenda kupeleka *KV* 50 wateja wanaohitajika kuonganishwa zaidi ya 300 kwenye kijiji kimoja mnaweka *limit* ya wateja waunganishwe chini ya 20 kwa *transformer* moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi najiuliza huyu mtaalam alikuwa anapiga hesabu alifika huko au aliandikia kwenye ofisi? Kama aliandikia kwenye ofisi hawa watu wa *TANESCO* waliopo huko kwa nini hawajashauri? Leo miradi ya *REA* yote sasa hivi wamekaa Wakandarasi wanasubiri muda wao uishe, mzigo utupiwe

TANESCO, *TANESCO* wakipewa tu wanaanza kufyatua tena katoa *transformer* hii kaipeleka chumbani, kaleta *transformer* nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tungeweza kutatua mapema haya mambo ya kufanya kazi mara mbilimbili yasingeweza kutokea. Kwa hiyo, mimi niombe tunakwenda kuweka umeme kwenye vitongoji kwenye bajeti ijayo, mfanye tathimini na uhalisia wa maeneo husika. Kwa mfano, mimi hapa kwenye Wilaya yetu ya Uyui walitakiwa waunganishwe wateja 6,120 mpaka leo tumeunganisha wateja 1,357. Sasa ukiangalia huyu Mkandarasi mkataba wake uliisha mwezi wa Disemba, 2022 na sasa hivi tumemuongezea muda sijui unaisha mwezi Juni, amebakiza miezi minne aondoke. Mtamuona *TANESCO* kaja na magari ya Serikali anaanza kubadilisha tena, kwa hiyo tuombe hayo mambo yawekwe sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuchangia hiyo lakini na mimi nirudi kwenye fedha zinazokwenda hasa kwenye *force account*. Mimi hapa nilikuwa nataka nishauri jambo moja, *force account* imetusaidia sana wananchi na hasa sisi Wabunge ambao tunatoka vijijini imetusaidia sana, lakini *force account* inatakiwa ikafanyiwe *assessment* nyingine tujue kwenye *force account* wangapi wamekufa kwa sababu ya *force account*, wangapi wameugua presha kwa sababu ya *force account,* nasema haya kwa sababu gani?

Mheshimiwa Spika, tumepeleka miradi huko leo Daktari kawa *engineer* wa majengo, Mwalimu kawa *engineer* wa majengo, mtu amesoma baiolojia, amesoma auguze watu sasa hivi anashinda madukani kununua *cement* na nondo, hiyo kazi haikumpeleka kule, lakini leo mtu badala ya kutibu wagonjwa au kufundisha anakazana kulinda pale msumari na *cement* zisiibiwe kwa sababu zikiibiwa anakuja kushughulikiwa yeye. Kwa hiyo, tunatakiwa tufanye *modality* nzuri ili hawa watumishi wetu tuwasaidie waweze kufanya kazi zao. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunasema tumesaidia kuleta *force account* lakini tumeleta majanga kwa baadhi ya watu. Leo

watumishi wanaandika barua ya kwenda kusoma hata kabla ya muda kwa sababu wakimbie hizi adha. Kwa hiyo, mimi nataka nishauri Serikali kama tunaisaidia kweli Serikali, *force account* ni nzuri tuiwekee utaratibu mzuri ili iweze kusaidia namna gani ya kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii *force account* hizi *BOQ* zinazokuja kutoka TAMISEMI, hivi *BOQ* inakwambia ufunge *beam* tatu kutoka chini, katikati, uende kwenye madirisha na uende mwisho. Hivi kule kuna matetemeko ya ardhi? Hawa wataalam wamesomea wapi? Leo tumejenga madarasa ambayo tungeweza kujenga shule mbili kwa shule moja, tunakwenda kulaza tofali la nchi sita tofali tunalaza, kuanzia chini mpaka juu. Sasa hebu tujiulize tulishapata matetemeko madarasa yakaanguka? Je, kwa nini kwenye shule *'A'* tunalaza, shule *'B'* hatulazi, kule hakuna watoto? Hivyo, wataalam wetu watusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa napata maajabu, hii *force account* kuna watu hapa wameshaanza kuiga *force account* hata kwenye Wizara zingine. Leo Wizara ya Mifungo tena imekuja na yenyewe na *force account* kujenga kwenye majosho. Sasa f*orce account* ya kwao bora hii ya TAMISEMI, wao sasa anayelipa anakaa Dodoma sijui Dar es Salaam Makao Makuu, fundi yupo kijijini, anaandika *invoice* hajui hata anampelekea nani, na yule pale anampelekea watu wa Wilayani nae anasema nimetuma kule kwa wakubwa. Huyu mkubwa ni nani? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba Waziri wangu wa Mifugo, *force account* imekushinda rudisha hela kwenye Halmashauri, kuna watu wanakudai mpaka saa hizi nikutajie majina na uwalipe. Kwanza, kuna huyu mtu mmoja anaitwa Gita Dotto Malema anadai shilingi 1,400,000 fundi huyo ambaye tulitakiwa tumsaidie, halafu kuna mwingine Noel Jumanne anadai shilingi zaidi ya shilingi milioni moja tangu mwaka 2022 hajalipa kisa *force account,* naye sijui alikuja hajafanya utafiti wa *force account* ikaletwa hivyo.

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya kumkera zaidi nikamtumia meseji nikamwambia Mheshimiwa Waziri, hebu

nisaidie hawa watu wanadai kwa muda mrefu wamekopa huko fedha ili waweze kulipwa, Waziri akamtumia mtaalam wake Wizarani jibu alilokuja kumrudishia akamwambi Mheshimiwa Waziri hilo deni kweli lipo Wilaya ya Uyui na huyo Ndugu Noel tumelifuatilia kwa ukaribu sana lakini wakati tunataka kulipa badala tumlipe Noel wa Uyui, tukamlipa Noel wa shamba gani sijui wapi huko, akalipwa mtu mwingine. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa ukija kuangalia, hao akina Noeli pamoja na kuwa labda majina yamefanana, walikuwa na *amount* sawa? Hawa Wahasibu huko Wizarani wanafanya kazi gani? Noeli sawa, majina yamefanana, hatukatai; na *amount* zimefanana? Haya huyo mwananchi amekuja kuniambia mimi. Nimeweza kufuatilia, nimekutana na kisanga hicho. Yule ambaye hana *connection* fedha yake inakwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii *Force Account* ichunguzwe na yenyewe. Leo tunaletewa *Force Account* inakuja *BOQ,* inakwambia kabisa nenda ukanunue bati namba fulani kwa fulani. Kumbe kule sijui wameshaweka *ten percent!* Wanatuambia mabati tukanunue *ALAF*, tena na namba wanakupa kabisa, wanakupiga *pin,* namba fulani. Zikaanza kupita harambee huko, changisha kama mabakuli, wewe peleka huko utakuta mgao wako umechelewa. Wakalundika fedha yote *ALAF*. *ALAF* mwenyewe akakosa kuzalisha, miradi ikachelewa. Kwa hiyo, lazima tuweke *strategy* ya kusaidia. Fedha zimekuja, lakini inakuwa ni kero. Mheshimiwa Rais, anataka aone matokeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naunga mkono Kamati zote mbili, *Force Account* ni nzuri, lakini sisi kama Wawakilishi wa wananchi tuweze kuisaidia Serikali ili azma ya Mheshimiwa Rais ilete matokeo kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, najaribu kuwaza yale Maazimio yalipo hapa na michango inayoendelea, sijaelewa bado, *Force Account* inatakiwa, au vipi? Mheshimiwa Daimu Iddi

Mpakate, atafuatiwa na Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo na Mheshimiwa Joseph George Kakunda, ajiandae.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii nami nichangie hoja zilizopo Mezani. Kwanza, naunga mkono hoja zote mbili za *PAC* pamoja na *LAAC*. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *LAAC* nitajikita zaidi kwenye masuala yanayaohusiana na *LAAC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais, wetu wa Awamu ya Sita, kwa kushusha fedha nyingi katika Halmashauri zetu. Hili jambo limetufanya tuwe na miradi mingi ambayo leo hii tunaona udhaifu ambao umetokana na utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, pili, namshukuru sana *CAG* kwa kazi kubwa aliyoifanya na kufichua yote haya ambayo tunayasema. Sisi Wajumbe wa Kamati siyo kwa akili yetu, ni wao, wenzetu wamefanya kazi hii bila kuwaogopa Wakurugenzi, bila kuwaogopa Wakuu wa Idara na kuleta taarifa zote hizi ambazo tunazizungumza leo kwamba zina changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitajikita zaidi kwenye *Force Account,* hasa kuhusu ukiukwaji wa Mwongozo wa Utekelezaji wa Miradi yetu. *Force Account* imeweka utaratibu, TAMISEMI wanatengeneza *BOQ* kulingana na mahitaji ya kazi ambayo wanataka kuifanya. Ninaamini TAMISEMI wana wataalamu wote ambao wamefanya kazi ile kwa uadilifu na kujua gharama halisi ya kila mradi ili waende kuushusha chini.

Mheshimiwa Spika, mfano halisi, ndugu zangu kitaalamu angalia hata bei ya sigara inavyokuwa, nchi nzima ni bei moja. Wataalamu walikaa wakakubaliana kulingana na gharama ya kila mahali waka-*standardize* wakaona gharama ya ununuzi na kuuza sigara ni kiasi hicho. *The same applied* kwa TAMISEMI, wameshafanya utafiti wa kutosha wa gharama za kila eneo na wakachukua *average* kwa ajili ya utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kinachojitokeza sasa ni watekelezaji, usimamizi unakuwa siyo mzuri. TAMISEMI wanatoa taarifa yao vizuri, Mwongozo upo kwa kila Halmashauri. Tulitegemea *variation* katika Halmashauri isizidi asilimia 10 kwa maana ya kuongeza na kupungua, lakini bahati mbaya *variation* ya maeneo mengi ni zaidi ya asilimia 15. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuchukue mfano, Mkoa wa Morogoro. Mvomero wana *variation* ya asilimia 51 katika ujenzi wa Sekondari zile za *SEQUIP* ambayo ni shilingi milioni 470, lakini wanahitaji zaidi shilingi milioni 241,363 na ushei ili kukamilisha mradi ule ili uweze kukamilika. Morogoro *DC* wao kidogo wana afadhali wana *variation* ya asilimia 15 ambayo inasimama shilingi milioni 73 kwenye ile shilingi milioni 470. Ulanga asilimia 34, Malinyi asilimia 26 na Mlimba asilimia 29.68. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini ninasema hivi? Wataalamu wetu kwenye Halmshauri, kila mtu na mtazamo wake. Kwa sababu kama wangekuwa wanasimamia vizuri na kutumia ofisi zetu za mkoa kusingekuwa na *variation* kutoka wilaya moja mpaka wilaya nyingine kiasi kwamba inafanya *Force Account* ionekane haina maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukingalia katika utekelezaji huo huo, usimamizi utakuta hata majengo yanayojengwa, ukweli ni kwamba kutokana na changamoto waliyozungumza wenzangu na taarifa ya Kamati ya wataalamu wa ujenzi kutokuwepo, basi hata changamoto yenyewe ya majengo yanakuwa ni *below standard*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hili jambo linasikitisha sana. Pamoja na kuona hivyo, lakini kuna maeneo *too much,* yamezidi. Mfano uliotolewa kwenye taarifa yetu, kwa mfano pale Newala, kwingine pale Namtumbo kwenye mradi ule wa Sekondari ya Wasichana wa shilingi bilioni tatu wanahitaji zaidi ya shilingi 1,450,000,000 *variation* ni zaidi ya asilimia 49. Kwa kweli nina mashaka na wataalamu wetu katika Halmashauri, kwamba hawataki kumsaidia mama miradi ikamilike wananchi wafaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kinachotokea wao ni kuangalia maslahi yao binafsi, mfano mmoja mdogo sana, utakuta kwenye *Force Account* wameanzisha mtindo wa kununua manunuzi yote ya vifaa kutokana na mtandao. Ukinunua kwenye mtandao unakuta mfuko mmoja wa simenti shilingi 28,000 au 25,000. Ukienda dukani au kwenye soko uhalisia ni shilingi 18,000 au 19,000.

Mheshimiwa Spika, hili jambo nalo mtandao unachangia kwa asilimia kubwa. Niliona sehemu tulikotembelea, wao wameweka bati mmoja shilingi 62,000, wakati bei ya soko ni shilingi 38,000 mpaka shilingi 42,000. Kwa hiyo, manunuzi ya kwenye mtandao yamefanya *Force Account* iwe na gharama kubwa kuliko vile ambavyo soko lilivyo. Kwa hiyo, nadhani kuna haja ya wenzetu kupitia sheria hii na mwongozo wa *Force Account* utumike kama ilivyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala la matumizi ya Kamati. Hizi Kamati zimekuwa kama *fingerprint* ya kusema kwamba tuna Kamati ya Manunuzi, tuna Kamati ya Mapokezi na tuna Kamati ya Usimamizi. Hizi zote hazifanyi kazi, imekuwa kama mapambo. Hawapewi Semina, wanaleta mzigo, wanaleta na *delivery note,* hakuna cha *invoice,* hawajakaa vikao vyovyote, vikao vinakaliwa juu na Halmashauri, wanarudisha kule wanapeleka vitu. Kwa kweli hili jambo linafanya kwamba *Force Account* inaonekana kwamba haina ufanisi mkubwa kwa sababu kuna watu wamejipanga kuihujumu *Force Account* kwa manufaa yao wenyewe badala ya manufaa ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli jambo hili kama hatutalitilia mkazo kwa kuwachukulia hatua wale wote waliohusika katika ubadhirifu huu wa kuongeza gharama ya ujenzi tofauti na iliyokadiriwa, nadhani tutakuwa hatuwatendei haki wananchi wetu, kwa sababu kuna majengo mengi sana yaliyojengwa kwa *Force Account* hayajakamilika.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph George Kakunda na Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, ajiandae.

MHE. MICHAEL C. MWAKAMO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ambayo nami nitatoa mchango wangu. Nami kama ambavyo wamesema wenzangu, nami ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati ya *LAAC,* Kamati ambayo kwa kweli kwa kiwango kikubwa tunafanya kazi kwa ushirikiano wa kutosha. Pia nampongeza sana *CAG* kwa sababu taarifa yake inatusaidia kuweza kubainisha machache ambayo tutayachangia kwenye Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la kwanza ni shukrani kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa namna anavyoendelea kutupatia pesa za utekelezaji wa miradi kwenye kila Jimbo. Wiki mbili zilizopita nilikuwa Jimboni na hapa nitoe shukurani za Wanajimbo, maana nilikwenda kukabidhi *ambulance* ambayo ilitoka katika Ofisi yake na wananchi wa Kibaha Vijijini wanampongeza na wanamshukuru sana kwa kuwapatia gari kwa ajili ya huduma za wagonjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili kwa jioni hii, napenda kutoa pole kwa Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo, Taifa leo ukilisikia kwa miezi michache au siku chache hizi, baadhi ya watu maarufu waliokuwa viongozi kwenye nchi yetu wamepoteza maisha. Nampa pole Mheshimiwa Rais kwa kupotelewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu Mstaafu ambaye naamini viongozi wetu na wengine wengi wapo huko sasa hivi kwa ajili ya maandalizi ya kumzika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, natoa pole kwa Wanajimbo la Kihaba Vijijini kwa kuondokewa na kipenzi chao, ambaye ndio alikuwa Mbunge wa kwanza wa Jimbo la Kibaha Vijijini, baba yangu Mheshimiwa Dkt. Ibrahim Said Msabaha, ambaye tumemzika jana. Nawapa pole sana Wanajimbo la Kibaha Vijijini, waendelee kuvuta subira kwa sababu yale ambayo walianza kuyapata kutoka kwake, kijana wake na kijana wao nitaendelea kuyapambania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu leo nitajielekeza kwenye maeneo machache, lakini kwa kweli kabisa kwa namna ambavyo Kamati tumepitia tunajielekeza sana kwenye *Force Account*. Hata wewe hapa katika kuanza kufuatilia na kutaka kutufanya tukae vizuri, ulitaka kuona kama Azimio lililo mbele yetu ndiyo mawazo ambayo watu wanaendelea kuchangia?

Mheshimiwa Spika, sisi kama Kamati tumepitia na tumeona *Force Account* kwa upande ilikuwa na faida kubwa sana, lakini zipo changamoto ambazo zimejitokeza kwenye *Force Account* na kwa sababu hiyo, chini ya Mwenyekiti wetu shupavu kabisa Mheshimiwa Halima Mdee, tukaja na maazimio yale ambayo tunaliomba Bunge liwe sehemu ya maazimio kwamba baadhi ya miradi mikubwa ifanywe nje ya *Force Account*. Tumetoa mawazo yetu pale kwamba baadhi ya miradi ambayo tunakuwa tumekubalina, basi iendelee kufanywa na *Force Account*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama Mjumbe wa Kamati, nitapita katika sura ile ambayo Mwenyekiti wetu alituongoza na Kamati tulikubaliana kwamba lazima kwenye na miradi ambayo itafanywa na *Force Account* na lazima kuwe na miradi ambayo pia inaweza ikatekelezwa na Wakandarasi. Kwa mfano, kwa nini tumefika kwenye mawazo ya namna hii? Nitapita kwenye maeneo machache ya kuona namna gani *Force Account* imeleta na imeonesha changamoto, na ndiyo maana Wajumbe wa Kamati tumekubaliana kwamba lazima kuwe na miradi ambayo inafaa kutekelezwa na Wakandarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, tumejaribu kupitia miradi michache, nitatoa hapa mifano miwili tu. Ukiangalia pale kwenye Halmashauri ya Mtama, walipewa shilingi milioni 470 kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Sekondari, lakini mpaka ambapo wamefikia, wamehitaji na wamekwenda kufanya ile kazi kwa shilingi milioni 655.272; lakini ukienda kuiangalia Nzega, tunajenga jengo lile lile, lenye mchoro ule ule ambao watalaamu wa kutoka TAMISEMI wameupeleka, Nzega wamepewa shilingi milioni 470, lakini mpaka taarifa ya *CAG* inatoka, wameshatumia shilingi milioni 849.575, na bado zipo kazi hazijakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nini maana yangu au maana yetu kama Wajumbe wa Kamati? Tunaona kwamba pamoja mawazo mazuri ambayo yalitolewa na Serikali kwenye kuitumia *Force Account,* lakini watekelezaji na wasimamizi wa *Force Account,* Halmashauri moja mpaka Halmashauri nyingine kila mmoja ana mtazamo wake na kila mmoja ana namna ya kufikiria anawezaje kukamilisha miradi. Kwa sababu haiwezekani kuwe na utofauti wa karibu shilingi milioni 200 kwenye jengo moja lenye thamani ambayo tayari lilishafanyiwa tathmini na wataalamu wa TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ilitakiwa kama ni tofauti ionekane ndogo sana. Ukienda katika hali hii, unakuta kwamba lipo tatizo la wasimamizi kila mmoja ana mtazamo wake kwenye hili. Kwa hiyo, tunaomba sana, mawazo yale yaliyotolewa na Kamati yaendelee kupata nguvu ya kufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukirudi kwenye utaratibu mzima wa wingi wataalamu, miradi yetu mingi inashindwa kukamilika kwenye ubora. Tunafahamu sote hapa kama Wabunge kwamba Serikali mwaka 2019 walikuja na mwongozo wa kusimamia majengo, ni jengo lipi linatakiwa liishi kwa umri gani? Sasa tutakuja kuona kwamba wataalamu wa kusimamia ubora wa majengo haya kwenye Halmashauri zetu, hawapo.

Mheshimiwa Spika, hapa tena ninatoa mifano michache uone. Kule Sikonge wametekeleza miradi 111, lakini wana Mainjinia wawili tu. Kule Kaliua wametekeleza miradi 141, wana Mainjinia wawili tu. Ukienda Tanganyika wametengeneza miradi 169, wana Mainjinia wanne. Kwa Halmashauri chache ambazo tumezipitia 21, tumegundua zina Mainjinia 79, lakini wametakiwa kusimamia miradi 3,167. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hebu tujiulize ndugu zangu, Injinia ndio mwenye jukumu la kusimamia mradi. Miradi elfu tatu ikasimamiwe na Mainjinia 79, tunategemea kwenda kupata ubora unaostahili? Ndiyo pale Serikali, kwa sababu nia ni kuwahudumia wananchi, kwa nia njema kabisa, wanaamua Mwalimu simamia Sekondari ijengwe, Mganga simamia Kituo cha Afya kijengwe. Lengo ni

kuweza kufikisha huduma kwa wananchi, lakini kiukweli zinafika huduma ambazo sasa zinakwenda kuharibu miradi, kwa sababu kila jengo lina thamani yake na lina muda wake wa kuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri ambao nafikiri tunatakiwa tuufanye, kwanza tukubaliane na mapendekezo ya Kamati, na ninawaomba ndugu Wajumbe katika hili tuwe na maazimio ya kweli. Miradi yote mipya ambayo inakwenda kuanzishwa, kwa mfano, unaenda kuanzisha Vituo vya Afya Vikubwa kabisa, ni vizuri miradi hii wakakabidhiwa Wakandarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii *Force Account* ambayo tayari na sisi tuliianzisha kwa mujibu wa sheria zetu, iendelee kubaki kusimamia miradi yenye ukarabati mdogo. Kwa sababu ni kweli, unakwenda kufanya ukarabati wa darasa lililochimbuka sakafu, unakataa kumtangaza Mkandarasi kwa suala la kumnunulia tu simenti kusogea pale, kumsogezea mchanga, halafu kuweka namna ya kulisimamia; tukifanya hivi, tutaenda kuokoa fedha nyingi kama ambavyo Serikali ilifikiria na pia tutajenga haya majengo na tutakosa hizi lawama ambazo leo tunatupiana hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukitusikiliza Waheshimiwa Wabunge unaweza ukaona kama kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanaonekana wanawaandama Wakurugenzi, lakini siyo kwamba tunawaandama kwa sababu eti hatuwapendi. Ndio wenzetu, ndio tunafanyanao kazi, na hakuna ambaye hajui kwamba hawa ni sehemu ya kazi ya Serikali. Tunachokizungumza, kwenye vikao vyetu vya Kamati, ukihojiana na hawa Wakurugenzi, ukiwasikiliza, kila mmoja anakutolea taarifa ya mradi huo huo unaofanana kwa lugha ambazo hazifanani. Zinasababisha Wajumbe kama watu wenye akili timamu kuona hapa ipo sababu inayomfanya huyu ajibu hivi na hapa ipo sababu inayofanya mtu huyu ajibu hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kwamba ni lazima Serikali iendelee kutekeleza miradi hii, lakini ni lazima tutumie mawazo ya Kamati, pia lazima tutumie ushauri unaotolewa na *CAG*, kwa sababu *CAG* anakuwa amepita kwenye yale maeneo na anaona

sababu za wazi zinazosababisha matatizo haya. Tukubaliane tuweke maazimio ambayo yatakwenda kutekeleza miradi hii.

Mheshimiwa Spika, mimi kama Mjumbe wa Kamati, naungana kabisa na ninaunga mkono Kamati yangu na ninaomba Bunge lifikirie hivyo kwamba miradi hii siyo yote inayostahili kufanywa na *Force Account,* kwa sababu hali ya utekelezaji wa miradi kule siyo nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lipo jambo lingine ambalo nalo tulitazame, na hili litazamwe kwa upana mkubwa sana na viongozi wa Serikali. Vifaa vyetu tunavyokwenda kutengenezea miradi yetu; simenti, nondo, rangi na vingine vyote, inawezekana lipo tatizo la ubora. Kwa sababu tukiangalia majengo ambayo yamejengwa miaka mingi ya nyuma, ukiangalia ubora wake, ukienda kulitazama na jengo linalojengwa leo jipya na vifaa hivyo, unapata mashaka kwamba yawezekana vifaa vyetu tunavyotengeneza kwenye viwanda vyetu vinaweza vikawa na ubora mdogo. Siyo kwamba nasema hivi kwa kuvituhumu hivyo viwanda vinavyotengeneza, lakini nataka Serikali itoe macho kwa kina ili iende ikatazame vifaa hivi vinavyotengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeenda baadhi ya maeneo, unaweza ukashangaa, ukiitazama *tiles* zinawekwa pale, kona hazifanani. Yaani maana yake, ukubwa wa *tiles* unatofautiana. Sasa ukishafikia kwenye hatua hii, maana yake ubora wa utengenezaji wa vifaa viwandani nao una changamoto zake.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph George Kakunda, atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Amos Bulaya na Mheshimiwa Ally Juma Makoa, ajiandae.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana nami kupata fursa hii ya kuchangia taarifa za Kamati zetu hizi mbili.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa jinsi ambavyo ameendelea kumimina fedha nyingi kwenye Majimbo yetu ili kutekeleza miradi mbalimbali ambayo inawagusa wananchi wetu moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, pili, nampongeza Mheshimiwa Rais, kwa jinsi ambavyo aliipokea Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, mwaka jana 2023 mwezi wa Tatu. Alionesha sura ya uchungu kulingana na mambo ambayo yalikuwa yameonekana ndani ya ripoti ile. Alitoa maelekezo ambayo mengi yamesaidia Serikali kufanya marekebisho mengi ya hapa na pale ambayo yamesaidia sana kuboresha maeneo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze *GAG* kwa taarifa ambayo ameendelea kuifanyia kazi kwa mujibu wa Ibara ya 143 na Ibara ya 144 ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania; na amekuwa anatoa ushauri, maoni, mapendekezo ambayo yamekuwa yakisaidia sana nchi hii kuweza kuthibiti maeneo mengi tu ya matumizi na kuboresha utendaji Serikalini.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa ambalo tunalo katika nchi yetu ni kwa watendaji kuwa na mwendokasi mdogo sana katika kutekeleza mapendekezo, maoni na ushauri wa *CAG*. Tukirekebisha hapo mambo mengi yatakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa taarifa za ukaguzi ambazo tulizijadili kwenye Kamati ni pamoja na ukaguzi wa ufanisi katika utekelezaji wa malengo ya maendeleo endelevu *SDGs*. Tumepitia Taarifa ya *CAG* na kwa kweli katika taarifa ile unaweza ukaona kwamba ufanisi wetu katika kutekeleza malengo ya maendeleo endelevu bado ni mdogo; na hautuhakikishii kwamba ifikapo mwaka 2030 tutafikia malengo ya maendeleo endelevu kama ilivyopitishwa na Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu gani? Miongoni mwa sababu ambazo zinaonesha kwamba tuna kasi ndogo katika kuelekea kuyafikia malengo ya maendeleo

endelevu ni pamoja na sisi wenyewe ndani hapa kama nchi kushindwa kukusanya mapato ya ndani ambayo tulikuwa tumeyabainisha wenyewe kwamba haya tutayakusanya.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2016 katika mikakati yetu tulikubaliana kwamba tutaanzisha vyanzo vipya vya mapato ambavyo ni dhamana za manispaa au *municipal bounds,* dhamana za uraia na uhamiaji, dhamana za hifadhi za mazingira, udhamini wa msongamano au *cloud financing,* miradi ya mfuko wa fedha, mifuko ya maliasili na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa Serikali haijajipanga namna ya kukusanya vyanzo hivi vya ndani ili viweze kutuongezea mapato ambayo yatasaidia kwenye utekelezaji wa malengo ya maendeleo endelevu. Sasa kama hatuna rasilimali fedha hii inatishia uwezo wetu wa kufikia malengo ya maendeleo endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kuwa hatujawasaidia wananchi wetu kikamilifu ili katika juhudi zao za kujiletea maendeleo na katika juhudi zao za kupambana na umasikini waweze kujikwamua na kulisaidia Taifa. Hivi ninavyozungumza wananchi wanashukuru sana. Tuliwapatia mbolea ya ruzuku kama sehemu ya mkakati lakini nakuhakikishia kwenye jimbo langu zaidi ya asilimia 60 ya mbolea iliyowekwa ardhini imeoshwa na maji ya mafuriko. Hatujawa na mkakati wa kuwasaidia wananchi namna gani sasa watajikwamua ili waweze kupata mazao ya chakula mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, wakulima wa tumbaku wamelima tumbaku mpaka nyuma ya nyumba. Maeneo mengi wamelima tumbaku kwa sababu wamevutiwa na bei ya tumbaku nzuri ya mwaka jana. Lakini mvua hizi za mafuriko zimesababisha tumbaku nyingi sasa imeharibika katika mashamba. Hatujawa na mkakati wa namna ya kuwasaidia wananchi wetu kujikwamua na tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini la tatu, asilimia 60 ya mabanda ya kukaushia tumbaku yameangushwa na mafuriko. Hatujawa na

mkakati wa kuwasaidia wananchi namna gani wanajikwamua na tatizo hilo, na hii ni hasara inayotokana na kwamba hatuna bima ya wakulima, yaani Tanzania hatujawa na bima ya wakulima (bima kwenye kilimo) kwa hiyo, akipata hasara anapata hasara mazima. Kwa hiyo jambo hili hatuwezi kupata maendeleo endelevu kama hatuna mikakati ya namna ya kuwasaidia wananchi wetu wajikwamue na matatizo ya *natural hazards* ambayo yanakuja kuwasababishia hasara kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nilitaka niliseme katika ukaguzi huu wa ufanisi wa maendeleo endelevu ni eneo la takwimu. Ili nchi iweze kujipima, lazima tuwe na mkakati mzuri wa kuratibu uzalishaji wa takwimu, uchakataji na upelekaji wa takwimu kuanzia ngazi za chini mpaka ngazi za juu. Tuna aina mbili ya takwimu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, aina ya kwanza ya takwimu ni takwimu za sensa na utafiti. Hizi zinakusanywa na *NBS* (Ofisi ya Takwimu ya Taifa), lakini aina ya pili ya takwimu ambayo ndiyo kubwa zaidi ni takwimu za kiutawala. Zinakusanywa na Ofisi za Vijiji, Kata, halmashauri mpaka inakuja Serikali kuu.

Mheshimiwa Spika, takwimu za sensa na utafiti ni asilimia 39 tu ya takwimu zote; na takwimu wa kiutawala ni asilimia 91. Tatizo kubwa ambalo lipo hapa nchini ni kwamba takwimu za utawala ambazo zimekuwa zinachakatwa, zinazalishwa na kuchakatwa na kuletwa huku juu ni asilimia 28 tu takwimu zote hizo asilimia 61. Kwa hiyo, ina maana kuna zaidi ya asilimia 30 ya takwimu ambazo hazikusanywi wala kuchakatwa. Hili linamfanya Mtakwimu Mkuu wa Serikali akose namna nzuri ya kuweza kuchakata takwimu zote za kitaifa ili aweze kushawishi vizuri Serikali mipango ya maendeleo. Namna hii hatuwezi kuratibu vizuri namna ya kuyafikia maendeleo endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukaguzi mwingine wa ufanisi ambao ningependa kuujadili hapa ni ukaguzi wa ufanisi katika ujenzi wa barabara za lami nchini. Ukaguzi huu umeonesha kuna ufanisi mdogo katika usimamizi wa mikataba ya ujenzi wa barabara na

ndiyo maana barabara nyingi zimekuwa zinaharibika ndani ya muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya *consortium* kubwa ya kimataifa ya tathimini za ujenzi wa barabara duniani ambayo inaitwa *DC Parking Lot International*, barabara ya *Asphalt* yaani hiyo lami aina *Asphalt,* iliyojengwa vizuri inatakiwa kudumu kwa muda wa miaka 25 bila matatizo makubwa. Katika miaka mitano ya kwanza inatakiwa isiwe na matatizo kabisa. Katika miaka 5 hadi 7 ndiyo kunaweza kukaanza mipasuko midogo midogo inaweza kuzibwa kwa urahisi. Katika miaka 7 hadi 15 mipasuko na vishimo vidogo vinavyoweza kuzibwa kwa urahisi vinaweza vikatokea. Lakini miaka 15-25 ndiyo utahitajika ukarabati wa gharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, sasa hapa Tanzania barabara zipo nyingi tu na mifano ipo ambayo inaonekana kabisa kwamba ndani ya miaka mitano barabara inahitaji ukarabati mkubwa ambao tungehitaji baada ya miaka 15-25. Mfano wa barabara ya Manyoni - Tabora tayari ina mashimo makubwa, ina maana tayari inahitaji ukarabati mkubwa lakini haina miaka minne.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hili jambo linahitaji kuangaliwa kwa ukaribu sana ili tuendelee kuhakikisha nchi yetu inapata maendeleo makubwa ambayo tunatarajia. Kwa hiyo, ni lazima maafisa Masuhuli wazingatie ufanisi…

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: …sheria ya ununuzi, wawe wazalendo na mimi katika hili…

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: …ningependa kusisitiza kabisa kwamba uzalendo ni kitu cha muhimu sana kuliko kusema tu tumetekeleza tumefanya hivi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ester Amos Bulaya atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mheshimiwa Geoffrey Idelphonce Mwambe ajiandae.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye Taarifa za Kamati zetu mbili. Kipekee kabisa niwapongeze Wenyeviti wa Kamati kwa taarifa zao nzuri, na Bunge kazi yetu kuamua Kamati zimefanya kazi, zimeleta, zimepika, wengine *LAAC* tunakaa mpaka saa sita usiku tuje tulete maoni ya kusaidia Taifa letu kwa sababu tuna nchi moja tu Tanzania ya kuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la *Force Account*. Kabla ya kuanzisha wazo la *Force Account* kulikuwa na misingi, taratibu, kanuni na miongozo mbalimbali, lakini pia kulikuwa na malengo ambayo tulikuwa tunatarajia tuyafikie kutokana na *Force Account*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja ya malengo ni kuwe na miradi yenye ubora, kupunguza gharama, kumaliza miradi kwa wakati. Waheshimiwa Wabunge lazima tujiulize kwa hali ilivyo na ripoti ya Kamati tuliyowaletea ambayo ni *sample* tu ya baadhi ya halmashauri, tumefikia malengo tuliyojiwekea? Kama hatujafikia tunahitaji tufanye nini kuokoa mabilioni ya shilingi yanayoenda kwenye halmashauri na mwisho wa siku hatupati matokeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja ya eneo la msingi ukienda kwenye miongozo ya TAMISEMI yenyewe, miongozo ya *Force Account,* ukienda kwenye Sheria ya *PPRA* moja ya *issue* ya msingi ambayo imesisitizwa kwenye *Force Account* lazima tuwe na wataalam wa kutosha kwa lengo la kuleta ufanisi na ubora wa majengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa *GAG* naye alifanya ukaguzi wa ufanisi kwenye miradi ya *Force Account* na ametuambia kwamba

wataalamu waliopo kwenye eneo la ujenzi, wahandisi, wasanifu majengo wapo 213. Wanaohitajika ni 859. Hivi kweli kwa idadi hii na mabilioni ya shilingi yanayoenda kwa wataalamu hawa wenye kusimamia miradi ya mabilioni ya shilingi, kutakuwa na ufanisi kweli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadhi ya wajumbe wamechangia hapa. Wametoa mfano, Namtumbo wahandisi wawili, wakadiriaji majengo mmoja, msanifu majengo mmoja. Idadi ya miradi ni 143. Kilwa, wahandisi ni wanne, mkadiriaji majengo mmoja, wasanifu majengo sifuri, miradi 157. Nzega - *DC*, mhandisi mmoja, mkadiriaji majengo mmoja, wasanifu majengo wawili, miradi 115. Mtwara - *DC*, wahandisi wawili, mkadiriaji majengo mmoja, wasanifu majengo sifuri, miradi 103. *Force account*, mabilioni ya shilingi, idadi ndogo namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mwongozo wa mwaka 2019 unaoleza ni namna gani majengo ya Serikali yaweze kuishi muda mrefu. Sasa kwa idadi hii ya wataalamu tumepita kwenye majengo ya bilioni za shilingi, shule inaisha, haijaanza kutumika kuta zina nyufa. Darasa limemalizika halijaanza kutumika, ukitembea na *high heels* unatoboa sakafu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tumeambiwa hapa kwenye mwongozo wa Wizara ya Fedha maana huku nako kuna kitengo cha mali za Serikali. Wanasema; "Ukijenga nyumba ya makazi inatakiwa iishi kwa miaka 50." Tujiulize Waheshimiwa Wabunge, kwa mradi huu wa *force account* kuna nyumba itakayoishi hapa miaka 50? *(Makofi)*

MHE. STELLA S. FIYAO: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Taarifa inatokea wapi? Mheshimiwa Esther Bulaya kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Stella Fiyao.

TAARIFA

MHE. STELLA S. FIYAO: Mheshimiwa Spika, nilitaka kumpa mzungumzaji taarifa kuwa kiukweli hii hali inatuletea hasara

kubwa sana kwenye halmashauri zetu. Mfano mzuri ni kule Momba, shule imejengwa ina mwaka mmoja lakini imeshachanika nyufa kutoka kwenye msingi mpaka juu. Kwa hiyo, hali ni mbaya sana, hii kitu inatuletea hasara sana kwenye halmashauri zetu.

SPIKA: Mheshimiwa Esther Bulaya unapokea taarifa hiyo.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, naipokea. Tumeambiwa kwenye nyumba za makazi tunajenga nyumba za waalimu, imekamilika imenyesha mvua paa linaondoka, kuna nyumba ya kukaa miaka 50? Tunaambiwa shule ikae miaka 75 kwa shule ambazo zinajengwa na fundi mchundo, kuna shule ya kukaa hapa miaka 75? Tunaambiwa hospitali ikae miaka 60, hakuna *engineer*, hakuna fundi mchundo. Kuna hospitali hapa ya kukaa miaka 60? Tunapeleka mabilioni ya shilingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini tunasema lengo hapa ni upunguza gharama, kuna pesa hapa zimeenda. Ukiona Mtama ijengwe pale shule miliioni 470 wenyewe wameongeza milioni 56 si lengo kupunguza gharama *Force Account*. Milioni 56 wanahitaji kukamilisha milioni 129 jumla ya mradi utagharimu milioni 655. Haya ukienda Nachingwea, 470 wameongeza 46 wanahitaji milioni 191 shule itagharimu milioni 718. Waheshimiwa Wabunge hatupingi ongezeko la gharama, lakini lazima liendane na hali halisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile hawa wakurugenzi wamekuja kwenye Kamati, tumekutana na mambo wenzenu, unamwambia tuambie ongezeko la nini? Hana *justification* ya ongezeko la gharama. *Force Account,* ndiyo maana tunasema, na ndiyo maana kuna mambo yanasemwa kuna cheni ya ulaji kutoka Wizara ya Fedha, kutoka TAMISEMI na kuja kwenye halmashauri. Ukimuomba mkurugenzi nipe *BOQ* mwingine hakupi mpaka umtishie kumfukuza kwenye Kamati. *Force Account*. Miradi mikubwa yote ni mibovu lakini ukienda kwenye ukarabati wa darasa unakuta hauna shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima tujipange, lazima tuone tulipoanguka. Tuwe na uchungu na fedha za walipa kodi. Nilikuwa naangalia hapa, Kamati ya *PAC* ni aibu, hivi magari kweli yanaweza yakawa dampo? *TAMESA* magari 547 na Serikali hii inapenda mashangingi, inapenda *VX*, inapenda *Land cruiser* zile *hard top*. Hivi nani anaweza akaacha gari yake gereji miaka miwili? Tunaona pesa hazina wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hizi pesa ambazo zimekaa kule *TEMESA*, magari 547 *is not fair,* ni nchi ni moja tu. Halafu kila siku wanaongeza idadi kule, halmashauri wanaomba hawana magari, kuna gari zimekaa pale kweli? Ndugu zangu tuna nchi moja tu inaitwa Tanzania, nzuri ya kuishi. Tunahitaji maamuzi, tunahitaji tuone huruma na fedha za walipakodi, wakati tunawaongezea kodi hizi pesa wanazozitoa ziende zikalete tija kwenye halmashauri zetu. Lazima tutimize wajibu wetu, tuwe na uchungu wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante, nakushukuru. naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ally Juma Makoa atafuatiwa na Mheshimiwa Geoffrey Idelphonce Mwambe. Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo ajiandae.

MHE. ALLY J. MAKOA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye Kamati hizi mbili. Nawapongeza Wenyeviti wote waliowasilisha mezani hoja hizi mbili na ninaunga mkono hoja pamoja na mapendekezo yote ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Rais na ninaipongeza Serikali yake kwa kupeleka fedha nyingi sana kwenye majimbo na kwenye halmashauri mbalimbali; na ukisikia hoja zetu zote hapa ni kwamba fedha zimekwenda nyingi sana lakini tatizo linalozungumzwa hapa na ukiangalia maoni ya *CAG* kunakuwa na usimamizi hafifu wa fedha zilizopelekwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hapa tatizo kubwa halipo tena kwenye Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan lakini tatizo lipo kwenye wale waliopewa mamlaka ya usimamizi. Sasa *CAG* tayari amekwishatuambia na Kamati zetu hizi mbili zimekwishaleta mapendekezo Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi sana kinachokosekana ni uadilifu, uaminifu pamoja na uzalendo wa watu wetu ambao wamepewa dhamana ya kuisaidia Serikali katika kuwatumikia wananchi. Jambo hili ni kubwa sana, kama tunataka kwenda sawa sawa ni lazima tujikite kwenye maadili ya watu wetu waliopewa dhamana. Lazima tupime uaminifu na uadilifu wa watu wetu hawa waliopewa dhamana ya kuzitumia hizo fedha kwa ajili ya miradi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, nitajikita katika hoja moja tu ya CAG ambayo na Kamati yetu tumeweza kuitolea mapendekezo, inayohusu usimamizi hafifu. Usimamizi huu hafifu ndio unapelekea miradi kuwa na *variation* kubwa, usimamizi hafifu unasababisha majengo yetu yajengwe chini ya viwango, lakini pia usimamizi hafifu unasababisha hasara kubwa sana kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halmashauri zilizokuja kuhojiwa, asilimia 100 wameshindwa kufuata miongozo wanayoletewa na Wizara ya TAMISEMI. Mmoja anaweza kufuata mwongozo asilimia 40, mwingine aka-*fail* kwenye mwongozo wa *force account* na mwingine anaweza aka-*fail* kwenye sehemu nyingine kama vile ile asilimia 10 ya wanawake, asilimia 4:4:2. Kwa hiyo, Wakurugenzi na Halmashauri nyingi zime-*fail* kuweza kufuata miongozo na ndiyo maana tatizo linakuwa ni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiukweli hali siyo nzuri sana, ukiangalia miradi yetu ambayo tunaletewa ambayo *CAG* kaipitia, kila halmashauri inakuja na ongezeko kubwa la zaidi ya kile kilichopangwa na TAMISEMI. Mimi siamini kwamba Wizara ikaleta ile *schedule of materials* halafu ikatoa nafasi kwa halmashauri na wataalam wa pale kutengeneza *BOQ,* halafu kukawa na

variation kubwa kiasi hicho na *variation* zenyewe hazina *justification*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiwauliza wahasibu na wakandarasi ambao wametengeneza hizo *BOQ* kiukweli utaionea huruma Serikali, anakwambia anahitaji shilingi milioni 200 ili aweze kukamilisha mradi ambao umepewa shilingi milioni 470. Ukimwambia tufafanulie hii shilingi milioni 200 inaongezeka wapi anaweze akaishia shilingi milioni 20 au 30. Hizi nyingine zote hana pa kuzipeleka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo tujikite kwenye maoni ya kwamba sasa TAMISEMI waweze kuwashughulikia watendaji wote ambao wamepewa dhamana halafu wanashindwa kutekeleza miongozo ambayo wamepelekewa. Kama ile mifumo ya ufuatiliaji wa miradi itakaa sawasawa, maana yake haya yote yanatokea ilhali pale halmashauri kuna viongozi, wilayani pale kuna viongozi na mkoa una viongozi lakini hali inakuwa kama hivi. Tunao Wakuu wa Wilaya, Mikoa, Ma-*DAS* na Ma-*RAS;* kama wote wakitekeleza wajibu wao vizuri kisawasawa tunaweza tukalinusuru Taifa letu na tukaweza kufanya miradi hii ikawa inaenda vizuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi wala sina shaka na *force account*, shida hapa ni uadilifu. Nilikuwa najaribu kuangalia miradi ambayo imetengenezwa na *force account,* lakini pia nikapitia baadhi ya miradi ambayo imetekelezwa na wakandarasi, badi hali ni ile ile, tatizo ni uadilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, iko miradi iliyotekelezwa na wakandarasi mwezi ulipita, leo ukienda kuitembelea ile miradi yote imesombwa na maji. Tofauti na kazi zilizofanywa na wazee wetu miaka ya 1970 na 1980; unaweza ukakuta miaka ile miradi yao mpaka leo ina-*survive,* lakini miradi ya wataalam wetu wa sasa inachukua muda mfupi. Kwa hiyo, tunafikia kupoteza fedha nyingi kwa sababu ya kukosa uadilifu. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, mimi pamoja na kuunga mkono hoja iliyoko mezani, bado nasisitiza kwamba hao hao waliopo kwa

uchache wake, hatuwezi kusubiri Serikali ikaajiri asilimia 100 ndipo miradi ikatekelezwa. Kwa hao hao ambao tunao wakati Serikali inaendelea kushughulika na kutafuta uwezo wa kuajiri basi waliopo waendelee kusisitizwa katika uadilifu wa kusimamia fedha za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

SPIKA: Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge tunao wageni waliokuja Bungeni kipindi hiki cha pili.

Tunao wageni wa Mheshimiwa Antony Mavunde ambaye ni Waziri wa Madini, hawa ni wanawake 60 wa Kikundi cha Uchumi wa Viwanda (WAUVI) kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao viongozi na wanachama 30 wa CCM kutoka Kata ya Nzuguni, Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Geoffrey Idelphonce Mwambe atafuatiwa na Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, ajiandae.

MHE. GEOFFREY I. MWAMBE: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia na kipekee nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema, lakini pia niweze kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali yake ya Chama Cha Mapinduzi ambayo inafanya kazi kubwa kule Masasi kwenye jimbo langu, lakini pia na Tanzania kwa ujumla. Tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu waweze kuwa na afya njema, tuweze kuyafanya mengi kuelekea mwakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuunga mkono mapendekezo yaliyoletwa kwetu na Wenyeviti wa Kamati zote mbili; Kamati ya *PAC* na Kamati ya *LAAC*. Ni mapendekezo muhimu ambayo tungeomba sana sana Bunge tuyabebe, lakini pia na wenzetu wa Serikali tukishaazimia hapa yakafanyiwe kazi,

na isije ikaonekana kwamba wakati wote kazi yetu ni kutoa mapendekezo halafu wanafanya kazi asilimia 40, 42 au 48 na baadaye kusema kwamba utekelezaji unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nayasema haya kwa sababu kiukweli nchi yetu ni tajiri sana. Tunazo rasilimali fedha, lakini utumiaji wa hizo fedha ndiyo imekuwa ni changamoto.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi huu wa ufanisi ambao umefanywa ni sehemu tu ya maeneo mapana ya matumizi ya fedha, na sampuli ya ukaguzi wake haifiki hata asilimia 10.

Waheshimiwa Wabunge, hiki mnachokiona hapa ni maeneo machache sana ambayo yamekaguliwa. Tungekagua nchi nzima kwenye taasisi zote hali ingekuwa ni mbaya zaidi. Natamani ifike wakati hata sisi Kamati ya Bunge ya *PAC* au Bunge lako, tuweze kufanya tathmini ya kiwango halisi ambacho kimepotea kwa matumizi ambayo hayajaenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, napenda kijielekeza kwenye maeneo kadhaa, na nisingependa kueleza kwa undani sana kwa sababu Wenyeviti wamezungumza ila nataka nitoe msisitizo tu kwenye yale mapendekezo ambayo yametolewa na viongozi wetu hasa Wenyeviti wa Kamati, lakini pia na ushauri kwa wenzangu upande wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, la kwanza tumeona, tunasema maji ni uhai na kupitia Ilani ya CCM tuna lengo la kupeleka maji kwa wananchi wote. Tumeona hapa kuwa ukaguzi wa ufanisi uliofanywa kwenye uendelezaji na matengenezo ya miradi ya maji una changamoto nyingi. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati yetu ya *PAC* amezungumza sana hapa, lakini pia tumekuja kubaini kwamba kuna tatizo kubwa sana la mipango kutokuwa kamilifu. Mipango yetu siyo *comprehensive*, tunafanya nusu nusu kwa miradi midogo midogo mingi kwneye nchi teyu matokeo yake tunatumia fedha nyingi, lakini pia na usimamizi unakuwa ni shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kusisitiza wenzetu wa Wizara waweze kubeba haya mapendekezo, lakini pia ningependa kutoa ushauri kwao; kwanza, ifanye tathmini ya dhati kabisa juu ya utendaji wa mamlaka hizi ambazo zinasimamia uendelezaji na usambazaji wa maji mijini na vijijini.

Pili, taasisi za Serikali zinadaiwa shilingi bilioni 31.7 hazijalipa bili za maji; hivyo, kuzifanya hizi taasisi ambazo zinasimamia usambazaji wa maji kupata shida kwa sababu bajeti yao sasa inakwazwa kwa sababu taasisi za Serikali ni nyingi na zinatumia pesa nyingi sana. Napenda kumuomba sana Mheshimiwa Aweso, Waziri wa Maji, hebu atuambie hapa ikiwezekana atoe agizo kufikia tarehe 1 Julai, taasisi zote za umma zifungiwe *prepaid meters* ili kusiwe tena na hili tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu, tumeona tuna miradi mingi ya kutengeneza umeme kwa kutuma maji. Sasa badala ya kuwa na miradi mingi midogo midogo ya kuchimba maji hapa na pale kwa nini tusitumie maji yanayotoka kwenye *turbines* zinazozalisha umeme na kuelekea baharini kwenda kupotea, kwa nini tusiyatumie yale maji kuya-*tap* na kuyapeleka kwa wananchi. Tutakuwa na miradi michache, mikubwa ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Bwawa la Mwalimu Nyerere ambalo ni kubwa mno, lile bwawa ukubwa wake ni takribani kilometa 100. Ni bwawa kubwa mno, maji ni mengi, yakishatoka pale, yamezungushwa kwenye *turbines* na kuzalisha umeme yanaenda baharini, yamepotea.

Mheshimiwa Spika, mimi ninaomba Wizara ya Maji na Wizara ya Nishati wangeweza kufanya kazi pamoja, pale ambapo pana mradi wa maji basi yale maji yakishatumika kwenye kutengeneza umeme, yaweze kuchukuliwa na kupelekwa kwa wananchi. Sisi watu wa Mtwara na Lindi tungetamani sana yale maji ya Rufiji ambayo ni mengi sana, ufanyike usanifu tuweze kupata *design* ya mradi wa maji ili maji mengine yaelekee upande wa Lindi na Mtwara na mengine waende Dar es Salaam ili kuweza kutatua changamoto, kuliko kujielekeza kwenye miradi midogo midogo ambayo tuko nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulipata taarifa kutoka kwa *CAG* juu ya ukaguzi uliofanywa kwenye vituo vya afya vya hiari na binafsi, hizi *charitable organizations* pamoja na hizi *private health facilities*. Kwa kweli vituo 518 vilikaguliwa na yalibainika mambo mengi. Kwanza, ni asilimia 18 tu ya vituo ndivyo vilionekana vina vyota tatu kwa kuwa vina *facilities* za msingi za kumhudumia mwananchi. Pia Baraza la Famasia inaonekana halikufanya mapitio ya miongozo yake kwa sababu kwenye vile vituo kunakuwa na famasi na maabara. Kwa hiyo, zile mbili huwa zinasimamiwa, ili tusipate kesi ambazo tumeziona karibuni hapa kwamba ukienda kwenye maabara za mitaani, lazima uandikiwe *UTI, Typhoid, H.Pylori* na kila kitu ili utoke pale na dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukaja kuona kwenye ukaguzi ule kwamba asilimia 32 ya leseni ambazo zilikuwa zinasimamia maabara na famasia zilikwisha muda wake, kwa hiyo, hata kupitia vile vigezo vya msingi vya usajili vilikuwa vimeshapitwa na wakati. Vituo 65 vya maabara vilivyokaguliwa ambavyo ni sawa na asilimia 49 vinaonekana kwamba havina wataalam wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, sasa kwangu mimi naona kama haishangazi kuona sasa kila familia kuna mgonjwa wa kansa na kila familia kuna mgonjwa anahitaji matibabu ya figo na hasa hii ambayo juzi Mheshimiwa Naibu Waziri alizungumza hapa kuhusu kusafisha figo *(dialysis)*. Sasa hivi *dialysis* ni *fashion*, tunahangaika kununua vifaa, haturudi nyuma kuangalia ni nini kimesababisha sasa magojwa ya figo kuwa ni mengi na magonjwa ya kansa kuongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninaomba Serikali mrudi kwenye utafiti, mkafanye *very scientific research* kwamba sababu ambazo zinatumika kwa sasa kuelezea hoja za kuongezeka kwa tatizo la kansa na figo ni nini. Mimi naona ni utumikaji wa madawa kiholela. Ningeweza kuwashauri sana Wizara, wenzetu kule Ujerumani, hizi *health facilities* zote pamoja na famasi zote zimeunganishwa kwenye Mfumo wa Afya wa Serikali. Ukienda hospitali labda Nzuguni kuna *clinic* pale, utakapomuona daktari akakuandikia anakwandikia kwenye *system* ya Serikali. Ukitaka

kwenda kuchukua dawa famasi mjini pale, sijui Nanenane au wapi; pale kwenye famasi wanaangalia jina lako kwenye *system* kwa sababu wao wenyewe wapo wanakuona kwamba ni daktari fulani alikuhudumia kule ndiyo wanakupa dawa, lakini huku sasa unapitia tu famasi, unapata dawa unakunywa haijalishi unaumwa, umepimwa wala hujijui. Kwa hiyo, kwa kweli tulilinde Taifa letu na tuwajibike upande na kuhakikisha lwamba wananchi wetu tunaokoa maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine dogo ambalo ninataka niliseme ni kuhusiana na uondoshaji wa magari ya Serikali, amelizungumza sana Mheshimiwa Simon Songe, Mjumbe mwenzangu wa Kamati ya *PAC* pale. Kwa kweli inaumiza, ukiacha mapendekezo ya Kamati, mimi nina ushauri kwa Serikali na hasa kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ni vizuri kupitia *GAMIS* tutengeneze *either* mfumo mwingine au tutengeneze *module* ndani ya *GAMIS* ili magari yote ya Serikali tuyaweke ndani ya mfumo halafu tu-*calculate formula* ya *salvage value* ili kila gari inapoanza kutumika barabarani i-*calculate salvage value* mpaka mwisho wa matumizi ya gari. Kama ni miaka mitano au labda, kilometa 200,000 na baada ya hapo gharama yake inajulikana na *disposition* inatakiwa ifanyike ndani ya siku 30 au 60 gari itoke tuweze kuokoa fedha ya umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na naunga mkono hoja kwa mara nyingine. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, atafuatiwa na Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, ajiandae.

MHE. SUMA I. FYANDOMO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia jioni ya leo. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa namna ambavyo ameniwezesha kwa kunipa afya njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Halima Mdee ambaye ndiyo Mwenyekiti wangu wa Kamati ya *LAAC* kwa namna ambavyo amewasilisha vizuri hoja ya Kamati, lakini pia

nampongeza Mheshimiwa Kaboyoka, Mwenyekiti wa *PAC*, mmewasilisha vizuri sana hoja za Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye mchango wangu mimi ninajikita kuchangia kwenye eneo la *force account* na niliwahi kuchangia mchango hapa unaohusu *force account*, naongea kwa uchungu sana, kwenye *force account* kuna fedha nyingi sana zinapelekwa kwa ajili ya miradi. Ni mabilioni ya pesa, lakini cha kusikitisha ukiangalia hapa kutoka kwenye Taarifa ya *CAG* kati ya miradi 175, miradi 24 ndiyo majengo ambayo yamejengwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna wazalendo ndani ya Taifa letu la Tanzania, lakini wakati huo huo kuna watu wengine ambao si wazalendo, yaani baadhi ya watumishi sio wazalendo.

Mheshimiwa Spika, hili Taifa la Tanzania litajengwa na sisi wenyewe Watanzania, haiwezekani tufikirie kwamba kuna watu watatoka nchi za Ulaya waje watujengee Taifa letu la Tanzania. Uzalendo unatakiwa ujae ndani ya mioyo yetu ili kusimamia fedha hizi za walipa kodi ambazo zinapelekwa kwenye hii miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kati ya miradi 175, ni miradi 24 kwa maana ya majengo ambayo yamepelekewa fedha nyingi za Serikali, ukitoa hapa majengo 24 tu ina maana majengo 151 hayako kwenye ubora. Ni nini maana yake? Majengo haya ndiyo ambayo wanapokuwa wanakwenda kukagua sasa kwamba hili jengo limesimamiwa na viongozi husika ambao walikuwa wanasimamia hayo majengo, matokeo yake mnakwenda kukagua hayo majengo *tiles* zinabomoka zenyewe, bado halijaanza kutumika. Mnaenda kukagua hayo majengo, maji yanamwagika, kwa sababu vifaa vile ambavyo wamefungia siyo *high quality*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilichangia hapa kuhusu *force account,* nilipata simu tofauti tofauti hata *voice notes* niko nazo kwenye simu ambazo hata mafundi ambao wanawatumia huko kwenye mambo ya *force account* hata wao hawapendi haya. Walikuwa

wananipongeza kwamba umesimama kuongelea *force account*, sisi kama mafundi utakuta tunawaambia kwamba hapa inatakiwa tuweke nondo milimita 16, wanasema tuweke nondo milimita 12. Sasa ubora utapatikana kutoka wapi? Lakini wakati huo huo kama itawekwa nondo milimita 16, kama zilitakiwa nondo nane sehemu husika zinawekwa nondo nne au tano, uimara utatoka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaongea kwa uchungu sana, mimi nikiwa Mjumbe wa Kamati ya *LAAC*, hawa ma-*engineer* wa Tanzania wengi ni wazalendo na ni watenda haki, kama wapo ni wachache sana. Kwa nini nasema hivi, hawa ma-*engineer* ambao wanatakiwa wawekwe, ambao ndio wataalam, kati ya 859 wanakuwepo wataalam 213, nini maana yake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika miradi utakuta Halmashauri moja ina miradi 150, ndani ya hiyo Halmashauri yupo *Engineer* mmoja na wakati huohuo *Engineer* mwenyewe hata usafiri wa kwenda kukagua hizo *site* kwamba basi ndiyo aweze ku-*move* aende hapa, aende hapa gari hakuna la kwenda kukagua miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikuwa na nia njema kabisa ya kuanzisha *force account* lakini matokeo yake sasa yamkini walianza vizuri lakini kadri siku zinavyozidi kwenda *force account* inakuwa ni tatizo ni ugonjwa mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili linajieleza wazi taarifa ya *CAG* ya Ukaguzi wa hayo majengo, kama ndani ya majengo 175, majengo 151 hayafai, unategemea nini baada ya miaka 10 ijayo, si yatakuwa ni magofu tu? Hayo majengo yatakuwa magofu tayari tumepata hasara ambapo hizo ni fedha za walipa kodi pia tunatakiwa kuwa na uchungu wa haya majengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natamani sana kuishauri Serikali kama watadhani *force account* iendelee kuwepo basi miradi ama kama ni ukarabati, fedha isizidi milioni 50 ikizidi sana milioni 100, akini haya majengo tunayojengewa bilioni tatu, bilioni nne kwa *force account*. Juzi nilikuwa nasikiliza Tunduma kwenye ziara ya

Mheshimiwa Makonda, shule ambazo zinakwenda kujengwa shule hii ni shule mpya, anapewa bilioni tatu, shule moja imejengwa kwa bilioni tatu, lakini ramani ni hiyo hiyo, shule nyingine wamejenga bilioni tatu zimekwisha na bado wanaitaka Serikali ipeleke fedha nyingine bilioni zaidi ya mbili ili wakamilishe shule.

Mheshimiwa Spika, wakati huohuo fedha zinaingizwa kwenye akaunti za shule, Mwalimu anaambiwa fedha zinaingizwa kwenye *account* yako usimamie shule mpya ndiyo inaenda kuanza kujengwa. Huyo Mwalimu lini amesomea Ukandarasi kwamba sasa Mwalimu anaacha kufundisha anaenda kuwa *Engineer* anaenda kusimamia majengo, wataandaa saa ngapi, maana Mwalimu wanamwambia yeye aunde Kamati, akiunda Kamati ambayo itakuwa inasimamia ujenzi huo kwa fedha mabilioni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, si tu Mkuu wa Shule hata wakati fulani fedha zinaingizwa kwenye *account* anaingiziwa *DMO*. *DMO* inabidi aunde kamati ya kusimamia majengo ya hospitali, sasa hawa wagonjwa watasimamiwa na nani, watatibiwa saa ngapi wakati wako *busy* kuangalia huku? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukizingatia kwa upande wa mashule hizo Kamati, wanashirikisha na wanakijiji ama wana mtaan pale wao ni wataalam hao unaowashirikisha na ukizingatia hawana posho, kwa hiyo hawawezi kuweka mkazo, kwamba lazima waende kule kusimamia, wanasimamia kwa posho ipi? Kwa maana bajeti hapa haipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali na ninaishauri haya ninayoyaongea hata Wakurugenzi, wakija mbele si lugha nzuri sana, wakija mbele ya Mheshimiwa kwenye Kamati yetu pale tunavyowahoji, tunavyowabana, Mkurugenzi anaweza akawa ana miezi miwili tu hapo hajui chochote. Hawa wataalam ambao wapo wakiambiwa elezeni kuliendelea nini, wanakuwa hawana majibu, hawajui chochote yaani hata mimi ambaye si fani yangu ile najua hapa ningetakiwa nijibu nini, najua hapa nilitakiwa niongee nini, si fani yangu, lakini wenyewe ambao ndiyo

wamesomea hawawezi kujibu, hawajui chochote. Pale kwenye Kamati ya *LAAC*, kwa kweli kwa wazalendo wa kweli *pressure* zinapanda kila siku unasikia uchungu moyoni jinsi fedha za Serikali zinakwenda ndivyo sivyo.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Hussein Amar.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Spika, nataka nimpe taarifa mzungumzaji haya anayozungumza ni kweli, kwa sababu tumeona hata kwenye ukaguzi wakati wa Mbio za Mwenge miradi mingi inakutwa ni mibovu na kuna wataalam.

SPIKA: Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo malizia mchango wako dakika moja, unaipokea taarifa hiyo.

MHE. SUMA I. FYANDOMO: Mheshimiwa Spika, ninaipokea hiyo taarifa. Katika kuipokea taarifa kwa majengo hayo tunayosema ni mabovu yaani ukilinganisha tu 175 ripoti ya *CAG* majengo 24 ndiyo salama tunakwenda wapi, baada ya miaka 10 ijayo majengo yatabaki magofu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia ninaunga mkono hoja, ila naomba Serikali ilichukulie kwa uzito sana kwamba *force account* isiendelee, ama sivyo kwa bajeti isiyozidi shilingi milioni 100, ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, ajiandae.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili na mimi niwe miongoni mwa Wabunge ambao wamechangia kuhusiana na taarifa za Kamati ya *PAC* na Kamati ya *LAAC*. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *PAC*.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kumpongeza sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuendelea kuiletea maendeleo nchi yetu ya Tanzania, ama kwa hakika Mama apewe maua yake kwa namna ambavyo ametuheshimisha Watanzania, lakini kubwa zaidi ambavyo ametuheshimisha wanawake wa Tanzania wote, tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumze nina mambo mawili tu leo sina mambo mengi, nina suala linalohusiana na miradi ya barabara lakini pia nina suala linalohusu *force account*, sasa naomba nianze na miradi ya barabara. Nichukue nafasi hii pia kumpongeza *CAG* ambaye pia ni jicho letu katika Kamati zetu hizi anafanya kazi nzuri sana ya kufukua fukua maovu na upigaji ambao unafanyika katika nchi yetu ya Tanzania. Hongera nyingi sana kwa Kaka yangu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali Ndugu Charles Kichere, nakupongeza pamoja na *delegation* yako yote kwa namna unavyofanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tarehe 15 Februari, 2024 naenda kuchangia kama ifuatavyo. Kumekuwa na ujenzi wa barabara pesa nyingi za Serikali zinapelekwa katika miundombinu ya ujenzi wa barabara huko, lakini Wabunge wengi wamezungumza uzalendo ndiyo tatizo, Mzalendo namba moja ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wanaofuata baadhi yetu wamekuwa si Wazalendo katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, pesa zinapelekwa lakini ukiangalia zipo barabara ambazo tayari zimeharibiwa sana ni barabara ambazo zinatakiwa kujengwa upya zenye zaidi ya kilometa 519 katika nchi yetu. Naomba nitaje hizo barabara na namna urefu wa kilometa zake zilivyo na namna ambavyo zimeharibiwa, kuna barabara ya Bagamoyo – Msata, yenye urefu wa kilometa 49, barabara hii utafikiri imejengwa wakati wa Uhuru, barabara ina mashimo, barabara imeharibika vibaya, sielewi aliyekuwa anajenga hii barabara alikuwa anatumia nini! Nataka niseme kwamba ujenzi huu wa hii barabara unatakiwa uanze upya maana yake ni kupelekea Serikali mzigo mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ipo Barabara ya Dodoma – Iringa, ina urefu wa kilometa 260, barabara hii ina viraka na barabara hii ni ya muda mfupi tu mpaka sasa hivi imeshaharibika vibaya. Barabara imemomonyoka, pia kwenye hii barabara ni barabara ambayo inaundwa na udongo ambao unakuwa na maji yaani chepechepe lakini kana kwamba haitoshi iliwekwa tabaka moja tu la lami, nataka niseme ni namna gani ambavyo pesa nyingi zimetumika lakini barabara haina ubora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Ruangwa - Nanganga - kilometa 69 barabara hii haifai. Nzega – Tabora - kilometa 50.3 barabara hii haifai. Masho – Mwigumbi - kilometa 50 haifai. Loliondo – Mto wa Mbu - kilometa 49 haifai. Tanga – Pangani - kilometa 50, haifai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niseme barabara hizi zina urefu wa kilometa zaidi ya 519, zimetumia pesa nyingi mabilioni ya pesa na sasa hivi hazifai tena zinatakiwa zikwanguliwe, zianze kujengwa tena kwa kiwango cha lami.

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Spika, tazama namna gani ambavyo pesa hii inapotea.

SPIKA: Mheshimiwa Jacqueline Msongozi Ngonyani, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Innocent Bashungwa.

TAARIFA

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Msongozi, anachangia vizuri lakini kwenye orodha anazozitaja baadhi ya barabara ndiyo kwanza zinajengwa sasa hivi. Kwa mfano, Barabara ya Tanga – Pangani, Mkandarasi yupo *site* anajenga hajaweka hata ile *sub base*, sasa kwenye mchango wake angebainisha na kujikita kwenye barabara ambazo anataka kujenga hoja, lakini si kuchanganya kwamba barabara zote zimeharibika wakati kuna barabara ambazo mpaka sasa hivi

hata *level* ya kuweka lami bado, lakini anahesabu kwamba barabara tayari imeharibika. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, unaipokea taarifa hiyo.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba unilindie muda huo, lakini jambo la pili, Mheshimiwa Waziri ana muda wake wa kuchangia na yeye kwa hiyo achaukue hizo *details* zote aziweke pembeni atapata muda muafaka.

Mheshimiwa Spika, hiki ninachokisema mimi sijakitoa kichwani kwangu ni jicho la *CAG* limeona. Kwa hiyo, mimi sijatoa kichwani kwangu. Naendelea kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, haya yote yanatokana na usanifu mbovu ambao unafanyika na Washauri Elekezi hawasimamii vizuri miradi hii, kungekuwa kuna Washauri Elekezi wazuri maana yake haya yasingejitokeza.

Mheshimiwa Spika, pia kumekuwa na ucheleweshaji wa malipo ya pesa kwenye miradi hiyo, jambo ambalo linapelekea kuweka hasara kubwa sana kwenye miradi hiyo, mpaka kufikia Juni, 2023 pesa za Kitanzania yaani riba ambayo inatakiwa Serikali ilipe ni zaidi ya bilioni 701. Nilikuwa najiuliza tu, hivi kwa nini sasa Serikali inampa Mkandarasi kazi ili hali inajua kwamba hakuna pesa na hatimae kwenda kutengeneza riba hii hapa ambayo ni hasara kubwa. Pesa hii shilingi bilioni 701, nilikuwa nafikiria tu hivi fedha hii isingeweza kwenda kujenga barabara ya Likuyufusi – Mkenda yenye urefu ya kilometa 124, inayotoka Songea Mjini mpaka kwenda kuunganisha Nchi ya Mozambique na Tanzania, ikaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Spika, pia nikawa najiuliza tu hivi pesa hii shilingi bilioni 700 inayoenda kupotea kwa maana ya Serikali kwenda kulipa riba hivi ingepelekwa pale kwenye barabara ambayo ni ya Mtwara, Pachani - Lingusenguse – Nalasi – Mbesa na hata kutokeza Tunduru yenye urefu wa kilometa 305, pesa hii ingetosha

kabisa kujenga na ingebaki ikaenda kujenga barabara ambayo inatoka Lumecha – Londo kwa Mpepo - Morogoro, inaunganisha Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Ruvuma, pesa hii ingetosha kabisa kujenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pesa hii sasa inaenda kuchukuliwa na inaenda kulipwa huko kwa sababu tu ya kwamba wale Wasanifu wameshindwa kufanya kazi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naenda sasa kwenye *force account*. Kwa masikitiko makubwa sana, masikitiko makubwa sana, kwamba *force account* imekuwa ni sehemu, ni kichaka cha kujificha watendaji wetu. Nia ya *force account* ilipokuwa inawekwa ilikuwa ni kusaidia ujenzi kwa haraka lakini pia kupunguza gharama, lakini kilichotokea sivyo. Nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mkurugenzi wa OSHA, Ndugu Khadija Mwenda, ambaye amefanya kazi nzuri sana kwenye Jengo la OSHA, pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, amejenga jengo lile, ametumia *force account*, amemaliza lile jengo na pesa imebaki, lakini wale wote ambao wameweza kufanya vizuri, wamepelekewa pesa na wametumia hiyohiyo mpaka wamemaliza hiyo miradi kwa kweli waandikiwe barua za pongezi. Hawa ambao wanafanya …

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Spika, wanafanya mishemishe za kutengeneza mazingira …

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Bashungwa mbona unanifanyia hivyo. *(Kicheko)*

SPIKA: Mheshimiwa Bashungwa, taarifa mbili kwa Mbunge mmoja? Haya karibu.

TAARIFA

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Msongozi ili aweze kuchangia vizuri. Bilioni 701 anazozitaja ni madeni ya Wakandarasi siyo riba, kwa hiyo kama anataka kujenga hoja ya riba ajenge kama hoja ya riba lakini hizi bilioni 701 ni madeni ya Wakandarasi, ambayo wanadai ya malimbikizo. *(Makofi)*

SPIKA: Aah! sasa hayo madeni ya Wakandarasi yana uwezo wa kuzalisha riba kiasi gani, bilioni 700 riba ikitokeza, itatokeza ngapi ili ndiyo aiseme hiyo Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, riba zinakuwa *calculated with time*. Kwa hiyo, mpaka Disemba mwaka jana ninaweza nikaleta taarifa kwa sababu ni hoja ya kitakwimu tulikuwa kwenye bilioni 68 hivi.

SPIKA: Bilioni 700 inaweza ikazalisha bilioni 68.

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ndiyo.

SPIKA: Haya. Mheshimiwa Msongozi

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, zinakuwa *generated with time* lakini kwa takwimu za mpaka Disemba, 2023 ilikuwa *around* hiyo bilioni 68.

SPIKA: Sawa. Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, kuna taarifa hapa inayohusu takwimu kwamba umesema bilioni 701. Bilioni 701 ni madeni kwa mujibu Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, anasema hayo ni madeni ambayo wanadai Wakandarasi, ambayo hayo madeni yana uwezo wa kuzalisha takribani bilioni 68 kwa mujibu wa Mheshimiwa Waziri, unaipokea taarifa hiyo.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Spika, yaani mimi namshauri tu Mheshimiwa Waziri awe anasoma. Kwa kweli, namheshimu sana lakini mimi haya mambo sijayatoa kichwani kwangu taarifa ya CAG hii hapa! Sijayatoa kichwani kwangu,

taarifa hii hapa imesomwa na Mheshimiwa Kaboyoka, Mwenyekiti wa Kamati pele amewasilisha sijaitoa kichwani kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea lakini pia naomba unilindie muda wangu.

SPIKA: Subiri kwanza Mheshimiwa, muda wako ulikuwa umeshaisha dakika moja malizia hoja yako.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nilikuwa nataka tu nifafanue namna ambavyo *force account* inafanyika. Ni kwamba pesa inatoka TAMISEMI, inapelekwa moja kwa moja kwenye *account* ya shule, Mwalimu Mkuu anaiona ile pesa anaitwa na Mkurugenzi Halmashauri. Akishafika kwa Mkurugenzi Halmashauri, Mkurugenzi ndiyo anaanza kumpangia sasa na kumpa maelekezo ya matumizi ya zile pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkandarasi anayeenda kujenga kule shuleni ni Mkandarasi ambaye anapewa maelekezo na anakabidhiwa na Mkurugenzi. Kwa hiyo, mwisho wa siku ikitokea kuna changamoto wale Wajumbe wa ile Kamati wakiuliza jambo yaani kama ni Mjumbe akiuliza jambo anaonekana huyo ni tatizo anapigwa chini, lakini mwisho wa siku Mkurugenzi yule anapoona kwamba mradi ule haujatosha, maana yake ni nini, anaanza kulaumiwa msimamizi lakini anasahau kwamba ile *ten percent* ameshaipiga kule na Walimu wamebaki tu ni kusimamia, kuangalia mbao zinafanyaje, kuangalia misumari inagongwaje na kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nataka kusema kwamba hii *force account* iangaliwe upya. Kama ingekuwa amri yangu pekee yangu ningesema futilia mbali turudi kwenye suala la Wakandarasi ili Mkandarasi akipewa ule mradi asipokamilisha atachukua na hela zake za mfukoni ataenda kuweka pale. Kama amefanya tofauti atachukuliwa atawekwa ndani, hapo nadhani umenielewa. *(Makofi)*

SPIKA: Haya, ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Spika, kwa maana ya hiyo dakika moja nakushukuru sana naunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, ajiandae.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie taarifa zetu hizi. Kwanza na mimi nikiri kukubaliana kabisa au kuunga hoja mkono taarifa zote mbili za Wenyeviti wetu wa *LAAC* na *PAC*, nikiwa natokea kwenye Kamati ya Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, tuliyojadili sana kwenye taarifa zetu kwa kipindi hichi ni taarifa za Ukaguzi wa Kiufanisi. Kuangalia si tu fedha tulizopeleka lakini fedha tulizopeleka zimekuwa na thamani gani au na mchango gani katika miradi ambayo tulikuwa tunaikusudia kama Taifa.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaeleza lolote, nitumie nafasi hii nami kumshukuru sana sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuitendea haki sana Halmashauri ya Wilaya ya Ubungo hususan Jimbo la Kibamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi sana, jimbo lile lilikuwa linakaribia kuzikwa (niseme). Wananchi wa jimbo lile walikuwa wanatamani hata kuhama, wote tu, lakini leo katika huduma za jamii zote; nikizungumzia shule, shule mpya saba; nikizungumzia eneo la afya, hospitali mpya kaijenga Mheshimiwa Rais Mama Samia, lakini shule ya Mkoa wa Dar es Salaam, ile ya shilingi bilioni 4.1 kaijenda ndani ya Jimbo la Kibamba. Pia juzi nimekabidhi *ambulance*.

Mheshimiwa Spika, mambo ni mengi, mambo ni mazuri. Yaliyobaki niliwahi kusema hapa, ni machache, lakini mwisho wa siku mambo ni bam bam.

Mheshimiwa Spika, uniruhusu nijielekeze kwenye maeneo machache. Moja, ni eneo la ufanisi wa ukaguzi katika miradi ya maji hasa mijini. Jicho letu *CAG* amefanya kazi kubwa sana. Pamoja na kazi kubwa ambayo anafanya mwamvuli wetu katika eneo la maji ndugu yangu Mheshimiwa Aweso, lakini ukweli jicho linamwonesha kuna upungufu mkubwa sana katika usimamizi wa miradi hasa miradi mikubwa.

Mheshimiwa Spika, moja, mipango hamna, taratibu hakuna katika ofisi au hizi mamlaka za maji bila usimamizi wa miradi husika. Hata matumizi ya ufanisi kwenye mitambo tunayowekeza, ile mitambo mikubwa ya gharama kubwa uwezo wa kuitumia hawana. Inawezekana hapa sasa kunahitajika kuwa na mafunzo ya hali ya juu kwa wataalamu wetu ili waweze kuitumia.

Mheshimiwa Spika, katika mamlaka nane ambazo jicho limeweza kuangalia au *CAG* ameweza kuzipitia unaweza kuona kwa kiwango cha chini kabisa Wakala wa Maji wa *RUWASA* na *SUWASA* chini ya 22% kuweza kusimamia mitambo iliyowekezwa. Zaidi ya hilo, kutosimamia kule maana yake imesababisha wananchi katika maeneo yale au halmashauri zile wameshindwa kupata maji ilhali uwekezaji ulikuwa unatosha kabisa wananchi wale waweze kupata maji.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana, angalau katika zile nane, mbili zilizofanya vizuri ni *DAWASA* na *DUWASA,* yaani kwa maana ya 100% hapa Dodoma na kwa 78.5% kwa Dar es Salaam. Kwa hiyo, unaweza ukaona angalau kuna mafanikio katika maeneo hayo. Mapungufu haya yote wanatoa sababu wao. Wana sababu kama tano; moja, ni kukatika kwa umeme, wanasema ni moja ya sababu inayowafanya washindwe kufanikisha usimamizi wa maji na kusambaza maji mijini.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kupungua kwa nguvu za umeme, *low voltage*. La tatu ni ubovu wa pampu na uchakavu wa miundombinu. Hii *sample* ilifanyika kwa miaka mitatu 2019/2020 hadi 2021/2022 miaka mitatu, lakini sasa hivi tunavyozungumza, Dar es Salaam Jimbo la Kibamba wana siku ya 34 changamoto ya maji zaidi ya mwezi mmoja watu hawana

maji, lakini sababu ni hizi hizi tena, wataalamu wanatuambia *low voltage*, miundombinu imechukuliwa na maji na sababu nyingine kama hizi pampu Ruvu Juu pale, ndani ya miaka mitatu labda haijatengenezwa.

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri atoe jicho, aangalie sana, kazi anaifanya kubwa, lakini anaweza kuangushwa na wataalamu wake katika jambo hili. Yaani ninavyozungumza, hatuna maji Dar es Salaam. Jimbo la Kibamba wananchi wa maeneo mengi hawana maji zaidi ya wiki tatu, lakini kuna mmoja alizungumza, Mheshimiwa Mwambe juu ya madeni, baadhi ya taasisi za Serikali kutolipa madeni ya maji. Zaidi ya shilingi bilioni 43.3 ni madeni.

Mheshimiwa Spika, kwanini hawalipi wakati kwenye bajeti zetu tukipitisha hapa tunaweka *token* kwenye *utility?* Shida ni nini? Wanatumia katika matumizi mengine au ni nini? Katika hili tumshauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ni vizuri na kama ananisikia vizuri, wataalamu wake kama wapo, ni vizuri sasa mkali-*reinvest* fedha kwa ajili ya *utility* ili moja kwa moja fungu la 21 – Hazina *(Treasure)* iweze kulipia madeni haya, kwa sababu hawa watu inaonekana tukiwapa wanatumia kwenye matumizi mengine, lakini tukizifunga, zitaenda kutusaidia katika malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, tunaambiwa eti ni taasisi zile nzito nzito. Kwa sababu mimi niliwahi kuhoji kwenye Kamati, sasa kama ni kwenye taasisi zile nzito, kama majeshi na megine na kadhalika, hizi fedha si ndiyo kwanza tunaweza tukaanza kuwapa wao! Tunampelekea nani? Tukimaliza madeni ya Serikali *(public dept)*, mishahara, tunapeleka kwao. Kwa hiyo, wataweza kulipa madeni. Nafikiri, ndiyo maana nakumbuka zamani tuliambiwa kaa, kaa. Ee, maneno mawili, lakini sijui kama tunaendelea nayo yale maneno mawili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikitoka katika eneo hilo, kuna jambo la Mradi wa *DMDP page* ya 114 ya taarifa ya Kamati yetu. Nashukuru sana katika ukaguzi wa ufanisi, katika mradi wa *DMDP* awamu ya kwanza ulifanya mambo mazuri na makubwa na

wananchi wengi wa Dar es Salaam wanajua, na Waheshimiwa Wabunge ambao wanakaa Dar es Salaam Kijichi nimeiona lami inatembea, Temeke nzima, Buza na maeneo machache ya Kinondoni kwa maana ya Sinza mataa mazuri, Mburahati na maeneo mengine yote ni *DMDP one,* tumefaanya kazi nzuri. Zaidi ya *US dollar* ya milioni 330.3 na zaidi ya milioni 300 hizi tumepata kutokea Benki ya Dunia. Kwa hiyo, tuwashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, upungufu mdogo ambao ninaamini katika nyakati za miradi ambayo inakuja karibuni watafanyia kazi, mfano changamoto ya muda kuongezeka kutoka miezi 15 hadi miezi 26, laini ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi kutoa siku 33 hadi siku 295 miezi 10 unachelewa kumlipa mkandarasi, lazima hata deni litaongezeka.

Mheshimiwa Spika, ziada ni *certificate of completion*. Unatoa *certification* ya kumaliza kazi kabla hata kazi haijaanza. Kwa hiyo, nawaomba sana *TARURA* kupitia hii *DMDP,* hii *DMDP* inayokuja sasa, ambayo sisi Dar es Salaam, nafuu imesomwa hapa, tunaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, siasa ya Dar es Salaam ni miundombinu. Hatuna siasa nyingine, nilisema asubuhi. Sisi hatuna siasa ya uvuvi, hatuna siasa ya kilimo, siasa yetu ya msingi ni barabara tu ili uchumi wetu uweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwenye eneo hili anatutendea haki, *DMDP* ya kwanza ilihusu wilaya tatu; Temeke, Ilala na Kinondoni, sasa hivi ameiongeza Kigamboni na Kibamba au Ubungo ambapo na wananchi wa Kibamba wanaenda kukutana na kilometa 23 hizi vizuri kabisa. Kwa hiyo, niwaambie kabisa, kazi ya Mheshimiwa wenu Issa Jumanne Mtemvu inaendelea kuwasemea Bungeni mliponileta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia kidogo sana ni eneo la urasimishaji. Kazi imeendelea kufanywa vizuri katika page ya 131 limesemwa jambo la urasimishaji. Namshukuru sana Mheshimiwa Mabula kwa kuendelea kufanya kazi nzuri akiwa Naibu na baadaye Waziri baada ya Mheshimiwa Lukuvi na sasa mdogo

wangu Mheshimiwa Jerry William Silaa, Mbunge wa Ukonga anaendelea kufanya kazi vizuri, anatupa ushirikiano mzuri katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatambua changamoto unazo sana, zimesemwa kwenye taarifa, sitaki kuzisema. Taarifa imesomwa na Mheshimiwa Mwenyekiti, japo changamoto nyingi ambazo zimesababisha, hamjafikia malengo. Mpaka sasa hivi chini ya 10% ndiyo hati nchini mmezipata. Kwa hiyo, nataka niseme, mmekuja kwenye bajeti ya sasa hii iliyopita ya 2023/2024, mlituambia dola za Kimarekani milioni 150 ambayo ni takribani shilingi bilioni 345, na shilingi bilioni 61 zitakuwa ni kwa ajili ya urasimishaji, naombeni mkazitumie.

Mheshimiwa Spika, najua mmeanza kazi kupitia madawati, mmefanya kazi nzuri sana, mnaanza kwa awamu, nendeni mkaharakishe ili wananchi wapate hati.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi naunga mkono hoja ya Kamati.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Esther Nicholous Matiko, atafuatiwa na Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe na watoa hoja wajiandae.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza kabisa nawapongeza Wenyeviti wetu wa Kamati ya *LAAC* na *PAC* kwa ripoti nzuri ambayo wametuletea hapa. Nitaunga mkono Maazimio yote kwa kweli, ni mazuri yaweze kufanyiwa kazi. Mimi ni Mjumbe wa *PAC* na nitazungumzia moja kati ya maazimio ambayo tumeyaweka ya uondoaji wa magari ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *CAG* alikuja ndani ya Kamati yetu na tukaita Maafisa Masuuli kuhusiana na ukaguzi wa ufanisi wa uondoaji wa magari ya Serikali aidha kwa kuyauza kwa njia ya mnada au kuwakopesha watumishi wa umma au kuwauzia watumishi wa umma. Kuna upungufu mwingi ambao uliainishwa

na kuoneshwa na *CAG,* madhalani kuegesha magari kwa muda mrefu bila kutengenezwa au kuondolewa kwa maana ya kuuzwa.

Mheshimiwa Spika, kwa ripoti ya *CAG* ilionesha magari 547 yaliweza kuegeshwa na katika hayo magari 547, asilimia 43 yalikuwa yamewekwa *TEMESA,* asilimia 53 yalikuwa kwenye hizi taasisi mbalimbali ambazo ni katika taasisi 10 tu ambazo alizitembelea, nje ya taasisi zote ambazo zipo katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika hayo magari yaliyoneshwa kuegeshwa zaidi ya miaka mitatu. Hii inasababisha athari mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mfano mojawapo, ukiyaegesha muda mrefu bila kuyaendesha yanachakaa na kupungua thamani. Hata ile *value for money* maana yake unakuta umeagiza gari kwa ajili ya matumizi fulani lakini unaliacha linalipaki kwa muda mrefu, nitolee mfano, mimi natoka Mara, gari lilikuwa katika Halmashauri ya Rorya, limeingizwa likiwa na *zero kilometer,* likafanya kazi wa muda wa miaka mitatu tu, lakini likaegeshwa kwa miaka 10 kwa hitilafu ndogo tu ndani ya *gear box,* baadaye likaja likauzwa kwa shilingi milioni nane, gari la zaidi ya shilingi milioni 130. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni upungufu ambao unaweza kuuona kwa magari yote 540 kwa hii *sample* ndogo tu ya taasisi 10 uweze ku-*assume* kwa magari ya taasisi zote ndani ya Serikali ni kiasi gani? Mabilioni ya fedha kiasi gani ya Watanzania yanapotea?

Mheshimiwa Spika, lingine, *CAG* aliweza kubainisha dosari katika uthaminishaji wa magari hayo wakati wanataka kuyauza ambapo katika taasisi ambazo alipitia alichukua *sample* ya magari 500 tu. Katika hayo magari 500, magari matano yalikuwa *overvalued* kati ya 1% na 36%. Magari matatu ndiyo yalianza kuuzwa kwa thamani halisi, lakini magari 492 yalikuwa *undervalued.* Yaani magari 310 yalikuwa *undervalued* kati ya 10% na 100%. Magari 148 yakawa *undervalued* kati ya 101% mpaka 200%, magari 34 yakawa *undervalued* katika 200% mpka 836%. Yaani kama gari ameliuza shiling milioni 10, kiuhalisia kama ni 836%

imekuwa *undervalued* ilitakiwa liuzwe shilingi milioni 83.6 na hii ndiyo maana *CAG* akaainisha ikasababisha hasara ya shilingi bilioni 2.7.

Mheshimiwa Spika, hii ni *sample* ndogo sana kwenye hayo magari unapata hasara ya shilingi bilioni 2.7 wana-*undervalue* magari haya bei zake. Wanauziana, baadaye wanaenda kuyauza kwa bei ya juu zaidi, unakuta wamepoteza fedha za Watanzania masikini walipa kodi, na sote tunajua kwamba magari ya Serikali yanayonunuliwa mengi ni zaidi ya shilingi milioni 100 kwenda juu, lakini wanakuja wanaya-*undervalue* wanauza shilingi milioni tano, shilingi milioni mbili, shilingi milioni 10, shilingi milioni 20. Hii haikubaliki.

Mheshimiwa Spika, hizi fedha zingeweza kupelekwa na hata zikajenga mabweni, hosteli za watoto wetu wakawa wanasoma kwenye shule za kata tukapunguza mimba za utotoni, lakini zinapotea hivi hivi. Hosteli tu inaweza ikajengwa kwa shilingi milioni 150. Mathalani hizi tu ndogo za *2.7 billion* zingeenda kujenga hosteli zaidi ya 18 watoto wetu wakasoma na tukaokoa mimba za utotoni ambazo zimekithiri hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine, ripoti iliweza kuainisha kwamba wakati wa uingizaji wa magari, maana yake hapa Wizara inayohusika ni Wizar aya Fedha, Wizara ya Ujenzi, na pia walikuja watu wa Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Uthaminishaji wa magari wakati wa ununuzi, tumeona gharama wanazoziweka siyo halisia. Yaani wanachukua tu *CF value* wakati imefika bandarini, wanaacha gharama nyingine ambazo zina-*count* kwa asilimia 53 kwa bei halisi kama zingeweza kuwekwa. Wanaacha vitu kama *VAT,* tunajua lazima ziwekwe hata kama zitakuwa zina *exemption,* kodi ya ushuru wa bidhaa, kodi ya ushuru wa forodha, kodi ya maendeleo ya reli na mengine mengi. Unakuta wanayaacha na usajili wa namba husika. Kwa hiyo, unakuta wana-*undervalue*.

Mheshimiwa Spika, ripoti ya *CAG* imeonesha kwamba walipitia magari 27 tu wakaona kulikuwa kuna *undervalue* kwa zaidi ya 83% ya hayo magari 27 ambayo ilisababisha hasara ya

shilingi milioni 957 za Kitanzania kwa magari 27 tu. Sasa ukichukua *sample* ya magari yote Tanzania, ni mabilioni ya hela ambayo yanapotea ambayo yangeweza kufanya kitu kingine, lakini unakuta yanapotea kwa uzembe tu mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kingine kwenye uondoshaji wa magari, tumeweza kuona kwamba kumekuwepo na ucheleweshaji wa vibali. Kama nilivyosema mwanzo, unakuta kama magari yanataka kuondolewa, kwa mfano Wizara ya Fedha, imeoneshwa kwamba wanatumia kati ya siku 57 mpaka siku 2,226, yaani kuweza kutoa *go ahead* ya gari kuweza kuondolewa inatumia miaka sita na mwezi mmoja kuweza kuidhinisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii kama nilivyosema ndiyo inasababisha gari kukaa zaidi ya miaka 10, miaka mitatu na kuendelea kuchakaa zaidi. Pia, hata Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imeainisha pia na wenyewe wanachukua kati ya siku nne mpaka siku 2,050 (miaka mitano) kuweza kuidhinisha uondoaji wa magari haya ili yaweze kuondolewa na kuweza kuuzwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya yote yanaweza kuonekana kama dosari. Walipokuja tuliweza kuwahoji wakakiri kwamba moja ni Mwongozo kupitwa na wakati kwamba wanatakiwa wauhuishe. Sasa unaweza ukajiuliza, mwongozo ambao umekaa muda mrefu tangu mwaka 1988, unauacha mpaka jicho la *CAG* lipite ndiyo uje kwenye Kamati na kukiri kwamba ni dhaifu ambalo unataka kufanya.

Mheshimiwa Spika, kingine walikiri kwamba ni kutumia mfumo ambao ni *manual,* hawaendi kwa kutumia mfumo wa kisasa wa TEHAMA. Tunajua kwamba kupitia *GAMIS* mbayo imeanzishwa 2018, Afisa Masuhuli wa Wizara ya Fedha akakiri kabisa mbele ya Kamati kwamba pamoja kuwepo kwa mfumo huu wa *GAMIS,* lakini hakujaweza kuwekwa *module* ya uondoaji wa magari yaa Serikali. Kwa hiyo, kuanzia 2018 mpaka sasa hivi wanaendelea kufanya vitu *manually, business as usual,* pesa za Watanzania zinapotea.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana maazimio yetu yamekuja hapo na ndiyo maana tunasema lazima yatiliwe mkazo kabisa. Huwezi kuwa una *system* ambayo ina-*account assets* nyingine za Serikali, unaacha hiki ambacho kinatumia fedha nyingi za Watanzania, unasema kwamba bado hamjaweka hiyo *module*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dosari nyingine ambayo ilionekana ni uwazi wa uondoaji wa haya magari ndani ya taasisi zetu. *CAG* aliweza kubainisha kwamba katika taasisi nane ambazo alitembelea, ni taasisi tatu tu ambazo ziliweza kutoa tangazo pale unapotaka kuondoa haya magari kwenye taasisi husika. Taasisi tano hazikuweza kutoa matangazo haya ikiwepo Wizara ya Fedha, Mahakama ya Tanzania, Jiji la Tanga, Halmashauri ya Mpwapwa na Wakala wa Barabara.

Mheshimiwa Spika, kutokuwepo na uwazi kunasababisha madhara haya. Kwanza, inanyima fursa watumishi wengine kuweza kujua kama kuna gari ambalo linataka kuwa *disposed* ili na wenyewe waweze kuomba. Pili, inatoa mwanya kwa baadhi ya Watumishi wa Umma kuweza kujinunulia. Tukienda tena mwakani kama gari inauzwa, anachukua huyo huyo, yaani unakuta ni wale wachache kwenye *cycle* wanachukua hayo magari.

Mheshimiwa Spika, kingine ilionesha kwamba ni mwongozo ambao haupo, ambao umepitwa na wakati, haujamtaka Afisa Masuuli kuweza kutoa tangazo pale ambapo anataka ku-*dispose* haya magari, kuwatangazia watumishi wa umma na kuweka uwazi zaidi. Sasa katika kwenda katika maazimo haya ya Kamati, tunaitaka Serikali iainishe mwongozo ambao uta-*incorporate* mambo yote ambayo ni kama udhaifu, lazima aweze kuonesha thamani halisi ya magari haya, ni muda gani yanatakiwa kuwa *disposed;* mfano, yakifikisha miaka mitano, yakipata ajali, ikiwa yamechakaa yanataka kutengenezwa, yaani ni lazima waainishe haya yote.

Mheshimiwa Spika, pia je, ni kwa baada ya muda gani? Kwa mfano, mimi Esther Matiko nimekopeshwa gari, ni baada ya

muda gani tena naruhusiwa kukopa gari katika taasisi husika? Haya yote yataweka uwazi mkubwa.

Mheshimwia Spika, mwisho kabisa, iwepo sheria; ije Sheria ya *Chief Valuer* awe anafanya uthamini wa mali zote za Serikali pamoja na haya magari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Deogratius Ndejembi na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, ajiandae.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kwanza niseme naunga mkono hoja ya Kamati zote ambazo zimewasilishwa Mezani. Niseme kwamba ufanisi wa Kamati zetu, *LAAC* pamoja na *PAC* umetokana pia na umahiri wako kwa namna ambavyo umeendelea kutupa ushirikiano sisi Wanakamati, kututia moyo na kutuomba tuhakikishe tunalitendea haki Bunge lako. Kwa hiyo, matunda ya ubora wa taarifa nzuri ambazo zimewasilishwa hapo Mezani yanatokana na ubora wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa niishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa namna ambavyo imepeleka pesa nyingi sana kwenye Majimbo yetu. Serikali ya Chama cha Mapinduzi imepeleka pesa za kutosha ni jambo ambalo halifichiki, nasi wote tukiwa hapa ndani tumekiri, na kwa namna tofauti kila mtu amemzungumzia vizuri sana Mama kwa namna ambavyo ameonesha moyo wake wa upendo kwa Watanzania wenzake na kudhihirisha kwamba kweli yeye ni Mama yamkini tofauti na watu walivyokusudia.

Mheshimiwa Spika, jicho letu la Bunge ambaye ni *CAG* anajaribu kuonesha namna ambavyo pesa hizi nyingi ambazo zimetafutwa na Mwanamama huyu shupavu na Mwanamama huyu mwenye huruma kuna mahali imeenda hazijatumika kikamilifu. Kwa hiyo, inawezekana mafanikio ambayo

tunayaongea sasa na muda huu yalipaswa kuwa maradufu, maradufu, maradufu.

Mheshimiwa Spika, yamkini hata bajeti ya *TARURA* ambayo tunaiongelea sasa ilibidi sasa hivi ingekuwa imeshafikia hata shilingi trilioni mbili kutokana na pesa nyingi ambazo zilikuwa zimetafutwa na Mheshimiwa Rais, zingeweza kusimamiwa kikamilifu zingeweza kufanya kazi ambayo imekusudiwa.

Mheshimiwa Spika, pia kumekuwa kuna kasumba moja, mimi nimfananishe Mheshimiwa Rais ni kama mzazi ambaye umemtafutia mtoto wako shule nzuri sana, ukamlipia na ukampa gharama yote ya kila kitu ambacho anakitaka, jukumu la mtoto. Jukumu la mtoto kufanya vizuri sio la mzazi tena ni la mtoto mwenyewe, hakuna namna ambavyo mzazi huyu atatoka pamoja na kumpenda mtoto wake ataenda kumfanyia mtihani ili aweze kufaulu awe kama mzazi wake, hapana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Rais ametekeleza vizuri majukumu yake kikamilifu, changamoto wako baadhi ya watu wachache wasio kuwa waaminifu, wasio kuwa wazalendo ndio ambao wanafanya mwaka jana tumesoma taarifa hii tunarudi kuongea mambo hayo hayo, *CAG* amebaini kitu hawataki kujirekebisha, halafu kwa bahati mbaya wamekuwa wakikimbilia kujificha kwenye kichaka cha Mheshimiwa Rais. Makosa wafanye wao na *CAG* amewabainisha kabisa, vitabu viko wazi vinawataja kama ni taasisi hii nani watendaji hawa wanatajwa, lakini unakuta oh, Serikali! Serikali? Mheshimiwa Rais hapa anaingiaje? Wewe kama ni mbadhirifu ni mbadhirifu tu na *CAG* amekuainisha. Wamtofautishe Mheshimiwa Rais na wizi na ubadhirifu ambao wao wanafanya wasimuunganishe kwenye hayo matukio. Yeye ni kama mzazi ambaye ametafuta shule nzuri kwa mtoto, jukumu la mtoto kufanya mtihani vizuri ni mtoto mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea na mchango wangu, kwenye ufanisi ambako *CAG* alitupitisha sisi kama Kamati na tukaja na maoni. Nataka angalau nirejelee kidogo ziara ya Mwenezi wetu wa Taifa Mheshimiwa Makonda.

Mheshimiwa Spika, nilijaribu kufuatilia kidogo kuona ziara ambazo alikuwa anafanya Mheshimiwa Makonda, nilikuwa naangalia labda *clip* moja kwenye kila mkoa nikaanza kuongeza *clip* mbili, nikaanza kuongeza *clip* tatu. Nilichokigundua, wananchi hawa inawezekana wamesikilizwa lakini changamoto zao hazijatatuliwa, na wakati mwingine kusababisha hata chama chetu kuonekana hakifanya majukumu yake ilihali kuna watu wachache ambao wamepewa dhamana wamekasimishwa madaraka yao hawajataka kutendea kazi majukumu ambayo wamepewa ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ana kipande kikubwa sana cha nchi hii hawezi kafanya kila kitu na ndio maana aling'amua madaraka yake akaweka huyu fanya hivi, huyu fanya hivi. Kwa ushauri tu, mimi niziombe baadhi ya wizara, mfano Wizara ya Katiba na Sheria, tunaomba ifike kule chini kusikiliza kero za wananchi. Yale mambo yote ambayo wananchi walikuwa wanalalamika, wao ndio wanasimamia Katiba na Sheria mahali ambapo panaonekana wananchi hawajatendewa haki, si wafike wawasikilize? Lakini Wizara ya Ardhi, ipo baadhi ya migogoro unaona kabisa, kwa mfano tuchukulie Waziri mwenye dhamana, Naibu Waziri, Katibu kwenye hii Wizara, Kamishana wa Ardhi wangekubali kuzunguka walau majimbo karibu 200 wangekutana na hayo matatizo ambayo hayakupaswa hata Mwenezi yeye awe anaendelea kuyatatua.

Mheshimiwa Spika, lakini na wizara zingine ambazo zinahusika na maisha ya wananchi moja kwa moja kwa mfano, tunaomba TAMISEMI wapite kwenye majimbo yetu, inawezekana mambo hayo hayo Wabunge wameshaongea hapa Bungeni lakini wakati mwingine walichukuliwa tofauti lakini Mwenezi amepita huko kwenye maeneo wananchi wameendelea kuyalalamikia hayo. Hayo mambo mengine sio ya Mheshimiwa Rais hata kidogo, Mama Dkt. Samia amekaimisha madaraka kwa watu wamsaidie.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo hiyo, wakati mwingine kwanza nirejee jukumu la Kamati yetu. Shughuli ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya *PAC,* kushughulikia maeneo yenye matumizi

mabaya ya fedha za umma katika Wizara, Idara, Wakala na Mashirika ya umma.

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine kumekuwepo na mianya ambayo inapelekea fedha zinapoingia zinatoboka na kutokwenda mahali ambako hakustahili. *CAG* katika ufanisi wa ukaguzi wake anaonesha kwamba kuwa na mifumo duni ya TEHAMA wakati mwingine inaweza ikasababisha kuwa na uvujivu wa pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali Mtandao, *eGA* ambaye yeye amepewa majukumu ya kusimamia miundo yote na mifumo yote ya TEHAMA hapa nchini. Yeye mwenyewe kuna mahali *CAG* anamzungumzia na kumkagua kuona kwamba yapo maeneo ambayop yeye hakutekeleza majukumu yake vizuri. Katika hili Serikali mtandao yeye mwenyewe pia ni chombo ambacho kinapaswa kuwezeshwa. Kijengwe vizuri atumie mifumo ambayo ni *high technology* ili aweze, yeye hawezi kusimamia mifumo yote kwenye taasisi mbalimbali ikiwa yeye mwenyewe anatumia mifumo ambayo sio *high technology*.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri ni *CAG* alitupitisha kwenye mifumo yake. Kiukweli kwa watu ambao wamesoma mambo ya TEHAMA ukiangalia namna ambavyo anafanya shughuli zake, anavyokagua mambo yake ya ki-TEHAMA unathibitisha kabisa uwezo wake kwamba anaweza aka-*penetrate* kwenye maovu yote na akaja na kitu ambacho ni cha maana.

Mheshimiwa Spika, *CAG* anasema kwamba kuwepo na mifumo duni katika taasisi zetu inasababisha vitu ambavyo vimesababisha, cha kwanza ni kuwa na sera ambayo imepitwa na wakati. Sera ambayo Serikali mtandao inatumia ni sera ambayo imeshapitwa na wakati ni ya miaka mitano huko kutoka 2017 mpaka 2022, hivyo kuwepo na sera hiyo mbovu inawafanya watu hawa washindwe klutekeleza majukumu yao vizuri na kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine kumekuwa na changamoto ambayo inawafanya hao watu wa *eGA*

wanaposhindwa kwenda kusimamia mifumo mbalimbali ambayo iko kwenye taasisi mbalimbali ilisababisha hasara kubwa ambayo Serikali yetu ya Tanzania ilipata kutokana na changamoto hizo ambazo hazitendewi haki kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, *CAG* anasema kwa mujibu wa ripoti ya usalama wa mitandao ya Tanzania mwaka 2017, Tanzania ilikadiriwa kupoteza Dola za Kimarekani, milioni 99 kwa kila mwaka kutokana na mashambulizi ya kimtandao, hii ni sawasawa na shilingi 268, 650,000,000.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Kengele imeshagonga Mheshimiwa.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine ambao CAG ameeleza…

SPIKA: Kengele imeshagonga Mheshimiwa.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Spika, la mwisho, jambo lingine ambalo *CAG* anaeleza, mifumo yetu mingi haisomani taasisi kwa taasisi, haisomani na haielewani, hivyo inasababisha kutokuwa na ufanisi mzuri katika kutekeleza majukumu ya ki-TEHAMA. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Spika, kwa ushauri Serikali iwekeze kwenye mambo ya Ki-TEHAMA kwa sababu dunia iliyoko sasa hivi iko kwenye kiwango kikubwa cha kutumia matumizi ya kompyuta ili tusiendelee kuibiwa, ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Deogratius Ndejembi atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa ajiandae.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI): Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kushukuru kwa nafasi hii ya kuchangia taarifa ya Kamati hizi mbili ambazo zimewasilishwa siku hii ya leo. Pia, nichukue nafasi hii kupongeza Kamati hizi mbili kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakifanya.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita katika Kamati ya *LAAC* ambapo pia nachukua nafasi hii kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati hii Mheshimiwa Halima James Mdee, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii Mheshimiwa Stanslaus Mabula na Wajumbe wa Kamati hii ya *LAAC* kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tuko tayari kupokea miongozo, maelekezo na maazimio ya Bunge lako Tukufu yatakayo toka hapa na tutakwenda kutekeleza kama vile ambavyo Kamati na Bunge lako Tukufu litaazimia hapa mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumesikia hapa Waheshimiwa Wabunge wengi wakichangia hoja juu ya *Force Account*, jambo hili ni zuri kwa maana nilinaokoa gharama kubwa. Ndio, kuna changamoto nyingi juu ya usimamizi wa miradi kupitia *Force Account*, na katika utatuzi wa changamoto hizi tayari Serikali imeajiri Wahandisi zaidi ya 362 kote nchini na katika hao kila halmashauri nchini walau ilipata mhandisi mmoja. Mwaka jana wa fedha Serikali iliajiri ma-*quantity Surveyor 100* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba mfumo mzima wa *Force Account* unafanya kazi bila kuwa na changamoto yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika*, Force Account,* natoa mfano; katika majengo yanayojengwa sasa ya shule za mikoa kuna mikoa ambayo ilitekeleza *Force Account to the T* kama ilivyotakiwa kwa mujibu wa sheria na wamefanikiwa vizuri sana na mpaka sasa shule hizo zimefika zidi ya asilimia 90 ya ujenzi wake katika zile shilingi bilioni tatu ambazo zilikuwa zimepelekwa. Hapo hapo kuna wengine ambao Mikoa mingine ilitangaza *tender* kupata wakandarasi na *BOQ* za Wakandarasi zilikuwa mara mbili ya

gharama ile ambayo ilikuwa imepelekwa na Serikali katika Mikoa hiyo, kwa hiyo utaona ni namna gani ambavyo *Force Account* inaokoa fedha nyingi ya Serikali katika ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa cha kusimamia ni ubora wa kile ambacho kinapatikana kama ambavyo kamati imewasilisha mbele ya Bunge lako. Nirejee tena kusema tuko tayari kwa ajili ya utekelezaji wa maelekezo ya Kamati yaliyotolewa na maazimio ya Bunge yatakayotolewa.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna michango ilikuja kwa ajili ya shule zile ambazo zilipelekewa shilingi milioni 470, tayari tathmini inafanyika na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuona ni wapi ambapo kuna mapungufu ili fedha iweze kutafutwa kujazilizia lakini wakati huo huo kuna ambao waliomba vibali maalum baada ya kupokea shilingi milioni 470 kuweza kujenga majengo ya ghorofa. Mfano, Tunduma *TC* walipopokea shilingi milioni 470 walikuwa na uhaba wa maeneo waliomba kibali cha kujenga ghorofa kwa kuongeza na mapato yao ya ndani, thamani nzima ya majengo yale itakuwa ni shilingi milioni 800. Liwiti, Shule ya Sekondari Liwiti, Halmashauri ya Manispaa ya Ilala waliomba kibali cha shilingi milioni 470 waweze kujenga ghorofa na wanaongeza kwenye mapato yao ya ndani, vilevile Nzega waliomba kibali kwa ajili ya kuweza kujenga ghorofa kwa mapato yao ya ndani.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kusimamia changamoto, narudia tena hatutamvumilia yeyote, kama ambavyo Kamati imependekeza, hatutamvumilia yeyote ambaye atazembea katika usimamizi wa fedha ya umma na tutachukua hatua mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tayari Serikali hii ya Awamu ya Sita imeanza kuchukua hatua kali dhidi ya wale wote ambao wameonekana kuzembea usimamizi wa miradi ya Serikali. Kuna wakurugenzi ambao wamepoteza teuzi zao kwa kutenguliwa, kuna wakuu wa idara za ujenzi ambao wametenguliwa teuzi zao, kuna wale wasimamizi wa miradi hii tayari wamechukuliwa hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nirejee tena nchi hii ni yetu sote na hapa mapendekezo ambayo yanatolewa ni kwa ajili ya kuboresha, katika kuhakikisha tunapata *value for money* katika fedha ya Serikali na Ofisi ya Rais, TAMISEMI italisimamia hilo chini ya uongozi mahili wa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa na kwa msaada mkubwa wa Kamati hii ya *LAAC* ambayo inatupa mapendekezo mazuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niseme naunga mkono hoja ya Kamati zote mbili zilizokuwa mbele yetu. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa naomba watoa hoja wajiandae.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, naomba na mimi nitumie fursa hii katika kuchangia kusema machache. Kwanza niwapongeze watoa hoja kwa taarifa nzuri ambazo wamezileta mezani.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema jana, moja ya mambo ambayo sisi Serikali hatubishani kabisa na Bunge ni masuala ya usimamizi wa fedha za walipa kodi wa nchi hii. Haya ni mambo ambayo hayana pande mbili, sisi na Wabunge tunaongea jambo moja.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa hapa Bungeni awamu ya tatu sasa na nimekuwa Serikalini awamu zote hizi tatu tangia nilipoingia hapa Bungeni. Moja ya Serikali ambayo inasikiliza tena kwa wakati hoja zinazotolewa na Bunge ni Serikali ya Awamu ya Sita, inasikiliza mara moja yanapokuwepo masuala na inachukua hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taarifa hizi ambazo zimefanyiwa kazi na Kamati za Bunge ni taarifa za mwaka juzi na siyo taarifa za mwaka huu. Ni taarifa za *CAG* za mwaka juzi na sio taarifa za mwaka jana. Matatizo haya ambayo yanabainishwa yalishasemwa kwenye taarifa zilizopita.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwa yamesemwa Serikali ilichukua hatua, tumeongea sana hili jambo la *Force Account*, na kwa nini Wabunge walikuwa wanalisemea sana, siyo tu kwenye taarifa hii, ilisemwa mwaka jana na ilisemwa na mwaka juzi. Ilikuwa inasemwa hivyo kwa sababu hakukuwepo na ukomo wala hakukuwepo na utaratibu unaoratibu jambo hili na ndio maana kwenye taarifa yamejitokeza haya.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana Tarehe 8 tumepitisha Sheria mpya na Tarehe 29, Septemba Mheshimiwa Rais alisaini Sheria tuliyopitisha hapa Bungeni. Kwa hiyo tunapoongea hapa ile Sheria ambayo Bunge lako lilipitisha ina miezi minne ndio unaenda mwezi wa tano, maana yake nini haya makosa ambayoyamebainishwa tayari Serikali lishachukua hatua na imefanyia kazi tena kwa kusaini Sheria mpya, kwa hiyo, tunatarajia baada ya Sheria hii kuanza kufanya kazi haya hayatajitokeza.

Mheshimiwa Spika, Sheria ile tuliyopitisha tuliweka mambo gani yaliyowekwa na Bunge:-

(i) Tulisema kwenye Sheria mpya Na. 76(1)(a) tulisema kazi za ujenzi ambazo ni ndogo zimetawanyika sana. Tulisema zile kazi zilizotawanyika sana, kujenga choo kwenye shule shikizi, hauwezi kusubiri kutangaza *tender,* unatafuta mafundi pale watengeneze choo;

(ii) Kazi za ujenzi ambazo zinatakiwa kutekelezwa kwa uharaka, daraja limekatika huwezi ukasubiri kutangaza *tender,* utafanya utaratibu wa haraka na utatekeleza kwa uharaka. Haya ni mambo ya msingi ambayo tunakubaliana;

(iii) Tukaweka masharti mengine kwamba matengenezo hayo yatakuwa ni sehemu ya shughuli za kawaida za kila siku;

(iv) Tukaweka tena masharti kwamba lazima pawe na watu wenye utaalam wa kuweza kusimamia jambo hili.

> Haya sio mambo ya kubishana wote tunakubaliana na haya Wabunge ambayo walikuwa wanayasema hata sisi wenzenu tulioko huku yametupata pia. Mimi ilitokea katika shule yangu moja pale Lulumba, katika mwaka ule shule ilikuwa kwenye tano bora za kitaifa, halafu ikatokea kwenye ujenzi *headmaster* hakusimamia vizuri wakataka wamtoe, mimi mwenyewe niliandamana kwenda kwa Waziri nasema Shule ya Iramba kabisa kule inaongoza kwenye *PCB* halafu yule Mwalimu Mkuu mnataka mmtoe kwa sababu ya ujenzi nikasema hapana huyu tulimleta ili wanafunzi wafaulu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, haya mnayoyasema, wote tunaongea lugha moja na ndio maana mlipoongea mwaka juzi na mwaka jana Serikali ilifanya haraka sana na tumeshabadilisha Sheria na kwenye ukomo tumeweka kiwango chochote kinachozidi milioni 100 hakitatekelezwa kwa *force aacount except* kwenye maeneo yenye udharura ambayo tunaweza kupeleka vyombo mahsusi vyenye ufundi maalum vikaenda kutengeneza. Mfano kama pale niliposema daraja limekatika, hayo ni maeneo ambayo wala hatubishani na wala hatuhitaji kubishana. Sisi Serikali tumekubaliana na Wabunge na Sheria imepitishwa tena kwa msaada wa Bunge tumepata hoja nyingi sana za msingi na kwenye kanuni tumezingatia mambo hayo.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna mambo ambayo kama nchi ni lazima tukubaliane; jambo la kwanza; Lazima Wakandarasi wetu wakue, wasing'ang'anie kujenga vyoo kwenye shule shikizi, wajenge miradi mikubwa. Tumepitisha kwenye Sheria kwamba wakandarasi wetu wanatakiwa wagombanie ile miradi mikubwa, Nchi yetu imekuwa bomba la kupitisha fedha. Tunatafuta fedha kule hata tukikopa ni fedha ambazo tutalipa kwa kodi zetu, wakandarasi wetu hawa wanang'ang'ania *sub contract, sub contract, sub contract* mpaka lini? Kujenga vyoo vya shule shikizi mpaka lini, kujenga Zahanati ya Kijiji ya milioni 12 mpaka lini? Darasa, darasa wajenge mafundi. Tugawe fedha zibaki kule kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, tumesema Wakandarasi Wakubwa wafanye miradi mikubwa na wale wa kutoka nje hatakama watachukua na wenyewe wana mataifa yao na wenyewe waombe kazi kwa wenyeji wa nchi hii ili wananchi wetu wa nchi hii wajijue kwamba wako kwenye Taifa lenye uhuru kwa zaidi ya miaka 60.

Mheshimiwa Spika, sasa leo hii tukisema mafundi wasifanye kazi, hizi kazi za shule shikizi ndio zifanywe na wakandarasi, choo cha shule shikizi kitangaziwe *tender*, tutakuwa tunasahau kumbukumbu ambazo tuliwahi kuzisema kwa ubaya sana haya mambo ya kuchelewesha hata kazi ndogo kwa ajili ya kusubiri kazi zifanywe kwa kutumia utaratibu wa *tender.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunakubaliana kuhusu uboro, ni jambo ambalo hatuna *compromise*. Tunakubaliana kuhusu udhibiti wa fedha, ni jambo ambalo halina *compromise* na hata hivi sasa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika mwaka mmoja tu baada ya kusikiliza hoja za Wabunge akaleta Sheria tumeshaipitisha, alishasaini na sasa kanuni ziko tayari tumeweka ukomo na tumeweka na utaratibu wa namna ya kuzingatia ubora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naamini hili jambo hata tusiliweke kwenye maazimio kwa sababu Bunge lilishatunga Sheria na Kanuni ziko tayari, wanasema tuweke utaratibu tumeshaweka, anasema tuweke ukomo tumeshaweka. Sasa tukubaliane tu kwamba labda Sheria ambayo tumeitunga mwaka jana hata haijaanza kufanya kazi kwamba haifai tuifute. Kama tunataka kufuta Sheria kwamba haifai hilo ni jambo lingine tunatakiwa twende kwenye Sheria, lakini kwa mujibu wa Sheria tuliyopitisha, tutakuwa na miradi ambayo itakuwa inafanywa kwa *force account.*

Mheshimiwa Spika, daraja limekatika hatutangazi *tender,* tutafanya kwa utaratibu wa haraka. Vyoo vya Shule shikizi hatutangazi *tender*, zahanati moja, darasa la milioni 12 hatutangazi. Tutatumia utaratibu wa mafundi walioko pale lakini tumeweka mwongozo ambao utawasimamia.

Mheshimiwa Spika, nimekwishaliongelea hili na sheria imetungwa na tumezingatia kanuni, na haya maoni yaliyotolewa na nyongeza ambazo tumezipata tutaboresha, na kwa bahati nzuri sana tuna muda wa kufanya hivyo kwenye kanuni.

Mheshimiwa Spika, haya mengine yameongelewa kwenye upande wa magari; haya pia siyo mambo tunayobishana nayo. Moja ya kitu ambacho Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anakipatia umhimu mkubwa sana ni usimamizi wa fedha za umma. Ndiyo maana tumekuwa tukiongeza fedha kwa *CAG* ili akague haya yote.

Mheshimiwa Spika, kwenye hili la magari mmpendekeza yale magari yote ambayo ni mabovu mabovu, lakini sisi mtazamo wa Serikali tunataka twende zaidi ya hapo. Mtakumbuka kwenye Hotuba ya Bajeti Kuu ya Serikali, tulitaka siyo tu kuondoa mabovu, Serikali tulitaka kuondoa magari. Bado linajadiliwa, limetengenezewa utaratibu ndani ya Serikali ili lijadiliwe na liweze kufanya vizuri, kuwe na utaratibu, hatuwezi tukawa na magari mengi yamezagaa na mengine hatujui yalipo, tunatumia gharama kubwa halafu tunafanya kama vile kufanya kazi ya kuwatumikia watu ni lazima upewe *incentive*. Hizi *incentive* zilikuwa zinatolewa wakati watumishi wa umma hawapo, yaani ukienda mtaani hivi hauwapati. Sasa hivi unaweza ukapanga hata safu nne, hata tano, yaani unabadilisha hii unaleta nyingine, unabadilisha hii unaleta nyingine, unabadilisha hii unaleta nyingine. Kwa hiyo, lazima watu wote waone ni heshima kuwatumikia wenzao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo haya yote ambayo yanafanyika hivi, yote yanatengenezewa mwongozo na haya ambayo Waheshimiwa Wabunge mmeyaweka hapa, sisi ndani ya Wizara tumeyapokea na kwa ajili ya muda ninaweza nisiweze kupitia moja baada ya lingine, lakini yote tumeyapitia, tutayafanyia kazi kwa haraka na usimamizi wake tutaufanyia kazi ili tuweze kuhakikisha kwamba rasilimali hizi zinafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwenye hili pia alitupia jicho, na si hili tu, ninyi mmeongelea magari ambayo yanakwenda sehemu tofauti tofauti, kuna maeneo mengine kwa upana wake ambao tunayafanyia kazi. Vifaa ambavyo viko kwenye Balozi zetu navyo kumekuwepo na ucheleweshaji wa aina hiyo hiyo. Yote na yenyewe aliunda Kamati ifanye kazi na wenyewe mmeona Kamati ile iliwasilisha juzi juzi hivi, na kila eneo ambalo lina dosari, Mheshimiwa Dkt. Samia amelitengenezea utaratibu wa kupata jawabu. Haya mambo tumpe heshima yake kwa kuchukua hatua, kwa sababu yangekuwa yanachukuliwa hatua, yeye ni Rais wa Sita asingeyakuta, angalau tumpe yeye kila jambo ambalo Bunge limesema kuna tatizo, amechukua hatua na hatua yenyewe inakwenda kwenye sheria ili kuweza kumaliza tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya muda niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba tumeyapokea, tunayafanyia kazi yale ambayo bado hatujayafanyia kazi kama Serikali na yale mengine ambayo yanahitaji tuyafanyie kazi zaidi, tutaendelea kuyafanyia kazi kwa utaratibu ule wa kiserikali. Serikali haijalala iko kazini, na haya ni mambo ambayo tunayafanyia kazi. Tunalihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali itahakikisha fedha zote za walipa kodi zinazopatikana zinafanya kazi kama ilivyokusudiwa na kama kuna mchwa hatutaacha hata chembe ya nyayo zake alizopitia kwenda kuharibu fedha za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 34(5) tutaendelea mpaka tumalize kazi iliyopo mbele yetu. Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Jerry Silaa, Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka ajiandae.

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja za Kamati mbili na mimi

niwapongeze Waheshimiwa Wenyeviti wote wawili wa Kamati hizi kwa hoja walizowasilisha.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, nchi yetu imekuwa na *checks and balances* ili kuweza kupata haya. Sisi kwa upande wa Serikali tunatekeleza na Bunge lina *monitor,* ku-*evaluate* na kutupatia ushauri. Kwa hiyo, ushauri wa Kamati tumeuchukua na tutaufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nitumie nafasi hii kutoa ufafanuzi wa baadhi ya mambo ambayo yamejitokeza wakati wa mjadala na nianze na hoja ambayo imesemwa na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, Waziri wa Fedha, baada ya Bunge letu kupitisha sheria ya kutoa wigo wa kusaidia wakandarasi wazawa kwa *threshold* kutoka bilioni 10 kwenda bilioni 50, tulikaa na Wizara ya Fedha na sisi Wizara ya Ujenzi tukaandaa *local content strategy* ya ku-*support* sheria hii.

Mheshimiwa Spika, wakati wa Bunge la Bajeti au kwa maelekezo yako, ningependa tuwaoneshe Bunge letu namna ambavyo tumejipanga ili kanuni ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha ataisaini ya kuongeza wigo ili wakandarasi wa ndani waweze kushiriki zaidi katika ujenzi wa nchi yetu, tukisema tuondoe *force account* tutakuwa huku tunatoa ustawi, lakini kwa mkono mwingine tunawaondolewa ustawi wakandarasi wetu wazawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo ningependa suala la *force account* tulipe muda, lakini pia muangalie ni kwa namna gani upande wa Serikali tumejipanga kwa hii sheria ambayo tumeipitisha ya kuongeza *threshold* ya ushiriki wa wakandarasi wa ndani kutoka bilioni 10 kwenda bilioni 50. Sisi Wizara ya Ujenzi kwenye hii *local content strategy* tunayo mambo mengi mazuri ambayo kupitia mfumo huu wa *force account* utasaidia sana wakandarasi wazawa.

Mheshimiwa Spika, vilevile hata hili ambalo limezungumzwa na Kamati ya *LAAC* kwa upande wa halmashauri zetu, wasanifu majenzi, wakadiriaji wa gharama za ujenzi, *engineers,* tunao

vijana wetu *graduate engineers* wengi ambao wanatafuta fursa za ajira, lakini kupitia *force account* baada ya hoja hizi za Kamati hizi mbili, kwa upande wa Serikali tutakaa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili tuangalie vijana wengi ambao wangependa kwenda *field* na kupata uzoefu ni namna gani wanaweza wakaenda kwenye halmashauri zetu kwa kupitia programu ambayo tunayo chini ya *ERB* (Msajili wa *Engineers* pamoja na Msajili wa Wakandarasi).

Mheshimiwa Spika, kupitia hii programu ya vijana *graduate engineers* ambao wanapitia programu ile, tutakaa na TAMISEMI tuangalie namna ambayo vijana hawa wanaweza wakaenda kwenye halmashauri wakashiriki katika kusimamia miradi, huku wanapata ujuzi lakini huku tunatatua changamoto ambayo imesemwa na Kamati zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kufanya haya tunaona ni jinsi gani kwenye upande wa *force account* tukilipatia muda na tukashirikiana, bado mfumo huu unaweza ukatusaidia kusimamia miradi huko kwenye halmashauri.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine ambalo ningependa kulitolea ufafanuzi na dada yangu Mheshimiwa Msongozi amekuja hapa tumeelewana vizuri, ni lile la madeni *versus* riba, zile bilioni 701 hata taarifa ya Mwenyekiti wa *PAC* ameitaja hapa kama ilivyo ni bilioni 701 ni madeni na siyo riba.

Mheshimiwa Spika, katika deni hilo nilitaja bilioni 68, baada ya ku-*check* na wataalamu wangu, kwa sababu ya *Hansard, as of December, 2023* ni bilioni 61. Kwa hiyo, naomba niweke rekodi sahihi. Kwa hiyo, bilioni 701 ni malimbikizo ya madeni na siyo riba.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni hili suala la *premature failure;* yaani barabara zinaharibika kabla ya ule muda uliopangwa au uliokadiliwa. Tumebainisha changamoto ambazo zinapelekea hili na niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, kwa miezi ambayo nimekaa kwenye Wizara tayari nimekwishakaa na

wataalamu. Changamoto ambazo zimejitokeza na ambazo zilikuwa zinasababisha haya ni *value chain* nzima kuanzia kubainisha miradi, hatua za manunuzi, usimamizi wa mikataba lakini na suala la baadhi ya watumishi kutokuwa waaminifu ku-*connive* na *consultants* pamoja na *contractors.* Haya yote tumekwisha yabainisha, na ndiyo maana nimesema kuna *checks and balances.* Tutajipanga kuhakikisha hii hali tunaikomesha kwenye sekta ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika pamoja na Waheshimiwa Wabunge, mmeona hata kwenye ziara zetu, nilipokwenda kule Kyela tukakuta mkandarasi ambaye amepewa kazi hana uwezo, amepewa kilometa 32, yuko nje ya muda, mitambo haijafika *site, key staff* hawajafika, lakini mkandarasi huyo huyo kule Sengerema Nyehunge amepewa kilometa 54. Tumechukua hatua na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ametusaidia, tunachukua hatua za kimkataba kumshughulikia huyo mkandarasi bila kuvunja sheria za nchi. Hata hivyo, wakandarasi wa aina hii tumeanza kuchukua hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, nikiwa natembelea barabara ya kule Mbinga (Amani Makolo – Luanda) tulikuta *consultant* ambaye ni mzembe, tulimsimamisha kazi lakini hapo hapo nikawambia wasaidizi wangu, inakuwaje miaka yote hii tunatumia *consultant* kutoka nje na bado tunakuwa na changamoto hizi hizi?

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kupitia hii *local content strategy,* tumeanza kuwajengea uwezo *consultant* wa ndani ili *with time* usimamizi wa barabara zetu usitegemee tu wakandarasi wa nje kwa sababu wakandarasi wa nje pamoja na *consultant* wa nje, changamoto hizi tumekuwa nazo wakiwa wanatusaidia kusimamia hii miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama nilivyosema kwa ujumla hoja zote za Kamati mbili tumezichukua, Serikali tunafanya kazi kwa kushirikiana, tunakwenda kujipanga lakini tumeanza kuchukua hatua.

Mheshimiwa Spika, kwenye hoja ya usimamizi usiorizisha wa barabara, pipo changamoto upande wa *consultants* hao niliowataja. Pia barabara nyingi kubwa unakuta ni hao wanaotoka nje. Tunawachukulia hatua za kimikataba.

Mheshimiwa Spika, vilevile, kwenye usimamizi wa hizi barabara, *Regional Managers* wa *TANROADS* nimegundua kumekuwa na changamoto, huku kuna ratiba labda ya Waziri fulani au kiongozi fulani kwenye Mkoa, *Regional Manager* anatakiwa kuwa kwenye kusimamia mradi wa barabara, lakini wakati huo huo kuna ziara za viongozi inabidi ashiriki. Kwa hiyo, wakati yuko kwenye ziara za viongozi, muda wa kwenda kusimamia barabara hana.

Mheshimiwa Spika, nimetoa maelekezo kwamba katika miradi yote lazima kuwe kuna *project engineers.* Kwa hiyo, tayari kila mradi ndani ya nchi yetu uwe mdogo au mkubwa, tumeweka utaratibu wa kuwa na *project engineers* ambao wanakuwa *site* muda wote ili kuwasimamia wakandarasi. Kwa hiyo, kwa kufanya hivi ninaamini kwamba tutatatua changamoto hizi ambazo zimetajwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, kulikuwa kuna suala la *variations;* yaani gharama kwenye mkataba unapokwenda kujenga, mkandarasi anakuja kuomba hela ya ziada ili kukamilisha ujenzi wa barabara. Kumekuwa na changamoto mbalimbali nyingine ikiwepo usanifu wa kina unapofanyika tunachelewa kuanza ujenzi wa barabara, inaweza ikachukua miaka mitano, miaka kumi, lakini kule mawandani unakuta hali imebadilika, eneo ambalo halikuwa na makazi unakuta watu wamekwishahamia au mvua za *El Nino* zimeharibu eneo husika. Kwa hiyo, unapokwenda kwenye ujenzi unakuta gharama halisi imekuwa kubwa kuliko usanifu uliofanywa miaka mitano au miaka kumi iliyopita.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimeelekeza *TANROADS* kwamba kabla hatujaanza taratibu za manunuzi, kuhakikisha barabara zote ambazo tumezisanifu tunazi-*review* ili mikataba tunayoingia na gharama za kujenga hizo barabara iwe na uhalisia ili kuepuka haya masuala ya *variation*, maana kukiwa na

variations, hujalipa hiyo *additional cost,* unaweza ukajenga hizi barabara ili mradi iishe na baadaye mnapata hizi changamoto za *premature failure.*

Mheshimiwa Spika pamoja na Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema Serikali hii ambayo inaongozwa na Jemedari wetu Mheshimiwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni Serikali sikivu, inaheshimu mchango na usimamizi wa Bunge kwa Serikali anayoiongoza. Sisi wasaidizi wake hatutakuwa kikwazo kwa hii dhamira ya Mheshimiwa Rais na *4R* ambazo anazisimamia ikiwemo suala hili la *checks and balances.* Masuala ambayo Bunge mnatuagiza, tutakuwa tayari kuyatekeleza na kuleta mrejesho kama ulivyo utaratibu wa Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Jerry William Silaa, atafuatiwa na Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka, Mheshimiwa Halima James Mdee ajiandae.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MANDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, nami nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hizi zilizopo mezani na mimi nichukue fursa hii kuwapongeza sana wenyeviti wa Kamati hizi mbili kwa taarifa zao. Niwapongeze sana wachangiaji waliochangia kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuishauri Serikali kwa niaba ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwenye Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali ukurasa wa 40 kulikuwa na hoja ya Mradi wa Urasimishaji wa Makazi. Serikali mwaka 2013 ilikuja na mpango wa miaka kumi wa kurasimisha makazi holela kwa maana yako maeneo mengi hasa Dar es salaam na miji mingi mikubwa ambayo tayari makazi yalijengwa bila kupangwa na kupimwa.

Mheshimiwa Spika, mradi huu ulikuja kama suluhu ya kuunganisha nguvu, kwa maana ya kutumia kampuni binafsi za upimaji na upangaji kama wataalamu na kuziba lile *gap* la upungufu wa wataalamu, kutumia wananchi kuchangia zoezi zima la kupanga na kupima, lakini pia Serikali kuratibu. Zoezi hili

likikamilika litasaidia kuongeza mapato lakini pia kupunguza migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, ardhi kwa mujibu wa sheria zilizotungwa na Bunge lako zinapaswa kumilikiwa kisheria. Umiliki wa ardhi mijini unasimamiwa na Sheria Na. 4 ya mwaka 1999, na kila mtu anayeishi kwenye eneo lililopangwa na kupimwa atamiliki ardhi yake kwa hati, na ndio umiliki ambao Serikali imekuwa ikihimiza kupitia Mradi wa Urasimishaji, na hii inaondoa migogoro kwa sababu umiliki huu huu wa kienyeji, nimetumia lugha ambayo si sahihi; ni umiliki wa haki ya Mungu, kwamba ili umthibitishie mtu unamiliki ni lazima uapie. Hata hivyo, zoezi la urasimishaji lilienda kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, nilitaarifu Bunge lako mpaka kufikia mwezi Januari, 2024 jumla ya vipande vya ardhi 2,400,000 vimetambuliwa na viwanja 2,500,000 vilikuwa vimekwishapangwa kwa maana ya *TP Drawings*. Kati ya hivyo, viwanja 1,400,000 upimaji wake umekamilika, kwa maana ya *survey,* na viwanja 1,100,000 sawa na asilimia 42 bado havijakamilika.

Mheshimiwa Spika, niombe pia kupitia Bunge lako niseme kwamba katika pesa ambazo zilikadiriwa kukusanywa ili zoezi hili likamilike, shilingi bilioni 331 ni bilioni 72 tu ndizo zimechangwa na wananchi, na ndiyo maana zoezi hili limekuwa linakwenda kukwama.

Mheshimiwa Spika, sasa ni nini suluhu? Suluhu namba moja, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, amekwishatoa maelekezo, na kupitia Mradi wa *LTIP* zimetengwa jumla ya dola milioni 62; zile dola milioni 21 alizosema Mheshimiwa Mtemvu ni kiasi cha fedha hizo na mradi huu unakwenda kukwamuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo maeneo yote na tumeanza na Dar es salaam, hapa Dodoma tumekwishafanya *pilot,* jimbo la Mtemvu yeye ni shahidi litakuwa la kwanza pale Dar es salaam na kazi kubwa inafanyika.

Mheshimiwa Spika, zoezi hilo la ukwamuaji linakwenda pamoja na kliniki za ardhi ambazo ukiangalia kwenye viwanja hivi 1,400,000 vilivyopimwa, ni ankara 623,000 tu ndizo zimeanza kufanyiwa *process* za kupata hati na ni hati 230,000 tu zimemilikishwa. Sasa kutoka viwanja 1,400,000 mpaka hati 230,000 ni namba ndogo lakini kliniki hizi zinamsogezea mwananchi huduma karibu zaidi na zinampunguzia urasimu wa kufuatilia hati. Hivi ninavyozungumza kliniki iko pale Kibo – Tegeta; na kuanzia Jumatatu tarehe 29 mpaka tarehe 25 kliniki ya ardhi itakuwa pale Bunju kwenye Wilaya ya Kinondoni. Hiyo wiki moja ni ile wiki ambayo na Wizara ya Ardhi kwa maana ya Waziri na watendaji wa makao makuu watakuwa pale Bunju kwa ajili ya kutatua migogoro ya ardhi pamoja na kuendelea kukwamua zoezi hili la urasimishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilithibitishe Bunge lako kwamba Wizara imejipanga, uongozi thabiti wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, umekwishatupatia maelekezo na pesa zipo. Ninaamini kwenye ripoti zijazo za *CAG* na ripoti zijazo za Kamati, zoezi la urasimishaji litakuwa limefika mahali pazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kulishukuru Bunge lako kwa miongozo na maelekezo mnayotupatia na wakati wote Serikali iko tayari kwa maelekezo, ushauri wa Bunge na wakati wote tunachukulia *very serious* ripoti hizi za Kamati na michango ya Wabunge wote waliochangia tumechukua na tutaifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kadri ya ratiba ya Bunge kwenye vikao vinavyokuja, tutakuwa tukitoa taarifa ya zoezi la urasimishaji na mazoezi mengine ya ardhi ili kuweza kuhakikisha kwamba kero za ardhi zinafika mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikushukuru tena na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali aje ahitimishe hoja ya Kamati.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, hitimisho la hoja; kwa mara nyingine tena nikushukuru wewe binafsi kwa kuendelea kutuongoza hapa Bungeni kwa weledi mkubwa. Aidha, naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja ya Kamati ya *PAC* ikiwa ni pamoja na Mawaziri wetu wanne ambao wote wamechangia katika hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya Kamati imechangiwa na jumla ya Waheshimiwa Wabunge tisa nitawataja tu upesi upesi, akiwepo Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mheshimiwa Venant D. Protas, Mheshimiwa Joseph G. Kakunda, Mheshimiwa Ester A. Bulaya, Mheshimiwa Geoffrey I. Mwambe Mheshimiwa Jacqueline N. Msongozi, Mheshimiwa Issa J. Mtemvu, Mheshimiwa Esther N. Matiko pamoja na Mheshimiwa Condester M. Sichalwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge, ningependa tu kutoa maelezo ya msisitizo katika maeneo machache yafuatayo, haya maeneo nataka Bunge lako lielewe kwamba sasa hivi tunasisitiza kuangalia mambo ya ufanisi kuliko kuangalia tu mambo ya hesabu. Kwa hiyo, kwa nini naeleza haya? Maana *value for money* tutaipata pale ambapo tutaona kaguzi za kifanisi au za kiufundi inasemaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana kihesabu unakuta kwamba kweli hela inaonekana zimetumika lakini je, kazi *field* iko wapi? Ndiyo maana sitajibu hoja zote Waziri amezitoa kwa vile nataka tu nionyeshe kwamba kuanzia sasa na kuendelea kazi yetu kubwa ya *PAC* itakuwa ruksa ya Mheshimiwa Spika kuangalia zaidi ukaguzi wa ufanisi na ukaguzi wa kiufundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe tu ufafanuzi kidogo maana ya ukaguzi wa ufanisi. Hii ni aina ya ukaguzi uliojikita kuangalia kama uwekevu tija na ufanisi yaani *economy efficiency na effectiveness* miongoni mwa taasisi za umma katika matumizi ya rasilimali ili kufikia malengo waliyojiwekea. Ukaguzi wa ufanisi huchunguza

iwapo shughuli mipango au miradi ya Serikali inayohusisha ukusanyaji wa matumizi ya fedha za umma inafanyika kwa kuzingatia kanuni hizo tatu, yaani uwekevu, ufanisi na tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa kiufundi *technical audit* ni ukaguzi unaojumuisha uchunguzi na tathmini huru juu ya upangaji, usanifu ununuzi na utekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa lengo la kutoa matokeo ya usimamizi na utekelezaji wa miradi hiyo. Wahusika juu ya masuala yote yanayoathiri utekelezaji na utendaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa kiufundi ni ukaguzi katika mchakato mzima wa utekelezaji wa mradi kuanzia hatua ya maandalizi ya awali utekelezaji wa mradi, ukamilishaji na makabidhiano ya mradi. Hujikita zaidi katika kutazama kama mradi utetekelezwa kwa wakati ndani ya gharama iliyokusudiwa, kwa ubora uliokusudiwa, na kama malengo ya uanzishwaji wa mradi yametimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama walivyochangia Waheshimiwa Wabunge nguvu kubwa sasa ya Bunge ni lazima ielekezwe kwenye kupitia na kujadili kaguzi za namna hii kwani zinasaidia sana kuweka uwajibikaji wa fedha za umma badala ya kuangalia kaguzi za hesabu tu yaani *financial audit reports* peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya uondoshaji wa magari imeongelewa kwa kina hasa magari kuuzwa bei ya chini ya soko, kutokuwepo kwa uwazi katika uondoshaji wa magari na kuchelewa kutoa vibali vya uondoshaji wa magari. Pia hoja ya utekelezaji wa malengo ya maendeleo endelevu imesisitizwa, umuhimu wa kusimamia ukusanyaji wa mapato kwa vyanzo vya ndani ilivyoainishwa na umuhimu wa takwimu ili kuweza kufanya tathmini ya utekelezaji wa mpango. Pia hoja nyingine ambayo imegusiwa kwa undani hasa na ripoti ya *CAG* juu ya matengenezo ya miradi ya maji wachangiaji wamesisitiza usimamizi unaofaa wa miradi ya maji ili kuleta tija, pia ulipaji wa madeni ni jambo muhimu katika kuhakikisha kwamba miradi yetu ya maji inakuwa endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge likubali kupokea Taarifa ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (*PAC)* kwa mwaka 2023 pamoja na maoni na mapendekezo ya Kamati ili yawe Maazimio ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

MHE. VENANT D. PROTAS: Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge kwa kazi nzuri pamoja na Kamati nzima, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji Wabunge kuhusu hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu ya Serikali kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2023.

(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja ya Kamati imekubaliwa na sasa maazimio yote yaliyo kwenye taarifa hiyo ni Maazimio ya Bunge na ni maelekezo mahsusi kwa Serikali.

(Maoni na Mapendekezo ya Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali (PAC) kuhusu shughuli za Mwaka 2023 yaliafikiwa na Bunge)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Halima James Mdee aje ahitimishe hoja ya Kamati yake.

MHE. HALIMA J. MDEE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, nami niwashukuru Wabunge wote waliochangia, jumla ya Wajumbe waliochangia ni 11, Mheshimiwa Munde T. Abdallah,

Mheshimiwa Twaha A. Mpembenwe, Mheshimiwa Venant D. Protas, Mheshimiwa Ally J. Makoa, Mheshimiwa Michael C. Mwakamo, Mheshimiwa Ester A. Bulaya, Mheshimiwa Suma I. Fyandomo, Mheshimiwa Jacqueline N. Msongozi, Mheshimiwa Esther N. Matiko, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu L. Nchemba, Mheshimiwa Deogratius Ndejembi na Mheshimiwa Innocent L. Bashungwa japokuwa kwangu aligusiagusia kiujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaanza kwa kujibu hoja kadhaa kisha nitaliomba Bunge likubali mapendekezo ya Kamati yetu kwa sababu hakuna mabadiliko yoyote ambayo yameletwa mbele ya Meza yako.

Mheshimiwa Spika, kwanza niseme hivi, kwamba ni kweli Mheshimiwa Rais anapenda na pamoja na timu yake kuelekeza fedha huko chini, humu kuna lugha hapa inatumika kwamba Mheshimiwa Rais ameshusha fedha, ni kweli kabisa jana wakati Kamati ya Bunge ya Bajeti inapitisha taarifa yake hapa ilituambia kwamba Deni la Serikali ni trilioni 87.4, wakasema ongezeko la deni limetokana na ukopaji kwa ajili ya kugharamia miradi ya kimkakati ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, elimu, afya, kilimo, mifugo na nishati ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taarifa yetu *LAAC* ilijikita kwenye eneo la elimu, eneo la afya, miundombinu inayofanania hivyo. Sasa tunachozungumza hapa ni kweli fedha inaweza ikatafutwa lakini fedha ikishatafutwa ikishuka huko chini inaenda kusimamiwa kwa ufanisi? Kama fedha haisimamiwi kwa ufanisi wa kuwajibika hapa ni nani? Yupo sahihi kabisa! Rais ni mtu mmoja lakini Rais si ana miguu, ana mikono ana vidole, sasa ninyi Wasaidizi wa Rais ndiyo inatakiwa mmsaidie Rais. Sasa si Wasaidizi wa Rais wanakuja hapa wanatumia mgongo wa kumpamba Rais wakati wao hawatekelezi wajibu wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilisema hapa, hii ni mikopo kwa sababu kila mmoja anajua bajeti yetu haijawahi kujitosheleza, kama tutaweza kujitosheleza tutalipa mishahara, tutalipa Deni la Taifa, ikiisha hivyo hatuna pesa abishe Mheshimiwa Mwigulu hapa. Sisi

tunachozungumza ni nini? Kwamba kunapokuwa kuna Mawaziri, kunapokuwa kuna Wakuu wa Mikoa, kunapokuwa kuna *RAS* kunapokuwa kuna ma-*DAS*, kunapokuwa kuna Wakuu wa Wilaya kunapokuwa kuna Wakurugenzi wanalipwa mishahara kuna wataalam wanafanya kazi gani? *Simple mathematics*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunachozungumza hapa ni kila mmoja atekeleze wajibu wake kwa nafasi yake, kila mmoja awajibishwe kwa nafasi yake lakini asionewe, awajibishwe baada ya kuchunguza na kujiridhisha ndipo tutatengeneza uwajibikaji kwenye Taifa hili, hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili suala la idadi ya wataalam amezungumza hapa ndugu yangu Mheshimiwa Ndejembi amesema wameajiri Wahandisi 362, sasa nisaidie tu Mheshimiwa Ndejembi nijibu pia na Mheshimiwa Mwigulu, sisi tunapofanya kazi yetu huwezi kutuambia ni ripoti ya miaka miwili mitatu iliyopita, utaratibu wa Kamati za *oversight* za Bunge ni kweli taarifa inatoka ya mwaka fulani lakini wakati wanakuja kukutana na Kamati ya Bunge kwa kipindi kile, wameenda kwenda kurudia tena hivi Serikali hapa mlikuwa mmekosea hapa, hapa na hebu tupeni majibu mpaka sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapozungumza wakati hili ni Bunge la mwezi wa pili si ndiyo? Bunge la mwezi wa pili, wakati tuko kwenye Kamati Januari Wakaguzi walikutana na Serikali. Kwa hiyo Taarifa hizi tunazozizungumza hapa za upungufu wa watumishi ni upungufu si wa miaka miwili iliyopita, hii ni taarifa *current*. Sasa basi tu-*assume* ni taarifa ya zamani, imesema mmeajiri Wahandisi 362, mmepeleka kila Halmashauri Mhandisi mmoja mmoja. Kilwa kwa mfano, tumesema ilikuwa na Wahandisi wanne mkadiraji majenzi mmoja, miradi 157 ya *force account,* tufanye mmempeleka watano, sasa Wahandisi watano ndiyo wasimamie miradi 157 ndiyo akili hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Nzega kulikuwa kuna Mhandisi mmoja, tu-*assume* alichokisema ndugu yangu ni *correct* haya wakadiriaji ujenzi, Mhandisi mmoja, Nzega akapelekwa mwingine wa pili, haya Wahandisi wawili ndiyo wanaweza kusimamia miradi ya

force account 115? Haiwezekani! Ndiyo maana watu walioleta hii *force account* ukisoma muongozo wa *PPRA* uko-*clear,* yaani huu muongozo una vipengele 36 ungefuatwa kwa ufanisi wake wala tusingekuwa tunatoana mapovu hapa, kwa sababu kila kitu kingeenda *smooth. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mwongozo unasema *general conditions for the use of force account, general conditions!* Inasema lazima taasisi nunuzi au *procuring entity* iwe na *qualified personnel* ambao wanatambulika na *relevant professional bodies to carry out and supervise the required works*. Yaani muwe na watu ambao wanakidhi vigezo, wana taaluma ile inayotakiwa na wanatambuliwa na vyombo vya kitaaluma kuweza kufanyiwa kazi, sasa hivi *nurse* amewahi kuwa, daktari amewahi kuwa, Mwalimu amewahi kuwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hayo mambo tunayazungumza kwa nia njema, hatutaki mje hapa mjitetee kwa sababu idadi ya wataalam ni pungufu ndiyo maana tunasema tugawane kazi. Ndiyo maana leo Kamati yetu ukiona hiyo miradi midogomidogo sijui milioni 50, milioni 20, milioni kumi, haina shida kwa sababu ni miradi *basic,* na tunaposema makandarasi hapa kwamba hatusemi wa nje, hivi kweli hatuna Watanzania wanaoweza kufanya kazi za hiyo thamani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii kwenye *force account, risk* ni kwa Serikali, hatu-*shift reliability* kwenda kwa mtu mwingine, mnatengeneza hamna wataalam, mnajenga vitu vya hovyo, vikiharibika huna mtu wa kumfanya awe *accountable! We should use simple common sense,* hakuna mtu anayetafuta mchawi hapa, tunataka kama mnampenda Rais kama mnavyosema, ninyi si ndiyo wasaidizi wake, msaidieni basi, halafu mkishamsaidia hamtahitaji kujieleza yeye mwenyewe ataona hawa wamenisaidia, hilo la pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, Mheshimiwa Msongozi nashukuru kwa mifano yako uliyoizungumza hapo, ndiyo yanayosemwa, kuwe na ukomo wa gharama, uliyozungumza Mheshimiwa Msongozi umezungumza katika lugha ya

kidiplomasia lakini inasemekana pesa wala hazitoshi kwa sababu pesa zikienda zina mikono mingi! Hiyo ndiyo ilivyo, kwamba zikienda zina mikono mingi, kazungumza Mheshimiwa Bulaya, kazungumza Mheshimiwa Msongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tunasema, tutasema mpaka mfanyeje? kuwe na ukomo. Mheshimiwa Mwigulu ninashukuru hukuleta lile pendekezo lako kwa sababu sisi tumesema hivi, kwenye moja kati ya mapendekezo yetu, kuwe na ukomo wa gharama za mradi wa *force account*. Sasa wewe ukituzungumzia kwa sababu Sheria ya Manunuzi tunayoipitisha ilikupa-*room* ya kutengeza Kanuni.

Mheshimiwa Spika, hakuna popote kwenye Sheria ya Manunuzi ambako tumezungumza hili jambo, ndiyo maana tukasema kwenye Kanuni mtakazozitengeneza Bunge liazimie ukomo uwepo. Sasa kama wewe umeshatengeneza Kanuni zako ulitakiwa useme hapa kwamba tumetengeneza Kanuni. Kanuni mpaka ifikie Kamati ya Sheria Ndogo ndiyo itakuwa imefikia Bunge, sasa hiki unachozungumza ni kitu ambacho unacho wewe sisi hatukijui, *it is well and good* kama umefanya hivyo *then* Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo italetewa tutaona kwamba kwenye hili eneo kuna ukomo ili wapewe fedha ambao wana uwezo wa kuifanyia kazi. Hilo ni jambo la tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha zitolewe kutokana na jiografia ya eneo, imeshazungumzwa vizuri. Nizungumze hoja nyingine ilizungumzwa na Mheshimiwa Ndejembi kama sikosei, wakitaka kuhalalisha milioni 800 na kadhaa ambazo tulizungumzia kuhusiana na Nzega. Kwanza nimsahihishe alitakiwa ajue lakini nataka nimsahihishe, kwamba Nzega ilitumia hela katika mazingira mawili. Mazingira ya kwanza ni hiyo milioni 470 ambayo ilishushwa lakini kulikuwa kuna fedha nyingine milioni 379. Hii milioni 379 siyo fedha ya ndani ya Nzega. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapato ya Nzega *DC* hawana ubavu wa kuwa na hii pesa kwenda kupeleka kwenye mradi mmoja, ubavu huo hawana. Hii pesa iliingia Halmashauri katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya elimu bure ikawa imekula *pause*

pale, watu walikuwa wanailia *timing* isishtukiwe hilo wanajua wenyewe. Mwaka 2021/2022 Halmashauri ya Nzega iliomba kibali cha kutumia shilingi milioni 379 kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Sekondari Kata ya Nzega. Kwa hiyo, kwanza nilitaka ajue siyo fedha ya ndani ni fedha ambayo ilikuwa kwenye Halmashauri, kwa ajili ya elimu bure, elimu bure haikufanyika, ikasubiri huko imetulia 2021/2022 wakaomba.

Mheshimiwa Spika, sasa swali linakuja, hivi labda niwarudie ili kuwaelimisha hiyo milioni 470 ilikuwa katika muktadha wa ujenzi wa vyumba nane vya madarasa, maabara za sayansi tatu, jengo moja la utawala, maktaba moja, chumba cha *ICT* kimoja, vyoo 20 vya wanafunzi yaani wavulana 10 na wasichana 10, matenki mawili ya maji kila moja lita 10,000 na nguzo ya kuweka tanki husika na miundombinu ya kawaida kwa ajili ya maji, ndiyo ilikuwa 470.

Mheshimiwa Spika, wenzetu wa Nzega wakatumia shilingi milioni 849, tunaambiwa walijenga ghorofa. Sasa sisi tuliokuwa kwenye Kamati ambao tuna taarifa hizi kwa mapana, hizi idadi za majengo ambayo yamezungumzwa hapa kama nilivyoyataja, ndiyo *exactly* idadi ya majengo ambayo Nzega wamejenga. Sasa tukajiuliza, halafu wamejenga ghorofa moja, hivi ghorofa ukijenga ile *floor* moja ile, yaani kale kanaitwa kasakafu eeh! Ile sakafu ambayo inatenganisha nyumba ya chini na nyumba ya juu ndiyo shilingi milioni zaidi ya 200 inayokaribia 300! Hivi huu msingi ambao sasa, maana na ninyi si mnajenga maghorofa yenu kwenu jamani, si ndio!

Mheshimiwa Spika, huu msingi ambao ndiyo unashindiliwa zaidi ili kuweza kubeba hivyo vyumba vingine vinne vya madarasa huko juu, ndio una *justify* milioni karibia 300 na nyongeza? Hapana. Kuna Halmashauri ya Arumeru nadhani, wao wamejenga ghorofa mbili, siyo haka kaghorofa kamoja ka Nzega, ghorofa mbili, haijafikisha hata shilingi milioni 700, kitu kimetulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunachojaribu kuzungumza hapa ni nini? Hatutaki muwe watetezi pale ambapo hamna

taarifa sahihi zilizofanyiwa uchunguzi za haya mambo. Mkigeuka watetezi, ndiyo maana hii nchi inakuwa ngumu kuibadilisha. Huwezi kubadilisha nchi pale ambapo mtu ambaye tunafikiria atakuwa msaada wa Rais katika kusimamia jambo, anakuwa ndio mtetezi. Mimi nilidhani angesema tumekuwa, tukafanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana sisi kwenye maazimio yetu tumewaambia, kwa sababu mwongozo wa Serikali umeeleza *categorically* kwamba uhai wa majengo yenu yanatakiwa yaweje? Miaka 50, miaka 75, wengine kwenye madaraja huko miaka 100. Tumewaambia nendeni mkafanye ukokotoo, mkakokotoe ili mjiridhishe kwamba je, kwenye hayo majengo yaliyojengwa, yamejengwa kwenye thamani inayotakiwa. Sasa badala mkafanye hiyo kazi halafu mje na *findings*, Waziri anasimama hapa anatetea nyongeza ya shilingi milioni 300 kwa sababu eti kuna ka-*floor* kamoja kalichotenganisha juu na chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu tulisema hapa, hakuna mtu anayebisha kwamba *practically* kilichoandaliwa na TAMISEMI kama *baseline* huku Makao Makuu kutokana na tafiti ambayo labda wamefanya kwenye maeneo fulani hakiwezi kuongezeka. Hakuna aliyebisha. Hata sisi kama Kamati hatujakataa kwamba kutoka shilingi milioni 470 inaweza ikaongezeka hadi shilingi milioni 500, hatujakataa, inaweza ikaongezeka hadi shilingi milioni 550, hatujakataa, lakini tunataka nyongeza iweze kuwa *justified*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa jamaa zetu tuliokuja kuhojiana nao, amezungumza Mheshimiwa mmoja hapa, unawaambia *okay*, sawa mmeongeza ngapi? Tuambie shilingi ngapi? Wakati huo wameshakaa na CAG mpaka wiki tatu zilizopita wameshindwa kuafikana, sisi tunawaambia *okay* tunawapa *benefit of doubt*. Tulitakiwa tusiwasikilize kwa sababu jicho letu mmeshindwa kulisaidia, wala kulipa kulipa majibu, tunawasikiliza basi. Kama wataweza kueleza sana, ataenda shilingi milioni 10, atapiga 20 halafu akifika 30 anaona maneno yanaisha. Anaanza kusema, Mheshimiwa sina maelezo ya ziada.

Mheshimiwa Spika, ukimwambia *okay,* naomba *BOQ*, yaani *BOQ* kuipata kwa wale jamaa ni vita. Sasa unajiuliza, kama ninyi ni wasafi na wanyoofu kama mnavyosema, kwa nini kunakuwa kuna mapambano makali pale Kamati ya Bunge inapotaka *BOQ* kutoka kwenu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi tunawaomba tu ndugu zetu hawa wajue kwamba hatuna nia mbaya. Tunakaa mpaka saa sita usiku Kamati yako, nawashukuru Wajumbe wangu kwa uvumilivu, kwa ajili ya kufanyia kazi mambo haya ambayo kimsingi yalitakiwa yafanywe na mabwana na mabibi au ndugu zetu hapa pamoja na ile mikono na miguu ya Rais, ili Bunge lako likija kusikiliza mambo haya, tunakutana na vitu ambavyo vimefanyiwa kazi na watu ambao wana akili zao timamu, na watu ambao wameajiriwa kwa ajili ya kufanya kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, baada ya maelezo hayo, kwa sababu tumekubaliana in *principle* kwamba tatizo lipo, na kwamba kuna usimamizi hafifu wa miradi, hatuna wataalam, *value for money* haipo. Kwa hiyo, tunaomba yale maazimio ambayo Kamati yako ya Bunge iliomba Bunge lako liazimie, tunaomba kuweka msisitizo kwenye mapendekezo ambayo Kamati imeyatoa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mapendekezo haya hayajafanyiwa mabadiliko na mtu yeyote, tunaomba Bunge hili Tukufu liweze kuyaazimia mapendezo yote na Serikali iyatekeleze kikamilifu ili kuondoa upungufu wote uliyobainika kwa manufaa na ustawi wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa kuhitimisha hoja, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijawahoji, alisimama Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuhusu maazimio. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu nimejaribu kupitia maazimio yanayohusu hii taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa muktadha ule uliouzungumzia, hakuna azimio ambalo linaathiri uwepo wa sheria na utungwaji wa kanuni. Kwa hiyo, hivi yalivyo pamoja na wewe kwamba ulisema kwamba mengine yaondoke, mimi nimeyapitia, hakuna hata moja ambalo lina uhusiano. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge sasa nitawahoji, kuhusu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2023.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Maoni na Mapendekezo ya Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu shughuli za Mwaka 2023 yaliafikiwa na Bunge)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, msiwe mnafanya masihara kwenye mambo mazito kama haya.

Wabunge wote wameafiki taarifa ya Kamati kwa hivyo maazimio ya Bunge sasa yanaenda kwa Serikali kama maelekezo mahususi baada ya kuwahoji. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa siku yetu ya leo. Nitumie fursa hii kuwashukuru sana Wenyeviti wa Kamati hizi mbili ambazo zimewasilisha leo lakini pia Makamu Wenyeviti wa Kamati hizi na Wajumbe wa Kamati hizi mbili zinazohusika na kutazama Hesabu za Serikali; moja, Serikali lakini nyingine Serikali za Mitaa. Tunawashukuru sana kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya na kwa muktadha huo huo tumshukuru pia CAG kwa kazi nzuri anayoifanya ya kutusaidia kutazama huko na huko na sisi tunaweza kufanya kazi yetu vizuri ya kuisimamia na kuishauri Serikali. *(Makofi)*

Pia, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa namna mlivyoshiriki katika zoezi hili zima la kuhakikisha tunaweza kuishauri na kuisimamia Serikali na hasa kwenye eneo hili ambalo Kamati zetu hizi mbili zinatusaidia kuangalia matumizi ya fedha za umma.

Waheshimiwa Wabunge, pia nitumie fursa hii kuishukuru Serikali kwa sababu upande wa Serikali wachache waliopata nafasi ya kuchangia wote wameonyesha utayari wa kwenda kuyafanyia kazi yale ambayo Bunge imesema na hakuna hata aliyesema kwamba hii haiwezekani ama hili limekaa namna gani. Wamesimama wote kwa ajili ya kutoa ufafanuzi kwenye baadhi ya hoja, lakini haikuwa kwenye kubishana na Kamati juu ya yale ambayo Kamati imeleta. Kwa hiyo, nawashukuru Serikali kwa ushirikiano ambao mmeutoa katika zoezi hili zima la taarifa zetu za Kamati.

Sasa kwa sababu taarifa ya Kamati ya mwisho tutaijadili kesho, basi yale mambo yaliyo ya jumla yatasemwa siku ya kesho kuhusu maazimio hayo ya Bunge na pale ambapo Bunge limetoa maoni ama mapendekezo, tunatarajia nini kutoka kwa upande wa Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kusema hayo, jambo moja tu, Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, alitoa ufafanuzi kuhusu madeni ambayo yametajwa kwenye Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali na kile kiasi ambacho kimetajwa ambacho kinahusu riba inayoweza kuzalishwa ama ambayo imezalishwa mpaka Desemba, 2023. Sasa kabla ya taarifa hii huko nyuma Kamati yetu hii imeshawahi kutoa taarifa ya madeni yanayofanana na hayo na nadhani wakati huo ilikuwa ni hapo hapo kwenye hizo hizo shilingi bilioni kama siyo 67, 68; na Bunge liliazimia wakati huo kwamba Serikali itafute namna ya kupunguza ule ucheleweshaji wa malipo kwa hawa wakandarasi ili hii riba, hata kama inaweza ikaonekana ni ndogo ukilinganisha na deni la shilingi milioni 701 lakini riba ya bilioni sitini na kitu ni kubwa. Kwa sababu ukianza kuangalia ni shule ngapi zingejengwa, ukiangalia ni zahanati ngapi zingejengwa, vituo vya afya vingapi, bado ni kubwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa sababu Mheshimiwa Waziri wa Fedha pia yuko hapa na nimeona kwa sababu maazimio haya tumeshalihoji Bunge, kwa hiyo, ni maelekezo kwa Serikali, mojawapo ya mambo ambayo wamesisitiza Kamati hii ya *PAC* mwishoni kabisa hapa; hili ni muhimu kwa sababu limeshajitokeza mara kadhaa, "Serikali iingie mikataba mipya ya ujenzi wa miradi pale tu inapokuwa na uhakika wa bajeti na fedha za miradi husika, ili kuepuka malipo ya riba kwa kuchelewa kulipa wakandarasi kwa wakati." *(Makofi)*

Sasa tunafahamu mazingira yako mengi, maana tukisema hivi watu wasije wakafikiri labda hatuelewi. Tunafahamu, kwa mfano, leo asubuhi tulikuwa tunajadili kuhusu fedha za dharura kwenda kushughulika na barabara za *TANROADS* na pia barabara za *TARURA* ili wananchi waweze kuendelea na shughuli zao za kiuchumi. Kwa hiyo, hilo tunalielewa, lakini kwa ujumla wake, lazima pia ieleweke kwamba Bunge linatamani tufike mahali ambapo hizi riba basi tuwe tunazipata na sisi kutoka ule upande mwingine badala ya sisi kila wakati ndio tunadaiwa riba; na hizo riba kila wakati ziko kwenye mabilioni. Basi ziwe zimechelewa kidogo ziwe kwenye mamilioni, badala ya kutaja kwenye mabilioni inaonekana ule uchelewaji unakuwa ni mkubwa, kwa hiyo, riba inazidi kuzaa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunawatakia kila la heri kwenye utekelezaji wa hawa maelekezo ya Bunge ambayo limewapa leo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nawashukuru kwa uvumilivu wenu. Muendelee kufanya hii kazi, ndiyo mliiomba kwa wananchi. Ahsanteni sana, nawatakia jioni njema.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

(Saa 7.16 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 16 Februari, 2024 Saa Tatu Asubuhi)